

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 17 Mei, 2014

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne. S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:

Hotuba ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Hotuba ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

MHE. MARY P. CHATANDA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEOYA JAMII, JINSIA NA WATOTO):

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

MHE. JUMA SURURU JUMA – (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII):

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha

Nakala ya Mtandao (Online Document)

2013/2014 na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

MHE.SALUM K. BARWANY - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

MHE. CECILIA D. PARESSO (K. n. y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

SPIKA: Ahsante sana. Naona hapa kunaanzishwa ka-precedence Manaibu Waziri wawili hapa wamekuja wanawasilisha kwa niaba ya Waziri wao wakamtaja na jina, hapana. Ni kwamba unawasilisha kwa niaba ya Serikali na ni Waziri anaweza akawa Waziri mwingine katika Wizara hiyo hiyo akateuliwa Waziri mwingine akasoma sasa atakuwa sio Mheshimiwa Kawambwa wala sio Mheshimiwa Sophia Simba.

Kwa hiyo mnawasilisha kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Sio kumtaja Waziri fulani, hapana anaweza kuteuliwa mwingine hapa Waziri akasoma kwa niaba ya Waziri. Kwa hiyo naomba hii msiiweke mnatugeuzia maneno hapa.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mwaka 2014/2015 Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu baada ya kuzingatia Taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyezeki wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto, sasa lijadili na Kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia kuwa na afya njema na hivyo kuweza kushiriki Mkutano huu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tafadhali niruhusu nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, Waziri Mkuu na Mbunge wa Katavi, kwa uongozi wao mahiri ambao umewezesha kushamiri kwa usawa wa jinsia na uzingatiaji wa haki za mtoto katika jamii ya Watanzania. Mwenyezi Mungu awajalie afya njema ili waendelee kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa uendeshaji bora wa shughuli za Bunge. Tunaendelea kumwomba Mwenyezi Mungu awajalie afya njema ili muweze kusimamia na kuratibu shughuli za Bunge kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia muda nilionao kuwasilisha hoja yangu naomba hotuba yote kama ilivyo katika kitabu cha hotuba iingie kwenye Hansard.

Mapitio ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 kwa kipindi cha Januari, 2011 hadi Machi, 2014.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari 2011 hadi Machi, 2014 Wizara yangu ilitekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 kupitia maeneo makuu manne. Maeneo hayo ni pamoja na ajira na uwezeshaji wa wananchi, elimu ya juu, uendeshaji wa makundi mbalimbali na demokrasia na madaraka ya umma. Katika kipindi husika utekelezaji wa maeneo hayo umekuwa na mafanikio kama inavyoelezwa kwa kirefu kwenye kitabu cha hotuba yangu ukurasa wa 3 hadi 11. Hali halisi ya Maendeleo ya Jamii na changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Spika, sekta ya Maendeleo hapa nchini imeendelea kukua na kutambulika kwa wadau mbalimbali kutokana namchang'o wake katika maendeleo ya Taifa letu. Naomba kuchukua fursa hii kueleza kwa kifupi hali halisi ya sekta hii katika maeneo ya ushiriki wa wananchi katika maendeleo ya kiuchumi, maendeleo ya jinsia, maendeleo ya watoto na ushiriki wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, wataalamu wa Maendeleo ya Jamii ni muhimu katika kuongeza ushiriki wa wananchi katika maendeleo. Kwa sasa kuna wataalamu wa Maendeleo ya Jamii 2,675 katika ngazi ya Halmashauri na 21 katika Sekretarieti za mikoa.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kwa takwimu hizo kuna upungufu asilimia 61 ya wataalamu hao katika ngazi ya Halmashauri na asilimia 16 katika ngazi ya Sekretarieti za mikoa. Aidha, wananchi wameendelea kunufaika na mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi yanayotolewa na vyuo 55 vya Maendeleo ya Wananchi vilivyo chini ya Wizara yangu. Mafunzo haya yanawawezesha kujajiri na kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, hali ya usawa wa kijinsia katika nyanja mbalimbali hapa nchini imeendelea kuimarika. Ukweli huu unadhihirishwa na ushahidi wa kitakwimu na taarifa zilizopo katika maeneo ya ushiriki wa wanawake katika siasa na ngazi za maamuzi, uwezeshaji wa wanawake kiuchumi, elimu, mafunzo na ajira. Kuongezeka kwa wanawake wajasiriamali wadogo na wa kati na upatikanaji wa haki za wanawake kisheria.

Mheshimiwa Spika, watoto ni sehemu muhimu ya jamii na ndio tegemeo la taifa lolote. Watoto wanahitaji kukua na kuwa raia wema hivyo wanatakiwa kupewa haki na mahitaji yao ya msingi ikiwa ni pamoja na kuishi, kupewa malezi stahiki, kulindwa, kuendelezwa kiakili kwa kutambua na kukuza vipaji vyao kutobaguliwa na kushirikishwa. Kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya Taifa ya Idadi ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 idadi ya watoto chini ya miaka 18 Tanzania Bara ni 21,866,258 sawa na asilimia 50.1 ya idadi ya watu wote.

Kati ya hao wasichana ni 10,943,846 na wavulana ni 10,922,412 kwa kuzingatia umuhimu wa watoto Wizara kwa kushirikiana na wadau inaendelea kuweka mazingira wezeshi ili watoto wote hapa nchini wapate huduma stahiki na haki zao za msingi kwa maendeleo ya sasa na ya baadaye ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, idadi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali chini ya Sheria ya NGO Na. 24 ya mwaka 2002 iliyorekebishwa mwaka 2005 imeendelea kukua mwaka hadi mwaka ambapo kufikia tarehe 17 Machi, 2014 idadi ya Mashirika hayo ilifikia 6,427 kutoka Mashirika 3,000 yaliyokadirwa kuwepo mwaka 2001 wakati Sera ya Taifa ya NGO ilipokuwa inaandaliwa sawa na ongezeko la asilimia 100.

Mashirika haya yanajishughulisha na kazi mbalimbali ikiwemo elimu, mazingira na mabadiliko ya tabianchi, afya maendeleo shirikishi, haki za binadamu, maendeleo ya jinsia, ushawishi na utetezi, kinga ya jamii, haki za watoto, kilimo, maji na ustawi wa jamii. Kuongezeka kwa idadi na shughuli za NGO's katika nchi yetu ni matokeo ya mazingira wezeshi yanayoendelea kuboreka mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina ya hali halisi ya sekta ya maendeleo ya jamii, mafanikio yaliyofikiwa na changamoto zilizopo yapo kwenye ukurasa wa 11 hadi 23 wa kitabu cha hotuba. Mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2013/2014 na malengo ya mwaka 2014/2015.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 Wizara yangu iliendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu yake kulingana na malengo yaliyopangwa. Katika Bajeti mwaka 2013/2014 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto iliidhinishiwa jumla ya shilingi 25,964,170,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi 5,397,496,000 zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi Mengineo na shilingi 8,656,200,000 kwa ajili ya malipo ya mshahara na shilingi 11,910,672,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2014 Wizara ilikuwa imetumia jumla ya shilingi 10,305,162,100 sawa na asilimia mia ya fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa na shilingi 2,923,620,590 sawa na asilimia mia ya fedha za Maendeleo zilizotolewa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2013/2014 na malengo ya mwaka 2014/2015 kwa kuzingatia maeneo yafuatayo. Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka 2013/2014 Wizara yangu ilidahili na kutoa mafunzo kwa wanachuo 2,869 kupitia vyuo 6 vya Maendeleo ya Jamii. Wanachuo 2,036 walidahiliwa katika ngazi ya cheti, 591 katika ngazi ya Stashahada, 234 ngazi ya Shahada na 8 katika ngazi ya Stashahada ya Udhamilii.

Aidha, Wizara yangu ilikarabati majengo na miundombinu katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Mlale, Misungwi na Mabugai. Katika mwaka 2014/2015 Wizara yangu itaendelea kukamilisha jengo la Maktaba ya Chuo cha Tengeru na Maabara ya Kompyuta katika Chuo cha Mabugai kwa lengo la kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 Wizara yangu ililipa shilingi 84,114,523 zikiwa ni gherama za ukarabati katika Vyuo Vya Maendeleo ya Wananchi vya Mputa na Muhukuru mkoani Ruvuma. Aidha, Wizara ilifanya ukarabati katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Tarime, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Mwanahala, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kilwa Masoko na Vyuo vya Msaginya, Mputa, Sofi na Singida.

Vile vile Chuo cha Masasi na Chilala na kuvipatia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 25 vifaa vya kujifunzia na kufundishia masomo ya Ufundis stadi. Katika mwaka wa 2014/2015 Wizara yangu itaendelea kudahili na kutoa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

mafunzo kwa wananchi na pia itakarabati majengo na miundombinu ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vya Mto wa Mbu, Msaginya na Nandembo.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuboresha mafunzo ya Maendeleo ya Wananchi kwa kutoa huduma kwa watoto kupitia Vituo vya Kulelea Watoto ndani ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ambapo jumla ya watoto 1033 walinufaika. Kuwepo kwa vituo hivyo katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kumeweza kumewezesha watumishi katika vyuo hivi na jamii inayovizunguka hususan wanawake kushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji mali kwa uhuru zaidi.

Kwa kipindi cha mwaka 2014/2015 Wizara itaendelea kuimarisha Vituo vya Kulelea Watoto katika vyuo 55 vya Maendeleo ya Wananchi kwa kutoa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Kutengeneza viwanja vya michezo na kuwajengea uwezo wakufunzi 30 kwa namna ya kuendesha Vituo vya Kulelea watoto wadogo na ujuzi wa kuwafundisha elimu ya awali.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Jinsia. Uwezeshaji wanawake kiuchumi ni suala muhimu katika kufikia usawa wa kijinsia na kupunguza umaskini wa kipato katika jamii. Katika mwaka 2013/2014 Wizara kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake iliziwezesha Halmashauri 39 kutoa mikopo yenye dhamani ya shilingi 428,000,000.

Katika kuhakikisha unafikia malengo yaliyopangwa Wizara ilifuatilia utendaji wa Mfuko katika mikoa 9 na kuiwezesha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kufuatilia utekelezaji wa Mfuko katika Halmashauri mbalimbali.

Halmashauri ambazo Kamati ya Bunge ilifanya ufuatiliaji huo ni Kinondoni, Ilala, Kibaha, Korogwe na Jiji la Tanga. Mikoa ambayo Wizara ilifuatilia shughuli za Mfuko ni Arusha, Manyara, Singida, Pwani, Tanga, Katavi, Rukwa, Morogoro na Kagera. Matokeo ya ufuatiliaji huo yameainishwa kwenye kitabu cha hotuba ukurasa 27.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015 Wizara yangu itaendelea kutoa fedha kwa Halmashauri nyingine zitakazokuwa zimemaliza marejesho pamoja na kufanya ufuatiliaji kwa mikoa na Halmashauri zilizobaki. Napenda kutumia fursa hii kuzikumbusha Halmashauri zote zilizokopeshwa kuzingatia mkataba wa marejesho. Aidha, nazikumbusha Halmashauri zote nchini kuchangia asilimia 5 ya mapato yao kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ili wanawake wengi zaidi wanufaika na huduma ya Mfuko huu. (Makofij)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kupitia Benki ya Wanawake Tanzania huduma za kibenki zimewafikia wananchi wengi zaidi wakiwepo wanawake kwani imeweza kufungua tawi la pili la Benki ya Wanawake Tanzania eneo la Kariakoo Mkao wa Dar es Salaam, Mtaa wa Agrey/Likoma.

Aidha, vituo 29 vya kutolea mikopo na mafunzo kwa wajasiriamali vimefunguliwa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza. Vituo hivyo ni kama ifuatavyo: Dar es Salaam (Tabata Kisukuru, Mbande, Sabasaba, Ubungo Kibangu, Chanika, Chamazi na Kunduchi Mtongani); Dodoma (Airport, Chamwino, Ipagala, Posta, Hazina Kikuyu, Kizota, Savanna Kikuyu, Chang'ombe, Mnadani, Veyula, Mpwapwa, Kongwa na Mbande) na Mwanza (Nyakato, Igogo, Nyegezi, Pansiansi, Igoma, Kissesa, Magu, Misungwi na Kitangiri). Kwa mwaka 2014/2015, Wizara yangu itaendelea kutoa ruzuku kwa Benki ya Wanawake Tanzania ili iweze kuwafikia wananchi wengi zaidi. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, ukatili wa kijinsia umeendelea kuwa ni tatizo katika jamii zetu ambapo wananchi wengi wameendelea kuumizwa na kuteseka na hata kuuawa kutokana na vitendo vya kikatili vinavyofanyika hapa nchini. Mwaka 2013/2014, Wizara ilifanya tathmini ya mafunzo yaliyotolewa kwa Kamati za Ulinzi na usalama katika Mkao wa Manyara kuhusiana na kupiga vita ukatili wa kijinsia. Moja ya matokeo ya tathmini hiyo imeonyesha kuwa Kamati husika zinahitaji kujengewa uwezo zaidi ili ziweze kufanya kazi zake kikamilifu.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kufanya tathmini ya mafunzo yaliyotolewa kwa Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya kuhusu mbinu za kutokomeza ukatili katika mikoa ya Mwanza, Shinyanga na Mara.

Aidha, itaendelea kuzijengea uwezo kamati za ulinzi na usalama ili ziweze kupambana na kutokomeza ukatili katika ngazi ya Wilaya na kuendelea kuiwezesha Kamati ya Kitaifa ya Kuzuia na Kuondoa Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto ili iweze kutekeleza shughuli zake kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, suala la uingizaji wa masuala ya kijinsia katika sera, mipango na Bajeti limekuwa likitiliwa mkazo ili kuhakikisha kuwa mipango na Bajeti za kila sekta, idara na taasisi mbalimbali inawanufaisha wote, yaani wanawake, wanaume, wavulana na wasichana.

Katika kipindi cha mwaka 2013/2014, Wizara kupitia wataalam wake ilifanya tathmini ya uingizaji wa masuala ya jinsia katika Halmashauri 6 ambazo ni Halmashauri ya Jiji la Tanga na Arusha, Halmashauri za Wilaya ya Iringa na Moshi pamoja na Manispaa ya Temeke na Morogoro. Lengo la tathmini ilikuwa ni kubaini mafanikio na changamoto zinazojitokeza katika uingizaji wa masuala ya jinsia katika sera na mipango na Bajeti mbalimbali.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya uingizaji wa masuala ya jinsia kwa wataalamu mbalimbali ili waweze kuelewa na kutekeleza mkakati huu ikiwa ni pamoja na kukamilisha Sera ya Taifa ya Jinsia.

Aidha, Wizara imeanza mchakato wa kuandaa taarifa ya hali ya jinsia nchini (*Tanzania Country Gender Profile*) na kuanzisha benki ya Takwimu ya usawa wa jinsia. Taarifa hii na Benki ya Takwimu zitawezesha kufanya maamuzi, upangaji wa mipango na upimaji utekelezaji wake ushawishi na uhamasishaji kuhusu masuala ya jinsia ili kuwa na maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilianda rasimu ya 7 na 8 ya nchi ya Mkataba wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake. Rasimu ya Taarifa hiyo imekamilika na inatarajiwa kujadiliwa na wadau wakiwemo Kamati ya Bunge ya Sekta ya Maendeleo ya Jamii kwa lengo la kupata maoni zaidi kwa ajili ya kuiboresha.

Mheshimiwa Spika, tarehe 8 Machi kila mwaka, Wizara imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali katika kuratibu Siku ya Wanawake Duniani. Katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu iliratibu maadhisho ya siku hiyo katika ngazi ya mikoa ambapo Kauli mbiu ilikuwa ni “Chochea Mabadiliko Kuleta Usawa wa Kijinsia” Kauli mbiu hii inasitiza na kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa kuzingatia masuala ya jinsia katika kupanga na kutekeleza mikakati na mipango ya maendeleo kwa kuzingatia ushiriki stahiki wa wanawake, wanaume, wavulana na wasichana katika kujiletea maendeleo yao na taifa kwa ujumla. Kwa mwaka 2014/2015, Wizara itaratibu maadhisho haya Kitaifa ili kuweza kupima mafanikio yaliyopatikana katika miaka mitano (2010 – 2015) katika juhudzi za kumwendeleza mwanamke pamoja na kubainisha changamoto zilizojitokeza kwa kipindi hicho toka maadhisho haya yalipofanyika kitaifa mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza mikataba na maazimio mbalimbali ambayo nchi imesaini na kurihia, mwaka 2013/2014, Wizara ilishiriki katika mkutano wa 58 wa Kamisheni ya Hali ya Wanawake na mkutano wa nchi za Maziwa Makuu kuhusu masuala ya jinsia. Lengo la mikutano hiyo ni kutafuta mbinu za pamoja za kukabiliana na changamoto mbalimbali, kubadilishana uzoefu na kukubaliana maeneo muhimu ya utekelezaji katika kuleta usawa wa kijinsia na maendeleo ya wanawake katika nchi husika.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kushiriki na kutoa mchango wake katika mikutano ya kikanda na kimataifa kuhusu utekelezaji wa masuala ya usawa wa kijinsia na kuwaendeleza wanawake.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Watoto: Maendeleo ya taifa lolote duniani hutegemea sana namna ambavyo linawalinda na kuwakuza watoto

Nakala ya Mtando (Online Document)

wake. Kwa kuzingatia hilo, Wizara yangu imekuwa ikichukua hatua mbalimbali katika kukabiliana na changamoto zinazowakabili watoto hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013/2014, Wizara yangu iliandaa mpango kazi wa jamii wa kudhibiti tatizo la watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani. Lengo likiwa ni kuongeza ushiriki wa wadau katika kudhibiti na kuondoa tatizo hilo kwa kuwaelimisha na kuhamasisha ili wabebe jukumu la kuwapatia watoto mahitaji na haki zao za msingi. Utekelezaji wa Mpango kazi unahusisha familia, jamii, Serikali, asasi za kiraia, vyombo vya habari na wabia wa maendeleo. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itasambaza mpango katika mikoa yote na kuratibu utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu imefanya marekebisho ya Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008 kuwa Sera ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2014 ili iweze kujumuisha masuala ya utoaji huduma fungamanishi na shirikishi za Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Mtoto.

Aidha, Sera hiyo imezingatia masuala ya kukabiliana na changamoto zinazotokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia pamoja na upatikanaji wa huduma za malezi na makuzi kwa watoto walio chini ya umri wa miaka nane. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itakamilisha Sera hiyo na mkakati wake wa utekelezaji. Aidha, Wizara itasambaza kwa wadau sera na mkakati huo kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, ukatili dhidi ya watoto ni moja ya changamoto zinazoathiri malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto. Katika kupunguza matukio ya ukatili huo, mwaka 2013/2014 Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliandaa Mpango Kazi Shirikishi wa Kuzuia Ukatili dhidi ya Watoto wa mwaka 2013 hadi 2016.

Aidha, Wizara yangu iliwezesha kufanyika kwa mukutano wa mwaka wa Kikosi Kazi cha Taifa cha Kuzuia Ukatili dhidi ya Mtoto ambapo sekta zote zinazohusiana na maendeleo ya mtoto zilitoa taarifa kuhusu mapendekezo ya namna ya kutekeleza mpango huo. (Makofii)

Pia, Wizara iliandaa mukutano uliowakutanisha watekelezaji wa Mpangokazi wa miaka mitatu wa kuzuia ukatili wa watoto na wadau wa maendeleo. Tayari wadau mbalimbali wa maendeleo wajitokeza kuchangia fedha za utekelezaji wa baadhi ya kazi zilizoainishwa katika mpango huu. Tunawashukuru sana wadau hawa. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia mpango huo kwa kushirikiana na kikosi kazi hicho.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu pia iliandaa kitini cha elimu ya malezi kwa familia kuhusu kukabiliana na ukatili dhidi ya watoto na kukisambaza kupitia mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii kutoka halmashauri za Hai, Temeke, Magu na Kasulu. Kitini hiki mkitatumiwa na wawezeshaji jamii katika kuwajengea uwezo wazazi na walezi ili kudhibiti ukatili dhidi ya watoto. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuratibu usambazaji wa kitini hicho katika halmashauri nyingine.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Wizara iliendelea kuratibu utoaji wa taarifa za ukatili dhidi ya watoto kupitia namba ya simu 116 inayosimamiwa na Shirika Lisilo la Kiserikali la C-SEMA. Hadi kufikia mwaka 2014 jumla ya simu 6,188 zilipigwa kupitia namba hiyo na kufanyiwa kazi. Mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia mtandao huo na kuendelea kutathmini ili kuwezesha kupeleka huduma hii katika maeneo mengine ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Watoto wanayo haki ya msingi ya kushiriki na kushirikishwa katika masuala yote yanayowahusu. Katika kuhakikisha ushiriki wa watoto katika kutoa maoni yao, mwaka 2013/2014, wizara iliandaa Mkutano Mkuu wa Baraza la Watoto ili kupitia Rasimu ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, wizara yangu iliratibu utekelezaji wa shughuli za mabaraza ya watoto katika ngazi ya Wilaya/Mikoa pamoja na Azimio la Bunjumbura kuhusu haki na ustawi wa watoto. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri kuimarisha Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na mabaraza ya watoto ya mikoa na wilaya ili yaweze kutoa fursa nzuri za ushiriki wa watoto katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu iliratibu maadhisho ya siku ya mtoto wa Afrika ambayo yaliadhimishwa katika ngazi ya mkoa.

Katika maadhisho hayo, kila mkoa ulipata fursa ya kuadhimisha siku hii muhimu kulingana na mazingira na uhitaji wa mkoa husika. Kauli mbiu ya mwaka 2013/2014 ilikuwa ni “Kuondoa Mila zenye kuleta Madhara kwa Watoto: ni Jukumu Letu Sote”. Lengo la kaulimbiu hii ni kuhamasisha jamii kubaini baadhi ya mila ambazo zimekuwa zikileta madhara kwa watoto na kuweka mikakati ya kuzitokomeza.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliratibu maadhisho ya siku ya Familia Duniani ambayo yalifanyika kimkoa. Kauli mbiu ya maadhisho haya ilikuwa ni “Imarisha na Endeleva Ushirikiano na Mshikamano wa Familia na Makundi Mbalimbali ya Jamii”. Kauli mbiu hii inasisitiza wazazi, walezi na jamii kuwajibika kwa pamoja katika malezi ya familia. Katika mwaka 2014/2015, Wizara

Nakala ya Mtandao (Online Document)

itaendelea kuratibu maadhimisho ya siku hizo kwa lengo la kuhamasisha jamii kuhusu haki na ustawi wa mtoto na maendeleo ya familia.

Mheshimiwa Spika, Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali: Katika kipindi cha mwaka 2013/2014, Serikali iliendelea kusajili Mashirika Yasiyo ya Kiserikali chini ya Sheria ya NGOs Na. 24 ya mwaka 2002. Jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 435 yalipatiwa usajili katika ngazi ya wilaya, mkoa, taifa na kimataifa.

Hii imefanya idadi ya NGOs kuongezeka kutoka mashirika 5,992 mwezi Julai, 2013 na kufikia Mashirika 6,427 mwezi Machi, 2014 ikiwa ni ongezeko la asilimia 7. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2014/2015, Wizara yangu itaendelea na usajili wa mashirika hayo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu pia iliratibu shughuli za NGOs kwa kuwezesha ushiriki wa wadau katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Hii ni pamoja na kuiwezesha Bodi ya uratibu wa NGOs kukagua shughuli za NGOs 21 na kufanya vikao vitatu katika mikoa ya Tanga, Lindi na Mbeya. Vikao hivyo vilifika maamuzi mbalimbali ikiwemo utatuzi wa migogoro katika Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Aidha, Wizara kupitia Bodi ya Uratibu wa NGOs ilikutana na wadau 175 na kujadili mafanikio na changamoto zinazokabili NGOs katika mikoa husika na kutoa elimu kuhusa Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001 na Sheria ya NGOs Na. 24 ya mwaka 2002.

Wizara pia imeanzisha utaratibu wa kukutana na NGOs zinazofanya kazi za watoto na wanawake na mapendekazo ya kuboresha ushirikiano yameandalowiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kujenga mazingira wezeshi na kuboresha uratibu wa mashirika haya, Wizara itatekeleza mambo mbalimbali katika kipindi cha mwaka 2014/2015. Kazi hizo ni pamoja na kufuatilia na kutathmini mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na hali ya uendeshaji wa mashirika hayo hapa nchini. Aidha, itawezesha kufanyika kwa tathmini kuhusu ufanisi wa Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kujenga mazingira wezeshi kwa NGOs.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Vilevile, Serikali kuitia Wizara yangu itawezesha kufanyika kwa mafunzo ya ndani kuhusu usajili, ufuatiliaji na tathmini ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii wa wilaya na mikoa kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kiutendaji ili kuboresha utoaji wa huduma za usajili na uratibu katika ngazi husika.

Mheshimiwa Spika, Uratibu wa Sera na Mipango: Katika mwaka 2013/14 uratibu na mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008 pamoja na mkakati wake ulifanyika. Katika mwaka 2014/2015, uratibu wa mapitio ya Sera ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001 na tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000 na Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo Ya Kiserikali ya mwaka 2001 utafanyika.

Aidha, uratibu wa mipango na bajeti ya mwaka 2015/2016 pamoja na uandaaji wa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa Wizara utaandaliwa ili kuimarisha ukusanyaji, uhifadhi na usimamizi wa takwimu na taarifa za sekta ya maendeleo ya jamii. Katika kuwapatia motisha wafanyakazi, Wizara yangu kwa mwaka 2013/14, ilipandisha vyeo watumishi 126 na kuwabadilisha kada watumishi wanne. Aidha, watumishi 86 walithibitishwa kazini. Kwa kipindi cha mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuwapandisha vyeo watumishi wake kwa mujibu wa Miundo ya Utumishi wa Kada zao na Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ili kuongeza tija katika utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekuwa ikitabili na upungufu mkubwa wa watumishi hasa katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Katika kukabili na changamoto hii mwaka 2013/2014, Wizara yangu iliajiri jumla ya watumishi 92 kutokana na kibali cha ajira kilichotolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Katika mwaka 2014/2015, Wizara inatarajia kuendelea kuajiri watumishi wengine ili kuendelea kupunguza pengo liliopo.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi, mwaka 2013/2014, Wizara iliwapatia watumishi vitendea kazi mbalimbali.

Kwa mwaka 2014/2015, Wizara yangu itajenga eneo la kuegesha magari la Makao Makuu ya Wizara, kununua jenereta na kuendelea kuwapatia wafanyakazi vitendea kazi mbalimbali.

SPIKA: Waheshimiwa, naomba mpunguze sauti, tuko katika kikao.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Aidha, Wizara itawawezesha watumishi kushiriki katika mashindano ya SHIMIWI ili kuboresha afya na kuimarisha mahusiano mionganoni mwa watumishi wa Serikali.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI na Virusi Vya UKIMWI mahala pa kazi. Katika mwaka 2013/2014, Wizara iliwapatia watumishi nasaha za namna ya kujikinga na maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuhamasisha watumishi wajitokeze kupima afya zao pamoja na kuwapatia huduma ya viini lishe na chakula.

Mheshimiwa Spika, mawasiliano kwa umma mawasiliano: Kwa mwaka 2013/2014, Wizara yangu iliandaa vipindi vya luninga, radio na mikutano na waandishi wa habari kwa ajili ya kuelimisha umma kuhusu masuala ya maendeleo ya jamii, jinsia, wanawake, familia, haki za watoto na uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Aidha, Wizara iliandaa matangazo mbalimbali kupitia magazeti, vipeperushi na mabango.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2013/2014, Wizara pia ilianzisha mawasiliano na umma kupitia mitandao ya kijamii. Mitandao hiyo ni pamoja na Blog ya wizara, facebook ya Wizara na twitter ya Wizara. Kwa mwaka 2014/2015, Wizara itaandaa mkakati wa mawasiliano na kuendelea kuwezesha mawasiliano kwa umma kupitia njia mbalimbali ikiwemo mitandao ya kijamii, radio, luninga, magazeti, gari la sinema, majarida, vipeperushi na uhamasishaji jamii kwa kushirikiana na Maafisa Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya Kata, Wilaya na Mkoa.

Mheshimiwa Spika, hitimisho: Mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Wizara wa mwaka 2013/14 na Malengo ya mwaka 2014/2015 yanaonesha jinsi Wizara yangu ilivyo na umuhimu katika kuleta usawa wa jinsia, upatikanaji wa haki na ustawi wa watoto, ongezeko la ajira kwa vijana na ushawishi wa jamii katika kupokea na kutekeleza miradi ya maendeleo endelevu. Ili Wizara itekeleze vema majukumu yake inahitaji ushirikiano mkubwa wa wadau mbalimbali na rasilimali fedha za kutosha.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kumshukuru sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana, kwa ushirikiano, ushauri na usaidizi mkubwa anaonipa katika kuongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, vilevile ninapenda kutoa shukrani za dhati kwa Katibu Mkuu Bibi Tayari Maembe, Naibu Katibu Mkuu Bibi Nuru H. Milao, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Wanawake Tanzania, Bibi Magreth Chacha, Wakuu wa Vyuo na wafanyakazi wote wa Wizara yangu wa ngazi zote, kwa jitihada zao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ambayo

Nakala ya Mtandao (Online Document)

ni pamoja na kuniwezesha mimi kuwasilisha Hotuba hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Kabla sijamaliza hotuba yangu sina budi kuwashukuru wadau wote tunaofanya nao kazi na wengine ambao kwa namna moja au nyingine tunashirikiana nao, peke yetu kama Wizara tusingefikia mafanikio niliyoyataja ninaomba kupitia Bunge lako Tukufu kutoa shukrani zangu za dhati kwa wafuatao:-

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Asasi ya Wanawake na Maendeleo (WAMA), Mfuko wa fursa sawa kwa wote (EOTF), Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA), Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Shirikisho la Vyama Vya Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (FAWETA), Medical Women Association of Tanzania (MEWATA), White Ribbon, Plan International Tanzania, Serve the Children, Mashirika mbalimbali yasiyo ya Kiserikali pamoja na wale wanaofanya kazi kwa maslahi ya jamii kwa namna moja au nyingine.

Ninapenda pia kuyashukuru Mashirika kutoka nchi rafikia ambayo yameendelea kutusaidia katika kufanya kazi na sisi. Mashirika hayo ni pamoja BFID, GPE, SIDA CANADA, KOIKA na UK EDUCATION.

Aidha, ninayashukuru Mashirika ya Umoja wa Mataifa ambayo ni UNICEF, UNDP, UNFPA na UN WOMEN kwa misaada yao mbalimbali iliyofanikisha utekelezaji wa majukumu mengi ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya mwaka 2014/2015 ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa mwaka 2014/2015, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe matumizi ya shilingi bilioni thelathini milioni mia mbili thelathini na tatu laki nne na sabini na nne elfu, (Sh. 30,233,474,000/=).

Kati ya maombi hayo shilingi bilioni ishirini na moja, milioni mia mbili na kumi na tano, laki tisa na thelathini elfu (Sh. 21,215,930,000/=) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Shilingi bilioni kumi na mbili, milioni mia nane kumi na nane laki nne na thelathini na nne elfu (Sh. 12,818,434,000/=) ni kwa ajili ya mishahara.

Shilingi bilioni nane, milioni mia tatu tisini na saba laki nne na tisini na sita elfu (Sh. 8,397,496,000/=) ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Shilingi bilioni tisa, milioni kumi na saba, laki tano na arobaini na nne elfu (Sh. 9,017,544,000/=) ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo, ambapo shilingi bilioni saba (Sh. 7,000,000,000/=) ni fedha za ndani na shilingi bilioni mbili,

Nakala ya Mtando (Online Document)

milioni kumi na saba, laki tano na arobaini na nne elfu (Sh. 2,017,544,000/=) ni fedha za nje. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. (Makofi)

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

HOTUBA YA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

HOTUBA YA WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO MHESHIMIWA SOPHIA M. SIMBA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2014/2015

A: UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba bunge lako tukufu baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, sasa lijadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka 2014/5015.

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu mwangi wa rehema kwa kutujalia kuwa na afya njema na hivyo kuweza kushiriki mkutano huu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

3. Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Mohammed Gharib Bilal, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu na Mbunge wa Mpanda Mashariki kwa uongozi wao mahiri ambao umewezesha kushamiri kwa usawa wa jinsia na uzingatiaji wa haki za mtoto katika jamii ya watanzania. Mwenyezi Mungu awajalie afya njema ili waendelee kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

4. Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa uendeshaji bora wa shughuli za Bunge.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Tunaendelea kumuomba Mwenyezi Mungu awajalie afya njema ili muweze kusimamia na kuratibu shughuli za Bunge kwa ufanisi.

5. Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ikiongozwa na Mwenyekiti wake mahiri Mheshimiwa Saidi Mohamed Mtanda (Mb.) na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Kapteni Mstaafu John Damiano Komba (Mb.) kwa kuichambua na kujadili bajeti ya Wizara yangu. Ushauri na maelekezo ya Kamati hiyo yametuwezesha kuboresha na kukamilisha bajeti katika muda muafaka.

6. Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Samuel Sitta (Mb.) kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge Maalum la Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Samiya Suluhu Hassan (Mb.) kuwa Makamu Mwenyekiti.

Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa (Mb.) kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Kalenga na Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete kuwa Mbunge wa Chalinze.

7. Mheshimiwa Spika, naomba nitangulize dua zangu kwa Mwenyezi Mungu azipokee na kuzilaza mahali pema peponi roho za Marehemu William Agustino Mgimwa aliyekuwa Mbunge wa Kalenga na marehemu Said Bwanamdogo aliyekuwa Mbunge wa Chalinze. Bunge hili litawakumbuka daima kwa michango yao.

8. Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa natumia fursa hii kuwapa pole wale wote waliopatwa na majanga pamoja na kufiwa na ndugu, jamaa na wapendwa wao katika matukio mbalimbali yaliyotokea nchini.

B: MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM YA MWAKA 2010 KWA KIPINDI CHA JANUARI, 2011 HADI MACHI, 2014

9. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2013/2014, Wizara yangu iliendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2010. Mafanikio ya utekelezaji wa Ilani kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2011 hadi Machi, 2014 ni haya yafuatayo.

I. Ajira na Uwezeshaji wa Wananchi.

10. Mheshimiwa Spika, Ibara ya 78 ya Ilani ya CCM, imeelekeza uimarishaji na upanuzi wa mafunzo ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili viweze kupokea vijana wengi zaidi na kuwapatia mafunzo ya stadi na maarifa ya kisasa katika fani za kilimo, biashara, ufundi na ujasiriamali.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

11. Mheshimiwa Spika, Mafunzo ya kuwapatia wananchi ujuzi na stadi mbalimbali ili waweze kujiajiri na kuongeza uzalishaji mali na kipato ni muhimu hasa katika kipindi hiki cha ukosefu mkubwa wa ajira. Wizara kupitia Vyuo 55 vya Maendeleo ya Wananchi, iliwapatia mafunzo wananchi 146,383 wakiwemo wanawake 70,841 na wanaume 75,542 kupitia kozi fupi, kozi ndefu na mafunzo nje ya vyuo kwa kipindi cha Januari, 2011 hadi Machi, 2014 (Jedwali Na. 1). Mafunzo yanayotolewa ni pamoja na: uashi, useremala, ufundu magari, ufundu chuma na uchomeleaji, kompyuta, ushonaji, umeme wa majumbani, kilimo, ususi na upishi. Aidha, Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya ufundu stadi yanayoratibiwa na Mamlaka ya Ufundu Stadi (VETA) kupitia vyuo 25 vya Maendeleo ya Wananchi ambapo kumekuwa na ongezeko la wanafunzi wanaopata mafunzo haya kutoka 1,125 mwaka 2013 hadi kufikia 2,722 mwaka 2014 (Jedwali Na. 2). Kuyaendeleza Makundi Mbalimbali Watoto.

12. Mheshimiwa Spika, Ilani ya CCM ya mwaka 2010 Ibara ya 204 (a), (h) na (j) inaiagiza Serikali kukamilisha Sera ya Malezi na Makuzi ya Mtoto na kupitisha Sera Fungamanishi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto ili watoto wote nchini waweze kunufaika kutokana na utekelezaji wake. Aidha, Ibara hiyo inaitaka Serikali kutekeleza mikataba ya haki za mtoto iliyoridhiwa na Bunge.

13. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azma hiyo, Wizara yangu imeendelea kufanya mapitio ya Sera ya Mtoto na kutekeleza mikataba ya kimataifa kuhusu haki na maendeleo ya mtoto iliyoridhiwa na Bunge lako tukufu. Wizara imefanya marekebisho ya Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008 na imeandaa rasimu ya Sera ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Mtoto (2014) ili iweze kubeba masuala ya utoaji huduma fungamanishi na shirikishi kwa mtoto. Masuala mengine yaliyoingizwa katika sera hiyo ni pamoja na kuboresha upatikanaji wa huduma muhimu kwa watoto walio chini ya umri wa miaka nane.

Aidha, katika kuwezesha utekelezaji wa mikataba ya kimataifa inayohusu haki na maendeleo ya mtoto, Wizara yangu inaandaa taarifa ya utekelezaji wa mikataba hiyo ili kuiwasilisha katika vikao vya tatu, nne na tano vya Mkataba wa Kimataifa kuhusu Haki za Mtoto (Convention on the Rights of the Child) katika mwaka 2014. Aidha, Wizara yangu imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitatu (2013 – 2016). Wanawake.

14. Mheshimiwa Spika, Ilani ya CCM ya mwaka 2010 Ibara ya 205 (e) na (f) inaitaka Serikali kuimarisha mifuko iliyopo ya mikopo na Benki ya Wanawake Tanzania ili wanawake wengi waweze kufaidika kiuchumi.

15. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azma hii ya Ilani, Wizara kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake ilizipatia halmashauri 62 mikopo yenye jumla ya shilingi milioni 612 kwa ajili ya kuwakopesha wanawake katika

Nakala ya Mtandao (Online Document)

maeneo yao ili kuwaendeleza kiuchumi. Halmshauri zilizopatiwa mikopo kupitia Mfuko huu katika kipindi cha kuanzia mwaka 2010/2011 hadi 2013/2014 ni kama inavyoonekana kwenye kiambatisho (Jedwali Na. 3).

16. Mheshimiwa Spika, Serikali pia iliendelea kuiwezesha Benki ya Wanawake Tanzania ili kuwafikia wananchi wengi zaidi hususan wanawake. Katika kipindi cha Januari 2011 hadi Machi, 2014 Benki ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi 24,392,382,000 kwa wananchi 11,754 Kati ya hao wanawake ni asilimia 88 (Jedwali Na. 4 (i) na 4 (ii)). III. Elimu ya Juu.

17. Mheshimiwa Spika, Ilani ya CCM ya mwaka 2010 Ibara ya 85 (e) imeelekeza Serikali kuongeza udahili kwa wanafunzi katika vyuo vya elimu ya juu. Wizara kupitia Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru iliendelea kudahili wanafunzi katika ngazi ya shahada ya kwanza katika fani za Upangaji na Usimamizi Shirikishi wa Miradi, Maendeleo ya Jamii, Maendeleo ya Jinsia na Stashahada ya Uzamili ya Maendeleo ya Jamii. Jumla ya wanachuo 546 wakiwemo wanawake 324 na wanaume 222 walidahiliwa kati ya Septemba, 2011 hadi Septemba, 2013 (Jedwali Na. 5 (i)).

18. Mheshimiwa Spika, pamoja na kutoa mafunzo ya elimu ya juu, Wizara iliendelea kutoa mafunzo ya taaluma ya maendeleo ya jamii kupitia vyuo vinane vinavyotoa mafunzo katika ngazi ya Astashahada na Stashahada. Vyuo hivyo ni Buhare, Missungwi, Rungemba, Uyole, Ruaha, Mlale, Mabughai na Monduli. Jumla ya wanachuo 11,368 wakiwemo wanawake 7,463 na wanaume 3,905 walidahiliwa katika vyuo hivi kwa kipindi cha Septemba, 2011 hadi Septemba, 2013 (Jedwali Na. 5 (ii)).

Kati ya idadi hiyo, ngazi ya Stashahada ni 2,445 na Astashahada ni wanachuo 8,923. Wahitimu katika fani hizi huajiriwa katika ngazi ya halmashauri na huwezesha jamii kutekeleza majukumu yao ya maendeleo kwa kutumia mbinu shirikishi na kuzingatia usawa wa kijinsia na haki za mtoto hivyo kuifanya jamii kuwa na maendeleo endelevu. IV. Demokrasia na Madaraka ya Umma.

19. Mheshimiwa Spika, Ibara ya 188 (a) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, inaitaka Serikali kuhakikisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanajishughulisha na majukumu yaliyoandikishwa kutekeleza na kwamba hayapati nafasi ya kujidesha kinyume na malengo yao. Kwa kuzingatia agizo hili la Ilani, Wizara yangu imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Moja ya hatua hizo ni pamoja na kutoa elimu kwa wadau 11,674 kati ya Januari, 2011 na Machi, 2014 kuhusu Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Sheria ya NGOs Na.24 ya mwaka 2002 iliyorekebishwa mwaka 2005.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

20. Mheshimiwa Spika, elimu hiyo ilitolewa kuititia Ofisi ya Msajili wa NGOs na mikutano ya wadau iliyofanyika katika mikoa ya Morogoro, Mtwara, Njombe, Mwanza, Ruvuma, Lindi, Mbeya na Tanga. Jumla ya Wadau 560 walipata elimu hii ikiwa ni pamoja na Maafisa Maendeleo ya Jamii wa mikoa na wilaya 24, wawakilishi kutoka katika Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 536 na wananchi mbalimbali. Lengo la kufanya hivyo ni kuziwezesha NGOs kufahamu wajibu wao na kujiendesha kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi.

Aidha, kwa upande wa Maafisa Maendeleo ya Jamii wa ngazi ya wilaya na mikoa elimu hiyo imelenga kuwajengea uwezo wa kufuatilia shughuli za NGOs katika maeneo yao na kutoa taarifa kwa Wizara pindi wanapobaini mashirika hayo kujiendesha kinyume na masharti ya usajili wao.

21. Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ambazo Wizara yangu imechukua katika kutekeleza agizo hili la Ilani ni pamoja na kuwateua Maafisa Maendeleo ya Jamii kuwa wasajili wasaidizi na waratibu wa mashirika haya katika ngazi za wilaya na mkoa ili kufuatilia shughuli za mashirika hayo katika ngazi husika. Aidha, Wizara imekuwa ikifuatilia na kutathmini utendaji na uendeshaji wa NGOs nchini ambapo kwa kipindi cha Januari, 2011 na Machi, 2014, NGOs 55 zilitembelewa na kukaguliwa katika maeneo yao ya utekelezaji.

Aidha, taarifa za mwaka za fedha na kazi zilizowasilishwa kutoka kwa mashirika 1,000 zilifanyiwa uchambuzi. Kutokana na ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za NGOs, shirika moja lilibainika kujiendesha kinyume cha taratibu na kufutiwa usajili wake.

Aidha, ilibainika kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali mengi yameendelea kutoa mchango mkubwa katika huduma za kijamii na masuala ya kisera.

22. Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyofikiwa katika utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2010, Wizara yangu ilikabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo ni pamoja na:-

(i) Uhaba wa wakufunzi wa kada mbalimbali katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi;

(ii) Upungufu wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia katika Vyuo tisa vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo 55 vya Maendeleo ya Wananchi;

(iii) Mahitaji ya mikopo ya Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake ni mengi ikilinganishwa na fedha zinazotolewa. Aidha, mikopo inayotolewa kwa vikundi ni midogo isiyokidhi mahitaji halisi ya biashara na mafunzo ya ujasiri amali yanayotolewa kwa wakopaji kutotosheleza kuwajengea uwezo unaohitajika;

(iv) Kutokuwepo kwa uwazi na uwajibikaji kwa baadhi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

C: HALI HALISI YA SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII NA CHANGAMOTO ZILIZOPO

23. Mheshimiwa Spika, Sekta ya maendeleo ya jamii hapa nchini imeendelea kukua na kutambulika na wadau mbalimbali kutoanka na mchango wake katika maendeleo ya taifa letu. Naomba kuchukua fursa hii kueleza kwa kifupi hali halisi ya sekta hii katika maeneo ya ushiriki wa wananchi katika maendeleo ya kiuchumi, maendeleo ya jinsia, maendeleo ya watoto na ushiriki wa mashirika yasiyo ya kiserikali katika maendeleo nchini Tanzania.

Hali ya Ushiriki wa Wananchi katika Maendeleo.

24. Mheshimiwa Spika, maendeleo ya jamii kama dhana ni hatua mbalimbali zinazowawezesha watu kutambua uwezo walio nao wa kubaini matatizo yao na kutumia fursa na rasilimali zilizopo ili kuondokana na ujinga, maradhi, njaa na umaskini kwa ujumla na hivyo kujiletea maisha bora.

Msisitizo wa dhana hii ni ushiriki wa watu katika kuamua, kupanga na kutekeleza mambo yote yanayohusiana na maisha yao na nchi yao. Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii ni mhimili muhimu kwa jamii katika kutekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo kwani ndiyo wenye jukumu la kushauri, kushawishi, kuelimisha, kuhamasisha na kuraghabisha wananchi kujiletea maendeleo kwa kutumia mbinu shirkishi katika programu mbalimbali wanazoibua na kubuni. Hivyo, wataalamu hao ni muhimu katika kuiwezesha jamii kuleta mabadiliko chanya kwa kushiriki katika masuala mbalimbali ya maendeleo.

25. Mheshimiwa Spika, Wataalamu wa maendeleo ya jamii hufanya kazi katika ngazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na wizara, wakala na mamlaka za Serikali, Sekretariat za mikoa, halmashauri za miji, wilaya, manispaa na majiji, miji, kata na vijiji. Wataalamu hao pia hufanya kazi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na taasisi mbalimbali za sekta binafsi.

Mfano, katika ngazi za halmashauri takwimu zinaonesha kuwa kuna wataalamu wa maendeleo ya jamii 2,675 ambapo 1,381 hufanya kazi katika makao makuu ya halmashauri na 1,294 hufanya kazi katika Kata.

Aidha, katika ngazi ya Sekretariat za mikoa kuna jumla ya wataalamu 21. Wataalamu hawa hutoa mchango mkubwa sana wa kuwaandaa wananchi kupokea na kutekeleza programu mbalimbali za huduma kama za afya, elimu, maji, nishati na miradi mingine ya kiuchumi na kijamii.

26. Mheshimiwa Spika, Sera ya Maendeleo ya Jamii ya mwaka 1996 inasisitiza kuwepo kwa mtaalamu mmoja kwa kila Kata hivyo mahitaji halisi ya wataalamu hao kwa ngazi husika ni 3,339.

Kwa takwimu hizo upungufu wa wataalamu kwenye kata ni 2,045 sawa na asilimia 61 ya mahitaji (Jedwali 6).

Aidha, katika ngazi ya Sekretariati za mkoa upungufu wa wataalamu hao ni asilimia 16. Hali hii inaathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa shughuli za Sekta ya Maendeleo ya Jamii. Katika kukabiliana na changamoto hii, Wizara yangu imeendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu –TAMISEMI kuhakikisha halmashauri zote zinaajiri wataalamu wa maendeleo ya jamii katika ngazi ya Kata.

27. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kutoa mafunzo na kuzalisha wataalamu wa Maendeleo ya Jamii kupitia vyuo tisa vya maendeleo ya jamii nchini. Katika kipindi cha mwaka 2011/2012 hadi mwaka 2013/2014 jumla ya wanachuo 11,914 walidahiliwa katika vyuo hivyo. Idadi hii kubwa ni matokeo ya utekelezaji wa mipango mbalimbali ya kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia ikiwemo ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu ya vyuo hivyo.

28. Mheshimiwa Spika, wananchi wameendelea kunufaika na mafunzo yanayotolewa na Vyuo 55 vya Maendeleo ya Wananchi vilivyo chini ya Wizara yangu. Idadi ya wananchi wanaodailiwa katika vyuo hivyo imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Mfano, kati ya mwaka 2010/2011 na mwaka 2013/2014 idadi ya wananchi waliodahiliwa kwa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi iliongezeka kutoka 32,133 hadi kufikia 40,692.

Aidha, baadhi ya wananchi walipata maarifa na ujuzi kupitia mafunzo nje ya chuo (*outreach courses*). Mafunzo hayo yanawawezesha washiriki kujajiri na kuajiriwa katika taasisi mbalimbali. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Vyuo hivi kwa miaka ya hivi karibuni vimeanza kupokea vijana wengi waliohitimu mafunzo ya sekondari sambamba na wale wa elimu ya msingi. Hali ya Maendeleo ya Jinsia

29. Mheshimiwa Spika, hali ya usawa wa kijinsia katika nyanja mbalimbali hapa nchini imeendelea kuimarika. Ukweli huu unadhihirishwa na ushahidi wa kitakwimu na taarifa zilizopo katika maeneo ya ushiriki wa wanawake katika siasa na ngazi za maamuzi; uwezeshaji wa wanawake kiuchumi; elimu, mafunzo na ajira; kuongezeka kwa wanawake wajasiriamali (wadogo na wakati) na upatikanaji wa haki za wanawake kisheria.

Nakala ya Mtando (Online Document)

30. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ushiriki wa wanawake katika ngazi za siasa na maamuzi, idadi ya mawaziri wanawake imeongezeka kutoka asilimia 15 mwaka 2005 hadi asilimia 30 mwaka 2013, wakuu wa mikoa wanawake kutoka asilimia 10 mwaka 2005 hadi asilimia 24 mwaka 2013. Majaji wanawake pia wameongezeka kutoka asilimia 33 hadi 61 kwa kipindi hicho na uwakilishi wa wanawake Bungeni umeongezeka kutoka asilimia 30.3 mwaka 2005 na kufikia asilimia 36 ya wabunge wote mwaka 2013.

31. Mheshimiwa Spika, katika uvezeshaji wanawake kiuchumi taasisi za fedha na mifuko mbalimbali vimeendelea kutoa mikopo ya fedha na mafunzo ya ujasiriamali kwa wanawake. Baadhi ya taasisi na mifuko hiyo ni pamoja na Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake, Benki ya Wanawake Tanzania, Women Covenant Bank, VICOBA na SACCOS. Mfano, Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake umetoa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 705 kwa kipindi cha kati ya mwaka 2011/2012 na mwaka 2013/2014.

32. Mheshimiwa Spika, Mila na desturi kandamizi bado ni changamoto katika kuhakikisha kuwa kunakuwepo na usawa wa kijinsia kwa kuzingatia haki na usawa wa binadamu. Mila zinazoleta madhara kwa wanawake na hasa watoto wa kike kama kukeketwa na kuozesha wasichana wa kike katika umri mdogo zimeendelea na bado ni changamoto katika maeneo kadhaa ya nchi yetu.

Wizara inachukua hatua mbalimbali kupambana na changamoto hizi ambazo ni pamoja na kutoa elimu kwa kushirikiana na wadau hasa NGOs na washirika wa maendeleo na kuiwezesha Kamati ya Kitaifa ya Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Maendeleo ya Watoto. Watoto ni sehemu muhimu ya jamii na ndiyo tegemeo ya Taifa lolote. Watoto wanahitaji kukua na kuwa raia wema, hivyo wanatakiwa kupewa haki na mahitaji yao ya msingi ikiwa ni pamoja na: Kuishi, kupewa malezi stahiki, kulindwa, kuendelezwa kiakili kwa kutambua na kukuza vipaji vyao, kutobaguliwa na kushirikishwa.

34. Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya Taifa ya Idadi ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, idadi ya watoto chini ya miaka 18 Tanzania Bara ni 21,866,258 sawa na asilimia 50.1 ya idadi ya watu wote. Kati yao wasichana ni 10,943,846 na wavulana ni 10,922,412.

35. Mheshimiwa Spika, Pamoja na Serikali kuweka mazingira wezeshi ya kuwapatia watoto haki zao kupitia sera, sheria, mipango, programu na mikakati mbalimbali, bado maendeleo ya mtoto yanakabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na: ukatili dhidi ya watoto, kuwepo

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, kushuka kwa maadili, ndoa na mimba za utotonii.

36. Mheshimiwa Spika, Kumekuwepo na jitihada mbalimbali za kukabiliana na changamoto hizo ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa Kituo cha Huduma za Pamoja (*One Stop Centre*) kwa majaribio katika Hospitali ya Amana - Manispaa ya Ilala kwa ajili ya kuhudumia watoto mbalimbali wanaofanyiwa aina mbalimbali za ukatili na kutoa elimu kwa wazazi na walezi juu ya wajibu wao katika malezi ya watoto.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau imewezesha kuanzishwa kwa mtandao wa mawasiliano wa kusaidia watoto (*Child Helpline*) namba 116 kwa ajili ya jamii inayotumika kutoa taarifa za ukatili dhidi ya watoto na ukiukwaji wa haki za watoto. Namba hii imeanza kufanya kazi katika maeneo machache kwa majaribio na utekelezaji wa kazi zake unaonesha mafanikio mazuri hadi sasa.

Hali ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

37. Mheshimiwa Spika, idadi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali chini ya Sheria ya NGOs Na. 24 ya mwaka 2002 iliyorekebishwa mwaka 2005 imeendelea kukua mwaka hadi mwaka. Kufikia tarehe 17 Machi, 2014 idadi ya mashirika haya ilifikia 6,427 kutoka mashirika 3,000 yaliyokadirwa kuwepo mwaka 2001 wakati Sera ya Taifa ya NGOs ilipokuwa inaandaliwa (Jedwali Na.7). Hili ni ongezeko la zaidi ya asilimia 100. Kati ya mashirika yaliyosajiliwa, 254 ni ya kimataifa na 6,173 ni ya ndani ya nchi yanayofanya kazi katika ngazi za wilaya, mkoa na taifa.

38. Mheshimiwa Spika, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yameendelea kutambulika kama wadau na wabia muhimu katika maendeleo. Mashirika haya yanajishughulisha na kazi mbalimbali ikiwemo elimu, mazingira na mabadiliko ya tabianchi, afya, maendeleo shirkishi, haki za binadamu, maendeleo ya jinsia, ushawishi na utetezi, kinga ya jamii, haki za watoto, kilimo, maji na ustawi wa jamii.

39. Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa idadi na shughuli za NGOs katika nchi yetu ni matokeo ya mazingira wezeshi yanayoendelea kuboreka mwaka hadi mwaka. Hii ni pamoja na uwepo wa Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001, Sheria ya NGOs Na.24 ya mwaka 2002 iliyorekebishwa mwaka 2005 na Kanuni za Maadili za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali za mwaka 2008.

Aidha, muundo wa kitaasisi unaowezesha NGOs kujitawala kwa uhuru na kujiratibu umeendelea kuwepo ikiwemo: Bodi ya Uratibu wa NGOs, Baraza la Taifa la NGOs, Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya na mikoa ambao ni Wasajili Wasaidizi na mitandao ya NGOs ya wilaya, mkoa na taifa.

40. Mheshimiwa Spika, pamoja na kuimarika kwa hali ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hapa nchini, bado kuna changamoto zinazohitaji kufanyiwa kazi. Changamoto zilizopo ni pamoja na sehemu kubwa ya shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutegemea wafadhili kutoka nje na kutokuwa na vyanzo vya uhakika vya ndani ya nchi hivyo kuathiri uendelevu wa shughuli hizo pindi wafadhili hao wanapositisha misaada. Changamoto nyiningine ni kutokuwepo kwa Kamati za Maadili ya NGOs katika baadhi ya mikoa na wilaya kunakoathiri uwezo wa NGOs kujitawala katika kuongeza uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali na uendeshaji wa mashirika hayo.

41. Mheshimiwa Spika, katika kutatua changamoto hizo wizara yangu imechukua hatua mbalimbali. Mojawapo ya hatua hizo ni kuhimiza Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutumia fursa ya marekebisho ya Sheria ya NGOs yaliyofanyika mwaka 2005 kuanzisha na kuendeleza miradi ya kuzalisha faida kwa ajili ya kutekeleza malengo yao hata pale wafadhili wanapositisha misaada.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la NGOs inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuliwezesha kuanzisha Kamati za Maadili ya NGOs katika ngazi ya wilaya na mikoa ikiwa ni utekelezaji wa Kanuni za Maadili ya NGOs. Mafanikio.

42. Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2013/2014, ni pamoja na:-

(i) Idadi ya vituo vya kutolea mikopo kwa wajasiriamali wadogo hususan wanawake imeongezeka toka vituo 21 mwaka 2012/13 hadi vituo 50 mwaka 2013/14, sawa na ongezeko la asilimia 58;

(ii) Matawi ya Benki ya Wanawake Tanzania yameongezeka toka tawi moja mwaka 2009/10 hadi matawi mawili mwaka 2013/14;

(iii) Kuongezeka kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yaliyosajiliwa toka mashirika 3,000 mwaka 2001/02 hadi mashirika 6,427 mwaka 2013/2014;

(iv) Wanafunzi waliojiunga na mafunzo ya ufundi stadi katika Vyuo 25 vya Maendeleo ya Wananchi wameongezeka toka wanafunzi 1,125 mwaka 2013 hadi wanafunzi 2,722 mwaka 2014;

(v) Wanafunzi waliojiunga na mafunzo ya elimu ya wananchi (Kozi ndefu) katika Vyuo 55 vya Maendeleo ya Wananchi wameongezeka toka wanafunzi 6,586 mwaka 2013 hadi wanafunzi 7,144 mwaka 2014;

(vi) Kuongezeka kwa Halmashauri zilizopata mikopo kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake toka Halmashauri 19 mwaka 2008/09 hadi Halmashauri 38 mwaka 2013/2014; na

(vii) Kuongezeka kwa Madawati ya Jinsia na Watoto toka madawati 9 mwaka 2008 hadi madawati 417 mwaka 2014. Changamoto.

43. Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Sekta ya Maendeleo ya Jamii inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Uhaba wa wakufunzi wa kada mbalimbali katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi;

(ii) Ukoefu wa vyombo vya usafiri katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na uchakavu wa vyombo vya usafiri Makao Makuu ya Wizara;

(iii) Upungufu wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia katika Vyuo tisa vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo 55 vya Maendeleo ya Wananchi;

(iv) Uchakavu wa majengo na miundombinu katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi;

(v) Kuendelea kukua kwa madeni ya watumishi, wakandarasi na watoa huduma mbalimbali Wizarani. Madeni yamefikia shilingi 2,558,735,065 katika deni hilo shilingi 774,308,379.84 ni madeni ya watumishi, shilingi 773,166,431.80 ni madeni ya wazabuni na shilingi 1,011,260,253.36 ni madeni ya wakandarasi;

(vi) Fedha kutolewa na Wizara ya Fedha bila kuzingatia Mpango Kazi na Mtiririko wa Mahitaji ya Fedha;

(vii) Mahitaji ya mikopo ya Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake ni mengi ikilinganishwa na fedha zinazotolewa.

Aidha, mikopo inayotolewa kwa vikundi kuwa kidogo isiyokidhi mahitaji halisi ya biashara na mafunzo ya ujasiriamali yanayotolewa kwa wakopajji kutotosheleza kuwajenjea uwezo unaohitajika;

(viii) Kupanua huduma za Benki ya Wanawake Tanzania ili kuwafikia wanawake wengi zaidi; na

Nakala ya Mtandao (Online Document)

- (ix) Kutokuwepo kwa uwazi na uwajibikaji kwa baadhi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.
- (x) Kuongezeka kwa matukio ya ukatili wa kijinsia katika jamii.

D: MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MWAKA 2013/14 NA MALENGO YA MWAKA 2014/2015

44. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/14, Wizara yangu iliendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu yake kulingana na malengo yaliyopangwa. Katika bajeti ya mwaka 2013/2014, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto iliidhinishiwa jumla ya shilingi 25,964,170,000 kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida, shilingi 5,397,496,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 8,656,002,000 kwa ajili ya malipo ya mishahara na shilingi 11,910,672,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

45. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2014, Wizara ilikuwa imetumia jumla ya shilingi 10,305,162,100 sawa na asilimia 100 ya fedha za Matumizi ya Kawaida zilizopokelewa na shilingi 2,923,620,590 sawa na asilimia 100 ya fedha za Maendeleo zilizotolewa.

46. Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha utekelezaji wa mpango wa mwaka 2013/14 na malengo ya mwaka 2014/15 kwa kuzingatia maeneo yafuatayo:-

Maendeleo ya Jamii.

47. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2013/2014 Wizara yangu ilidahili na kutoa mafunzo kwa wanachuo 2,869 kupitia vyuo tisa vya Maendeleo ya Jamii vya Tengeru, Buhare, Rungemba, Monduli, Missungwi, Ruaha, Uyole, Mlale na Mabughai. Wanachuo 2,036 walidailiwa katika ngazi ya cheti, 591 katika ngazi ya stashahada, 234 ngazi ya shahada na 8 katika ngazi ya Stashahada ya Uzamili. Aidha, Wizara yangu ilikarabati majengo na miundombinu katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Mlale, Misungwi na Mabughai.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu itaendelea kukamilisha jengo la maktaba ya Chuo cha Tengeru na maabara ya kompyuta katika chuo cha Mabughai kwa lengo la kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

48. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2013/14 Wizara yangu ililipa shilingi 84,114,523 zikiwa ni gherama za ujenzi zilizoongezeka katika ujenzi wa bwalo, jiko na nyumba za watumishi katika vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vya Mputa na Muhukuru mkoani Ruvuma.

Aidha, Wizara ilifanya ukarabati wa mabweni na jengo la utawala katika chuo cha Maendeleo ya Wananchi Tarime; ukarabati wa nyumba za watumishi na uwekaji wa mfumo wa umeme katika chuo cha Maendeleo ya Wananchi Mwanhala; ukarabati wa jengo la utawala na bweni katika chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kilwa Masoko; ukarabati wa mabweni na nyumba za watumishi katika chuo cha Maendeleo ya Wananchi Msaginya, Mputa, Sofi na Singida; ujenzi wa vyoo katika chuo cha Maendeleo ya Wananchi Masasi na Chilala; na kuvipatia vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 25 vifaa vya kujifunzia na kufundishia masomo ya ufundi stadi.

49. Katika mwaka 2014/2015 Wizara yangu itaendelea kudahili na kutoa mafunzo kwa wananchi na pia itakarabati majengo na miundombinu ya vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vya Mto wa Mbu, Msaginya na Nandembo.

50. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuboresha mafunzo ya maendeleo ya wananchi kwa kutoa huduma kwa watoto kupitia vituo vya kulelea watoto ndani ya vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 55 ambapo jumla ya watoto 1,033 walinufaika. Kuwepo kwa vituo hivi katika vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kumewawezesha watumishi katika vyuo hivi na jamii inayovizunguka vyuo hususan wanawake kushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji mali kwa uhuru zaidi. Aidha, vituo hivi vimewawezesha washiriki wanawake 97 wenye watoto wadogo kupata mafunzo wakiwa na watoto wao vyuoni.

51. Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka 2014/15, Wizara itaendelea kuimarisha vituo vya kulelea watoto katika vyuo 55 vya maendeleo ya wananchi kwa kutoa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kutengeneza viwanja vya michezo. Aidha, Wizara itawajengea uwezo wakufunzi 30 kwa ajili ya kuwawezesha kupata elimu ya kuendesha vituo vya kulelea watoto wadogo ikiwa ni pamoja na kuwapatia ujuzi wa kufundisha watoto hao elimu ya awali. Mafunzo ya kuwajengea uwezo wakufunzi katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi yatakuwa yanatolewa kwa awamu kulingana na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu. Maendeleo ya Jinsia.

52. Mheshimiwa Spika, uwezeshaji wanawake kiuchumi ni suala muhimu katika kufikia usawa wa kijinsia na kupunguza umaskini wa kipato katika jamii. Katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake iliziwezesha Halmashauri 39 kutoa mikopo yenye thamani ya shillingi milioni 428. Katika kuhakikisha Mfuko unafikia malengo yaliyopangwa, Wizara ilifuatilia utendaji wa Mfuko katika mikoa tisa na kuiwezesha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kufuatilia utekelezaji wa Mfuko katika Halmashauri mbalimbali.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Halmashauri ambazo Kamati ya Bunge ilifanya ufuatiliaji huo ni Kinondoni, Ilala, Kibaha, Korogwe na Jiji la Tanga. Mikoa ambayo Wizara ilifuatilia shughuli za Mfuko ni Arusha, Manyara, Singida, Pwani, Tanga, Katavi, Rukwa, Morogoro na Kagera. Matokeo ya ufuatiliaji yanaonesha kwamba Halmashauri nyingi hazichangii asilimia tano ya mapato yao kama inavyotakiwa. Kutokana na matokeo hayo, Halmashauri ziliagizwa kuchangia katika Mfuko huo.

53. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu itaendelea kutoa fedha kwa Halmashauri nyingine zitakazokuwa zimemaliza marejesho pamoja na kufanya ufuatiliaji kwa mikoa na halmashauri zilizobaki. Napenda kutumia fursa hii kuzikumbusha halmashauri zote zilizokopeshwa kuzingatia mkataba wa marejesho.

Aidha, nazikumbusha halmashauri zote nchini kuchangia asilimia tano ya mapato yao kwenye Mfuko wa Maendeleo wa wanawake ili wanawake wengi zaidi wanufaike na huduma za Mfuko huu.

54. Mheshimiwa Spika, kuitia Benki ya Wanawake Tanzania huduma za kibenki zimewafikia wananchi wengi zaidi wakiwepo wanawake kwani imeweza kufungua tawi la pili la Benki ya Wanawake Tanzania eneo la Kariakoo Mkao wa Dar es Salaam, Mtaa wa Agrey/Likoma.

Aidha, vituo 29 vya kutolea mikopo na mafunzo kwa wajasiriamali vimefunguliwa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza. Vituo hivyo ni kama ifuatavyo: Dar es Salaam (Tabata Kisukuru, Mbande, Sabasaba, Ubungo Kibangu, Chanika, Chamazi na Kunduchi Mtongani); Dodoma (Airport, Chamwino, Ipagala, Posta, Hazina Kikuyu, Kizota, Savanna Kikuyu, Chang'ombe, Mnadani, Veyula, Mpwapwa, Kongwa na Mbande); na Mwanza (Nyakato, Igogo, Nyegezi, Pansiansi, Igoma, Kisesa, Magu, Misungwi na Kitangiri). Kwa mwaka 2014/2015, Wizara yangu itaendelea kutoa ruzuku kwa Benki ya Wanawake Tanzania ili iweze kuwafikia wananchi wengi zaidi.

55. Mheshimiwa Spika, Ukatili wa kijinsia umeendelea kuwa ni tatizo katika jamii zetu ambapo wananchi wengi wameendelea kuumizwa na kuteseka na hata kuuawa kutokana na vitendo vya kikatili vinavyofanyika hapa nchini.

Mwaka 2013/2014, Wizara ilifanya tathmini ya mafunzo yaliyotolewa kwa Kamati za Ulinzi na usalama katika Mkao wa Manyara kuhusiana na kupiga vita ukatili wa kijinsia. Moja ya matokeo ya tathmini hiyo imeonyesha kuwa Kamati husika zinahitaji kujengewa uwezo zaidi ili ziweze kufanya kazi zake kikamilifu. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kufanya tathmini ya mafunzo

Nakala ya Mtandao (Online Document)

yaliyotolewa kwa Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya kuhusu mbinu za kutokomeza ukatili katika mikoa ya Mwanza, Shinyanga na Mara.

Aidha, itaendelea kuzijengea uwezo kamati za ulinzi na usalama ili ziweze kupambana na kutokomeza ukatili katika ngazi ya wilaya na kuendelea kuiwezesha Kamati ya Kitaifa ya Kuzuia na Kuondoa Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto ili iweze kutekeleza shughuli zake kikamilifu.

56. Mheshimiwa Spika, suala la uingizaji wa masuala ya kijinsia katika sera, mipango na bajeti limekuwa likitiliwa mkazo ili kuhakikisha kuwa mipango na bajeti za kila sekta, idara na taasisi mbalimbali inawanufaisha wote, yaani wanawake, wanaume, wavulana na wasichana.

Katika kipindi cha mwaka 2013/2014, Wizara kuitia wataalamu wake ilifanya tathmini ya uingizaji wa masuala ya jinsia katika Halmashauri 6 ambazo ni Halmashauri ya Jiji la Tanga na Arusha, Halmashauri za Wilaya ya Iringa na Moshi pamoja na Manispaa ya Temeke na Morogoro.

Lengo la tathmini ilikuwa ni kubaini mafanikio na changamoto zinazojitokeza katika uingizaji wa masuala ya jinsia katika sera na mipango na bajeti mbalimbali. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya uingizaji wa masuala ya jinsia kwa wataalamu mbalimbali ili waweze kuelewa na kutekeleza mkakati huu ikiwa ni pamoja na kukamilisha Sera ya Taifa ya Jinsia.

Aidha, Wizara imeanza mchakato wa kuandaa taarifa ya hali ya jinsia nchini (Tanzania Country Gender Profile) na kuanzisha benki ya Takwimu ya usawa wa jinsia. Taarifa hii na Benki ya Takwimu zitawezesha kufanya maamuzi, upangaji wa mipango, ushawishi na uhamasishaji kuhusu masuala ya jinsia ili kuwa na maendeleo endelevu. Aidha, zitasaidia kupima utekelezaji wa mipango na programu mbalimbali kuona kama zinaweza kupunguza changamoto za kijinsia na kuleta usawa unaotarajiwa.

57. Mheshimiwa Spika, mwaka 2013/2014, Wizara ilianda rasimu ya 7 na 8 ya nchi ya Mkataba wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake. Maandalizi ya taarifa hiyo yaliwashirikisha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Watendaji wa Madawati ya Jinsia kutoka Wizara mbalimbali, asasi za kijamii na Maafisa wa Maendeleo Jamii. Rasimu ya Taarifa hiyo imekamilika na inatarajiwa kujadiliwa na wadau mbalimbali wakiwemo Kamati ya Bunge ya Sekta ya Maendeleo ya Jamii kwa lengo la kupata maoni zaidi kwa ajili ya kuiboresha.

58. Mheshimiwa Spika, tarehe 8 Machi kila mwaka, Wizara imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali kuratibu maadhisho ya Siku ya Wanawake Duniani. Kwa mwaka 2013/2014, maadhisho ya Siku ya Wanawake Duniani yalifanyika kimkoa ambapo lengo kuu lilikuwa ni kuwakutanisha wanawake wa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

ngazi zote ili waweze kubadilishana uzoefu wa masuala mbalimbali yanayowakabili, kubaini fursa zilizopo katika kujiletea maendeleo na kutafuta ufumbuzi wa changamoto mbalimbali zinazowakabili. Katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu iliratibu maadhisho ya siku hiyo katika ngazi ya mikoa ambapo Kauli mbiu ilikuwa ni "Chochea Mabadiliko Kuleta Usawa wa Kijinsia" Kauli mbiu hii inasitisiza na kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa kuzingatia masuala ya jinsia katika kupanga na kutekeleza mikakati na mipango ya maendeleo kwa kuzingatia ushiriki stahiki wa wanawake, wanaume, wavulana na wasichana katika kujiletea maendeleo yao na taifa kwa ujumla. Kwa mwaka 2014/2015, Wizara itaratibu maadhisho haya Kitaifa ili kuweza kupima mafanikio yaliyopatikana katika miaka mitano (2010 – 2015) katika juhudzi za kumwendeleza mwanamke pamoja na kubainisha changamoto zilizojitokeza kwa kipindi hicho toka maadhisho haya yalipofanyika kitaifa mwaka 2010.

59. Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza mikataba na maazimio mbalimbali ambayo nchi imesaini na kuridhia, mwaka 2013/2014, Wizara ilishiriki katika mkutano wa 58 wa Kamisheni ya Hali ya Wanawake na mkutano wa nchi za Maziwa Makuu kuhusu masuala ya jinsia. Lengo la mikutano hiyo ni kutafuta mbinu za pamoja za kukabiliana na changamoto mbalimbali, kubadilishana uzoefu na kukubaliana maeneo muhimu ya utekelezaji katika kuleta usawa wa kijinsia na maendeleo ya wanawake katika nchi husika. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kushiriki na kutoa mchango wake katika mikutano ya kikanda na kimataifa kuhusu utekelezaji wa masuala ya usawa wa kijinsia na kuwaendeleza wanawake. Maendeleo ya Watoto.

60. Mheshimiwa Spika, maendeleo ya taifa lolote duniani hutegemea sana namna ambavyo linawalinda na kuwakuza watoto wake. Kwa kuzingatia hilo, Wizara yangu imekuwa ikichukua hatua mbalimbali katika kukabiliana na changamoto zinazowakabili watoto hapa nchini.

61. Mheshimiwa Spika, mwaka 2013/2014, Wizara yangu iliandaa mpango kazi wa jamii wa kudhibiti tatizo la watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani. Lengo likiwa ni kuongeza ushiriki wa wadau katika kudhibiti na kuondoa tatizo hilo kwa kuwaelimisha na kuhamasisha ili wabebe jukumu la kuwapatia watoto mahitaji na haki zao za msingi. Utekelezaji wa Mpango kazi unahusisha familia, jamii, serikali, asasi za kiraia, vyombo vya habari na wabia wa maendeleo. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itasambaza mpango katika mikoa yote na kuratibu utekelezaji wake.

62. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu imefanya marekebisho ya Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008 kuwa Sera ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2014 ili iweze kujumuisha masuala ya utoaji huduma fungamanishi na shirikishi za Malezi, Makuzi na

Nakala ya Mtando (Online Document)

Maendeleo ya Mtoto. Aidha, Sera hiyo imezingatia masuala ya kukabiliana na changamoto zinazotokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia pamoja na upatikanaji wa huduma za malezi na makuzi kwa watoto walio chini ya umri wa miaka nane. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itakamilisha Sera hiyo na mkakati wake wa utekelezaji. Aidha, Wizara itasambaza kwa wadau sera na mkakati huo kwa ajili ya utekelezaji.

63. Mheshimiwa Spika, ukatili dhidi ya watoto ni moja ya changamoto zinazoathiri malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto. Katika kupunguza matukio ya ukatili huo, mwaka 2013/2014 Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilianda Mpango Kazi Shirikishi wa Kuzuia Ukatili dhidi ya Watoto wa mwaka 2013 hadi 2016.

Aidha, Wizara yangu iliwezesha kufanyika kwa mukutano wa mwaka wa Kikosi Kazi cha Taifa cha Kuzuia Ukatili dhidi ya Mtoto ambapo sekta zote zinazohusiana na maendeleo ya mtoto zilitoa taarifa kuhusu mapendekezo ya namna ya kutekeleza mpango huo.

Pia, Wizara ilianda mukutano uliowakutanisha watekelezaji wa Mpangokazi wa miaka mitatu wa kuzuia ukatili wa watoto na wadau wa maendeleo na tayari wadau kadhaa wa maendeleo wajitokeza na kuanza kuchangia fedha za utekelezaji wa baadhi ya kazi zilizoainishwa katika mpango huu. Tunawashukuru sana wadau hawa. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia mpango huo kwa kushirikiana na kikosi kazi hicho.

64. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu pia ilianda kitini cha elimu ya malezi kwa familia kuhusu kukabiliana na ukatili dhidi ya watoto. Kitini hicho kitatumiwa na wawezeshaji jamii katika kuwajengea uwezo wazazi na walezi ili kudhibiti ukatili dhidi ya watoto. Aidha, kuanzia ngazi ngazi ya familia Wizara ilitoa mafunzo kuhusu Kitini hicho kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii kutoka halmashauri za Hai, Temeke, Magu na Kasulu. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuratibu usambazaji wa kitini hicho katika halmashauri nyingine.

65. Mheshimiwa Spika, vilevile, Wizara iliendelea kuratibu utoaji wa taarifa za ukatili dhidi ya watoto kupitia namba ya simu 116 inayosimamiwa na Shirika Lisilo la Kiserikali la C-SEMA. Hadi kufikia Machi, 2014 jumla ya simu 6,188 zilipigwa kupitia namba hiyo na kufanyiwa kazi. Mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia mtando huo na kuendelea kutathmini ili kuwezesha kupeleka huduma hii katika maeneo mengine ya nchi.

66. Mheshimiwa Spika, Watoto wanayo haki ya msingi ya kushiriki na kushirikishwa katika masuala yote yanayowahusu. Katika kuhakikisha ushiriki wa watoto katika kutoa maoni yao, mwaka 2013/2014, wizara ilianda Mkutano

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mkuu wa Baraza la Watoto ili kuitia rasimu ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, wizara yangu iliratibu utekelezaji wa shughuli za mabaraza ya watoto katika ngazi ya Wilaya/Mikoa pamoja na Azimio la Bunjumbura kuhusu haki na ustawi wa watoto. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri kuimarisha Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na mabaraza ya watoto ya mikoa na wilaya ili yaweze kutoa fursa nzuri za ushiriki wa watoto katika maeneo husika.

67. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu iliratibu maadhimisho ya siku ya mtoto wa Afrika ambayo yaliadhimishwa katika ngazi ya mkoa. Katika maadhimisho hayo, kila mkoa ulipata fursa ya kuadhimisha siku hii muhimu kulingana na mazingira na uhitaji wa mkoa husika. Kauli mbiu ya mwaka 2013/2014 ilikuwa ni "Kuondoa Mila zenye kuleta Madhara kwa Watoto: ni Jukumu Letu Sote". Lengo la kaulimbiu hiyo ni kuhamasisha jamii kubaini baadhi ya mila ambazo zimekuwa zikileta madhara kwa watoto na kuweka mikakati ya kuzitokomeza.

68. Mheshimiwa Spika, Vile vile, Wizara yangu iliratibu maadhimisho ya siku ya Familia Duniani ambayo yalifanyika kimkoa. Kauli mbiu ya maadhimisho haya ilikuwa ni "Imarisha na Endeleva Ushirikiano na Mshikamano wa Familia na Makundi Mbalimbali ya Jamii". Kauli mbiu hii inasitiza wazazi, walezi na jamii kuwajibika kwa pamoja katika malezi ya familia. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuratibu maadhimisho ya siku hizo kwa lengo la kuhamasisha jamii kuhusu haki na ustawi wa mtoto na maendeleo ya familia.

Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

69. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha mwaka 2013/2014, Serikali iliendelea kusajili Mashirika Yasiyo ya Kiserikali chini ya Sheria ya NGOs Na.24 ya mwaka 2002. Jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 435 yalipatiwa usajili katika ngazi ya wilaya, mkoa, taifa na kimataifa. Kati ya hayo, mashirika ya kimataifa ni 23 na mashirika ya ndani ya nchi yaani ya ngazi za wilaya, mkoa na taifa ni 412. Hii imefanya idadi ya NGOs kuongezeka kutoka mashirika 5,992 mwezi Julai, 2013 na kufikia mashirika 6,427 mwezi Machi, 2014 ikiwa ni ongezeko la asilimia 7.

Aidha, katika kipindi cha mwaka 2014/2015, Wizara yangu itaendelea na usajili wa mashirika hayo.

70. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu pia iliratibu shughuli za NGOs kwa kuwezesha ushiriki wa wadau katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Hii ni pamoja na kuiwezesha Bodi ya uratibu wa NGOs kukagua shughuli za NGOs 21 na kufanya vikao vitatu katika mikoa ya Tanga,

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Lindi na Mbeya. Vikao hivyo vilifikia maamuzi mbalimbali ikiwemo utatuzi wa migogoro katika Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Aidha, Wizara kuititia Bodi ya Uratibu wa NGOs ilikutana na wadau 175 na kujadili mafanikio na changamoto zinazozikabili NGOs katika mikoa husika na kutoa elimu kuhusa Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001 na Sheria ya NGOs Na. 24 ya mwaka 2002. Wizara pia imeanzisha utaratibu wa kukutana na NGOs zinazofanyakazi za watoto na wanawake na mapendekezo ya kuboresha ushirikiano yameandaliwa. Kwa mwaka 2014/2015, Wizara yangu itaendelea kuiwezesha Bodi ya Uratibu wa NGOs kufanya vikao vinne na kukutana na wadau ili kuboresha uratibu wa NGOs nchini na pia itaendelea na utaratibu wa kukutana na NGOs zinazofanyakazi na watoto na wanawake ili kuboresha ushirikiano na utekelezaji wa majukumu haya.

71. Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kujenga mazingira wezeshi na kuboresha uratibu wa mashirika haya, Wizara yangu itatekeleza mambo mbalimbali katika kipindi cha mwaka 2014/2015. Kazi hizo ni pamoja na kufuatilia na kutathmini mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na hali ya uendeshaji wa mashirika hayo hapa nchini.

Aidha, itawezesha kufanya kwa tathmini kuhusu ufanisi wa Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kujenga mazingira wezeshi kwa NGOs. Vilevile, Serikali kuititia Wizara yangu itawezesha kufanya kwa mafunzo ya ndani kuhusu usajili, ufuatiliaji na tathmini ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii wa wilaya na mikoa kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kiutendaji ili kuboresha utoaji wa huduma za usajili na uratibu katika ngazi husika. Uratibu wa Sera na Mipango

72. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 uratibu na mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008 pamoja na mkakati wake ulifanyika. Katika mwaka 2014/2015, uratibu wa mapitio ya Sera ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001 na tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000 na Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo Ya Kiserikali ya mwaka 2001 utafanyika.

Aidha, uratibu wa mipango na bajeti ya mwaka 2015/16 pamoja na uandaaji wa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa Wizara utaandaliwa ili kuimarisha ukusanyaji, uhifadhi na usimamizi wa takwimu na taarifa za sekta ya maendeleo ya jamii. Watumishi 20 wa Wizara watajengewa uwezo wa ukusanyaji takwimu, ufuatiliaji na tathmini. Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu

73. Mheshimiwa Spika, watumishi ni rasimali muhimu yenye kutekeleza majukumu ya kila siku ya Wizara. Kutokana na umuhimu wake inahitaji kusimamiwa vizuri, kujengewa uwezo wa kiutendaji na mazingira mazuri ya kazi

Nakala ya Mtando (Online Document)

ili kuongeza ufanisi na tija. Katika mwaka 2013/2014, Wizara iliwezesha watumishi 62 kupata mafunzo ya muda mrefu na mfupi, ndani na nje ya nchi ili kuwaongezea ujuzi na utaalamu katika utekelezaji wa majukumu yao. Katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu itaendelea kuwawezesha watumishi 84 kupata mafunzo mbalimbali ya muda mfupi na mrefu ndani ya nchi.

74. Mheshimiwa Spika, katika kuwapatia motisha wafanyakazi, Wizara yangu kwa mwaka 2013/2014, ilipandisha vyeo watumishi 126 na kuwabadilisha kada watumishi wanne. Aidha, watumishi 86 walithibitishwa kazini. Kwa kipindi cha mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuwapandisha vyeo watumishi wake kwa mujibu wa Miundo ya Utumishi wa Kada zao na Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ili kuongeza tija katika utendaji kazi.

75. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekuwa ikikabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi hasa katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Katika kukabiliana na changamoto hii mwaka 2013/2014, Wizara yangu iliajiri jumla ya watumishi 92 kutokana na kibali cha ajira kilichotolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma chenye Kumbukumbu Namba BC.62/97/014/2011 cha tarehe 4 Juni, 2012. Kwa mwaka 2013/14 Wizara iliwasilisha maombi ya kibali cha ajira ya watumishi 603. Katika mwaka 2014/2015, Wizara inatarajia kuendelea kuajiri watumishi wengine ili kuendelea kupunguza pengo lililopo.

76. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi, mwaka 2013/2014, Wizara iliwapatia watumishi vitendea kazi mbalimbali. Kwa mwaka 2014/2015, Wizara yangu itajenga eneo la kuegesha magari la Makao Makuu ya Wizara, kununua jenereta na kuendelea kuwapatia wafanyakazi vitendea kazi mbalimbali. Aidha, Wizara itawawezesha watumishi kushiriki katika mashindano ya SHIMIWI ili kuboresha afya na kuimarisha mahusiano mionganoni mwa watumishi wa Serikali.

77. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/14, Wizara yangu iliendelea kuwezesha sekta binafsi za ulinzi na usafi kutoa huduma hizo kwa Wizara kwa lengo la kuboresha mazingira ya utendaji kazi na usalama wa vifaa na mali. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuwezesha sekta binafsi kutoa huduma hizo.

78. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI na Virusi Vya UKIMWI mahala pa kazi. Katika mwaka 2013/2014, Wizara iliwapatia watumishi nasaha za namna ya kujikinga na maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuhamasisha watumishi wajitokeze kupima afya zao pamoja na kuwapatia huduma ya viini lishe na chakula. Mawasiliano kwa umma.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

79. Mheshimiwa Spika, mawasiliano ni nguzo muhimu katika kuwawezesha wananchi kufahamu huduma zinazotolewa na Wizara na pia kuiwezesha kupata mrejesho kutoka kwa wadau ili kuboresha huduma hizo. Kwa mwaka 2013/2014, Wizara yangu iliandaa vipindi vya luninga, radio na mikutano na waandishi wa habari kwa ajili ya kuelimisha umma kuhusu masuala ya maendeleo ya jamii, jinsia, wanawake, familia, haki za watoto na uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Aidha, Wizara iliandaa matangazo mbalimbali kupitia magazeti, vipeperushi na mabango.

80. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2013/2014, Wizara pia ilianzisha mawasiliano na umma kupitia mitandao ya kijamii. Mitandao hiyo ni pamoja na:

Blog ya wizara, www.maendeleoyajamijiinsianawatoto.blogspot.com; Facebook ya wizara, facebook.com/maendeleoyajamii; na twitter ya wizara, Twitter.com/wmjjwtz.

Kwa mwaka 2014/2015, Wizara itaandaa mkakati wa mawasiliano na kuendelea kuwezesha mawasiliano kwa umma kupitia njia mbalimbali ikiwemo mitandao ya kijamii, radio, luninga, magazeti, gari la cinema, majarida, vipeperushi na uhamasishaji jamii kwa kushirikiana na Maafisa Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya kata, wilaya na mkoa.

E: HITIMISHO

81. Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Wizara wa mwaka 2013/2014 na Malengo ya mwaka 2014/2015 yanaonesha jinsi Wizara yangu ilivyo na umuhimu katika kuleta usawa wa jinsia, upatikanaji wa haki na ustawi wa watoto, ongezeko la ajira kwa vijana na ushawishi wa jamii katika kupokea na kutekeleza miradi ya maendeleo endelevu. Ili Wizara itekeleze vema majukumu yake inahitaji ushirikiano mkubwa wa wadau mbalimbali na rasilimali fedha za kutosha.

F: SHUKRANI

82. Mheshimiwa Spika, napenda sasa kumshukuru sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Dk. Pindi Hazara Chana (Mb.), kwa ushirikiano, ushauri na usaidizi mkubwa anaonipa katika kuongoza Wizara hii. Vilevile, napenda kutoa shukrani za dhati kwa: Katibu Mkuu, Bibi Anna Tayari Maembe, Naibu Katibu Mkuu, Bibi Nuru H. M. Millao; Wakurugenzi; Wakuu wa Vitengo; Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Wanawake Tanzania - Bibi Magreth Chacha; Wakuu wa Vyuo; na Wafanyakazi wote wa Wizara yangu wa ngazi zote, kwa jitihada zao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara, ambayo ni pamoja na kuniwezesha mimi kuwasilisha hotuba hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

83. Mheshimiwa Spika, kabla sijamaliza hotuba yangu, sina budi kuwashukuru wadau wote tunaofanya nao kazi na wengine ambao kwa namna moja au nyingine tunashirikiana. Peke yetu kama Wizara tusingefikia mafanikio niliyoyataja. Naomba kupitia Bunge lako tukufu, kutoa shukrani zangu za dhati kwa wafuatao: Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (*NHIF*), Asasi ya Wanawake na Maendeleo (*WAMA*); Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (*EOTF*); Mtandao wa Jinsia Tanzania (*TGNP*); Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (*TAWLA*); Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (*TAMWA*); Shirikisho la Vyama vyta Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (*FAWETA*); Medical Women Association of Tanzania (*MEWATA*); White Ribbon; Plan International; Save the Children; Mashirika mbalimbali yasiyo ya Kiserikali pamoja na wale wanaofanya kazi kwa maslahi ya jamii kwa namna moja au nyingine.

Napenda pia kuyashukuru Mashirika kutoka nchi rafiki ambayo yameendelea kutusaidia na kufanya kazi na sisi. Mashirika hayo ni pamoja na: DFID; GPE; CIDA; KOICA na UK Education.

Aidha, nayashukuru Mashirika ya Umoja wa Mataifa ambayo ni: UNICEF; UNDP; UNFPA na UN WOMEN kwa misaada yao mbalimbali iliyofanikisha utekelezaji wa majukumu mengi ya Wizara yangu.

G. MAKADIRIO YA BAJETI YA WIZARA MWAKA 2014/2015.

84. Mheshimiwa Spika, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa mwaka 2014/15, sasa naliomba Bunge lako tukufu liidhinishe matumizi ya shilingi 30,233,474,000. Kati ya maombi haya:-

- (a) Shilingi 21,215,930,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida;
- (b) Shilingi 12,818,434,000 ni kwa ajili ya mishahara;
- (c) Shilingi 8,397,496,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo;
- (d) Shilingi 9,017,544,000 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo shilingi 7,000,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 2,017,544,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

MHE. MARY P. CHATANDA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO): Kwanza kabisa ninaomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kuweza kuwasilisha Taarifa hii hapa, na ni mara yangu ya kwanza kuweza kusimama hapa.

Kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jmii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) na Kanuni ya 117(11) za Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Aprili, 2013, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, ili niwasilishe Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 Pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, na kuliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii na kujadili.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza wajibu wake Kamati ilikutana na watendaji wa Wizara walio chini ya Fungu 53 tarehe 1 Mei, 2014 na tarehe 2 Mei, 2014 Jijini Dar es salaam na kupokea taarifa kuhusu utekelezaji wa majukumu wa Wizara, malengo yaliyopangwa kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2013/2014 pamoja na kujadili Bajeti iliyohusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015. Aidha, Kamati ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Maagizo ya Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya utelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2013/2014. Katika Mwaka wa Fedha 2013/2014, Wizara ilipangiwa Bajeti ya shilingi 25,964,470,000/= kati ya fedha hizo shilingi 8,656,002,000/= inajumuisha mishahara na shilingi 5,397,496,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Shilingi 11,910,672,000/= kwa ajili ya Miradi mbalimbali ya Maendeleo ambapo shilingi 6,500,000,000/= ni fedha za ndani na shilingi 5,410,672,000/= ni fedha za nje.

Hadi kufikia Machi, 2014 Wizara ilikuwa imepokea shilingi 1,964,133,299/= sawa na asilimia 36 ya Bajeti ya matumizi mengineyo. Aidha, katika fedha za Miradi ya Maendeleo Wizara ilikuwa imepokea shilingi 2,923,620,590/= sawa na asilimia 25 ya Bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge ambapo 2,706,106,502/= ni fedha za ndani na shilingi 217,514,088/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kutopatikana kwa fedha hizo Kamati inaitaka Serikali ikamilishe utoaji wa fedha hizi kwa kipindi kilichosalia ili Wizara iweze kutekeleza majukumu iliyojipangia kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014. Katika Mwaka wa Fedha unaoisha Juni 30, 2014, Kamati

Nakala ya Mtando (Online Document)

ilitoa maoni na ushauri kwenye maeneo mbalimbali, hasa kwenye maeneo yanayohusu:-

1. Kuongeza fedha za ndani kwenye miradi ya maendeleo.
2. Kufanya marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971.
3. Kuongeza Bajeti kwa ajili ya kuimarisha Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.
4. Benki ya Wanawake Tanzania kuuza hisa zake ili kuongeza mtaji utakaosaidia kuweza kufungua matawi na kutimiza azma ya Serikali ya kuwawezesha wanawake wa Tanzania kiuchumi na kupanua wigo wa huduma zake hadi vijiji.
5. Serikali kuititia Halmashauri za Wilaya zitenge Bajeti kwa ajili ya kuajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii na zipange Bajeti ya kutosha na kutoa kipaumbele katika ukarabati wa majengo na miundombinu.
6. Asilimia tano (5%) ya fedha za maendeleo ya mfuko wa wanawake ziende katika mfuko wa wanawake kuititia Halmashauri husika.
7. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iangalie namna nzuri ya kuhakikisha mabaraza ya watoto yanatambulika na kupata nguvu ya kisheria.
8. Serikali itafiti na kubaini michango inayotolewa na mashirika yasiyo ya kiserikali katika kuleta mandeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa ushauri wa Kamati umezingatiwa, hata hivyo Kamati inaitaka Serikali kutekeleza ushauri wa Kamati kwenye maeneo ambayo bado hayajafanyiwa kazi. Maeneo hayo ni pamoja na Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ni mtambuka na haijapewa uzito unaostahili kwenye mpango wa maendeleo vijiji kwani inawahuisha wanawake katika ustawi wa amani ya Taifa letu na maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 inabainisha wazi kuwa umri unaoruhusiwa kuingia katika ndoa ni kuanzia miaka 18 kwa kijana wa kiume na kuanzia miaka 15 kwa kijana wa kike. Hata hivyo, Sheria hii inakinzana na Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 ambayo inamtambua mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka 18 kama mtoto. Kwa mantiki hii, Sheria ya Ndoa ambayo imekuwepo na kutumika kwa takribani miaka 41 sasa inaruhusu watoto

Nakala ya Mtando (Online Document)

kuingia katika ndoa. Kwa kuwa Tume ya Marekebisho ya Sheria imekwishapeleka mapendekezo ya kurekebisha Sheria ya Ndoa kwenye Wizara ya Katiba na Sheria, Kamati inasisitiza kuwa marekebiso ya Sheria hii yafanywe haraka ili kuweza kuwanusuru watoto.

Mheshimiwa Spika, umaskini na jamii kutotambua umuhimu wa elimu kwa watoto wa kike vimekuwa vikichagiza baadhi ya jamii kuwa ozesha watoto wa kike katika umri mdogo ili kupata mali na kama njia ya kuwaondoa katika familia hasa kwa kuwa hawaoni umuhimu wa kuwasomesha. Baadhi ya jamii zenyetamaduni huu, wasichana wamekuwa wakifungishwa ndoa kabla ya kufikisha umri wa miaka 18. Kamati inaishauri Serikali kuajiri wafanyakazi wa kutosha katika sekta ya maendeleo ya jamii ambao watasaidia kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa elimu kwa mtoto wa kike na athari za ndoa za utotonii ambazo huchangia kiwango kikubwa vifo vya akina mama na watoto.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kwamba elimu ikitolewa kwa jamii husika kutakuwa na mwamko mkubwa wa kopinga ndoa za utotonii, watoto wa kike wataelimishwa na hatimaye Taifa litakuwa na jamii iliyoelimika.

Aidha, Serikali iendelee kuwaelimisha wanawake juu ya sheria mbalimbali zinazotoa fursa kwa wanawake kumiliki ardhi na mali pamoja na sheria zinazowalinda dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015; Makadirio ya ukusanyaji wa mapato. Ukusanyaji katika Mwaka wa Fedha wa 2014/2015 Wizara inatarajia kukusanya jumla ya shilingi 1,845,300,000/= kuitia ada za wanafunzi kutoka katika vyuo vinane vya Maendeleo ya Jamii vya Buhare, Uyole, Rungemba, Mlale, Misungwi, Ruaha, Mabughai na Monduli.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Matumizi ya kawaida na Maendeleo. Ili Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto iweze kutekeleza majukumu yake katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Wizara imetengewa jumla ya shilingi 30,233,474,000/= kati ya fedha hizo shilingi 21,215,930,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 9,017,544,000/= ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi 12,818,434,000/= ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 8,397,496,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, kati ya fedha za Miradi ya Maendeleo, shilingi 7,000,000,000/= ni fedha za ndani na shilingi 2,017,544,000 ni fedha za nje.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimwa Spika, maeneo yaliyopewa kipaumbele kwa mwaka 2014/2015 ni pamoja na:-

(i) Kampeni ya utokomezaji wa ukatili dhidi ya wanawake, wasichana na watoto.

(ii) Uwezeshaji wa wanawake kiuchumi.

(iii) Uboreshaji wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii pamoja na kuimarisha uendeshaji wa vyuo hivyo na kuanzisha mafunzo ya huduma za malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto katika vyuo 30 vya Maendeleo ya Wananchi.

(iv) Uandaaji wa taarifa ya hali ya Jinsia nchini (*Tanzania Country Gender Profile*) na kuanzisha Benki ya Takwimu ya Usawa wa Jinsia.

(v) Uaandaji wa mfumo wa tathmini na ufuatiliaji (*Monitoring and Evaluation Framework*).

(vi) Uboreshaji na uandikishaji, ufuatiliaji na uratibu wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali.

(vii) Kupunguza madeni ambapo shilingi 460,000,000 zimetengwa na Wizara katika Bajeti ya Mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa na Bajeti ndogo inayotengwa kwa Wizara hii kila mwaka bila kujali umuhimu wa Wizara katika kuimarisha masuala yote yanayohusu Maendeleo ya jamii, usawa wa jinsia, haki za watoto na ustawi wa familia. Hata hivyo mbali ya Bunge kuidhinisha fedha kwa Wizara hii bado fedha hizo hazitolewi kwa wakati na wakati mwengine hazipelekwi kabisa. Aidha, bajeti hii ndogo inaathiri uwezo wa Wizara katika kutekeleza viptaumbele ilivyojiwekea katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Moani na Ushauri wa Kamati. Baada ya kujadili Bajeti hii kwa kina Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri ufuatao:-

(a) Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Licha ya kuwa Bajeti inayotengwa kwa ajili ya Wizara ni ndogo bado kumekuwa na ucheleweshaji wa fedha hizo kutoka Hazina. Hali hii imekuwa ikiathiri Wizara katika kutekeleza majukumu yake na hasa Miradi ya Maendeleo.

Kwa mfano, katika mwaka wa fedha unaomalizika Juni 30, 2014 hadi kufikia mwezi Machi, 2014 Wizara ilikuwa imepokea shilingi 2,923,620,590/= sawa na

Nakala ya Mtandao (Online Document)

25% kati ya shilingi 11,910,672,000/= ya Bajeti ya fedha za maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge.

Kati ya fedha hizo shilingi 2,706,106,502/= ni fedha za ndani na shilingi 217,504,088/= ni fedha za nje. Aidha hali hiyo imeathiri utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya wananchi kwaso kikubwa.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba Miradi ya Maendeleo iliyokusudiwa haikuweza kutekelezwa ipasavyo, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kiasi cha fedha kilichosalia kinapatikana.

Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuainisha vyanzo vypya vya mapato na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ili kuweza kutenga fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo na sio kama ilivyo sasa ambapo fedha nyingi za miradi ya maendeleo zinategemea vyanzo vya nje ambavyo upatikanaji wake umekuwa sio wa uhakika.

(b) Marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971. Kama kamati ilivyobainisha awali kwamba sheria hii pamoja na mambo mengine haimtendei haki mtoto wa kike kamati bado inatilia mkazo suala la Serikali kuleta Bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971.

(c) Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

(i) Mfumo wa Retention. Mfumo huu unakitaka chuo kupeleka maduhuli kwenye Retention Account na baadaye fedha hizo zirudishwe chuoni kwa ajili ya kukiendeleza chuo. Mfumo huu umekuwa na tatizo la kurudisha fedha kidogo na wakati mwingine kutorudisha kabisa, hivyo kuathiri utekelezaji wa shughuli za vyuo. Kwa mfano tangu mfumo huu kuanza kutumika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungembba kimepeleka kwenye Retention Account shilingi 208,000,000/=, lakini kiasi cha fedha kilichorudishwa ni shilingi 33,000,000/= tu. Aidha, Katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ruaha, kuanzia mwezi Septemba

hadi Disemba, 2013, chuo kilipeleka kwenye Retention Account shilingi 200,000,000/= zimerudishwa shilingi 76,000,000/= tu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na fedha zinazokusanywa na chuo (maduhuli) kutorudishwa chuoni kama ilivyotarajiwa, Kamati inashauri Serikali kurudisha mfumo wa zamani wa fedha hizi kupelekwa Hazina Ndogo (*retention at the source*) badala ya kutumia mfumo wa sasa wa kupeleka kwenye Retention Account ambao una matatizo makubwa ya kurejesha kiasi kidogo cha fedha na wakati mwingine kiasi hicho kidogo kutorudishwa kwa wakati.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kamati inaamini kwamba endapo makusanyo yanayopelekwa katika mfuko wa retention zitarudishwa zote matatizo mengi yataweza kutatuliwa na chuo chenyewe.

(ii) Ukarabati wa majengo na miundombinu ya Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba kipo Mkoani Iringa, katika Mji wa Mafinga. Kwa kuwa miundombinu ya umeme wa gridi imefika hapo chuoni, Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na TANESCO wafanye tahmini ya ghamama za kuingiza umeme huo wa gridi katika majengo ya chuo ili iweze kuingizwa badala ya kutumia umeme wa jenereta ambao nguvu yake ya usambazaji ni ndogo na ghamama za uendeshaji ni kubwa.

(iii) Umuhimu wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Wananchi kupata vyombo vya Usafiri.

Mheshimiwa Spika, vyuo hivi vinakabiliwa na upungufu mkubwa wa vyombo vya usafiri kama vile magari na pipipiki, kutokana na upungufu huo vyuo hasa vya Maendeleo ya Wananchi kama vile Chuo cha Chilala – Rutamba, vinashindwa kuendesha mafunzo ya vitendo kama fani ya ufundi magari, umeme wa magari. Aidha kutokana na vyuo hivi kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi na watumishi vyombo vya usafiri ni muhimu.

Kwa kuwa hivi karibuni Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imetaifisha magari mengi mali ya Kampuni ya SBT Japan, tunaomba Serikali kwa kushirikiana na TRA kutoa kipaumbele na kuvipatia Vyuo hivi magari kama ambavyo imefanya kwa Taasisi nyingine za Serikali. Kamati inaishauri Serikali kugawa magari hayo kwa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii hususani Chuo cha Rungemba ambacho hakina nyenzo ya usafiri wa aina yoyote ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu kwa maendeleo ya Taifa.

(iv) Mgogoro wa ardhi kati ya chuo cha Rungemba na Wananchi.

Mheshimiwa Spika, kutokana chuo kutokuwa na hati miliki ya eneo ambalo limejengwa chuo hali inayosababisha wananchi kudai kwamba eneo hilo ni lao Kamati inaishauri Serikali kuharakisha upatikanaji wa Hati hiyo kwakuwa mchakato wa kipata hati hiyo umechukua muda mrefu na hivyo kusababisha Chuo kushindwa kupanga mipango yake ya muda mrefu na muda mfupi jambo hili limelizwe mapema.

Mheshimiwa Spika, ajira kwa wahitimu wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii; kuna upungufu mkubwa wa wataalam wa maendeleo ya jamii katika

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Halmashauri na hasa katika Kata kwa idadi ya 2,045 licha ya kwamba vyuo vyetu vinaendelea kutoa wastani wa idadi ya wahitimu 4,900 kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha katika bajeti kwa ajili ya kuwaajiri wataalam wa maendeleo ya jamii wanaotoka vyuoni moja kwa moja kama inavyofanyika kwa ajira za Walimu.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kukifanya Chuo cha Maendeleo ya Jamii, Tengeru kuwa Taasisi ya Elimu ya Juu ulianza tarehe 15/11/2010 kwa chuo kuunda kikosi kazi cha ufuatiliaji kilichoandaa mapendekezo na kuyawasilisha katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Chuo kujitegemea uliwasilishwa kwa Waziri wa Elimu ambaye ana dhamana ya Vyuo vya Ufundis vilivyo chini ya Baraza la Elimu ya Ufundis Tanzania (*NACTE*). Baada ya Waziri wa Elimu kuridhia na kusaini, Muswada, ulipelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushauri, uandishi wa kisheria na uchapaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, Muswada ulichapishwa katika Gazeti la Serikali Namba tisa (Na. 9) la Tarehe 25 Januari, 2013 kwa jina la Tengeru *Institute of Community Development (Establishment Order, 2013)*. Kamati iliarifiwa kwamba Muswada wa kukibadilisha Chuo cha Maendeleo ya Jamii, Tengeru ili kuijendesha kama Taasisi ya Elimu ya Juu limeletwa Bungeni likisubiri kuwasilishwa na Waziri mwenye dhamana kama inavyoolekezwa na Sheria iliyanzisha Baraza la Elimu ya Ufundis. Kamati inataka Serikali kuleta Muswada ndani ya Bunge ili ujadiliwe na hatimaye sheria ya kukiwezesha chuo kuijendesha kama Taasisi ya Elimu ya Juu iweze kupitishwa.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake ulianzishwa kutohakana na Azimio la Bunge liliopitishwa Agosti, 1993 kwa mujibu wa kifungu 17(1) cha Sheria ya *Exchequer and Audit Ordinance* (Cap. 439) No. 21 ya mwaka 1961, kama mojawapo ya mikakati ya kuwawezesha wanawake kuijimarisha na kuwawezesha kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Mfuko huu ni kuwawezesha wanawake wote walio katika Halmashauri kwa kuwakopesha fedha kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali na kupambana na umaskini kwa kuunda vikundi na kupatiwa mikopo.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni kawaida kwa Halmashauri nyingi kutozingatia sheria inazozitaka kutenga asilimia tano (5%) ya mapato yao kwa ajili ya maendeleo ya wanawake, Kamati inazitaka Halmashauri zote nchini

Nakala ya Mtando (Online Document)

kutenga asilimia tano ili kuchochea maendeleo ya wanawake. Aidha, Kamati inashauri fedha hizo kutumika kama zilivyokusudiwa na uwepo usimamizi thabiti katika Halmashauri ili kuhakikisha hakuna ubadhirifu utakaofanywa katika matumizi ya fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Halmashauri ya Mji Korogwe na Halmashauri nyingine ambazo zimekuwa mfano wa kuigwa kwa kuwa zimekuwa na utamaduni wa kutenga kiasi hicho cha fedha na kutumika kama kilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Wanawake Tanzania ilianzishwa kwa lengo la kuwakomboa wanawake kiuchumi kwa kuwawezesha kupata mikopo kwa riba nafuu na kwa ajili ya kukuza mtaji ya biashara. Hata hivyo, lengo hilo linaonekana kutofikiwa kikamilifu katika siku za karibuni hasa kutokana na ukweli kwamba kiwango cha fedha ambazo zinatolewa kwa ajili ya benki kama sehemu ya kukuza mtaji wake ni kidogo sana ikilinganishwa na matarajio ya awali.

Mheshimiwa Spika, wakati Rais, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, akiielezea madhumuni ya kuanzishwa kwa benki hii alisema Serikali itatoa jumla ya shilingi bilioni mbili (2,000,000,000/=) kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo ili kuiwezesha benki hii kuimarika kimitaji.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 na mwaka 2011/2012, Benki ya Wanawake ilipokea kiasi cha sh. 2,000,000,000/= kama ilivyoelekezwa. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2012/2013, kiasi cha sh. 1,300,000,000/= tu ndiyo kilitolewa na kiasi cha sh. 700,000,000/= bado hakijatolewa na Serikali. Kipindi cha mwaka 2013/2014 kiasi cha sh. 450,000,000/= tu ndiyo kimetolewa na Serikali na kiasi cha sh. 1,550,000,000/= bado hakijatolewa mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, tangu Benki ianzishwe mpaka sasa ni kiasi cha shilingi bilioni 8.7 tu ndiyo kilichopo kama mtaji na kufuatia Sheria za Benki Kuu ya Tanzania ili Benki iweze kuijendesha kibiashara inapaswa iwe na mtaji kuanzia sh. 15,000,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali kutoa kiasi chote cha fedha ambazo hakikupelekwa kwenye Benki ya Wanawake ili kutimiza azma ya kauli ya Rais ya kuifanya Benki hii kuijendesha kibiashara na kutoa fursa kwa wanawake wengi nchini kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kukupongeza kwa umahiri na busara zako katika uendeshaji wa Vikao vya Bunge. Nawapongeza pia Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa jinsi wanavyokusaidia katika

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kutekeleza majukumu yako. Nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Sophia Mnyambi Simba; Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana; Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu Anna T. Maembe; Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Nuru H. M. Milao na Wakurugenzi, Wakuu wa Idara, Wakuu wa Vitengo na Taasisi pamoja na Watumishi wote wa Wizara kwa ushirikiano wao mkubwa uliowezesha Kamati kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashilillah, akisaidiwa na Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndugu Charles Mloka, Makatibu wa Kamati, Ndugu Aziza Makwai, Ndugu Hanifa Masaninga na Ndugu Abdallah Hancha, kwa ushauri na uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (Makofii)

SPIKA: Ahsante sana.

**Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii
Kuhusu Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii,
Jinsia na Watoto kwa Mwaka 2014/2015
kama ilivyowasilishwa Mezani**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU
UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO
KWA MWAKA**

**WA FEDHA WA 2013/2014 PAMOJA NA MAONI YA
KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA
WA FEDHA WA 2014/2015**

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) na Kanuni ya 117(11) za Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Aprili, 2013, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, ili niwasilishe Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, na kuliomba Bunge lako Tukufu lipokee taarifa hii na kuijadili.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza wajibu wake Kamati ilikutana na watendaji wa Wizara walio chini ya **Fungu 53** tarehe 01 na 02 Mei, 2014 jijini Dar es salaam na kupokea taarifa kuhusu utekelezaji wa majukumu wa Wizara, malengo yaliyopangwa kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2013/2014 pamoja na kujadili bajeti iliyohusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015. Aidha, Kamati ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Maagizo ya Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2013/2014

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha **2013/2014**, Wizara ilipangiwa bajeti ya shilingi **25,964,470,000/=** kati ya fedha hizo shilingi **8,656,002,000/=** inajumuisha mishahara na shilingi **5,397,496,000/=** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Shilingi **11,910,672,000/=** kwa ajili ya Miradi mbalimbali ya Maendeleo ambapo shilingi **6,500,000,000/=** ni fedha za ndani na shilingi **5,410,672,000/=** ni fedha za nje. Hadi kufikia Machi, 2014 Wizara ilikuwa imepokea shilingi **1,964,133,299/=** sawa na **asilimia 36** ya bajeti ya matumizi mengineyo. Aidha, katika fedha za Miradi ya Maendeleo Wizara ilikuwa imepokea shilingi **2,923,620,590/=** sawa na **asilimia 25** ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge ambapo **2,706,106,502** ni fedha za ndani na shilingi **217,514,088/=** ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kutopatikana kwa fedha hizo kamati inaitaka Serikali ikamilishe utoaji wa fedha hizi kwa kipindi kilichosalia ili Wizara iweze kutekeleza majukumu ilijoipangia kwa Mwaka wa Fedha **2013/2014**.

3.0 UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha unaoisha Juni 30, 2014, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwenye maeneo mbalimbali, hasa kwenye maeneo yanayohusu:-

1. Kuongeza fedha za ndani kwenye miradi ya maendeleo.
2. Kufanya marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971.
3. Kuongeza bajeti kwa ajili ya kuimarisha Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.
4. Benki ya Wanawake Tanzania kuuza hisa zake ili kuongeza mtaji utakaosaidia kuweza kufungua matawi na kutimiza azma ya Serikali ya kuwawezesha wanawake wa Tanzania kiuchumi na kupanua wigo wa huduma zake hadi vijijini.

5. Serikali kupitia Halmashauri za Wilaya zitenge bajeti kwa ajili ya kuajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii na zipange bajeti ya kutosha na kutoa kipaumbele katika ukarabati wa majengo na miundombinu.

6. Asilimia tano (5%) ya fedha za maendeleo ya mfuko wa wanawake ziende katika mfuko wa wanawake kupitia Halmashauri husika.

7. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iangalie namna nzuri ya kuhakikisha mabaraza ya watoto yanatambulika na kupata nguvu ya kisheria.

8. Serikali itafiti na kubaini michango inayotolewa na mashirika yasiyo ya kiserikali katika kuleta mandeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa ushauri wa Kamati umezingatiwa, hata hivyo Kamati inaitaka Serikali kutekeleza ushauri wa Kamati kwenye maeneo ambayo bado hayajafanyiwa kazi. Maeneo hayo ni pamoja na Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ni mtambuka na haijapewa uzito unaostahili kwenye mpango wa maendeleo vijijini kwani inawahuisha wanawake katika ustawi wa amani ya Taifa letu na maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 inabainisha wazi kuwa umri unaoruhusiwa kuingia katika ndoa ni kuanzia miaka 18 kwa kijana wa kiume na kuanzia miaka 15 kwa kijana wa kike. Hata hivyo, Sheria hii inakinzana na Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 ambayo inamtambua mtu ye yeyote aliye chini ya umri wa miaka 18 kama mtoto.

Kwa mantiki hii, Sheria ya Ndoa ambayo imekuwepo na kutumika kwa takribani miaka 41 sasa inaruhusu watoto kuingia katika ndoa. Kwa kuwa Tume ya Marekebisho ya Sheria imekwishapeleka mapendeleko ya kurekebisha Sheria ya Ndoa kwenye Wizara ya Katiba na Sheria, Kamati inasisitiza kuwa marekebisho ya Sheria hii yafanywe haraka ili kuweza kuwanusuru watoto.

Mheshimiwa Spika, umaskini na jamii kutotambua umuhimu wa elimu kwa watoto wa kike vimekuwa vikichagiza baadhi ya jamii kuwa ozesha watoto wa kike katika umri mdogo ili kupata mali na kama njia ya kuwa ondoa katika familia hasa kwa kuwa hawaoni umuhimu wa kuwasomesha. Baadhi ya jamii zenye utamaduni huu, wasichana wamekuwa wakifungishwa ndoa kabla ya kufikisha umri wa miaka 18.

Kamati inaishauri Serikali kuajiri wafanyakazi wa kutosha katika sekta ya maendeleo ya jamii ambao watasaidia kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa elimu kwa mtoto wa kike, na athari za ndoa za utotoni ambazo huchangia kiwango kikubwa vifo vya akina mama na watoto.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kwamba elimu ikitolewa kwa jamii husika kutakuwa na mwamko mkubwa wa kupinga ndoa za utotoni, watoto wa kike wataelimishwa na hatimaye Taifa litakuwa na jamii iliyoelimika. Aidha, Serikali iendelee kuwaelimisha wanawake juu ya sheria mbalimbali zinazotoa fursa kwa wanawake kumiliki ardhi na mali pamoja na sheria zinazowalinda dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia.

4.0. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

4.1 Makadirio ya Ukusanyaji wa Mapato

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2014/2015 Wizara inataraja kukusanya jumla ya shilingi **1,845,300,000/=** kuitia ada za wanafunzi kutoka katika vyuo vinane vya Maendeleo ya Jamii vya Buhare, Uyole, Rungemba, Mlale, Misungwi, Ruaha, Mabughai na Monduli.

4.2 Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo

Mheshimiwa Spika, ili Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto iweze kutekeleza majukumu yake katika mwaka wa fedha wa **2014/2015**, Wizara imetengewa jumla ya shilingi **30,233,474,000/=** kati ya fedha hizo shilingi **21,215,930,000/=** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **9,017,544,000/=** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi **12,818,434,000/=** ni kwa ajili ya mishahara na shilingi **8,397,496,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, kati ya fedha za Miradi ya Maendeleo, shilingi **7,000,000,000/=** ni fedha za ndani na shilingi **2,017,544,000** ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, maeneo yaliyopewa kipaumbele kwa mwaka 2014/2015 ni pamoja na:-

- i. Kampeni ya utokomezaji wa ukatili dhidi ya wanawake, wasichana na watoto.
- ii. Uwezeshaji wa wanawake kiuchumi.
- iii. Uboreshaji wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii pamoja na kuimarisha uendeshaji wa vyuo hivyo na

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kuanzisha mafunzo ya huduma za malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto katika vyuo 30 vya Maendeleo ya Wananchi.

iv. Uandaaji wa taarifa ya hali ya jinsia nchini (*Tanzania Country Gender Profile*) na kuanzisha Benki ya Takwimu ya Usawa wa Jinsia.

v. Uaandaji wa mfumo wa tathmini na ufuatiliaji (*monitoring and evaluation framework*).

vi. Uboreshajji na uandikishajji, ufuatiliaji na uratibu wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali.

vii. Kupunguza madeni ambapo shilingi 460,000,000 zimetengwa na Wizara katika Bajeti ya mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa na bajeti ndogo inayotengwa kwa Wizara hii kila mwaka bila kujali umuhimu wa Wizara katika kuimarisha masuala yote yanayohusu maendeleo ya jamii, usawa wa jinsia, haki za watoto na ustawi wa familia.

Hata hivyo mbali ya Bunge kuidhinisha fedha kwa Wizara hii bado fedha hizo hazitolewi kwa wakati na wakati mwingine hazipelekwi kabisa. Aidha, bajeti hii ndogo inaathiri uwezo wa Wizara katika kutekeleza vipaumbele ilivyojivekea katika mwaka huu wa fedha.

5.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya kujadili Bajeti hii kwa kina Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri ufuatao:-

(a) Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto

Mheshimiwa Spika, licha ya kuwa Bajeti inayotengwa kwa ajili ya Wizara ni ndogo bado kumekuwa na ucheleweshajji wa fedha hizo kutoka Hazina. Hali hii imekuwa ikiathiri Wizara katika kutekeleza majukumu yake na hasa Miradi ya Maendeleo. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha unaomalizika Juni 30, 2014 hadi kufikia mwezi Machi, 2014 Wizara ilikuwa imepokea shilingi **2,923,620,590/=** sawa na 25% kati ya shilingi **11,910,672,000/=** ya bajeti ya fedha za maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo shilingi **2,706,106,502/=** ni fedha za ndani na shilingi **217,504,088/=** ni fedha za nje. Aidha hali hiyo imeathiri utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya wananchi kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba miradi ya maendeleo iliyokusudiwa haikuweza kutekelezwa ipasavyo, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kiasi cha fedha kilichosalia kinapatikana. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuainisha vyanzo

vipya vya mapato na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ili kuweza kutenga fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo na sio kama ilivyo sasa ambapo fedha nyingi za miradi ya maendeleo zinategemea vyanzo vya nje ambavyo upatikanaji wake umekuwa sio wa uhakika.

(b) Marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971

Mheshimiwa Spika, kama kamati ilivyobainisha awali kwamba sheria hii pamoja na mambo mengine haimtendei haki mtoto wa kike kamati bado inatilia mkazo suala la Serikali kuleta Bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971.

(c) Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi

i. Mfumo wa Retention

Mheshimiwa Spika, mfumo huu unakitaka chuo kupeleka maduhuli kwenye Retention Account na baadaye fedha hizo zirudishwe chuoni kwa ajili ya kukiendeleza chuo. Mfumo huu umekuwa na tatizo la kurudisha fedha kidogo na wakati mwingine kutorudisha kabisa, hivyo kuathiri utekelezaji wa shughuli za vyuo. Kwa mfano tangu mfumo huu kuanza kutumika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba kimepeleka kwenye Retention Account sh. **208,000,000/=**, lakini kiasi cha fedha kilichorudishwa ni shilingi **33,000,000/=** tu. Aidha, Katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ruaha, kuanzia mwezi Septemba hadi Disemba, 2013, chuo kilipeleka kwenye Retention Account shilingi **200,000,000/=** zimerudishwa shilingi **76,000,000/=** tu.

Mheshimiwa Spika, kutohana na fedha zinazokusanywa na chuo (maduhuli) kutorudishwa chuoni kama ilivyotarajiwa, Kamati inashauri Serikali kurudisha mfumo wa zamani wa fedha hizi kupelekwa Hazina Ndogo (*retention at the source*) badala ya kutumia mfumo wa sasa wa kupeleka kwenye Retention Account ambao una matatizo makubwa ya kurejesha kiasi kidogo cha fedha na wakati mwingine kiasi hicho kidogo kutorudishwa kwa wakati.

Kamati inaamini kwamba endapo makusanyo yanayopelekwa katika mfuko wa retention zitarudishwa zote matatizo mengi yataweza kutatuliwa na chuo chenyewe.

ii. Ukarabati wa majengo na miundombinu ya Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba kipo Mkoani Iringa, katika Mji wa Mafinga. Kwa kuwa miundombinu ya umeme wa gridi imefika hapo chuoni, Kamati inashauri Serikali kwa kushirikiana na TANESCO

wafanye tahmini ya gharama za kuingiza umeme huo wa gridi katika majengo ya chuo ili iweze kuingizwa badala ya kutumia umeme wa jenereta ambao nguvu yake ya usambazaji ni ndogo na gharama za uendeshaji ni kubwa.

iii. Umuhimu wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Wananchi kupata vyombo vya Usafiri

Mheshimiwa Spika, vyuo hivi vinakabiliwa na upungufu mkubwa wa vyombo vya usafiri kama vile magari na pikipiki, kutokana na upungufu huo vyuo hasa vya Maendeleo ya Wananchi kama vile Chuo cha Chilala-Rutamba vinashindwa kuendesha mafunzo ya vitendo kama fani ya ufundi magari, umeme wa magari, aidha kutokana na vyuo hivi kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi na watumishi vyombo vya usafiri ni muhimu.

Kwa kuwa hivi karibuni Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imetaifisha magari mengi mali ya Kampuni ya SBT Japan, tunaomba Serikali kwa kushirikiana na TRA kutoa kipaumbele na kuvipatia Vyuo hivi magari kama ambavyo imefanya kwa Taasisi nyingine za Serikali.

Kamati inashauri Serikali kugawa magari hayo kwa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii hususani Chuo cha Rungemba ambacho hakina nyenzo ya usafiri wa aina yoyote ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu kwa maendeleo ya Taifa.

iv. Mgogoro wa ardhi katika chuo cha Rungemba na Wananchi

Mheshimiwa Spika, kutokana chuo kutokuwa na hati miliki ya eneo ambalo limejengwa chuo hali inayosababisha wananchi kudai kwamba eneo hilo ni lao kamati inaishauri Serikali kuharakisha upatikanaji wa hati hiyo kwakuwa mchakato wa kuipata hati hiyo umechukua muda mrefu na hivyo kusababisha Chuo kushindwa kupanga mipango yake ya muda mrefu na muda mfupi. Jambo hili limalizwe sasa.

v. Ajira kwa Wahitimu wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii

Mheshimiwa Spika, kuna upungufu mkubwa wa wataalamu wa maendeleo ya jamii katika Halmashauri na hasa katika kata kwa idadi ya 2,045 licha ya kwamba vyuo vyetu vinaendelea kutoa wastani wa idadi ya wahitimu 4,900 kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha katika bajeti kwa ajili ya kuwaajiri wataalamu wa maendeleo ya jamii wanaotoka vyuoni moja kwa moja kama inavyofanyika kwa ajira za walimu.

vi. Mchakato wa kukifanya Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kuwa Taasisi ya Elimu ya Juu

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kukifanya Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kuwa Taasisi ya Elimu ya Juu ulianza tarehe 15/11/2010 kwa chuo kuunda kikosi kazi cha ufuatiliaji kilichoandaa mapendekezo na kuyawasilisha katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mhehimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Chuo kujitegemea uliwasilishwa kwa Waziri wa Elimu ambaye ana dhamana ya Vyuo vya Ufundis vilivyo chini ya Baraza la Elimu ya Ufundis Tanzania (NACTE). Baada ya Waziri wa Elimu kuridhia na kusaini, Muswada ulipelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushauri, uandishi wa kisheria na uchapaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, Muswada ulichapishwa katika Gazeti la Serikali Na. 9 la Tarehe 25/01/2013 kwa jina la Tengeru *Institute of Community Development (Establishment Order, 2013)*. Kamati iliarifiwa kwamba Muswada wa kukibadilisha Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru ili kuijendesha kama Taasisi ya Elimu ya Juu limeletwa Bungeni likisubiri kuwasilishwa na Waziri mwenye dhamana kama inavyoolekezwa na sheria iliyoanzisha Baraza la Elimu ya Ufundis. Kamati inataka Serikali kuleta muswada ndani ya Bunge ili ujadiliwe na hatimaye sheria ya kukiwezesha chuo kuijendesha kama Taasisi ya Elimu ya Juu iweze kupitishwa.

(d) Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake

Mheshimiwa Spika, mfuko huu ulinzishwa kutokana na Azimio la Bunge lililopitishwa Agosti, 1993 kwa mujibu wa kifungu 17(1) cha Sheria ya Exchaquer and Audit Ordinance (Cap. 439) No. 21 ya mwaka 1961. Kama mojawapo ya mikakati ya kuwawezesha wanawake kujimarisha na kuwawezesha kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, dhamira ya mfuko huu ni kuwawezesha wanawake wote walio katika Halmashauri kwa kuwakopesha fedha kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali na kupambana na umaskini kwa kuunda vikundi na kupatiwa mikopo.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni kawaida kwa Halmashauri nyingi kutozingatia sheria inazotaka kutenga asilimia tano (5%) ya mapato yao kwa ajili ya maendeleo ya wanawake, Kamati inazotaka Halmashauri zote nchini kutenga asilimia tano ili kuchochea maendeleo ya wanawake. Aidha, Kamati inashauri fedha hizo kutumika kama zilivyokusudiwa na uwepo usimamizi thabiti katika Halmashauri ili kuhakikisha hakuna ubadhilifu utakaofanywa katika matumizi ya fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Halmashauri ya Mji Korogwe na Halmashauri nyingine ambazo zimekuwa mfano wa kuigwa kwa kuwa zimekuwa na utamaduni wa kutenga kiasi hicho cha fedha na kutumika kama kilivyokusudiwa.

e) Benki ya Wanawake Tanzania

Mheshimiwa Spika, Benki hii ilianzishwa kwa lengo la kuwakomboa wanawake kiuchumi kwa kuwawezesha kupata mikopo kwa riba nafuu na kwa ajili ya kukuza mitaji ya biashara. Hata hivyo, lengo hilo linaonekana kutofikiwa kikamilifu katika siku za karibuni hasa kutohana na ukweli kwamba kiwango cha fedha ambazo zinatolewa kwa ajili ya benki kama sehemu ya kukuza mtaji wake ni kidogo sana ikilinganishwa na matarajio ya awali.

Wakati Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, akielezea madhumuni ya kuanzishwa kwa benki hii alisema Serikali itatoa jumla ya shilingi bilioni mbili (**2,000,000,000/=**) kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo ili kuiwezesha benki hii kuimarika kimtaji.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 na mwaka 2011/2012 Benki ya Wanawake ilipokea kiasi cha shilingi **2,000,000,000/=** kama ilivyoelekezwa. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2012/2013 kiasi cha sh. **1,300,000,000/=** tu ndiyo kilitolewa na kiasi cha shilingi **700,000,000/=** bado hakijatolewa na Serikali. Kipindi cha mwaka 2013/2014 kiasi cha shilingi **450,000,000/=** tu ndiyo kimetolewa na Serikali na kiasi cha shilingi **1,550,000,000/=** bado hakijatolewa mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, tangu Benki ianzishwe mpaka sasa ni kiasi cha shilingi **8,746,053,000/=** tu ndiyo kilichopo kama mtaji, na kufutia Sheria za Benki Kuu ya Tanzania ili Benki iweze kuijendesha kibiashara inapaswa iwe na mtaji kuanzia shilingi **15,000,000,000/=**.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali kutoa kiasi chote cha fedha ambazo hakikupelekwa kwenye Benki ya Wanawake ili kutimiza azma ya kauli ya Rais ya kuifanya Benki hii kuijendesha kibiashara na kutoa fursa kwa wanawake wengi nchini kujikwamua kiuchumi.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kukupongeza kwa umahiri na busara zako katika uendeshaji wa Vikao vya Bunge. Nawapongeza pia Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa jinsi wanavyokusaidia katika kutekeleza

Nakala ya Mtandao (Online Document)

majukumu yako. Nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto - Mheshimiwa Sophia Mnyambi Simba (Mb); Naibu Waziri - Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana (Mb); Katibu Mkuu wa Wizara – Ndugu Anna T. Maembe; Naibu Katibu Mkuu Ndugu - Nuru H. M. Milao na Wakurugenzi, Wakuu wa Idara, Wakuu wa Vitengo na Taasisi pamoja na Watumishi wote Wizara kwa ushirikiano wao mkubwa uliowezesha Kamati kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wa kipekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Kamati. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Said Mohamed Mtanda, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Capt. John D. Komba, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Mohamed Said Mohamed, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Nasib Suleiman Omar, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Mustafa Haidi Mkulo, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Salum Halfan Barwany, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Kiumbwa Makame Mbaraka, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Salvatory Naluyaga Machemli, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Moza Abedi Saidy, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Agness Elias Hokororo, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Mary Pius Chatanda, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Juma Othman Ali, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Jaddy Simai Jaddy, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Dkt. Maua Abeid Daftari, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Rose Kamili Sukum, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Joshua Samweli Nassari, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Rosemary Kasimbi Kirigini, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Philip Augustino Mulugo, Mb - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashillalah akisaidiwa na Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndugu Charles Mloka, Makatibu wa Kamati, Ndugu Aziza Makwai, Ndugu Hanifa Masaninga na Ndugu Abdallah Hancha, kwa ushauri na uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, na naomba kuwasilisha.

Said Mohamed Mtanda, Mb

MWENYEKITI

KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII

17 Mei, 2014

SPIKA: Sasa nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii, Mheshimiwa Barwany!

**Taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Kuhusu
Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia
na Watoto kwa Mwaka 2014/2015 kama
ilivyosomwa Bungeni**

**MHE. SALUM K. BARWANY - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
KWA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni za kudumu za Bunge, Kanuni ya 99(9), naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ya makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015 ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii Mosi, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na afya. Pili, kwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa imani kubwa aliyokuwa nayo kwangu na kwa uteuzi huu wa kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni. Nasema ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Jamii ni dhana yenyе dhima ya kuwezesha wananchi kutambua uwezo wao na changamoto zilizopo na kutumia rasilimali zilizopo katika kukabiliana na maadui ujinga, umaskini, maradhi na ujisadi. Maendeleo ya jamii yanaweka mkazo katika kushirikisha umma katika kufikiri, kuamua, kupanga na kutekeleza mambo yanayohusu maisha yao na Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia dhana hii Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ina dhima ya pekee katika ustawi na uchumi wa wananchi na nchi kwa ujumla. Hata hivyo, Wizara hii imekuwa ikichukuliwa kwa mtazamo potofu kuwa ni 'Wizara ya Wanawake' na hivyo kutoyapa uzito unaostahili masuala ambayo yanashughulikiwa na Wizara hii ya maendeleo ya jamii, jinsia na watoto.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, maoni haya ya Kambi Rasmi ya Upinzani ninayoyawasilisha yajadiliwe na Wabunge wengine na kujibiwa kwa ukamilifu na Serikali kuwezesha mabadiliko na maendeleo ya jamii yenze usawa wa kijinsia nchini.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo na bajeti ya mwaka 2013/2014. Hadi kufikia Machi, 2014 Wizara hii ilipokea asilimia 25 tu ya bajeti ya maendeleo na asilimia 36 tu ya bajeti ya matumizi mengineyo. Huu ni udhaifu mkubwa wa Serikali inayoongozwa na CCM. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, hali hii inasikitisha sana kwa kuwa hadi mwezi Machi, tayari mfumo mpya wa Bajeti ulikuwa umetimiza robo tatu ya mwaka. Tunajuliza, hata kama Serikali ikiamua kutoa asilimia 75 ya fedha zilizobaki kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika robo mwaka iliyobaki, je, shughuli hizi za maendeleo zitaleta tija na ufanisi? (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali ya CCM kuacha kuwahadaa Wabunge na wananchi kila mwaka kwa kutenga viwango vikubwa vya fedha katika kuitisha bajeti za Wizara, ilhali ikijua kuwa, mosi; haina fedha hizo kwa kuwa ina matumizi makubwa yasiyoangalia maendeleo na ustawi wa jamii wala kuakisi maisha ya umaskini ya Watanzania. (Makofii)

Pili, Serikali ya CCM inajua kabisa haina uwezo wa kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania kama ilivyoahidi na kuwahadaa wananchi katika chaguzi kuu, iwe kwa kasi mpya ama kwa Matokeo Makubwa Sasa! (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2014/2015, Serikali ya CCM imetenga kiasi cha shilingi bilioni tisa kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 8.3 kwa matumizi mengineyo. Je, fedha hizi zilizoombwa ni katika kutekeleza majukumu ya kweli ya Wizara au zinasemwa ili kuwahadaa wananchi wakati kiuhalisia Serikali inajua haina fedha za kutosha za kupeleka katika Wizara hii? (Makofii)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Bajeti zinazotengwa kila mwaka kwa Wizara hii ni ndogo, bado fedha zinazotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo zinacheleshwa na hivyo kuathiri kasi ya Wizara katika kutekeleza majukumu yake. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kupunguza matumizi yasiyo muhimu pamoja na kukusanya kodi ipasavyo ikiwemo kupunguza misamaha ya kodi kwa makampuni na mashirika makubwa ili kuzipa uwezo Wizara zinazohudumia wananchi kwa ujumla!

Mheshimiwa Spika, upungufu wa Wataalam wa Maendeleo ya Jamii. Tumeshuhudia idadi kubwa ya wahitimu katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ambao hawana ajira. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kutoa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

nafasi za ajira kwa wataalam wa maendeleo ya jamii ili kuweza kuziba upungufu uliopo katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, pia, changamoto kubwa iliyopo ni kukosekana kwa nafasi za ajira kwa wataalam wa maendeleo ya jamii katika sekta mbalimbali. Mwaka wa fedha wa 2012/2013, tulisema wazi kuwa wataalam wa maendeleo ya jamii huhitimu vyuo mbalimbali, lakini kuwepo kwao hakuoneshi tija kwa Taifa, hivyo, fani hii imeendelea kupuuzwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013/2014 bado utekelezaji wa suala ili umesuasua. Wizara ituambie ni mkakati gani uliopo ambao umewekwa kwa ajili ya kukabiliana na upungufu wa wataalam wa maendeleo ya jamii ili kuweza kuziba pengo katika Halmashauri kwa mwaka huu wa fedha wa 2014/2015? Pia katika kuhakikisha kuwa Maafisa Maendeleo ya Jamii, wanapata nafasi za ajira katika sekta mbalimbali nchini ili kuongeza tija kwa Taifa?

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaendelea kusisitiza umuhimu wa kuboresha na kuhakikisha kuwa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na wananchi nchini vinapewa kipaumbele. Tunaendelea kuibana Serikali kutoa majibu ni kwa nini imeendelea kutoa kiwango kidogo cha fedha kwa ajili ya kukarabati majengo na miundombinu katika vyuo ambavyo bado ni chakavu kutokana na ukosefu wa matengenezo ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, Vyuo hivi vimeendelea kukumbana na changamoto nyingine kama vile uhaba wa vyombo vya usafiri, upungufu mkubwa wa watumishi wa kada mbalimbali, nyumba za watumishi, madarasa, karakana, mabweni, vifaa na mitambo ya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Spika, hali za vyuo hivi inasikitisha sana na si kama ambavyo viliachwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere na kama Serikali hii sikuvi ya CCM ni waenzi na wafuasi wa sera za maendeleo za Baba wa Taifa, wasingekuwa wa kwanza kuvidumaza, kuvipoteza na kuvuua Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ambavyo yeye olivipigania ili kujenga jamii ya haki, usawa na utu.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, fedha zilizotengwa kwa ajili ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDC) zilikuwa ni shilingi bilioni 2.3 fedha za ndani, lakini, hadi kufikia mwezi Machi, 2014 kiasi cha fedha za miradi ya maendeleo kilichotolewa kwa ajili ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ni kiasi cha shilingi milioni 42. 2 sawa na asilimia 1.8 ya fedha zote zilizotengwa. Aidha, ujenzi na ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ultengewa kiasi cha shilingi milioni 100 ambapo hadi kufikia Machi, 2014 ni milioni 25 sawa na asilimia 25 ya Fedha zilizotengwa.

Swali kwa Serikali, je, kwa hali hii Serikali ya CCM ina nia ya dhati ya kusimamia sekta ya Maendeleo ya Jamii nchini? Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuipa kipaumbele Wizara hii na kuhakikisha kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya Maendeleo ya vyuo hivi zinatolewa kabla ya mwaka wa fedha wa 2013/2014 ili kuviokoa vyuo hivyo ambavyo vingi ni chakavu na havina uwezo wa kutosha kukabiliana na changamoto za uendeshaji ili kuleta mwamko wa maendeleo katika jamii ya Kitanzania kwa kuongeza wataalam wa kutosha wa fani hii.

Mheshimiwa Spika, kuperomoka kwa maadili nchini. Jamii ya Kitanzania imegubikwa na vitendo vyaa picha zisizo za kimaadili ambazo husambazwa katika mitandao ya kijamii. Tumeshuhudia picha na video mbalimbali za Watanzania ambazo zinadhalilisha si tu jamii ya Kitanzania bali pia vinaondoa thamani na utu wa binadamu. Kesi nyngi zimetokea ambapo watu walio katika mahusiano hupiga picha chafu na wanapoachana picha hizo husambazwa katika mitandao ya kijamii lakini wanaozisambaza hawachukuliwi hatua.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa, wanaopiga picha hizo wana makosa lakini pia kuacha picha hizi zisambazwe katika mitandao ya kijamii na blogu mbalimbali nayo inachangia kuperomosha maadili ya jamii yetu. Serikali, kwa kupitia Wizara imechukua hatua gani ili kudhibiti vitendo hivyo? (Makofii)

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa mwaka wa Fedha 2013/2014, tulizungumzia kuhusu vitendo vyaa kudhalilisha wanawake, maarufu kama Kanga Moko na Wizara ilichukua hatua ya kufuatilia na kutekeleza mapendekezo hayo ya Kambi ya Upinzani, lakini bado tunashangaa kuona jinsi Watanzania walivyo wabunifu wa vitendo vyaa kudhalilisha na ni washabiki wa mambo haya ambayo yanaendelea kutoa taswira mbaya ya jamii ya Kitanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kumeibuka kitu kipyaa maarafu kama ngoma ya Kigodoro ambayo inapigwa katika maeneo mbalimbali hapa nchini hasa katika Jiji la Dar es Salaam. Pia, ngoma hii imeambatana na matoleo ya filamu ambazo zinaonesha vitendo hivyo si kwa lengo la kuielimisha jamii, lakini kwa kushabikia vitendo hivyo hali inayochangia pia kuperomosha maadili ya jamii ya Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa jambo la filamu linatakiwa kusimamiwa na BASATA (Baraza la Sanaa la Taifa), lakini Wizara hii ina dhamana ya kuhakikisha vitendo kama hivi vinakemewa na kudhibitiwa ili kulinda utu, hadhi, thamani na utamaduni wa Mtanzania. Kwa mfano, mapema mwaka huu huko Chanika Dar es Salaam, bibi mtu mzima alibakwa na kundi la vijana

Nakala ya Mtandao (Online Document)

wasiojulikana waliokuwa wametoka katika ngoma ya kigodoro ambapo wakazi wa maeneo mbalimbali hukesha kwa kucheza ngoma na muziki usiku kucha.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana halisi ya neno hili maarufu lilipotoholewa na kwa maadili ya jamii yetu, hatuwezi kufafanua zaidi maana ya neno hili ila ni jambo la aibu kubwa kwa jamii iliyoyaa kistaarabu, kushabikia mambo kama haya ambayo si tu yanadhalilisha utu wa Tanzania bali pia yanachangia kutokea kwa vitendo vya wizi na uporaji, ubakaji, ulawiti, ulevi, hali ambayo inachangia kwa kiasi kikubwa kasi ya maambukizi ya UKIMWI na magonjwa mengine ya kujamiihana.

Mheshimiwa Spika, mfumo dume na vitendo vya kikatili wa kijinsia dhidi ya wanawake mwaka 1993, Azimio la Umoja wa Mataifa juu ya Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake liliutafsiri ukatili dhidi ya wanawake kama ifuatavyo:-

"Kitendo chochote cha ukatili wa kijinsia kinachosababisha au kinachoweza kusababisha maumivu au mateso ya kimwili, kingono au kiakili kwa wanawake, ikiwemo vitisho, kulazimishwa au kunyimwa uhuru vinavyotokea katika jamii au kwenye maisha binafsi."

Mheshimiwa Spika, Takwimu hazingop. Utafiti wa mwaka 2010 unaohusu afya na takwimu za uzazi, vifo na maradhi uliofanywa na Serikali pamoja na utafiti wa matendo ya ukatili dhidi ya watoto ya mwaka 2011 unaonesha kuwa asilimia 45 ya wanawake wametendewa ukatili wa kijinsia. Ukatili dhidi ya wanawake majumbani umeendelea kuongezeka, ambapo takwimu mbalimbali na tafiti zinaonesha kuwa kati ya wanawake watatu, wawili wanatendewa ukatili wa kijinsia na waume zao. (Makof)

Mheshimiwa Spika, vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake vimeshamiri na ndio msingi mkuu wa sauti zetu sisi wenye dhamana kuwatetea wanawake ambaa ni nguzo za familia katika jamii zetu. (Makof)

Mheshimiwa Spika, Benki ya Wanawake Tanzania, kwa mujibu wa taarifa ya Wizara, kwa kipindi cha kuanzia Julai 2013 Benki hii ilitoa jumla ya mikopo 9,380 yenye thamani ya shilingi bilioni 8.1, ambapo kati ya wateja hao wanawake ni 7,395 sawa na asilimia 79 ya wateja wote waliopewa mikopo ni wanawake. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Wizara kueleza, je, katika mikopo hii iliyotolewa na Benki ya Wanawake wa Tanzania, ni asilimia ngapi ilinufaisha wateja wa vijiji? (Makof)

Mheshimiwa Spika, taarifa za Wizara zinaonesha kuwa, Benki hii imefungua Tawi la pili katika Mkoa wa Dar es Salaam, jambo ambalo limeendelea kuleta malalamiko kuwa Benki hii haina msaada kwa watu walio mbali na Mkoa huo. Hali kadhalika, benki imefungua vituo 29 vya kutolea

mikopo kwa wajasiriamali wadogo kwenye Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza. Bado swalii lipo, je, watu walio katika Kanda ya Kusini za Iringa, Mbeya, Mtwara, Lindi na Kaskazini kwa mfano, Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga imewekewa mkakati gani kwa mwaka huu wa 2014/2015 ili kuwafikia wajasiriamali wengine ambao hawana uwezo wa kufikia huduma hizo katika vituo tajwa kutokana na uwezo wao mdogo wa kifedha na umbali wa vituo? (Makofi)

SPIKA: Mnajua mkipiga makofi sana, hatusikii anachokisema. Naomba uendelee Mheshimiwa Barwany!

MHE. SALUM K. BARWANY - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, uendeshaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali; kumekuwa na ongezeko la uandikishwaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ambapo tunakiri kuwa yanatekeleza majukumu makubwa katika kusimamia maendeleo ya jamii. Changamoto kubwa ni uwepo wa baadhi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ambayo yameanzishwa mifukoni yakapewa usajili na kunufaika na fedha za ufadhili ambazo kimsingi huwa haziwafiki walengwa.

Mheshimiwa Spika, Mashirika haya yamesajiliwa, lakini yamekuwa yakiwatumbia watoto yatima wanaoishi katika mazingira magumu kama chambo cha kupata misaada kutoka kwa wafadhili ambayo huwa haitumiki kuwaendeleza wala kuwashudumia walengwa ipasavyo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali sio kuwasilisha muhtasari wa matokeo iliyoyachagua bali ripoti kamili ya tafiti zilizofanywa kuhusu mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa mwaka 2012. Aidha, kufuatia kuwasilishwa kwa taarifa hiyo, pongezi zitolewe kwa mashirika yaliyofanya vizuri na orodha ya mashirika yaliyoshindwa kutimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, ili kutokuingilia uhuru wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, wakati umefika sasa wa Serikali kuwasilisha Bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria inayosimamia Mashirika hayo kwa kuzingatia kwamba Sheria hiyo ilipitishwa ‘kwa nguvu’ huku kukiwa na malalamiko mionganoni mwa wadau.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza hatua ilizochukua dhidi ya Shirika Lisilo la Kiserikali liitwalo Wanawake na Maendeleo (WAMA) ambalo Mwenyekiti wake ni Mama Salma Kikwete, Mke wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. WAMA ilituhumiwa ndani ya Bunge hili mwezi Aprili 2012 kwamba ilitumiwa kisiasa na Mama Kikwete kwenye Kampeni za Uchaguzi za mwaka 2010 kwa lengo la kumsaidia aliyekuwa mgombea Urais wa CCM wakati huo Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Spika itakumbukwa kwamba kufuatia majibu ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Mheshimiwa Sophia Simba Bungeni ya mwaka huo wa 2012 kuhusu madai hayo kutokuridhisha, mwongozo uliombwa kwa Spika kuwezesha hatua kuchukuliwa dhidi yake, lakini mpaka sasa muongozo huo haujatolewa. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, Serikali inayoongozwa na CCM imekuwa ikiyafuta Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yasiyofungamana na chama chochote pale ambapo inaona yanafanya harakati za kudai haki kwa niaba ya makundi mbalimbali ya kijamii kama ilivyolifuta Baraza la Wanawake Tanzania (BAWATA) na Shirika la Vijana la National Youth Forum (NYF).

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali hiyo hiyo imekuwa ikifumbia macho pale Mashirika yanapotumika kisiasa kwa manufaa ya CCM na Serikali yake. Hali hii imeachwa muda mrefu na kuota mizizi mpaka Taifa limeshuhudia uteuzi wa wajumbe 201, wengi wao wakiwa wanatoka kwenye Mashirika na Taasisi zingine Zisizo za Kiserikali iwe ni Asasi za Kiraia, Taasisi za Dini na nyinginezo namna ulivyofanyika sehemu kubwa kwa maslahi ya CCM. Matokeo yake ni kutengenezwa kwa 'genge la kutetea misimamo ya CCM' kinyume na Rasimu iliyowasilishwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa kuzingatia maoni ya wananchi. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, changamoto za watu wenyе ulemavu nchini; Watu wenyе ulemavu ni watu ambao wanatakiwa kuthaminiwa katika jamii kutokana na hali halisi ya maumbile yao waliozaliwa nayo. Hivyo basi, ni budi jamii hiyo ikapewa kipaumbele katika masuala muhimu nchini hususani masuala ya elimu, afya, uwezeshaji wa kiuchumi, uongozi pamoja na masuala mengine ya kijamii ikiwemo michezo na ushirikishwaji katika maamuzi.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha kuwa pamoja na umuhimu wake katika Taifa letu, lakini Wizara hii imeshindwa kuweka katika majukumu yake, jukumu la kulinda na kuwahudumia watu wenyе ulemavu kwa kuwaendeleza, kuwalinda na kuhakikisha kuwa hawabaguliwi na wanapewa hadhi sawa na wananchi wengine wote katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, kuuawa kwa mwanamke Munghu Lugata, mlemavu wa ngozi toka Kijiji cha Gasuma, Mkoani Simiyu, Kaskazini Magharibi mwa nchi yetu, kumeacha hisia na uchungu kwa walemavu wengine waliopata mikasa hiyo. Matukio mengi ya mauaji ya walemavu nchini yamekuwa yakihuishwa na imani za kishirikina huku waganga wa jadi wakihuishwa.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Simiyu ni moja katika maeneo ya Kaskazini Magharibi mwa Tanzania yenye matukio mengi ya mauaji hayo. Mikoa mingine

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kwa mujibu wa takwimu za Shirika Lisilo la Kiserikali la Under the Same Sun, zinaonesha kuwa Mikoa mingine kama Tabora, Shinyanga, Rukwa, Mara na Kagera pia inaongoza kwa matukio ya kikatili dhidi ya wale mavu.

Mheshimiwa Spika, aidha, taarifa zaidi zinazeleza kuwa mpaka mwezi Mei mwaka huu yameripotiwa matukio 140 dhidi ya watu wenye ulemavu wa ngozi; 73 yaliyopelekea mauaji na 67 yakiwa ni mashambulio ya kujeruhi katika sehemu mbalimbali za mwili ikiwemo kukatwa kwa viungo kama mikono, miguu, vidole na cha kusikitisha zaidi asilimia 75 ya matukio hayo yalilengwa kwa wanawake na watoto.

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2010, Waziri Mkuu Mizengo Pinda, wakati akiwahutubia wananchi, kwenye maadhimisho ya Siku ya Wale mavu wa Ngozi Tanzania yaliyofanyika viwanja vya Garden Mkoani Iringa alisema kuwa: "Napenda kuwaonya watu wote wanaojihusisha na vitendo viovu vya ukataji wa viungo na wauaji wa wale mavu wa ngozi popote walipo kuwa siku zao zinahesabika. Ndugu zetu wenye ulemavu wa ngozi nawahakikisha Serikali itashinda vita hii na mtaishi kwa uhuru ndani ya nchi yenu."

Mheshimiwa Spika, ikiwa imepita takribani miaka minne toka Waziri Mkuu atoe kauli hiyo, je, matukio ya ulemavu yamepungua kwa kiasi gani? Je, siku za watu wanaofanya vitendo vya ukatili dhidi ya wale mavu zimeshahesabika au bado zinaendelea kuhesabika? Je, Wizara hii imeweka mikakati gani kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapewa kipaumbele katika shughuli za maendeleo ya jamii ili kujenga utu na usawa katika jamii yetu?

Mheshimiwa Spika, matukio yafuatayo yameonesha kuwa kauli za Serikali pamoja na machozi ya Waziri Mkuu hayajaweza kutatua vitendo vya kikatili dhidi ya watu wenye ulemavu hasa wa ngozi kwa kuwa yametokea sehemu mbalimbali nchini kama ilivyoorodheshwa katika ripoti ya Kituo cha Sheria na Haki za Binaadamu;

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2013, Maria Chambanenge wa Sumbawanga, alikatwa mkono na wavamizi wawili ambao walikamatwa hapohapo na mkono wa mhanga, ulikutwa kwa Mganga wa Kienyeji ambapo katika tukio hilo mtoto mdogo wa Bi. Maria naye alijeruhiwa.

Mheshimiwa Spika, Mwezi Februari mwaka 2013, tukio lingine dhidi ya Mwigulu Magese Matonange wa Sumbawanga aliye kuwa akitoka shule alikatwa mkono na wavamizi wawili ambao walikimbia nao. Mwezi huo huo pia, Makunga Baraka wa Simiyu alivamiwa na kundi la watu ambao hawakufanikiwa baada ya kufukuzwa na wanakijiji na kufanikiwa kukimbia.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Ndugu Lugogola Bunzari wa Tabora, aliuliwa baada ya mkono wake kukatwa kinyama na nywele zake kuvutwa kikatili pamoja na ngozi ya paji lake kuchunwa huku Babu yake Bunzari Shinga (miaka 97) aliuliwa wakati akimsaidia mjukuu wake na wakati huo baba wa marehemu aliumizwa vibaya katika jaribio la kumsaidia mwanae.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka jamii kubadilika na kuachana na imani potofu ambazo zinahatarisha maisha na usalama wa watu wengine na ambazo zinarudisha nyuma jithada zinazofanywa za kupiga vita ukatili kwa watu wenyewe ulemavu wa ngozi, Tanzania wanawake na watoto.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, tunawataka wananchi wote, kuwafichua wale wote wanaojishughulisha na vitendo viovu na kutoa taarifa kwa vyombo vyaa dola na mamlaka sahihi ili hatua zaidi ziweze kuchukuliwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Pensheni kwa Wazee; suala la pensheni kwa Wazee sasa limekuwa wimbo ambaa wananchi wameuchoka. Kwa muda mrefu suala hili limekuwa likipigwa danadana, kuanzia Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Kazi na Ajira, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Wizara ya Fedha, ni wazi kuwa hata Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake, Jinsia na Watoto inajaribu kukwepa utekelezaji huu wa ahadi ambayo Serikali ya CCM ilitumia ili kupata kura za wazee kwenye Uchaguzi Mkuu wa 2005 na 2010.

Mheshimiwa Spika, dhamana ya kulismamia suala la wazee ni la Maendeleo ya Jamii kwa kuwa wazee ni sehemu ya jamii na Wizara ina wajibu mkubwa wa kuhakikisha wazee hawa wanapata huduma zao muhimu kama vile CCM imekuwa ikijinadi kwenye llani zake za Uchaguzi. Umefika wakati sasa, Waziri mwenye dhamana atoe maelezo ya kina, ni mikakati gani ambayo Wizara imejiwekea ili kuhakikisha suala la pensheni kwa wazee linatekelezwa kwa mwaka huu wa fedha wa 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Watoto; Ongezeko la Watoto wa Mitaani na athari zake katika Taifa; wakati piramidi ya idadi ya watu nchini Tanzania inaonesha kuwa idadi kubwa ya watu nchini Tanzania ni watoto wenyewe umri wa chini ya miaka 15 na vijana, asilimia 44 ya watu wote hapa nchini ni watoto wenyewe umri chini ya miaka 15, ambapo ongezeko la watoto wa mitaani limeendelea kuwa na athari huku sababu mbalimbali kama umaskini katika familia, mifarakano na ukosefu wa amani kwenye familia na wazazi kutowajibika katika malezi na makuzi ya watoto wao vikipelekea watoto hao kuishi katika mazingira hatarishi.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine ni vitendo vya ukatili, udhalilishaji na unyanyasaji wa watoto kutoka kwa familia na jamii kwa ujumla; nyingine ni kufariki kwa wazazi hasa kutokana na magonjwa mbalimbali, pia huchangiwa na ndoa za umri mdogo pamoja na mimba zisizotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona kuwa vitendo vya ukatili na udhalilishaji dhidi ya watoto vimeendelea kuongezeka na vingine kufumbiwa macho huku Serikali ya CCM ikiwa kimya dhidi ya wahalifu wanaotenda vitendo hivyo, kwani mara kadhaa imeripotiwa kwenye Vyombo vya Habari kufuatia watuhumiwa na vitendo hivyo kuachiwa na Vyombo vya Usalama katika mazingira ya rushwa na kulindana.

Mheshimiwa Spika, ripoti ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (*LHRC*) nchini Tanzania imesema watoto wapatao 800 walilawitiwa mwaka 2013. Inashangaza pia kuona baadhi ya kesi za ulawiti na ubakaji humalizwa nje ya Mahakama ama mfumo wa Sheria jambo ambalo linaendelea kuhatarisha maisha na ustawi wa watoto hapa nchini. Serikali ni lazima ikabiliane na kesi zote za ulawiti na ubakaji kwa uangalifu mkubwa na hata kwa kuhakikisha kuwa washtakiwa wanafikishwa mbele ya Vyombo vya Sheria hata kama familia za waathirika zimekubaliana kumalizana nje ya mfumo huo ili kujenga jamii ya kistaarabu yenyе kuheshimu na kuwalinda watoto. (*Makofij*)

Mheshimiwa Spika, taarifa yangu ni ndefu, naomba iwekwe yote katika Hansard.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya watoto hawa wa kike wamekuwa wakikatishwa masomo yao kutokana na kufanyiwa vitendo vya kudhalilishwa au kuozwa ndoa za utoton, lengo likiwa ni mzazi kujipatia fedha zinazotokana na mahari. Baadhi ya watoto na wanawake kutokana na vitendo hivyo wamekuwa wakiambukizwa magonjwa yakiwemo ya ngono yanayowafanya kujutia kuishi kwao na wakati mwingine wakifikiria ni bora wasingezaaliwa.

Mheshimiwa Spika, maoni na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali; katika ripoti ya jumla ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi maalum kwa kipindi kinachoishia tarehe 31 Machi, 2014, ilitaja sababu nne kubwa zifuatazo zinazofanya Serikali kushindwa kutoa huduma za msingi kwa watoto wanaoishi katika Mazingira magumu:-

(i) Uwepo wa mifumo isiyo endelevu na isiyokidhi viwango.

(ii) Kutokuwepo kwa Maafisa wa Ustawi wa Jamii wa kutosha katika maeneo mbalimbali.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(iii) Kutokuwa na uratibu katika ngazi zote za Serikali kwa kuwa kila taasisi iwe ni katika Serikali (katika ngazi ya Kitaifa au Serikali za Mitaa) au washirika wanaotekeleza utoaji wa huduma za msingi kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, Mitandao ya Utumwa wa Kingono ndani ya Nchi; ni dhahiri kuwa, maendeleo ya jamii lazima yaangalie pia ustawi wa jamii ikiwemo kuwalinda vijana wa Kitanzania, wasichana na wavulana kutoka katika utumwa wa kingono. Hapa nchini, kumekuwa na mtandao mpana unaochukua wasichana toka vijijini na kuwaleta mijini kwa kisingizio cha kuwafanyisha kazi za ndani, lakini huishia kuwa makahaba jambo ambalo si sahihi kisheria. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Mitandao ya Utumwa wa Kingono Nje ya Nchi; wimbi la mabinti wa Kitanzania wanaosafiri nchi za nje, limeongezeka, lakini pia likiwa limebeba taswira mbaya kwa Taifa letu kwa ujumla. Ni dhamana ya Wizara hii kuhakikisha kuwa, maendeleo ya jamii hasa haki za wanawake zinalindwa na kupiganiwa kwa hali na mali hata kama suala la kisera linasimamiwa na Wizara nyingine kwa mfano, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, taarifa mbalimbali za kuaminika zinaonesha kuwa kuna mitandao ya wanaowasafirisha wasichana hao wa Kitanzania kutoka nchini inafanya hivyo kwa makubaliano ya kuwatafutia ajira katika hoteli kubwa na badala yake wanapofika nchi za nje kwa mfano China, huwafanyisha wasichana hao vitendo vyta ukahaba bila ridhaa yao. Mitandao hiyo ikishasafirisha wasichana hao huwanyang'anya wasichana hao passport zao za kusafiria na kujikuta wakishindwa kurejea nchini hali inayowafanya waendelee kuwa watumwa wa kingono na ukahaba.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wasichana, waliosafirishwa nchi nyingine mbalimbali duniani wamebainika pia kujihusisha na biashara za dawa za kulevyo. Aidha, tunaitaka Wizara hii kukomesha mitandao yote ya kingono iliyopo ndani ya nchi kwa kuwa tatizo hili ni pana zaidi ya linavyozungumzwa. Tunaitaka Wizara, kuanzisha msako rasmi wa madanguro yote kwa kushirikiana na Wizara nyingine zenye dhamana ili kudhibiti mtandao huu ambaa umevuka mipaka.

Mheshimiwa Spika, ni rai ya Kambi ya Upinzani kuwa Serikali sasa itakuwa macho na vitendo vyote vyta udhalilishaji ili kuweza kujenga jamii yenye kuheshimu, kulinda na kuthamini utu kama moja ya nguzo muhimu za jamii.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Sheria; Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 ni kati ya Sheria zinazotajwa kuwa kandamizi hasa kwa kuwa imepitwa na wakati. Wakati Maboresho ya Sera na Sheria nyingine zimefanywa kutokana na mazingira na wakati, sheria hii imeendelea kutumika kwa takribani miaka 42

Nakala ya Mtandao (Online Document)

huku marekebishesho yake yakichukua muda mrefu. Tunasikitishwa na mlolongo mrefu uliopo katika kuboresha sheria hii kandamizi, kwa kuwa inatoa mwanya kwa ndoa za utotoni hasa ukizingatia kuwa inaeleza kuwa mtoto wa kike wa miaka 15 anaweza kuolewa.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kuwa Sheria hii ipo katika hatua za Marekebishesho ila ni wakati sasa Serikali ifanye jitihada zaidi kuhakikisha sheria hii inafanyiwa marekebishesho kabla ya mwaka 2014 kwisha. Aidha; Sheria ya Elimu ya mwaka 1978 iliyofanyiwa marekebishesho 2002 inayoruhusu mwanafunzi mjamzito kufukuzwa shule, ni kati ya Sheria zinazopigiwa makelele kwa kuwa zinawanyima watoto wa kike fursa ya kujiedeleza kielimu mara baada ya kujifungua. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kusimamia msingi wa kuwapa nafasi watoto wa kike...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante.

MHE. SALUM K. BARWANY - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, nashukuru na naomba kuwasilisha. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana kwa kusoma vizuri.

Taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Kuhusu Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka 2014/2015 kama ilivyowasilishwa Mezani

HOTUBA YA MHESHIMIWA SALUM KHALFAN BARWANY (MB) MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

(Inatolewa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge kanuni ya 99(9) Toleo la mwaka 2013)

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa kanuni za kudumu za Bunge, Kanuni ya 99 (9) naomba kuwasilisha maoni ya Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni ya makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015 ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii Mosi, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na afya. Pili, kwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa imani kubwa aliyokua nayo kwangu na kwa uteuzi huu wa kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni. Aluta Continua!

Mheshimiwa Spika; Maendeleo ya Jamii ni dhana yenyе dhima ya kuwezesha wananchi kutambua uwezo wao na changamoto zilizopo na kutumia rasilimali zilizopo katika kukabiliana na maadui ujinga, umasikini, maradhi na ufisadi. Maendeleo ya jamii yanaweka mkazo katika kushirikisha umma katika kufikiri, kuamua, kupanga na kutekeleza mambo yanayohusu maisha yao na taifa lao.

Kwa kuzingatia dhana hii Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ina dhima ya pekee katika ustawi na uchumi wa wananchi na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika; Hata hivyo, Wizara hii imekuwa ikichukuliwa kwa mtizamo potofu kuwa ni ‘Wizara ya Wanawake’ na hivyo kuacha kuyapa uzito unaostahili masuala ambayo yanashughulikiwa na Wizara hii ya maendeleo ya jamii, jinsia na watoto.

Maoni haya ya Kambi Rasmi ya Upinzani ninayoyawasilisha yajadiliwe na wabunge wengine na kujibiwa kwa ukamilifu na Serikali kuwezesha mabadiliko na maendeleo ya jamii yenyе usawa wa kijinsia nchini.

1.1 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO NA BAJETI YA MWAKA 2013/2014

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi 2014 wizara hii ilipokea asilimia 25 tu ya bajeti ya maendeleo na asilimia 36 tu ya bajeti ya matumizi mengineyo. Huu ni udhaifu mkubwa wa Serikali inayoongozwa na CCM. Hali hii inasikitisha sana kwa kuwa hadi mwezi Machi, tayari mfumo mpya wa Bajeti ulikuwa umetimiza robo tatu ya mwaka. Tunajuliza, hata kama Serikali ikiamua kutoa asilimia 75 ya fedha zilizobaki kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika robo mwaka iliyobaki, je shughuli hizi za maendeleo zitaleta tija na ufanisi? Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ya CCM kuacha kuwahadaa wabunge na wananchi kila mwaka kwa kutenga viwango vikubwa vya fedha katika kuitisha bajeti za wizara, ilhali ikijua kuwa, mosi; haina fedha hizo kwa kuwa ina matumizi makubwa yasiyoangalia maendeleo na ustawi wa jamii wala kuakisi maisha ya umasikini ya watanzania, pili; Serikali ya CCM inajua kabisa haina uwezo wa kuleta maisha bora kwa kila mtanzania kama ilivyoahidi na kuwahadaa wananchi katika chaguzi kuu, iwe kwa kasi mpya ama kwa matokeo makubwa sasa!

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2014/2015 Serikali ya CCM imetenga kiasi cha shilingi Bilioni 9 kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 8.3 kwa matumizi mengineyo. Je, fedha hizi zilizoombwa ni katika kutekeleza majukumu ya kweli ya wizara au zinasemwa ili kuwahadaa wananchi wakati kiuhalisia Serikali ya CCM inajua haina fedha za kutosha za kupeleka katika wizara hii? Pamoja na kuwa Bajeti zinazotengwa kila mwaka kwa wizara hii ni ndogo, bado fedha zinazotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo zinacheleshwa na hivyo kuathiri kasi ya Wizara katika kutekeleza majukumu yake. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kupunguza matumizi yasiyo muhimu pamoja na kukusanya kodi ipasavyo ikiwemo kupunguza misamaha ya kodi kwa makampuni na mashirika makubwa ili kuzipa uwezo Wizara zinazohudumia wananchi kwa ujumla!

2.0 MAENDELEO YA JAMII

2.1 UPUNGUFU WA WATAALAMU WA MAENDELEO YA JAMII

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu tumeelezea changamoto za upungufu wa wataalamu wa maendeleo ya jamii ambapo hali hairidhishi katika ngazi ya Kata na Kijiji, ambako wataalamu hao wanahitajika zaidi kuwafikia Wananchi na kuwahamasisha ili kujiletea maendeleo yao. Sera ya Maendeleo ya Jamii imeelekeza awepo angalau mtaalamu mmoja wa Maendeleo ya Jamii kwenye kila Kata. Hivi sasa ni asilimia 56 tu ya Kata zote 2,637 zina Wataalam wa Maendeleo ya Jamii. Hii ina maana kuna upungufu wa wataalam 2045 kwenye kata nchini. Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa, maafisa maendeleo ya jamii wanatengewa fungu la kutosha ili kuweza kutawanywa katika kata zote nchini ili kutekeleza shughuli za maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia idadi kubwa ya wahitimu katika vyuo vya maendeleo ya jamii ambao hawana ajira. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kutoa nafasi za ajira kwa wataalamu wa maendeleo ya jamii ili kuweza kuziba upungufu uliopo katika halmashauri zetu. Lakini pia, changamoto kubwa iliyopo ni kukosekana kwa nafasi za ajira kwa wataalamu wa maendeleo ya jamii katika sekta mbalimbali. Mwaka wa fedha wa 2012/2013, tulisema wazi kuwa wataalamu wa maendeleo ya jamii huitimu vyuo mbalimbali, lakini kuwepo kwao hakuoneshi tija kwa taifa, hivyo fani hii imeendelea kupuuzwa. Mwaka 2013/2014 bado utekelezaji wa suala ili umesua sua. Wizara ituambie ni mkakati gani uliopo ambao umewekwa kwa ajili ya kukabiliana na upungufu wa wataalamu wa maendeleo ya jamii ili kuweza kuziba pengo katika halmashauri kwa mwaka huu wa fedha wa 2014/2015 ? Lakini pia katika kuhakikisha kuwa maafisa maendeleo ya jamii, wanapata nafasi za ajira katika sekta mbalimbali nchini ili kuongeza tija kwa taifa?

2.2 VYUO VYA MAENDELEO YA JAMII

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaendelea kusisitiza umuhimu wa kuboresha na kuhakikisha kuwa vyuo vya maendeleo ya jamii na wananchi nchini vinapewa kipaumbele. Tunaendelea kuibana Serikali kutoa majibu ni kwa nini imeendelea kutoa kiwango kidogo cha fedha kwa ajili ya kukarabati majengo na miundombinu katika vyuo ambavyo bado ni chakavu kutokana na ukosefu wa matengenezo ya mara kwa mara. Vyuo hivi vimeendelea kukumbana na changamoto nyingine ambazo kama vile uhaba wa vyombo vyua usafiri, upungufu mkubwa wa watumishi wa kada mbalimbali, nyumba za watumishi, madarasa, karakana, mabweni, vifaa na mitambo ya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Spika, hali za vyuo hivi inasikitisha sana na si kama ambavyo viliachwa na Baba wa Taifa, Hayati J. K Nyerere! Na kama Serikali hii sikivu ya CCM ni waenzi na wafuasi wa sera za maendeleo za Baba wa Taifa, wasingekua wa kwanza kuvidumaza, kuvipoteza na kuviuva vyuo vya maendeleo ya jamii ambavyo Yeye alivipigania ili kujenga jamii ya haki, usawa na utu.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 fedha zilizotengwa kwa ajili ya vyuo vya maendeleo ya wananchi (FDC) zilikuwa ni shilingi bilioni 2.3 fedha za ndani. Lakini, hadi kufikia mwezi Machi 2014 kiasi cha fedha cha miradi ya maendeleo kilichotolewa kwa ajili ya vyuo vya maendeleo ya wananchi ni kiasi cha shilingi milioni 42. 2 sawa na asilimia 1.8 ya fedha zote zilizotengwa. Aidha, ujenzi na ukarabati wa vyuo vya maendeleo ya jamii ilitengewa kiasi cha shilingi milioni 100 ambapo hadi kufikia Machi 2014 m ni milioni 25 sawa na asilimia 25 ya Fedha zilizotengwa. Swali kwa Serikali, je kwa hali hii Serikali ya CCM ina nia ya dhati ya kusimamia sekta ya Maendeleo ya Jamii nchini? Kambi rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuipa kipaumbele wizara hii na kuhakikisha kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya Maendeleo ya vyuo hivi zinatolewa kabla ya mwaka wa fedha wa 2013/2014 ili kuvikoka vyuo hivyo ambavyo vingi ni chakavu na havina uwezo wa kutosha kukabiliana na changamoto za uendeshaji ili kuleta mwamko wa maendeleo katika jamii ya kitanzania kwa kuongeza wataalamu wa kutosha wa fani hii.

2.3 KUPOROMOKA KWA MAADILI NCHINI

Mheshimiwa Spika, ni masikitiko makubwa kuwa jamii ya kitanzania sasa imezidi kuperomoka maadili kila kukicha. Na kadri Serikali inapokua kimya kukemea vitendo vichafu vinavyochafua taswira ya jamii ya Kitanzania, maadili yetu yanazidi kuteketea hasa kutoxana na masuala ya ukuaji wa teknolojia nchini.

Mheshimiwa Spika, jamii ya kitanzania imegubikwa na vitendo vyatika picha zisizo za kimaadili ambazo husambazwa katika mitandao ya kijamii. Tumeshuhudia picha na video mbalimbali za watanzania ambazo zinadhalilisha si tu jamii ya kitanzania bali pia vinaondoa thamani na utu wa binadamu. Kesi nyingi zimetokea ambapo watu walio katika mahusiano hupiga picha chafu na wanapoachana picha hizo husambazwa katika mitandao ya kijamii lakini wanaozisambaza hawachukuliwi hatua. Pamojana kuwa, wanaopiga picha hizo wana makosa lakini pia kuacha picha hizi zisambazwe katika mitandao ya kijamii na blogu mbalimbali nayo inachangia kuperomosha maadili ya jamii yetu. Serikali, kwa kuitia wizara imechukua hatua gani ili kudhibiti vitendo hivyo?

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa mwaka wa Fedha 2013/2014 tulizungumzia kuhusu vitendo vyatika kudhalilisha wanawake maarufu kama Kanga Moko na Wizara ilichukua hatua ya kufuatilia na kutekeleza mapendekezo hayo ya Kambi ya Upinzani, lakini bado tunashangaa kuona jinsi Watanzania walivyo wabunifu wa vitendo vyatika kudhalilisha na ni washabiki wa mambo haya ambayo yanaendelea kutoa taswira mbaya ya jamii ya kitanzania.

Mheshimiwa Spika, kumeibuka kitu kipyaa maarafu kama ngoma ya Kigodoro-Kantangaze ambayo inapigwa katika maeneo mbalimbali hapa nchini hasa katika jiji la Dar es Salaam. Lakini pia, ngoma hii imeambatana na matoleo ya filamu ambazo zinaonesha vitendo hivyo si kwa lengo la kuelimisha jamii lakini kwa kushabikia vitendo hivyo hali inayochangia pia kuperomosha maadili ya jamii ya Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa jambo la filamu linatakiwa kusimamiwa na BASATA (Baraza la Sanaa la Taifa), lakini wizara hii ina dhamana ya kuhakikisha vitendo kama hivi vinakemewa na kudhibitiwa ili kulinda utu, hadhi, thamani na utamaduni wa mtanzania. Kwa mfano, mapema mwaka huu huko Chanika Dar es Salaam, bibi mtu mzima alibakwa na kundi vijana wasiojulikana waliokua wametoka katika ngoma ya kigodoro ambapo wakazi wa maeneo mbalimbali hukesha kwa kucheza ngoma na muziki usiku kucha. Na ndo maana halisi ya neno hili maarufu lilipotoolewa, na kwa maadili ya jamii yetu, hatuwezi kufafanua zaidi maana ya neno hili ila ni jambo la aibu kubwa kwa jamii iliyo ya kistaarabu kushabikia mambo kama haya ambayo si tu yanadhalilisha utu wa mtanzania bali pia yanachangia kutokea kwa vitendo vyatika wizi na uporaji, ubakaji, ulawiti, ulevi, hali ambayo inachangia kwa kiasi kikubwa kasi ya maambukizi ya UKIMWI na magonjwa mengine ya kujamiihana.

3.0 MFUMO DUME NA VITENDO VYA UKATILI WA KIJINSIA DHIDI YA WANAWAKE

Mheshimiwa Spika, mwaka 1993, Azimio la Umoja wa Mataifa juu ya Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake lliutafsiri ukatili dhidi ya wanawake kama:

"Kitendo chochote cha ukatili wa kijinsia kinachosababisha au kinachoweza kusababisha maumivu au mateso ya kimwili, kingono au kiakili kwa wanawake, ikiwamo vitisho, kulazimishwa au kunyimwa uhuru vinavyotokea katika jamii au kwenye maisha binafsi."

Mheshimiwa Spika, Kama ilivyoadikwa katika Mwongozo wa Sera ya Ukatili wa Kijinsia (MOHSW 2011), ukatili wa kijinsia (GBV) ni tatizo kubwa ambalo linawanyima uhuru wanaume, wanawake na watoto kufurahia haki za msingi za binadamu na kufanya wapendavyo. Licha ya tatizo hilo kuwepo katika nchi nyingi duniani lakini halipewi kipaumbele wala halishughulikiwi ipasavyo. Ukatili wa kijinsia unatokana na tofauti za kijinsia na baadhi ya mila na desturi potofu ambazo mara nyingi zinasababisha kuwepo kwa tofauti za kijinsia katika ngazi mbalimbali za jamii. Wanawake kutothaminiwa katika familia, hali duni ya uchumi na kutofahamu sheria kunawafanya washindwe kupata msaada pindi kunapotokea ukatili wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, Takwimu haziongopi. Utafiti wa mwaka 2010 unaohusu afya na takwimu za uzazi, vifo na maradhi uliofanywa na serikali pamoja na utafiti wa matendo ya ukatili dhidi ya watoto ya mwaka 2011 unaonyesha kuwa asilimia 45 ya wanawake wametendewa ukatili wa kijinsia. Ukatili dhidi ya wanawake majumbani umeendelea kuongezeka, ambapo takwimu mbalimbali na tafiti zinaonesha kuwa kati ya wanawake watatu, wawili wanatendewa ukatili wa kijinsia na waume zao.

Vilevile, utekelezaji wa Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 inayowapa haki wanawake na wanaume kuuza na kumiliki ardhi umekuwa mgumu kwa sababu idadi kubwa ya wanawake mijini na vijijini haiwajui sheria hii. Changamoto mbalimbali ikiwemo, upatikanaji wa hati miliki umekuwa ni mgumu kwa wanawake kutokana na kipato kidogo, mfumo dume na kutokuwa na ushirikiano mzuri baina ya wanawake, wanaume na taasisi zinazosimamia sekta hii.

Mheshimiwa Spika, katika misingi ya kuhakikisha jamii ya kitanzania inayapa uzito masuala ya ukatili wa kijinsia na kupinga vitendo vyote vinavyodhalilisha na kushusha thamani ya mwanamke, Kambi rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza hatua madhubuti ambazo zitasaidia kukabiliana na matatizo haya ukiachana na kutoa elimu kwa umma, kuandaa semina kwa mwaka huu wa 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake vimeshamiri na ndio msingi mkuu wa sauti zetu sisi wenyе dhamana kuwatetea wanawake ambaо ni nguzo za familia katika jamii zetu.

3.1 Benki ya Wanawake Tanzania

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Wizara, kwa kipindi cha kuanzia Julai 2013 Benki hii ilitoa jumla ya mikopo 9380 yenye thamani ya shilingi bilioni 9.1 ambapo kati ya wateja hao wanawake ni 7395 sawa na asilimia 79 ya wateja wote waliopewa mikopo ni wanawake. Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Wizara kueleza, je katika mikopo hii iliyotolewa na Benki ya Wanawake wa Tanzania, ni asilimia ngapi ilinufaisha wateja wa vijijini?

Mheshimiwa Spika, taarifa za Wizara zinaonyesha kuwa Benki hii imefungua tawi la pili katika mkoa wa Dar Es Salaam, jambo ambalo limeendelea kuleta malalamiko kuwa Benki hii haina msaada kwa watu walio mbali na mkoa huo. Hali kadhalika, benki imefungua vituo 29 vya kutolea mikopo kwa wajasiriamali wadogo kwenye Mikoa ya Dar Es Salaam, Dodoma na Mwanza, bado swali lipo, je watu walio katika kanda ya Kusini za Iringa, Mbeya, Mtwara, Lindi na kaskazini kwa mfano mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga imewekewa mkakati gani kwa mwaka huu wa 2014/2015 ili kuwafikia wajasiriamali wengine ambaо hawana uwezo wa kufikia huduma hizo katika vituo tajwa kutokana na uwezo wao mdogo wa kifedha na umbali wa vituo?

3.2 USHIRIKISHWAJI WA WANAUME KATIKA MASUALA YA MAENDELEO YA JAMII

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuongelea wajibu wa Serikali na jamii kuendelea kuwashirikisha wanaume katika masuala ya jinsia na maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa shughuli za wizara umeweka vipaumbele vingi katika kupigania haki za wanawake, jambo ambalo nasi kama Kambi hatupingani nalo. Lakini, kuna umuhimu mkubwa wa wanaume kuwa sehemu ya mipango mikakati ya Serikali katika utekelezaji wa malengo yake ikiwamo; kuzuia ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake, utekelezaji wa watoto, vitendo vya udhalilishaji wa watoto, ndoa za utotoni, ukatili dhidi ya watoto, na masuala nyeti ya maendeleo ya jamii. Na jambo hili ni muhimu kupewa kipaumbele kwa kuwa hata katika baadhi ya jamii, wanaume nao wanakumbana na changamoto za kijinsia. Hivyo kama Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, ni dhahiri kuwa sisi wanaume pia tuna nafasi kubwa ya kuongeza msukumo na kuwa chachu ya mabadiliko katika maendeleo ya jamii yenye usawa wa kijinsia. Wanaume wakishirikishwa, taifa litasimama imara!

3.4 UENDESHAJI WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI

Mheshimiwa Spika, kumekua na ongezeko la uandikishwaji wa mashirika yasiyo ya kiserikali, ambapo tunakiri kuwa yanatekeleza majukumu makubwa katika kusimamia maendeleo ya jamii. Changamoto kubwa, ni uwepo wa baadhi ya mashirika yasiyo ya kiserikali ambayo yameanzishwa mifukoni, yakapewa usajili na kunufaika na fedha za ufadhili ambazo kimsingi huwa haziwafiki walengwa. Mashirika haya yamesajiliwa, lakini yamekua yakiwatumia watoto yatima, wanaoishi katika mazingira magumu kama chombo cha kupata misaada kutoka kwa wafadhili ambayo huwa haitumiki kuwaendeleza wala kuwashumia walengwa ipasavyo.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali sio kuwasilisha muktasari wa matokeo iliyoyachagua bali ripoti kamili ya tafiti zilizofanywa kuhusu mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika: Aidha, kufuatia kuwasilisha kwa taarifa hiyo pongezi zitolewe kwa mashirika yaliyofanya vizuri na orodha ya mashirika yaliyoshindwa kutimiza wajibu itajwe.

Kwa upande mwingine, ili kutokuingilia uhuru wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali wakati umefika sasa wa Serikali kuwasilisha bungeni muswada wa marekebisho ya Sheria inayosimamia Mashirika hayo kwa kuzingatia kwamba Sheria hiyo ilipitishwa 'kwa nguvu' huku kukiwa na malalamiko mionganoni mwa wadau.

Mheshimiwa Spika: Kwa upande mwingine, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza hatua ilizochukua dhidi ya Shirika lisilo la Kiserikali liitwalo Wanawake na Maendeleo (WAMA) ambalo Mwenyekiti wake ni Mama Salma Kikwete, Mke wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

WAMA ilituhumiwa ndani ya Bunge hili mwezi Aprili 2012 kwamba ilitumiwa kisiasa na Mama Kikwete kwenye Kampeni za Uchaguzi za mwaka 2010 kwa lengo la kumsaidia aliyekuwa mgombea urais wa CCM wakati huo Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Spika: itakumbukwa kwamba kufuatia majibu ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Mheshimiwa Sophia Simba bungeni ya mwaka huo wa 2012 kuhusu madai hayo kutokuridhisha, muongozo uliombwa kwa Spika kuwezesha hatua kuchukuliwa dhidi yake lakini mpaka sasa muongozo huo haujatolewa.

Serikali inayoongozwa na CCM imekuwa ikiyafuta Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yasiyofungamana na chama chochote pale ambapo inaona yanafanya harakati za kudai haki kwa niaba ya makundi mbalimbali ya Kijamii kama ilivyolifuta Baraza la Wanawake Tanzania (BAWATA) na Shirika la Vijana la National Youth Forum (NYF).

Hata hivyo, Serikali hiyo hiyo imekuwa ikifumbia macho pale Mashirika yanapotumika kisiasa kwa manufaa ya CCM na Serikali yake. Hali hii imeachwa muda mrefu na kuota mizizi mpaka taifa limeshuhudia uteuzi wa wajumbe 201 wengi wao wakiwa wanatoka kwenye Mashirika na Taasisi zingine Zisizo za Kiserikali iwe ni asasi za kiraia, taasisi za dini na nyinginezo namna ulivyofanyika sehemu kubwa kwa maslahi ya CCM. Matokeo yake ni kutengenezwa kwa 'genge la kutetea misimamo ya CCM' kinyume na rasimu iliyowasilishwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa kuzingatia maoni ya Wananchi.

3.5 CHANGAMOTO ZA WATU WENYE ULEMAVU NCHINI

Mheshimiwa Spika, watu wenyewe ulemavu ni watu ambao wanatakiwa/kuthaminiwa katika jamii kutohana na hali halisi ya maumbile yao waliyozaliwa nayo. Hivyo, basi ni budi jamii hiyo ikapewa kipaumbele katika masuala muhimu nchini hususani masuala ya elimu, afya, uvezeshaji wa kiuchumi, uongozi pamoja na masuala mengine ya kijamii ikiwemo michezo na ushirikishwaji katika maamuzi.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha kuwa pamoja na umuhimu wake katika taifa letu lakini Wizara hii imeshindwa kuweka katika majukumu yake, jukumu la kulinda na kuwashudumia watu wenyewe ulemavu kwa kuwaendeleza, kuwalinda na kuhakikisha kuwa hawabaguliwi na wanapewa hadhi sawa na wananchi wengine wote katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, vitendo vya ukatili dhidi ya watu wenyewe ulemavu vimeendelea kushamiri hapa nchini na hivyo kuhatarisha usalama wa watu hao. Matukio mbalimbali ya ukatili dhidi ya watu wenyewe ulemavu yameendelea kuripotiwa katika vyombo vya habari. Hali hii inatoa taswira kuwa, bado Serikali haijafanya kazi kubwa kuwalinda watu wenyewe ulemavu nchini. Na katika idadi ya watu wanaofanyiwa ukatili, wengi ni watoto ambao hawana hatia lakini wamekua wahanga wakubwa wa ukatili huo.

Mheshimiwa Spika, kuuawa kwa mwanamke Munghu Lugata mlemavu wa ngozi toka kijiji cha Gasuma mkoani Simiyu Kaskazini Magharibi mwa nchi yetu kumeacha hisia na uchungu kwa walemavu wengine waliopata mikasa hiyo. Matukio mengi ya mauaji ya walemavu nchini yamekuwa yakihuishwa na imani za kishirikina huku waganga wa jadi wakihuishwa. Mkoa wa Simiyu ni moja katika maeneo kaskazini magharibi mwa Tanzania yenye matukio mengi ya mauaji hayo.

Mikoa mingine kwa mujibu wa takwimu za Shirika lisilo la Kiserikali la Under the Same Sun, inaonesha kuwa mikoa mingine kama Tabora, Shinyanga, Rukwa, Mara na Kagera pia inaongoza kwa matukio ya kikatili dhidi ya walemavu. Aidha, taarifa zaidi zinazeleza kuwa mpaka mwezi Mei mwaka huu yameripotiwa

matukio 140 dhidi ya watu wenyewe ulemavu wa ngozi; 73 yaliyopelekea mauaji na 67 yakiwa ni mashambulio ya kujeruhi katika sehemu mbalimbali za mwili ikiwemo kukatwa kwa viungo kama mikono, miguu, vidole n.k. na cha kusikitisha zaidi asilimia 75 ya matukio hayo yalilengwa kwa wanawake na watoto.

Mwaka 2010, Waziri Mkuu Mizengo Pinda, wakati akiwahutubia wananchi, kwenye maadhimisho ya Siku ya Walemovu wa Ngozi Tanzania yaliyofanyika viwanja vya Garden mkoani Iringa alisema kuwa

"Napenda kuwaonya watu wote wanaojihusisha na vitendo viovu vya ukataji wa viungo na wauaji wa walemovu wa ngozi popote walipo kuwa siku zao zinahesabika. Ndugu zetu wenyewe ulemavu wa ngozi nawahakikisha Serikali itashinda vita hii na mtaishi kwa uhuru ndani ya nchi yenu".

Mheshimiwa Spika, ikiwa imepita takribani miaka minne toka Waziri Mkuu atoe kauli hiyo, je, matukio ya ulemavu yamepungua? Je siku za watu wanaofanya vitendo vya ukatili dhidi ya walemovu zimeshahesabika au bado zinaendelea kuhesabika? Je, wizara hii imeweka mikakati gani kuhakikisha watu wenyewe ulemavu wanapewa kipaumbele katika shughuli za maendeleo ya jamii ili kujenga, utu na usawa katika jamii yetu?

Mheshimiwa Spika, matukio yafuatayo yameonesha kuwa; kauli za Serikali pamoja na Machozi ya Waziri Mkuu hayajaweza kutatua vitendo vya kikatili dhidi ya watu wenyewe ulemavu hasa wa ngozi kwa kuwa yametokea sehemu mbalimbali nchini kama ilivyoorodheshwa katika ripoti ya Kituo cha Sheria na Haki za Binaadamu¹:

- Mwaka 2013, Maria Chambanenge wa Sumbawanga alikatwa mkono na wavamizi wawili ambao walikamatwa hapohapo na mkono wa mhanga, ulikutwa kwa mganga wa Kienyeji ambapo katika tukio hilo mtoto mdogo wa Bi. Maria naye alijeruhija.
- Mwezi Februari mwaka 2013, tukio jingine dhidi ya Mwigulu Magese Matonange wa Sumbawanga aliyejua akitoka shule alikatwa mkono na wavamizi wawili ambao walikimbia nao.
- Mwezi huo huo pia, Makunga Baraka wa Simiyu alivamiwa na kundi la watu ambao hawakufanikiwa baada ya kufukuzwa na wanakijiji na kufanikiwa kukimbia.
- Lugogola Bunzari wa Tabora, aliuliwa baada ya mkono wake kukatwa kinyama na nywele zake

kuvutwa kikatili pamoja na ngozi ya paji lake kuchunwa huku babu yake Banzari Shinga (miaka 97) aliuliwa wakati akimsaidia mjukuu wake na wakati huhuo baba wa marehemu aliumizwa vibaya katika jaribio la kumsaidia mwanae.

Mheshimiwa Spika, Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka jamii kubadilika na kuachana na imani potofu ambazo zinahatarisha maisha na usalama wa watu wengine na ambazo zinarudisha nyuma jitihada zinazofanywa za kupiga vita ukatili kwa watu wenye ulemavu wa ngozi, wanawake na watoto. Hali kadhalika, tunawataka wananchi wote, kuwafichua wale wote wanaojishughulisha na vitendo hivyo na kutoa taarifa kwa vyombo vya dola na mamlaka sahihi ili hatua zaidi ziweze kuchukuliwa kwa mujibu wa sheria.

3.6 Pensheni kwa Wazee

Mheshimiwa Spika, suala la pensheni kwa wazee sasa limekua wimbo ambao wananchi wameuchoka. Kwa muda mrefu suala hili limekua likipigwa danadana, kuanzia Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Kazi naAjira, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Fedha, na ni wazi kuwa hata wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake, Jinsia na Watoto inajaribu kukwepa utekelezaji huu wa ahadi ambayo Serikali ya CCM ilitumia ili kupata kura za wazee kwenye uchaguzi mkuu wa 2005 na 2010.

Mheshimiwa Spika, dhamana ya kulisimamia suala la wazee ni la maendeleo ya jamii kwa kuwa wazee ni sehemu ya jamii na wizara ina wajibu wa kuhaikikisha wazee hawa wanapata huduma zao muhimu kama ambavyo CCM imekua ikijinadi kwenye ilani zake za uchaguzi. Umefika wakati sasa, waziri mwenye dhamana atoe maelezo ya kina, ni mikakati gani ambayo wizara imojiwekea ili kuhaikikisha suala la pensheni kwa wazee linatekelezwa kwa mwaka huu wa fedha wa 2014/2015?

4.0 MAENDELEO YA WATOTO

Mheshimiwa Spika, tafiti mbalimbali zilizofanyika zinazohusu watoto hapa nchini, zimeonesha kuongezeka kwa idadi ya watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, wakati watoto yatima wakifikia milioni 2.4. Katika tafiti hizo, zimeonesha kuwa, tatizo la watoto wanaishi katika mazingira hatarishi limeonekana Mijini na Vijiji na kubwa zaidi kwenye Miji mikubwa ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Tanga, Moshi, Dodoma na Mbeya.

Idadi ya watoto wanaoishi mitaani imeendelea kuongezeka kutoka 1,579 mwaka 2007 hadi 2,010 mwaka 2011, wakati watoto 11,216 wanaoishi katika Vituo vya Kulelea Watoto kati yao 6,089 ni wavulana na 5,127 ni wasichana. Aidha, idadi ya Watoto Yatima waliopo nchi nzima wamefikia 2,400,000 kati ya hao Wasichana ni 1,055,000 na Wavulana ni 1,345,000, ambapo idadi ya watoto 2,700 kati ya miaka 0-14 wanaishi na Virusi vya Ukimwi nchini.²

Mheshimiwa Spika, takwimu hizo zinatoa viashiria na taswira pana juu ya watoto wanaoishi katika Mazingira hatarishi hali ambayo inachangia kwa ongezeko la watoto mitaani pamoja na kukithiri kwa vitendo vya ukatili dhidi ya watoto. Katika taarifa ya jumla ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali juu ya ufanisi kwa mwaka 2014, inaonesha ia mfumo wa udhibiti takwimu na taarifa za watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi ni dhaifu na haukidhi matakwa ya watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi.³

²Ripoti ya “Ukatili Dhidi ya Watoto Tanzania. Matokeo ya Uta ti wa Kitaifa, 2009: Muhtasari wa Kuenea kwa Ukatili wa Kijinsia, Kimwili na Kiakili, Muktadha wa matukio ya Ukatili wa Kijinsia, Afya na Athari ya Tabia ya Ukatili iliyotokea utotoni, Dar es Salaam, Tanzania”, UNICEF Tanzania

³Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali Hadi Machi 2014 ukurasa wa 11

4.1 Ongezeko la Watoto wa Mitaani na Athari zake katika Taifa

Mheshimiwa Spika, wakati piramidi ya Idadi ya Watu nchini Tanzania inaonesha kuwa idadi kubwa ya watu nchini Tanzania ni watoto wenyе umri wa chini ya miaka 15 na vijana. Asilimia 44 ya watu wote hapa nchini ni watoto wenyе umri chini ya miaka 15, ambapo ongezeko la watoto wa mtaani limeendelea kuwa na athari huku sababu mbalimbali kama umasikini katika familia, mifarakano na ukosefu wa amani kwenye familia na Wazazi kutowajibika katika malezi na makuzi ya watoto wao vikipelekeea watoto hao kuishi katika mazingira hatarishi. Sababu nyingine ni vitendo vya ukatili, udhalilishaji na unyanyasaji wa watoto kutoka kwa familia na jamii kwa ujumla, nyingine ni kufariki kwa wazazi hasa kutokana na magonjwa mbalimbali, pia huchangiwa na ndoa za umri mdogo pamoja na mimba zisizotarajiwa.

4.2 Mimba za Utotoni, Zisizotarajiwa, na Utoaji Mimba.

Mheshimiwa Spika, kulingana na Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009, sehemu ya pili inayohusu haki na ustawi wa mtoto (a), kipengele cha 4-14 inataja haki za mtoto kuwa ni pamoja na kulindwa dhidi ya ubaguzi wa aina yoyote, haki yake kupata chakula bora, malezi bora, huduma za afya, elimu, uhuru wa kuamua,

kucheza na kupumzika. Pia, sheria hiyo inataja majukumu ya mzazi kwa mtoto kuwa ni pamoja na kuhakikisha mtoto wake anaishi, anathaminiwa, anaheshimiwa, anapata muda wa kupumzika. Nyingine ni kumlinda dhidi ya mateso, vurugu, uonevu, ukatili au kupata madhara kimwili au kisaikolojia. Pia, mtoto ana haki ya kutoa maoni, kusikilizwa na kuheshimiwa katika uamuzi unaomhusu.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona kuwa vitendo vya ukatili na udhalilishaji dhidi ya watoto vimeendelea kuongezeka na vingine kufumbiwa macho huku Serikali ya CCM ikiwa kimya dhidi ya wahalifu wanaotenda vitendo hivyo, kwani mara kadhaa imeripotiwa kwenye vyombo vya habari kuhusu watuhumiwa na vitendo hivyo kuachiwa na vyombo vya usalama katika mazingira ya rushwa na kulindana.

Mheshimiwa Spika, ripoti ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) nchini Tanzania imesema watoto wapatao 800 walilawitiwa mwaka 2013. Ripoti ya shirika hilo imeweka wazi kwamba kumekuwa na ongezeko kubwa la vitendo vya ukatili kwa wanawake na watoto nchini Tanzania ambapo kumi kati yao wakiwa wamefanyiwa ukatili huo na wazazi wao wenyewe. Watoto wamekuwa katika maisha ya hatari zaidi nchini hasa kutokana na watu wa karibu wakiwemo wazazi wa kiume na hata kaka na wajomba zao kubainika wanawafanya vitendo vya ubakaji.

Mheshimiwa Spika, inashangaza pia kuona baadhi ya kesi za ulawiti na ubakaji umalizwa nje ya mahakama ama mfumo wa Sheria jambo ambalo linaendelea kuhatarisha maisha na ustawi wa watoto hapa nchini. Serikali ni lazima ikabiliane na kesi zote za ulawiti na ubakaji kwa uangalifu mkubwa, na hata kwa kuhakikisha kuwa washtakiwa wanafikishwa mbele ya vyombo vya Sheria hata kama familia za waathirika zimekubaliana kumalizana nje ya mfumo huo ili kujenga jamii ya kistaarabu yenyе kuheshimu na kuwalinda watoto.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya watoto hasa wa kike wamekuwa wakikatishwa masomo yao kutokana na kufanyiwa vitendo vya kudhalilishwa au kuozwa ndoa za utotoni, lengo likiwa ni mzazi kuijapatia fedha zinazotokana na mahari. Baadhi ya watoto na wanawake kutokana na vitendo hivyo wamekuwa wakiambukizwa magonjwa yakiwamo ya ngono yanayowafanya kujutia kuishi kwao na wakati mwengine wakifkiria ni bora wasingeziалиwa.

Mheshimiwa Spika, ripoti ya utafiti uliofanywa na Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (Tamwa) katika mikoa 18 ya Tanzania Bara na Visiiani umebaini kuendelea kushamiri kwa vitendo hivyo huku matukio 996 ya udhalilishaji yaliripotiwa kutokea katika wilaya sita za Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kati ya matukio hayo, 242 yalihusu ubakaji, vipigo vilikuwa 388, ndoa za utotoni 42, kutelekezwa 96, mimba za utotoni 228 huku hali kwa

upande wa Tanzania Bara ukionyesha kuwa Wilaya ya Babati mkoani Manyara ikiongoza ikiwa na matukio 132. Ripoti ya Utafiti wa Ukatili dhidi ya Watoto Tanzania, iliyotolewa na serikali pamoja na Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto (Unicef) mwaka 2011, ilidhihirisha kuwa msichana mmoja kati ya watatu na mvulana mmoja kati ya saba nchini Tanzania hukumbwa na unyanyasaji wa kijinsia kabla ya kufikisha umri wa miaka 18. Viwango vya unyanyasaji wa kimwili navyo viliendelea kuwaathiri watoto kwani karibu wasichana na wavulana watatu kati ya wanne wamepigwa ngumi, kuchapwa au kupigwa mateke wakati wa utoto wao huku robo ya watoto wote wamefanyiwa ukatili wa kihisia.

Mheshimiwa Spika, haya ni matukio ambayo yamekuwa yakiendelea kuwakumba watoto ambao ni taifa la kesho, hivyo kuwafanya kutokufikia malengo yao. Serikali kwa kiasi kikubwa imefanya mambo haya yaendelee kuongezeka kutokana na kufumbia macho mambo haya na haiwezi kujinasua kwa kuwa imeshindwa kabisa kudhibiti ukatili huu dhidi ya watoto nchini wa kiwango kikubwa.

4.4 Mimba za Utotoni

Mheshimiwa Spika, Shirika la Umoja wa Mataifa linalohusika na idadi ya watu UNFPA lilizindua ripoti yake na kuitaja Tanzania kama mojawapo ya nchi ambazo zinakabiliwa na ongezeko kubwa la mimba za utotoni na hivyo kuwafanya wasichana wengi kukatiza masomo yao. Ripoti hiyo iliyozinduliwa tarehe 30 Oktoba 2013 imeangazia hali ya idadi ya watu na kusema kuwa kati ya mimba milioni moja zinazotungwa nchini Tanzania, asilimia 23 ya mimba hizo zinawahuwu wasichana walio chini ya umri wa miaka 19. Kwa mujibu wa ripoti hiyo, idadi ya watoto wa kike wanaopata mimba bado ni kubwa na kwamba takwimu za sasa zinaonyesha kuwa kila kwenye wasichana 10, 4 kati yao wamepata mimba. Baadhi ya mambo yaliyotajwa kusababisha hali hiyo ni pamoja na kuwepo kwa mila potofu ambazo zinawakandamiza na kuwabagua watoto wa kike. Jambo jingine lililoelezwa na ripoti hiyo ni kuendelea kuongezeka kwa ndoa za utotoni ambazo hutumika kama kigezo cha kujipatia mali kwa baadhi ya wazazi.

Mheshimiwa Spika, licha ya mimba za utotoni kuwa na thari kubwa lakini pia suala la watoto wa kike kukatishwa masomo baada ya kupata mimba, ni jambo ambalo serikali inatakiwa kulipitia upya ili kuwapa watoto hawa fursa ya kujikombua kifikra na kiuchumi. Ni wazi kuwa, suala la wanafunzi kutoruhusiwa kuendelea na masomo baada ya kupata mimba ni njia mojawapo ya kupunguza mimba za utotoni, lakini bado ina athari kubwa kwa kuwa inamnyima mtoto wa kike fursa ya kuweza kuijendeleza kimasomo. Wanafunzi wa kike wanapopata mimba hulazimika kukatiza masomo na ndoto zao za kufanikiwa kupitia elimu huzimika. Mimba za utotoni ni matukio yanayoelekea kuzoeleka na kuchukuliwa kuwa ni ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa hakuna mikakati makini ya kudhibiti hali hiyo zaidi ya utekelezaji wa sheria kwamba anayepata mimba lazima afukuzwe shule. Takwimu mbalibali zinaonesha kuwa takribani wasichana zaidi ya 55,000 wamekuwa wakifukuzwa shule kwa sababu ya ujauzito au nyinginezo katika kipindi cha muongo mmoja, hii ni kwa mujibu wa ripoti mpya kutoka Kituo cha Haki za Uzazi (the Centre for Reproductive Health). Ripoti hiyo iitwayo Forced Out: Mandatory Pregnancy Testing and The Expulsion of Pregnant Students In Tanzanian School ilizinduliwa mwaka jana , Dar Es Salaam.

Aidha, idadi ya mimba zisizotarajiwa inazidi kuongezeka na hii inapelekea pia kuongezeka kwa vifo vya wanawake. Kulingana na rejea ya sera ilioandalialiwa na wadau mbalimbali, pamoja na wizara ya afya ilioitwa "WOMEN AND CHILDREN FIRST; Countdown to ending preventable maternal, newborn and child deaths", kutokwa na damu wakati wa uzazi au OBSTETRIC HAEMORRHAGE na matatizo ya damu au HYPERTENSIVE DISORDERS uchangia takribani asilimia 50 ya vifo vya wanawake katika uzazi. Katika kupunguza idadi ya vifo hivi, ni lazima kuhakikisha idadi ya mimba zisizotarajiwa zinapunguzwa kupitia mipango thabiti ya Uzazi wa Mpango.

Pia, ongezeko la utoaji mimba usio salama (UNSAFE ABORTIONS) pia linazidi kuongeza upana wa tatizo. Upatikanaji wa takwimu za kiwango cha mimba zinazotolewa nchini ni chamngamoto, lakini kulingana na taarifa za Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, takribani asilimia 16% ya vifo vya wanawake wakati wa uzazi vinatokana na matatizo yanayojitezea wakati wa utoaji mimba. Haya ni matatizo yanayowakuta mama, dada zetu, na mbaya zaidi asilimia kubwa ni watoto wetu - hawa hawa tunaowafukuza shule. Lazima hatua za makusudi kabisa na za haraka zichukuliwe ili kuhakikisha upatikanaji wa njia bora na salama za kujikinga (za uzazi wa mpango) zinapatikana kwa urahisi pamoja na kutoa uelewa mzuri wa elimu ili kupunguza idadi ya mimba zisizotarajiwa, utoaji mimba usio salama na matatizo yatokanayo. Hii ni pamoja na kuiongezea uwezo na kuboresha ufanisi wa Bohari ya Taifa ya Dawa (MSD) na upatikanaji wa huduma za afya kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea kuishinika Serikali, kufuta adhabu hiyo ili kuwapa fursa watoto wa kike kwa kuwa kila mmoja wetu katika jamii anahitaji nafasi ya pili ili kuweza kurekebisha makosa.

4.5 Maoni na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali Juu ya Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi

Mheshimiwa Spika, katika ripoti ya jumla ya Mdhibiti na Mkaguzi wa hesabu za serikali kuhusu ukaguzi maalumu kwa kipindi kinachoishia tarehe 31 Machi 2014, ilitaja sababu nne kubwa zifuatazo zinazofanya Serikali Serikali kushindwa kutoa

huduma za msingi kwa watoto wanaoishi katika Mazingira hatarishi kuwa ni pamoja na;

- a) Uwepo wa mifumo isiyo endelevu na isiyokidhi viwango vya utoaji wa huduma kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi. Sehemu kubwa ya utoaji wa huduma za msingi kwa watoto hao ilitegemea zaidi misaada mingi iliyotolewa na wafadhili na pia asasi za kiraia na zisizo za kiserikali ziliachiwa jukumu la utoaji huduma za msingi kwa watoto hao bila usimamizi madhubuti;
- b) Kutokuwepo kwa Maafisa wa Ustawi wa Jamii wa kutosha waliopatiwa mafunzo ya kusimamia utoaji wa huduma za msingi kwa watoto wanaoishi katika Mazingira Hatarishi;
- c) Kutokuwa na uratibu katika ngazi zote za Serikali kwa kuwa kila taasisi iwe ni katika Serikali (katika ngazi ya kitaifa au Serikali za Mitaa) au washirika wanaotekeleza utoaji wa huduma za msingi kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi wanatoa huduma hiyo bila kushirikiana. Hali hii imesababisha muingiliano wa utendaji kazi na hivyo kutokuwa na ufanisi katika matumizi ya rasilimali chache zilizotengwa kwa huduma hizo za msingi kwa watoto hao.

4.6 Mitandao ya Utumwa wa Kingono

4.6.1 Mitandao ya Utumwa wa Kingono ndani ya Nchi

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa maendeleoya jamii lazima yaangalie pia ustawi wa jamii ikiwamo kuwalinda vijana wa kitanzania, wasichana na wavulana kutoka katika utumwa wa kingono. Hapa nchini, kumekua na mtandao mpana unaochukua wasichana toka vijijini, na kuwaleta mijini kwa kisingizio cha kuwafanyisha kazi za ndani lakini huishia kuwa makahaba jambo ambalo si sahihi kisheria. Wasichana hao hufanywa kuwa watumwa wa ngono katika madanguro na baadhi hoteli kubwa ambayo yanamilikiwa na watu mbalimbali. Wasichana hao, huuzwa kwa baadhi ya wafanyakishara wakubwa, watalii, wanasiasa na huwa chini ya wamiliki wa madanguro. Hali hii inasikitisha sana, na ni kinyume na haki za binadamu na maadili ya watanzania. Mtandao huu wa ngono pia, huwashawishi wanafunzi wa kike ambaa huaga kwao kuwa wanakwenda shulenii, lakini huishia kwenye madanguro, gesti na baadhi ya hoteli maarufu kwa ajili ya kuuza miili.

Mheshimiwa Spika, mtandao huu umesambaa karibu sehemu kubwa ya nchi ikiwemo miji mikubwa ya Dar Es Salaam, Mwanza na Arusha. Mitandao hiyo ya ndani wa ngono ikihusisha watoto wadogo na wanafunzi imeshamiri nchini na inalijengea taifa picha ya aibu mbele ya jamii pana ya kimataifa.

Kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Utangazaji la Uingereza la BBC⁴ iliyowahi kuibua mjadala mkubwa na kuwaweka watu presha juu, watoto wanaojihusisha na biashara hiyo walieleza jinsi walivyodanganywa kuzamia jijini Dar kufanya kazi nzuri za kuwapatia mkate wao wa siku, lakini wakaishia kwenye biashara ya ukahaba. Watoto hao walieleza kuwa, kutokana na ugumu wa maisha vijijini walipata matumaini kuwa jijini kuna matunda, lakini walipofika wakawa wakifugwa kama watumwa kwa kazi moja tu, kuuzwa kwa wanaume wapenda ngono za rejareja.

Katika mjadala huo ulioendeshwa kwa siku tatu, vitoto hivyo vibichi viliweka wazi kuwa wanapochukuliwa na wanaume hulipwa Sh. 50,000 lakini huambulia Sh. 10,000 kwani fedha nyingine huchukuliwa na tajiri. Ukweli ni kwamba hali ni mbaya kupita maelezo. Tunatoa wito kwa idara zote zinazohusika kunusuru kizazi cha kesho kwa kuwaepusha na mateso wanayoyapata huku janga la ukimwi likichukua kasi. Pia, tunaiomba jamii kupinga kwa nguvu zote kwa kuripoti kwenye vyombo husika uwepo wa biashara hiyo haramu.

4.6.1 Mitandao ya Utumwa wa Kingono Nje ya Nchi

Mheshimiwa Spika, wimbi la mabinti wa kitanzania wanaosafiri nchi za nje, limeongezeka lakini pia likiwa limebeba taswira mbaya kwa taifa kwa ujumla. Ni dhamana ya wizara hii kuhakikisha kuwa, maendeleo ya jamii hasa haki za wanawake zinalindwa na kupiganiwa kwa hali na mali hata kama suala la kisera linasimamiwa na Wizara nyingine kwa mfano Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa kimataifa.

Mheshimiwa Spika, taarifa mbalimbali za kuaminika zinaonesha kuwa kuna mitandao ya wanaowasafirisha wasichana hao wa kitanzania kutoka nchini inafanya hivyo kwa makubaliano ya kuwatafutia ajira katika hoteli kubwa na badala yake wanapofika nchi za nje kwa mfano China, huwafanyisha wasichana hao vitendo vya ukahaba bila ridhaa yao. Mitandao hiyo ikishasafirisha wasichana hao huwanyang'anya wasichana hao hati zao za kusafiria na kujikuta wakishindwa kurejea nchini hali inayowafanya waendelee kuwa watumwa wa kingono na ukahaba. Baadhi ya wasichana, waliosafirishwa nchi nyengine mbalimbali duniani wamebainika pia kujihusisha na biashara za dawa za kulevyta. Vitendo hivi si tu vinaivunjia nchi yetu heshima, lakini pia vinaleta changamoto katika maendeo ya jamii na masuala ya ukatili dhidi ya wanawake ambayo kama taifa hatupaswi kuyafungia macho.

Mheshimiwa Spika, Aidha, tunaitaka wizara hii kukomesha mitandao yote ya kingono iliyopo ndani ya nchi kwa kuwa tatizo hili ni pana zaidi ya

linavyozungumzwa. Tunaitaka Wizara, kuanzisha msako rasmi wa madanguro yote kwa kushirikiana na wizara nyingine zenyenye dhamana ili kudhibiti mtandao huu ambao umevuka mipaka.

Mheshimiwa Spika, ni rai ya kambi ya upinzani kuwa Serikali sasa, itakua macho na vitendo vyote vya udhalilishaji ili kuweza kujenga jamii yenye kuheshimu na kulinda thamani ya utu kama moja ya nguzo kuu za Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Kwa upande mwingine, Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitishwa na suala la mabinti zaidi ya 250 ambao wametekwa na kundi hatari la Boko Haram, na tunaungana na Nigeria pamoja na dunia nzima katika kuhakikisha mabinti hao wako salama na wanarudishwa kwa wazazi wao kwa kuipitia kampeni ya kimataifa ya Bring Back Our Girls.

5.0 MAREKEBISHO YA SHERIA

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 ni kati ya Sheria zinazotajwa kuwa kandamizi hasa kwa kuwa imepitwa na wakati. Wakati Maboresho ya Sera na Sheria nyengine yamefanyika kutokana na mazingira na wakati, sheria hii imeendelea kutumika kwa takribani miaka 42 huku marekebiso yake yakichukua muda mrefu. Tunasikitishwa na mlolongo mrefu uliopo katika kuboresha sheria hii kandamizi, kwa kuwa inatoa mwanya kwa ndoa za utotonii hasa ukizingatia kuwa inaeleza kuwa mtoto wa kike wa miaka 15 anaweza kuolewa. Tunafahamu kuwa Sheria hii ipo katika hatua za Marekebiso ila ni wakati sasa, Serikali ifanye jitihada za juu zaidi kuhakikisha Sheria hii inafanyiwa marekebiso kabla ya mwaka 2014 kuisha.

Aidha, sheria ya elimu ya mwaka 1978 iliyofanyiwa marekebiso 2002 inayoruhusu mwanafunzi mijamzito kufukuzwa shule, ni kati ya Sheria zinazopigiwa makelele kwa kuwa zinawanyima watoto wa kike fursa ya kuijendeleza kielimu mara baada ya kujifungua. Kambi rasmi ya Upinzani, inaitaka Wizara hii kusimamia msingi wa kuwapa nafasi watoto wa kike waliopata mimba mashulenii, ili kuweza kujenga jamii yenye kujenga baddala ya kubomoa zaidi kwa kushinikiza mabadiliko ya Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, aidha ni jambo la kushangaza kuona kuwa pamoja na kujisifu kama taifa liliondelea na la mfano wa kuigwa kwa nchi za Afrika, bado tuna changamoto kwenye sheria za mirathi ambazo zinarudisha nyuma maendeleo ya wanawake na jamii kwa ujumla. Sheria hizi kandamizi, zinaendelea kukandamiza wanawake ambao siku zote tunasema ni gurudumu la maendeleo na nguzo muhimu ya familia. Hiyo, kambi rasmi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa Sheria zote kandamizi dhidi ya wanawake,

Nakala ya Mtandao (Online Document)

ikiwemo Sheria ya Ndoa, Sheria ya Mirathi, zinarejewa ili kumweka mwanamke katika mazingira salama zaidi.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa ili kufikia malengo ya taifa kwa pamoja ni lazima kujenga jamii yenyewe umoja na usawa itakayoleta maendeleo ya pamoja katika masuala ya maendeleo ya jamii, jinsia na watoto.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha.

.....
Salum Khalfan Barwany (MB)

Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani
Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

17 Mei 2014.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na wachangiaji wafuatao: Kwanza kabisa tunaanza na Mheshimiwa Amina Nasoro Makilagi, atafuatiwa na Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Rwakatare, atafuatiwa na Mheshimiwa Faida Mohammed Bakari na wengine nitawataja baadaye.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niwe mchangiaji katika Wizara hii ambayo ni Wizara mtambuka kwa maendeleo ya Taifa, maana ni ukweli usiopingika kwamba bila Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto hakuna kilimo, hakuna maji wala hata hakuna ujenzi kwa sababu Wizara hii kwa kweli ndiyo mhimili wa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajielekeza katika hoja ambazo nimejiandaa kuzungumza, naomba nizungumzie kidogo sana kwenye hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani na pale alipoanza kumtuhumu Mpewda wetu Mama yetu, Mama Salma Kikwete kwamba mwaka 2010 alitumia Taasisi ya WAMA kufanya kampeni na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto alipoulizwa swali katika Bunge lililopita alishindwa kujibu na hatua zozote hazikuchukuliwa juu yake.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo kwamba tuhuma hizo hazikuwa za kweli na Bunge lako Tukufu lilikubali kwamba hapakuwa na tuhuma yoyote, Mama Salma Kikwete alifanya kampeni kama wake wa Viongozi wengine duniani akiwemo na Mke wa Barwany na yeye alifanya kampeni kule Lindi na Mke wa Mbewe na wake wa Viongozi wote walifanya kampeni. (Makofij)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala la wanawake wa Viongozi kufanya kampeni ni jambo ambalo halina upinzani na nitashangaa kuona unakwenda kugombea bila kupata support ya mama. Bahati njema hatujawahi kupokea tuhuma zozote za mtu yeyote anayemtuhumu mama Salma Kikwete kwamba alitumia taasisi ya WAMA dhidi ya pongezi za wananchi na wanawake ambazo wamekuwa wakitoa kumshukuru kwa kazi njema anayoifanya ya kupunguza vifo vyta wanawake na watoto, kupinga mimba za utotoni na kadhalika kupitia taasisi yake ya WAMA.

Mheshimiwa Spika, naomba wote kwa pamoja tuungane kumshukuru Mama Salma Kikwete na kwa kweli tuendelee kumuombea dua, Mwenyezi Mungu ampe maisha marefu, aendelee kutumika na Mwenyezi Mungu ndiye atakayemlipa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, zimetolewa tuhuma kwamba Chama cha Mapinduzi kimekuwa na tabia ya kufuta Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ambayo hayana mlengo wa Chama cha Mapinduzi na wakatolea mfano Shirika la BAWATA.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mwanzilishi wa BAWATA, maana asiyejua tumwelimithe, tulianzaje hii BAWATA. Ni wazo la Jumuiya ya Umoja wa Wanawake wa Tanzania tulipoingia katika mfumo wa Vyama vingi vyta Siasa, tulikubaliana kupitia Mkutano Mkuu wetu wa UWT, chini ya Uongozi wa Mpendwa wetu Mama Anna Abdallah, tukasema tuwe na chombo kitakachotunganisha wanawake wote.

Mheshimiwa Spika, ilipofika mwaka 1995 tukawakabidhi kazi tuliyowapatia, kilichotokea Mungu anajua na mimi nilikuwa Mjumbe najua kilichotokea. Kwa kuwa, jambo hili lipo Mahakamani na Mahakama imeshatoa uamuzi wake, tusiendeleze hapa, ila nitatumia nafasi na naomba nitoe nafasi kwa wale ambao wanataka kuijua vizuri BAWATA na kilichotokea wakati huo, milango iko wazi na elimu hiyo itakuwa ya bure. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nijielekeze kwenye masuala yaliyosemwa kwamba, Chama cha Mapinduzi kimekuwa kinafanya hata ubabe kupitia Wabunge 201. Hili ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hapa tunajadili bajeti. Sasa kama kuna mtu anazungumzia Bunge lililopita, tusubiri kwenye Bunge la Katiba. Nichukue nafasi hii kuwakaribisheni wale wote wenye malalamiko juu ya Wajumbe 201 njooni uwanjani, jengeni hoja tuzungumze uwanjani na kwa kweli nitumie nafasi hii kuwakaribisheni sana karibuni sana katika Bunge lijalo na sio mbali ni mwezi wa Nane. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo sasa naomba nijielekeze katika Bajeti...

Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Nimeshasema mnaposhangilia hapa siyo kupiga kelele. Kuna utaratibu wa kushangilia humu ndani, maana tukianza vigelegele humu ndani inakuwa sivyo. Tunaendelea Mheshimiwa. (*Kicheko*)

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba mshangalie kwa kupiga meza Kibunge.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba niendelee kwa kujielekeza sasa katika hoja ambazo nimejiandaa kuzungumza. Kwa kweli naomba Mheshimiwa Spika, nianze kumpongeza Waziri na Timu yake yote ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya katika mazingira magumu sana ya ufinyu wa bajeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikitembea maeneo mbalimbali, nimejionea mwenyewe jinsi Maafisa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto wanavyohangaika, walivyo na ufinyu wa Bajeti, fedha zinazotoka Wizarani ni ndogo, fedha zinazotengwa na Halmashauri ni ndogo. Ningependa kuchukua nafasi hii kuwapa pole. Napenda pia niiombe Serikali yetu Tukufu kwamba ifike wakati sasa na Wizara hii kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati hii kwamba sasa Wizara hii pia ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, naomba njielekeze kuzungumzia mauaji ya wanawake mbalimbali na hasa nizungumzie mauaji ya wanawake wa Butiama. Pamoja na jitihada zilizofanywa na Serikali pamoja na Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, nichukue nafasi hii kumpongeza Mama Sophia Simba na timu yake kwa jinsi walivyochukua uzito wa mauaji ya wanawake hapa nchini. Nimeshuhudia mimi mwenyewe mauaji yale ya wanawake Butiama, hukukaa nyuma umeshiriki hata mazishi na wakati mwininge nilikwenda na wengine na wengine.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile kupitia Taasisi ya Dawati la Wanawake kuna hatua ambazo mmechukua. Sasa ningependa kupata majibu wakati uki-wind up hotuba yako, sasa ni hatua gani zitakazochukuliwa kuhakikisha haya mauaji yanakomeshwa. Yanakomeshwa maana kwa kweli kama walivyosema wanawake ma-albino, wanawake wenye ulemavu na sasa yametokea tu mauaji ambayo hayaeleweki. Tunataka kusikia kauli ya Serikali inasema nini sasa juu ya mauaji haya ya wanawake ambayo kwa kweli siyo tabia ya Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie masuala ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake. Naomba nishukuru Bunge lako Tukufu chini ya uongozi wako Mheshimiwa Spika, Bunge lililopita wanawake na wanaume wa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Bunge hili bila kujali itikadi zetu. Tulisimama kwa pamoja, tukapaza sauti zetu, tukaiomba Serikali itenye fedha shilingi bilioni mbili kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na hasa wale wa Vijijini.

Mheshimiwa Spika, nimesikitika kuona kwamba mpaka sasa fedha zilizokwenda ni milioni 500 peke yake. Tunashukuru kwa hicho kidogo kilichopatikana kwa sababu ukilinganisha na miaka mingine kilikuwa hakitengi. Ombi langu, naomba fedha hizi kama ambavyo Kamati imeshauri, zitoke zote shilingi bilioni mbili muda haujafika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Ooh!

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naomba kuunga mkono hoja. (Makofi)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mchungaji Rwakatare atafuatiwa na Mheshimiwa Faida Mohamed!

MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi ya kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipigania katika vita mbalimbali vyta maisha na kunistamisha mpaka leo niko Bungeni. Ahsante kwa nafasi ya kuweza kuchangia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, awali ya yote ningependa kuchukua nafasi hii kwa niaba ya wanawake wa Morogoro, kutoa pole zetu za dhati kwa Mheshimiwa Sophia Simba ambaye amefiwa na mtoto wake mpendwa Triford. Kijana wetu ameondoka kama ua lilitonyakua juani, Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi. Amina. Mungu akufariji hiyo njia mama. Jipe moyo, Bwana alikupa, Bwana ametwaa, jina la Bwana libarikiwe. Amina.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitoe pongezi kwa Waziri, Mheshimiwa Sophia Simba na Naibu Waziri na Katibu Mkuu na Timu yao yote kwa kuandaa hotuba nzuri na pia kwa kuweza kufanya na vyote na bajeti finyu; wameweza kukarabati vyuo, wameweza kuwezesha akinamama, wameweza kutoa elimu mbalimbali kwa akinamama, jamani hongereni mwendelee mbele. Mungu siku moja atawapa bajeti kubwa na mtawea kufanya mambo makubwa. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Amina.

MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE: Ningemba pia nitoe rai kwa Serikali, kweli wanapanga bajeti, lakini bajeti hizi haziwashukii kama ziliviyopangwa. Naomba tujitahidi kwa hali na mali angalau basi hata nusu,

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Iakini inaposhuka robo au pengine percent 30 zinakuwa haziwezi kukidhi na kufanya kazi katika Wizara hii vizuri, halafu baadaye tunatoa lawama. Naomba jamani hizi bajeti pamoja na ufinyu wake ziwashukie na ziweze kuwafikia walengwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba nijikite kwenye maboresho ya vyuo. Ningombma maboresho ya Vyuo vya Rungemba na Bigwa vizingatiwe. Chuo cha Rungemba kinatoa diploma, Iakini hali yake ni mbaya. Tulikuwa tunaomba katika chochote kile ambacho mtapata, mkiangalie kwa jicho la huruma chuo hiki na kama kweli tuko serious, jamani kutoa kwa mama na baba maendeleo ni lazima tuboreshe vyuo vyetu ili waweze kusoma mahali ambapo panaweza na wao kuona kwamba kweli wako chuoni.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa hali na mali tuweze kuangalia pia Chuo kile cha Bigwa, Morogoro. Maombi ni mengi kule Morogoro wanawake, wanaume wengi wanapenda, Iakini bahati mbaya pale nafasi ni ndogo. Madarasa hayatoshi, naomba utusaidie kuweka madarasa ili watoto wetu waweze kupata nafasi ya kusoma katika vyuo hivi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ningependa pia nigosie unyanyasaji wa kijinsia. Unyanyaji wa kijinsia kwa akinamama hasa ukeketaji, tabia hii bado inaendelea. Naomba tuikemee kwa hali na mali. Naomba hasa wanaume kwa sababu watu wanakeketwa kwa sababu ya wanaume, basi wanaume pia mtusaidie kukemea. Kuna makabila ambayo yanasema, siwezi kuo kama mwanamke hajakeketwa. Sasa jamani tushirikiane kwa sababu ina madhara mengi kuliko faida. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tukemee na itokomezwe kabisa tabia hii ya kukeketwa. Siku hizi wameanza kukeketa vichanga kama vile wanavyotahiri wavulana wadogo. Kusudi baadaye wasimakatwe na Polisi. Hiyo pia tuchunguze watoto wanapokwenda kliniki tuwachekei, wazazi wanaoleta watoto wa kike ambao wameshakeketwa wachukuliwe hatua, kwa sababu kwa kweli ni udhalilishaji, hatua kali tena ni udhalilishaji mkubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ningombma tena nichukue nafasi hii naomba kwa pamoja tukemee juu ya ngoma mbaya. Ziko ngoma za kigodoro kule Dar es Salaam, iko ngoma ya kibao kata, ziko ngoma za ndembandemba, watu wanavaa kanga moja.

MBUNGE FULANI: Kanga moko.

MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE: Ndiyo kanga moko. Sasa hiyo yote tukemee kabisa kabisa kwa kweli kwa sababu ni chimbuko la UKIMWI. Tusione kama watoto wanajifurahisha, Iakini kweli tuwasaidie kuwafundisha,

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kuwaelekeza na hivyo ndiyo tutaweza kuwa na watoto bora, vijana bora na wasiokuwa na UKIMWI. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Tanzania bila UKIMWI inawezekana. Kama tutakemea mambo mbalimbali ambayo hayapendezi Mungu na wala hayapendezi Taifa. Mavazi mabaya, mavazi ya kushusha suruali mpaka chini bado yanaendelea. Tukemee wanawake kuvalisha matiti nje. Jamani vitu hivi tukemee, sisi ni wazazi. Hata kama siyo mtoto wako, mtoto wa mwenzio ni mtoto wako. Tukemee watoto wetu wawe decent, watoto wetu wawe na heshima na tuwakemee vile vile. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba pia niweze kukemea kwa pamoja na nyinyi, tabia mbaya za unyanyasaji au ukatili wa kingono. Ukatili wa kingono, wanawake wanaoa wanawake wenzao, nyumba ntobo. Hiyo pia tukemee, huko Musoma, watusaidie Wabunge wa huku tusimame kukemea. Mwanamke ataoaje mwanamke mwenzake! Au mwanaume ataoaje mwanaume mwenzake! Tukemee vitu vyote hivi havipendezi, vinamchukiza Mungu. Tukemee ili Mungu aweze kutusaidia. (Makofi)

WABUNGE FULANI: Amina.

MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE: Nikemee pia tabia mbaya ya wanaume kupiga wanawake. Ni aibu, ni ushamba kumpiga mke wako. Ni ujingga pia, mwenyewe utampeleka hospitali. Mwanamke anapigwa na kanga, mwanamke anapigwa na kitenge, eee mwanamke anapigwa na mkufu wa dhahabu. Sasa tena jamani yanakuwa mambo ya ngumi, yametoka wapi?

Mpenzi wako, mama wa watoto wako, unampiga kama mtoto kwa nini? Kwani hamwezi kuongea? Kwani hamwezi kuyapanga mambo chumbani kwenu? Kwani hamuwezi kwenda kwa Wachungaji wawaombee. Eee, tupo ili tuweze kurekebisha mambo. Jamani tupendaje, jamani tushikamane kwa njia hiyo. (Makofi)

SPIKA: Hata watoto siyo wa kuwapiga na watoto pia msiwapige.

MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. (Makofi)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Faida Mohamed Bakari atafuatiwa na Mheshimiwa Capt. John Komba!

MHE. FAIDA MOHAMED BAKARI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi nami nichangie katika hotuba ya Waziri wa Maendeleo ya

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Jamii, Jinsia na Watoto. Awali ya yote napenda kumpa pole Mama yetu Sophia Simba, Mwenyezi Mungu akupe subira *Inshallah*.

WABUNGE FULANI: Amina.

MHE. FAIDA MOHAMED BAKARI: Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wanawake na wananchi wa Mkoa wa Kusini Pemba kwa jinsi ya dua zao mbalimbali ambapo nilikuwa nikiumwa. Napenda kuwaambia kwamba sasa hivi namshukuru Mwenyezi Mungu sijambo na tuko pamoja na tutakuwa pamoja katika kutekeleza majukumu yetu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, napenda kusema ufinyu wa bajeti wa Wizara hii. Kila bajeti tunaitetea Wizara hii juu ya ufinyu wa bajeti, lakini kila kukicha bajeti inapungua. Hivyo sisi wanawake au jamii itakuwaje kama bajeti ya Wizara hii kila siku inapungua? Naomba bajeti ya Wizara hii iweze kuongezwa ili waweze kumudu kufanya kazi zao kwa ufanisi. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Benki ya Wanawake. Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 Ibara ya 205(e) na (f) inaitaka Serikali kuimarisha Mifuko iliyopo ya mikopo na Benki Wanawake Tanzania ili wanawake wengi waweze kufaidika kiuchumi. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, inashangaza sana kwamba fedha imepatikana nyingi. Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anajitahidi katika kutekeleza majukumu yake katika kuisaidia benki hii. Benki ni ya wanawake wote wa Tanzania, lakini nashangaa kwa nini Benki hii ya wanawake iko hapo Dar es Salaam tu ama Tanzania Bara tu. Hivyo wanawake wa Zanzibar wao hawana haki na Benki hii? Kila siku nasimama naomba Benki hii na Wanawake wa Zanzibar tunaomba, Wabunge tunaomba, benki hii nayo ianzishwe Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Zanzibar pia kuna wanawake, Zanzibar pia kuna wananchi ambao pia wanahitaji mikopo kutokana na benki hii, lakini hadi leo benki hii haijaanzishwa Zanzibar, kila tukiuliza hapa process zinaendelea, process zinaendelea. Ofisi imeshapatikana, mara haijapatikana! Sasa ni lini benki hii hasa itaanzishwa katika Kisiwa cha Zanzibar, kule Pemba na Unguja ili na wanawake wa Zanzibar nao wafaidike na mikopo hii waendeleze biashara zao. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Napenda kuipongeza ripoti hii hapa ya *Tanzania Human Right Report* ya 2013. Tulifanyiwa Semina juzi hapo, wakaja na ripoti hii nzuri sana, ripoti hii hapa imetayarishwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu cha Tanzania Bara, (LHRC) na kile Kituo cha Huduma za Kisheria cha Zanzibar (ZLSC).

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kitabu hiki, ripoti hii ya 2013 kwanza napenda kuwapongeza kuandika ripoti zao kwa wakati. Humu katika kitabu hiki hapa ukikiangalia utalia. Kuna ripoti mbalimbali za unyanyasaji wa binaadamu, unyanyasaji wa wanawake, unyanyasaji wa watoto, unyanyasaji wa wazee na kila aina ya mambo mbalimbali ambayo wananchi sisi tunapata shida kutohana na madhila mbalimbali tunayofanyiwa na wenzetu.

Mheshimiwa Spika, niliumia sana kuna bwana mmoja, kizito mmoja hapo Dar es Salaam huwa anakaa karibu na shule fulani, huwa anawachukua watoto wadogo, anawapeleka nyumbani kwake na walimu wanajua na ripoti hii inajulikana. Hii kesi ipo, aliwachukua mpaka Bagamoyo akaenda kufanya nao vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, Ripoti hii ilipopelekwa na kushtakiwa yule baba, nashangaa wale wazazi, imo humu, imo humu, wale wazazi wamekataa kwa sababu ya kupewa hongo na yule bwana. Hivi wewe mzazi unakataa kwamba mwanao hajafanya kitendo hicho kwa sababu ya pesa? Kweli sisi wanawake jamani tujiulize, mtoto wako anafanyiwa kitendo kichafu kama hicho halafu wewe mwenyewe unakataa, unasema hajafanywa! (Makofij)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kesi hii mpaka leo ipo. Naomba Mheshimiwa Waziri aifuatilie kesi nitakuja kumletea hii ripoti ataiona. Aifuatilie ripoti hii watoto hawa wapate haki zao, kwa sababu watoto wananyanyasika sana na si hawa tu ni watu wengi, hata watu wazima wanafanyiwa unyanyasaji, lakini Sheria haichukui mkondo wake. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, mauaji ya wakongwe, wazee wetu hawa, mzee ni mzee. Hivi leo tuwaone wazee wetu kwamba si wazee tena kwa sababu wameshakuwa wazee? Kwani sisi hivi tulivyo ndivyo tulivyokuwa? Tulikuwa wachanga sasa hivi tuko age hii na baadaye tutakuwa wazee kama wao. Leo mauaji ya wazee yameshamiri sana katika Mikoa mbalimbali katika nchi yetu ya Tanzania. Wamefanya kama ni mchezo kuwaua wazee wetu.

Mheshimiwa Spika, mzee akionekana tu ana macho mekundu basi anauliwa mzee huyo. Kwa nini hatuoni huruma sisi binadamu, wazee wetu wengine wanazikwa wakiwa hai, wanakatwa viungo vyao, wazee wetu wamekosa nini, hivyo mzee amefanya kosa Mwenyezi Mungu kumjalia mzee huyu kukuzaa wewe binadamu. Vijana wanawaua wazee, hasa hasa wazee wa kike wanauliwa na vijana ambao hawana maadili mema ya Kitanzania, iweje leo kijana wa Kitanzania anamuua mzee kwa sababu ya macho yake mekundu.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, siyo vizuri. Naomba sana Serikali ichukue hatua kali kwa wanaopatikana na vitendo kama hivyo. Ngoja nipumue kidogo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, sambamba na mauaji ya *albino*, Mwenyezi Mungu hajafanya makosa kuwaumba wenzetu na ngozi hiyo. Leo binadamu sisi ambao tuna ngozi zetu hizi za kawaida tunawaua ma-*albino* wametukosea nini?

SPIKA: Tunaendelea, ahsante sana.

MHE. FAIDA MOHAMED BAKARI: Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (Makofii)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Naomi Mwakyoma Kaihula, atafuatiwa na Mheshimiwa Moza!

MHE. NAOMI A.M. KAIHULA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Napenda nimshukuru Mungu sana kutoka moyoni kwamba amenipatia nafasi nyingine niweze kuzungumzia machache katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli dakika ni chache sana, lakini machache nitakayozungumza, nafikiri yatakuwa mchango mkubwa katika Bunge lako. Kwanza kabisa ningependa kupongeza sana jinsi tunavyokwenda. Napenda niwatoe wananchi, Bunge linakwenda vizuri kwa sababu kuna Upinzani. Mjue kwamba Upinzani kazi yake kubwa moja ni kuhakikisha tunaisimamia Serikali iliyoko madarakani na sisi tunaisimamia Serikali ya CCM na mambo yenyewe mmeyaona.

Mheshimiwa Spika, mnajua Serikali hii ya CCM ni sawa na hadithi zile zilizokuwa zinafundisha kama Karumekenge alikataa kwenda shule mpaka mtiririko ukafanya ndio akaenda. Sasa kufuatana na hayo mmeona nyie wenyewe kutopteka na jinsi ambavyo Hotuba ya Kambi ya Upinzani ilivyotoka; niwaambie tu bila ushabiki, bila kitu chochote, mambo haya naiomba sana Wizara ya Maendeleo ya Jinsia iweze kuyachukua na kuyafanyia kazi kama dira. Kwa sababu, ni mambo ambayo yamejaa uhalisi, ni mambo ambayo yanatuelekeza, tunaweza kujiona. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, pia niwaambie kabisa tunapozungumzia maendeleo ya jamii, jinsia na watoto hatumaanishi wanawake. Maana imejengeka dhana humu kwamba, ni wanawake, sio wanawake na hata tunapozungumzia watoto wamalaya, jamani msifikiri ni wasichana tu, nataka niwaambie akinababa mchukue kwamba, hata watoto wenu wako hatarini. Wako hapa watoto wenu wanaitwa poa, ni hatari sasa hivi, chukueni, amkeni, nendeni huko.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza haya naipongeza sana Hotuba ya Kambi ya Upinzani ya leo na ifanyiwe kazi vizuri na Bunge lako Tukufu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo napenda nieleze ni kwamba, mimi ni Katibu Mkuu wa Baraza la Wanawake wa CHADEMA (BAWACHA). Mimi ni Mwanaharakati, naomba ku-declare interest, pia mimi ni mmojawapo katika waanzilishi wa BAWATA. Najua mchakato wa BAWATA jinsi ulivyokwenda, najua jinsi ambavyo tuligombania Baraza la Wanawake liwepo na Serikali hatimaye ikaridhia, lakini kwa roho upande.

Mheshimiwa Spika, baadaye lilipoundwa tulifanya kazi, Serikali ya CCM ikaona kwamba, tunakwenda kasi; mnajua wenzangu mimi huwa nazungumza mambo ya ukweli kabisa, ikaona wanawake hawa watatudhibiti, kwa hiyo, ikaleta hila lile Baraza ikalifuta. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, lakini naomba tu uelewe, Katibu Mkuu Baraza la UWT, ujue kwamba, katika UWT pia kuna hila kwa sababu, mnatumika zaidi na Chama cha CCM kuwalinda, ili muweze kuwashangilia wanapochaguliwa. Ndio kisa hasa cha kuhakikisha kwamba, hakuna Baraza lolote lenye nguvu linaloibuka kama BAWATA, hata BAWACHA na ndio maana tumekuwa tukiomba hata katika Hotuba zangu zilizopita nilipokuwa Waziri Kivuli, tulizungumza kwamba, tunawaomba hilo jina la UWT mnaonaje kama mngelibadilisha kusudi liwepo, halafu tuhakikishe tuungane tuwe na Baraza la Wanawake wa CHADEMA kama tunavyoomba katika Katiba ijayo kwamba, kuwepo na Kamisheni ambayo itakuwa inatuunganisha, itakuwa bora zaidi kuliko tukiwa tunagawanyika. Wanatumia hila ya *divide and rule*, wagawanye na uwatawale; wanawake tutatawaliwa daima. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba ujue kwamba, tunaomba hivi, hilo Baraza lilipofutwa...

SPIKA: Naomba uniambie mimi.

MHE. NAOMI A. M. KAIHULA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nimeona nimjibu kwa sababu, ye ye alizungumzia zaidi kuhusu hilo.

Mheshimiwa Spika, hilo Baraza inatupasa tuombe watwambie baada ya kufutwa, inaelekeea lilishinda, BAWATA ilishinda hiyo kesi. Sasa kama BAWATA ilishinda hiyo kesi haikuruhusiwa kuendelea, lakini sasa hivi tunaona kwamba kazi zile ambazo zingekuwa zinafanywa na wanawake wote ndio zimepelekwa kwenye WAMA, kwa nini zipelekwe kwenye WAMA? (Makofii)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, hiyo WAMA ambayo mke wa Rais anatumia na pia nanihii ya Serikali, kwa nini isiwe Baraza la Wanawake ambalo litatuunganisha sisi; nyie mtakuwa UW-CCM na BAWACHA, tukawa watu wamoja, tukaunda Baraza la Wanawake wa Tanzania, badala ya kuwa na Makamisheni tu? Naomba jambo hili lichukuliwe. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, muda ni mchache, naomba nizungumzie...

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Spika, Taarifa. Kuweka sawa takwimu.

SPIKA: Muda hautoshi, naomba aendeleee. Endelea!

MHE. NAOMI A. M. KAIHULA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Baada ya kuzungumza haya naomba nizungumze kidogo kuhusu suala la watoto katika...

*(Hapa kengele ya kwanza ililia kuashiria kukaribia kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. NAOMI A. M. KAIHULA: Mheshimiwa Spika, ya kwanza?

SPIKA: Taarifa Mheshimiwa nanihii? Ya kwanza?

MHE. NAOMI A. M. KAIHULA: Mheshimiwa Spika, ya kwanza.

SPIKA: Endelea Mheshimiwa!

MHE. NAOMI A. M. KAIHULA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa hiyo, naomba hivi, sisi Tanzania tuwe na akili, nimezungumzia hapa mara nyingi kwamba, nchi ya Tanzania kama kweli inataka kuendelea kupitia Wizara yake ya Maendeleo ya Jamii, ni lazima ijipange kuwa na pesa ya kuwatunza watoto wake. Kwa ajili ya kutokuwa na pesa ya kuwatunza watoto wake ndio matokeo mengi mabaya yote haya yanatokea.

Mheshimiwa Spika, nilipendekeza kwamba, katika madini, katika rasilimali, kutengwe hata 1% ambayo iwe inakwenda katika bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kusudi iweze ku-take care ya elimu, matunzo kuanzia mtoto akiwa mimba. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, yaani wenzetu walioendelea wanaweka hiyo percent ambayo inasaidia baadaye kuwatunza watoto kuanzia akiwa mimba, afya, elimu, lishe na kila kitu. Hata wakifika umri wa miaka 18 hakuna tena kukaa na wazazi wao na kuja kuwaua kama wanavyowaua sasa hivi wakidai urithi. Wanawaambia kwamba, nenda kwa baba yako kwa sababu, zile pesa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

zilizokuwa zikiwekwa, zilizotengwa kutoka katika rasilimali ya nchi zinatumika kuwatanza na kuwapangia na kila kitu. Kwa hiyo, naomba kwamba, Bunge lako Tukufu, ni wakati mzuri sasa hivi kuiwezesha hiyo Wizara ya Maendeleo na Jinsia kusudi iweze kuwa na uwezo huo wa kutunza watoto katika vitu vingi ambavyo mwenzangu atakayekuja baadaye atavielezea. (Makof)

Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru kwa ajili ya wakati mzuri huu. Mungu awabariki na tuendelee kuwa hivi. (Makof)

SPIKA: Ahsante.

TAARIFA

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kweli, ni mara yangu ya kwanza kusimama angalau kuzungumzia haya aliyosema. Kwamba, la kwanza UWT haina hila; Umoja wa Wanawake wa Tanzania umeshiriki kukomboa nchi yetu ya Tanzania. Umoja wa Wanawake umeshiriki kudai uhuru wa Watanzania. Umoja wa Wanawake (UWT) una Katiba yake tena umesajiliwa kwa mujibu wa Sheria. Umoja huu wa Wanawake una Katiba, tofauti na Taasisi nyingine, UWT una Katiba. (Makof)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Spika, Umoja wa Wanawake wa Tanzania, hata Viti Maalum ulividai ndio maana katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hapa matokeo ya Wabunge Wanawake kutoka Vyama vyta Upinzani ni matokeo ya Jumuia ya Wanawake wa Tanzania. Maana UWT ingekuwa na hila kusingekuwa na wanawake wengi wa Upinzani. Ni UWT ndio iliamua kujinyonyoa ikasema sasa badala ya kwenda na wanawake wachache tushirikishe wanawake wengi, ili tupaze sauti moja. Sasa mtu mwenye hila anakuwaje UWT? (Makof)

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu BAWATA nimesema sio mahali pake hapa. Tudai *forum* nje tuzungumzie BAWATA ilikotoka na ilikoishia. (Makof)

SPIKA: Naomba usichangie.

Mheshimiwa Mnyika, unajua kabisa tunapoongea Taarifa mtu mmoja akimaliza na mwingine anasema, lakini ikianza kelele inakuwa sio vizuri; ingawa wengine wameniandikia barua za kipuuzi.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni Taarifa ikiombwa, Mzungumzaji anakaa ili apewe Taarifa.

SPIKA: Sasa ngoja kwanza, nitakupa ruhusa uongee.

Haya, Mheshimiwa Mnyika!

TAARIFA

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ningependa kumpa Taarifa mzungumzaji, Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), ultumikia na kuwawakilisha wanawake wote wakati wa mfumo wa Chama Kimoja cha Siasa. Hii ilikuwa kwa Jumuiya mbalimbali, ilikuwa kwa Wafanyakazi, ilikuwa kwa Vijana, na kadhalika.

Baada ya kuanza kwa mfumo wa Vyama Vingi, wanawake sasa kwenye ulingo wa kisiasa wamegawanyika kwa misingi ya Vyama mbalimbali, CUF wana Jumuiya ya Wanawake, CHADEMA wana Jumuiya ya Wanawake, TLP wana Jumuiya ya Wanawake na kadhalika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, alichokisema mzungumzaji aliyetangulia ni kwamba, pamoja na ukweli huo wa kihistoria, UWT bado inafanya hila ya kuwafanya watu waamini kwamba, ndio umoja unaowawakilisha wanawake wote Tanzania. (Makofi)

Matokeo yake UWT inakwamisha kuanzhishwa kwa Umoja wa Wanawake wote Tanzania, Baraza la Wanawake Tanzania, ilifanya jitihada za kufutwa kwa Baraza la Wanawake Tanzania. Kwa kuwa, Mahakama sasa imesema kwamba, Serikali ilivunja Sheria kwa kulifuta Baraza la Wanawake Tanzania, alichokisema mzungumzaji aliyetangulia ni kwamba, umefika wakati sasa kuanzhishwa chombo hiki na sio kwa wanawake tu, hata kwa vijana vilevile, umefika wakati wa kuwa na Baraza la Vijana Tanzania, ili kuwa na chombo cha kuwaunganisha katika maendeleo ya nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitaka kumpa Taarifa Mzungumzaji aliyetangulia.

SPIKA: Mheshimiwa Mnyika, sifa zote umetoa...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, Taarifa.
Mheshimiwa Spika, sikubaliani...

Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Naomba mkae, hakuna cha Taarifa yoyote; nani anayezungumza? Naomba mkae wote.

Hakuna mtu anayezungumza hapa, vyote mnavyosema ni kweli. Wewe ni John Mnyika, akizaliwa John Mnyika mwingine wewe utajitoa? Haiwezekani! (Kicheko)

Tunaendelea. Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza? Aah, nilisema Mheshimiwa Moza kwanza, halafu Conchesta. Mheshimiwa Moza ameondoka? Yupo, Mheshimiwa Moza kwanza, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Conchesta.

MHE. MOZA A. SAIDY: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Nashangazwa sana na malumbano ya mambo ya huko mengine.

Mheshimiwa Spika, naomba kunukuu. Wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anasoma Hotuba yake hapa Bungeni, katika ukurasa wa 28, alisema kuwa hadi kufikia Disemba, 2013, Mfuko wa Wanawake ulikuwa umetoa mikopo ya thamani ya shilingi bilioni 5.4.

Mheshimiwa Spika, lakini Hotuba ya Mheshimiwa Waziri aliyesoma leo ukurasa wa 15, alieleza kuwa, kati ya mwaka 2011/2012 na mwaka 2013/2014, Wizara imekopesha jumla ya milioni sita, kumi na mbili; je, nani mkweli kati ya Waziri kuitia Mheshimiwa Nagu ama Waziri husika? Naomba Mheshimiwa Waziri, aje anipe ufanuzi huo. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nianze na suala la pensheni. Ni dhamana ya Maendeleo ya Jamii kusimamia wazee wanapata huduma zao muhimu, lakini mpaka leo imekuwa hadithi katika nchi yetu, hasa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana hii aweze kuwaeleza umma wa Watanzania, Wizara ina mkakati gani kuhusu suala la pensheni kwa wazee mwaka huu wa 2014/2014, ili kuachana na danadana ya kuelekea Uchaguzi Mkuu badala ya kuwaacha wazee wakihangaika na maisha yao ya kila leo?

Mheshimiwa Spika, napenda kujua, hivi pensheni hii ina ugumu gani wa kuweza kusimamiwa na kuweza kupewa wazee hawa kwa muda ambao unastahili, unasogezwa muda hadi kufikia uchaguzi ambao sasa hivi tumebakiza mwaka mmoja tu? Au wazee hawa tumekuwa tunawafanya kama kivuli, hawahitaji kupata stahili zao?

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la ajira. Bado kuna wingu kubwa la ajira ya watoto; watoto wamekuwa wakitumikishwa kinyume cha taratibu na

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Sheria. Pamoja na kutumiwa watoto hawa, haki zao za msingi kwenye ajira ngumu hizo wanazikosa.

Mheshimiwa Spika, watoto wanaochukuliwa kupelekwa nje wanadanganywa hapa na Serikali inatambua kabisa kwamba, kuna wakala yupo anayepitisha watoto hawa kuwapeleka nje watoto wetu. Wanakwenda kutumikishwa kule mpaka wanafanyishwa vitendo vingine ambavyo si vya kiungwana, lakini bado hawapewi haki zao, wakifika kule wananyang'anywa na Passport zao. Sasa nataka kujua Serikali yetu inasimamia nini kuhusiana na suala hili la haki za watoto? Yule Wakala anayepitishwa watoto wetu kwa nini asisimamishwe kwa zoezi zima ambalo anapeleka watoto nje?

Mheshimiwa Spika, kuna mtoto yupo mpaka sasa hivi, alichukuliwa kutoka hapa Tanzania akapelekwa Uarabuni. Kafika kule kaenda kutumikishwa kwa mama mwengine, yule mtoto alipoona maisha magumu akahamia kwa mama mwengine. Yule mama kamchukua yule mtoto kampeleka Mahakamani na yule mtoto yuko gerezani mpaka leo. Hata hivi nilikuwa nikiomba wanieleze yuko sehemu gani, ili tuweze kumwomba Balozi anayehusika kule asaidie yule mtoto aweze kurudishwa hapa nchini Tanzania. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, watoto wetu wamekuwa katika maisha magumu sana. Tunalo wimbi kubwa sana la watoto wa mitaani. Watoto hawa pia wanahusiana pia na wazazi kuwatelekeza watoto, hususan wanaume kuwakimbia watoto, kuwakimbia wake zao, na kusababisha wimbi kubwa la watoto nyumbani kuona maisha ni magumu wanakwenda kujitolea huko nje. Sasa hii elimu pia ingeweza kutolewa kwa wanaume ili waweze kuvumilia maisha ya ugumu ndani ya nyumba zao ili waweze kulea watoto. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, wanaume ni sehemu ya pamoja ya mikakati ya Serikali katika malengo yake ikiwa kuzuia ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake, utelekezaji wa watoto, vitendo vya udhalilishaji watoto, ndoa za utotoni, ukatili dhidi ya watoto na masuala nyeti ya maendeleo ya jamii, hivyo wanaume hukutwa na changamoto. Hivyo, maendeleo ya jamii yenye usawa wa kijinsia, wanaume wakishirikishwa Taifa hili litakuwa imara.

Mheshimiwa Spika, watoto wamekuwa wakiozeshwa wakiwa katika umri mdogo. Tunalifahamu hilo hata sisi wenyewe Serikali inatambua na hilo. Watoto wengi wanaozwa kwenye umri mdogo, mtoto anaozwa chini ya miaka 15, nane na anazaa mtoto kwa mtoto, haya ni maisha ambayo kwa kweli hayastahili yanamnyima mtoto haki yake. Anakosa haki ya elimu, anakosa haki ya kuchangia na yeye pia mawazo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala lingine la ajira kwa vijana. Ajira kwa vijana wanaojajiri mambo ya bodaboda. Bodaboda hizi zimeanzishwa kwa

mikopo; wanakopeshwa vijana wetu, wanakwenda kutumikia kule, lakini wanapopata ajali hawaangaliwi, hawana stahili yoyote ya malipo yoyote, lakini hapohapo pikipiki hizi zinakuja zikiwa na *helmet* moja, *helmet* nyingine zile ni kama za kujengea nyumba. Sasa utakuta kwamba, vijana hawa wanafukuzana na Askari wanakamatwa, wanapelekwa Magerezani au wanatozwa *fine* ya 30,000/= na wakati hawana hata uwezo wa pesa hizo.

Mheshimiwa Spika, sasa suala hili lingeangaliwa upya. Wizara yangu yenye dhamana, niko kwenye Kamati hii ya Maendeleo ya Jamii, lakini iangalie tena kwa upande wa pili. Ajira, pamoja kwamba, imetolewa pendekeso kwamba, walichokuwa wakidhamini ni hizo pikipiki, lakini sasa wangedhamini na mipango mingine ambayo inawezekana, vijana hawa wakapata ajira.

Mheshimiwa Spika, nije dhidi ya ukatili wa akinamama. Akinamama wengi wanapata ukatili, wanapigwa, wananyongwa, wanauawa na kesi zinafikishwa Mahakamani na ushahidi unakuwepo. Aidha, ushahidi unaweza ukawepo wa mtoto, lakini bado unakataliwa na unakuta mshtakiwa anatoka nje; sasa hali hii ya Wanawake kufanyiwa vitendo vya ukatili itakwisha lini katika nchi yetu ya Tanzania na bado vimekuwa vikiongezeka siku hadi siku, je, Serikali yetu inasema nini kuhusiana na masuala haya? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, inasikitisha sana pia kuona wenzetu wenyе ngozi ambayo iko tofauti kuonekana kwamba, ndiye dili au uganga wa kupatia mali kwa maisha ya Watanzania wenyе akili finyu. Kwa kweli, hata hilo jambo analolifanya haliwezi kumfikisha sehemu yake. Kwa nini umma usipewe elimu ya kuwa, mwanadamu mwenzako sio chombo cha kukupatia wewe mali, sio chombo cha kupitia wewe daraja. Ningombwa elimu hii iweze kutolewa, watu hawa wawaone wenzao kama watu wa kawaida na sio kwenda kuwadhalilisha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimesikitishwa sana na mauaji yote yanayotokea ya wenzetu *albino*. Pia nasikitishwa pia na mauaji yanayotokea ya wazee wetu vikongwe, kwani ukongwe unamkuta kila mtu na ukongwe unapomfikia mtu, mtu hubadilika sura, hubadilika macho, sasa isionekane kwamba, ndio mchawi, mkafanya vitendo vya kumuua. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono. (Makofi)

SPIKA: Ahsante. Nilikuwa nimemwita Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, atafuatiwa na Mheshimiwa Maryam Msabaha.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nichangie kidogo katika Wizara hii ya Maendeleo ya Wanawake, Jinsia na Watoto.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza niunge mkono mawazo ya Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wake wa 43, hitimisho pale. Mheshimiwa Waziri ameonesha vizuri ni jinsi gani Wizara hii inavyokuwa Wizara Mtambuka na inavyopaswa kufikiriwa kwamba, kazi ya Wizara hii ni kusimamia maendeleo katika nyanja mbalimbali ikiwemo afya, kilimo pamoja na maendeleo ya kijinsia, lakini pamoja na mawazo yake mazuri, Serikali na jamii inaona kwamba, kweli Wizara hii ni Wizara ya wanawake tu na ndio maana inapuuzwa, Wizara hii inadharauliwa.

Mheshimiwa Spika, ukitaka kuona jinsi Wizara hii inavyodharauliwa, nenda ukaone Ofisi katika Mikoa, nenda ukaone Ofisi katika Wilaya, ukaone wafanyakazi wanavyofanya kazi, hawana vitendea kazi, hawana magari, yaani ukifika katika Ofisi za Maendeleo ya Jamii katika ngazi za Halmashauri katika Wilaya na katika Mikoa utaona ni jinsi gani Serikali inavyoipuza na kuidharau Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inaendelea hata katika bajeti yao. Japokuwa Kamati imesema pamoja na Kambi ya Upinzani, lakini naomba niweke msisitizo; ukiangalia katika Randama yao, ukurasa wa 20 pamoja na ukurasa wa 21, utaona ni jinsi gani Serikali inavyotoa pesa ambazo kwa kweli, zinaogopesha au wakati mwingine zinatia hofu juu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, hebu tazama Kifungu Namba 2001, Ujenzi na Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ya Wananchi. Njoo kile Kifungu Namba 2002, ambacho kinahusu Ujenzi na Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Pesa inatolewa bilioni mbili, inaidhinishwa bilioni 2.3, lakini inatolewa milioni 42 mpaka robo tatu ya mwaka. Kwa hiyo, unaweza kuona dhamira ya Serikali haieleweki katika Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata katika ujenzi na ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo wameomba milioni mia moja lakini imetolewa milioni ishirini na tano tu. Kwa hiyo, unaweza ukaona kwamba kwa kweli hii Wizara itafanyaje hizi kazi ambayo kazi yake kubwa ni kusimamia na kuhamasisha maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hata kwenye Benki ya Wanawake, tumetetea bilioni mbili ya kila mwaka mfululizo tukiwa kwenye Bunge hili, lakini unaangalia mwaka huu wamepewa miliano mia tano na kumi na tano. Sorry nianze na ule Mfuko ambao 5% ambayo inatoka kwenye Wizara. Wanatengewa bilioni mbili, lakini wamepewa milioni 15.6. Kwa hiyo, unaweza ukaona je, huu Mfuko unawezajie kusaidia wanawake kama kweli fedha kiduchu namna hii ndiyo inayotolewa. Kwenye Benki ya Wanawake hivyo hivyo inapaswa Serikali kutenga bilioni mbili kila mwaka, lakini kipindi hiki mpaka Machi imetoa milioni mia nne hamsini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unaanza kuwa na mashaka kwamba kweli, je, Serikali inadhamiria ili Benki ya Wanawake iweze kuendelea na kuweza kupeleka matawi mengine katika Mikoa mingine pamoja na shughuli zote alizosema Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wake wa 28 za kupeleka vikundi mbalimbali na kuhamasisha wanawake katika Mkoa wa Dodoma, Dar es Salaama na Mwanza, lakini siamini kama hii kazi inaweza kufanyika vizuri kama Serikali inatoa pesa kidogo namna hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba Serikali iitazame Wizara hii kama Wizara ambayo kazi yake kubwa ni kuhamasisha wananchi na ndiyo maana tunaomba Serikali iwaajiri wale Mama Maendeleo (*Social Workers*). Kama huna *Social Workers* huwezi kuwahamasisha wananchi katika ngazi ya familia. Huko nyuma walikuwepo wanakwenda nyumba hadi nyumba, wanahamasisha wananchi mambo ya afya, wanahamasisha kilimo na wale wamesomea hizi taaluma, wana taaluma za kufanya uhamasishaji, wanataaluma za kuangalia watoto. Kwa hiyo, wanaweza kwenda katika familia na kusaidia wananchi waweze kushiriki katika maendeleo na hivyo kuongeza ushiriki wa wananchi katika kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, napenda niongelee watoto wa mitaani. Watoto wa mitaani wamekuwa tishio katika nchi yetu. Ziko sababu mbalimbali zimetajwa, zimetajwa na Kambi ya Upinzani, zimetajwa na Kamati; ukatili, ukatili ndani ya familia, ufukara uliokithiri katika nchi hii. Nchi hii imejaa umaskini, labda sisi tuliokuwa hapa, tunakaa hapa katika viyoyozi labda hamwangalii ngazi ya kijiji, watu wanavyoadhirika, watu wanakosa hata hela ya mlo mmoja. Kwa hiyo, watoto wanakimbia wengine wenyewe kwa kuwa na matamanio ya kwenda mjini kupata maisha mazuri, wakifika mjini wanakuta hakuna kazi wanafanyiwa vitendo vya ajabu, wanlawitiwa, wanapewa hata magonjwa mengine.

Mheshimiwa Spika, naomba niulize Wizara mna mkakati gani mmesema mnashirikiana na wadau upo mkakati upi tuuelewe ambao unasaidia watoto hawa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ina matumizi mabaya, matumizi katika sherehe za nchi, matumizi katika ziara za Kiserikali ambazo zinakwenda misafara watu mia moja, watu sabini...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji*)

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona mdau katika Wizara hii. Nianze kabisa kwa kulaani kitendo cha Boko Haram wa Nigeria kwa kuteka wasichana mia mbili na naomba Boko Haram wawarejeshe wasichana wale na nikiwa kama mama ambaye nina uchungu na wasichana hawa basi Boko Haram mara moja wawaachie watoto wale. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, nipongeze Mashirika yote ya Dini mahali popote na Masista wote, hawa wamekuwa wadau wakubwa kabisa wa kulea watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Wamebeba mzigo mkubwa wa Serikali leo hii nataka niihoji Serikali ambayo inajjita ni Serikali sikivu, ni lini watatenga maeneo kwa sababu tuna maeneo ya kutosha, tuna rasilimali za kutosha, tutenge maeneo tuwajengee watoto wetu wanaoishi katika mazingira magumu. Sisi tukiwa kama viongozi tutenge siku kama ni siku ya Jumamosi, ni siku ya Ijumaa, siku mbili katika wiki tushiriki katika nguvu zetu kuwajengea watoto hawa vituo vya kuwalelea na shule za kusoma.

Mheshimiwa Spika, jamani Mikoa tuseme tuangalie Mikoa kama Mkoa wa Dodoma, tukija tuijangalia Dodoma, usiku nendeni pale karibu na CCM mkaangalie watoto wanavyowasha makaratasi, wanavaa viporo, wanalala na viporo, kweli Serikali hii iko wapi, kama ni Serikali sikivu, tutenge maeneo na hawa mafisadi ambaao wanakula fedha za umma, wanaofilisi Serikali, tuchukue mali zile tuhudumie watoto wa mitaani.

Mheshimiwa Spika, leo ukifika kituo cha Ubungo watu wamegeuza nyumba wanalala. Leo ukiwa kama unatoka mahali popote huko kama Ni Dubai utasikia kwenye ndege wanassema Dar es Salaam, lakini watoto hawa wamekuwa kero. Kwa kweli watoto wamekuwa kero, hii tuangalie Serikali na tuangalie Serikali tupige kelele ni namna gani wataongeza Wizara hii, Wizara hii siyo ya wanawake, Wizara hii imebeba jinsia zote.

Mheshimiwa Spika, leo hii kuna wanaume pia wananyanyaswa na wake zao, leo hii kuna wanaume wanapigwa na wake zao, leo hii kuna wanaume pia wanaachiwa watoto na wake zao, tuangalie matatizo yaliyozunguka Wizara, tuangalie kingine nataka tukomeshe hawa watu ambaao wanaanzisha NGOs kwa kupitia migongo ya watoto hawa, kwa sababu wanapiga watoto picha, wanaanzisha NGO, wanaomba pesa, wakishapata pesa zile wanajinufaisha wenyewe watoto wale hawanufaiki. Tuangalie na tubadilishe Sheria.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria wewe ni mdau wa watoto na Naibu Waziri wa sasa hivi umehamishiwa upo kwenye hii Wizara, najua pia umesoma Sheria, tuangalie zile Sheria kandamizi zote tuziondoshe, watoto wasome na wale ambaao wanalawiti watoto wasipelekwe magerezani wakatolewa, wanyongwe wafe kabisa wasirudi na wale ambaao

Nakala ya Mtandao (Online Document)

wanaharibu watoto, kuna watoto wanaharibika, watoto wanaharibika kabisa wanaharibiwa na watu wenyewe akili zao timamu na matajiri wenyewe akili zao timamu kwa ajili ya kutaka utajiri kwa kwenda kulawiti watoto, hawa pia tuwafunge na ipitishwe Sheria ya kuwanyonga.

Mheshimiwa Spika, kingine ninachotaka kusema ni wafanyabiashara ambao wanatumia wanawake, tena watoto wadogo wadogo, wanakwenda kuwachukua watoto wale wanatumia kwenye Mahotelii makubwa kama vivutio vya biashara zao, pia hili tuangalie tukomeshe.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nimesikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Wanawake na Watoto, lakini mama yangu Sophia pia hii hotuba ya Barwany kuna mambo mazuri aliyoyazungumza mle ndani, chukua uyafanyie kazi ili Wizara yako iwe na mashiko. Mama yangu usifanye Wizara hii tutaandamana mpaka kwa Rais ili Wizara hii itendewe haki na kama Spika ni mwanamke pia uangalie Wizara hii tuitendee haki. Tukiangalia humu tusitumie wanawake kwa ajili ya kutupigia kura, tuangalie wanawake hawa nao wanufaika vipi wanavyotupigia kura, tusiangularie wanawake hawa tu wakati eti tunaangalia vitu kidogo kidogo tunawatumia, tuangalie ni miradi gani ambayo tutawapa ili waepukane na mazingira magumu ambayo wanaishi.

Mheshimiwa Spika, tuangalie na wale akina baba ambao wanatupa watoto ambao wana uwezo wachukuliwe sheria nao wapate kule watoto wao, tuwaangalie wale watoto kwa sababu kuna watoto Dar es Salaam wanalala kwenye mitaro na watoto wale wanabakwa, hivyo kila siku watoto wataongezeka. Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya wote tushirikiane tuhakikishe tatizo hili la watoto wa mitaani linaondoka. Hii siyo kazi ya Serikali na wale ambao wanaona kama Wizara hii ni ya akina mama, Wizara hii siyo ya akinamama, Wizara hii imebeba jamii ambayo inatupigia kura. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, mimi niliyesimama leo hapa ni Makamu Mwenyekiti wa Wanawake Taifa (BAWACHA). Kwa hiyo, nazungumzia wanawake wote na tuangalie ni kitu gani kitatuunganisha wanawake bila kujali mambo ya siasa na tufuutilie NGO ambazo zinaanzishwa kwa ajili ya kuwanufaisha watu...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Huyu ndiye anaitwa Msabaha ana *natural idea* ya kwake, mpaka unaona anasikika vizuri masikioni. Niite na wanaume pia halafu anasema Spika aongoze maandamano kupinga. Mheshimiwa Kapteni Komba, atafuatiwa na Mheshimiwa Badwel.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Spika, naomba nichangie Wizara hii. Kwanza kabisa niiombe familia ya Marehemu Amina Ngaluma msanii mwenzangu aliyefariki siku mbili, tatu zilizopita kwamba wawe na amani Mungu alitupa na Mungu amechukua ni msanii ambaye ni maarufu sana katika nchi yetu, amefanya kazi katika vikundi mbalimbali *African Stars, Tanzania One Theatre* na vikundi vingine vya nje, Uarabuni huko, lakini Mungu amemchumua, basi jina la bwana lihimidiwe.

Mheshimiwa Spika, pili, nitoe pongezi kwa Waziri Sophia Simba na mwenzake Pindi Chana. Waziri Sophia Simba ni Waziri peke yake ambaye kwa kweli katika miaka yote niliyoishi katika Jimbo langu ni Waziri aliyetembea siku tatu mfululizo bila kuchoka kuwahimiza wanawake wa Nyasa namna gani ya kujiondoa walipo na kwenda ambako wanatakiwa waende. Mama Sophia Simba nakupongeza sana na Mungu akubariki sana na ndiyo maana hata kwenye kitabu chako cha hotuba yako picha ya kwanza inayoonekana mbele ni ya watoto kutoka Ziwa Nyasa, Mbambabay nakushukuru sana. (Makof)

Mheshimiwa Spika, nikirudi kwenye hii hotuba ya Kambi ya Upinzani, yako mambo nakubaliana nayo, lakini yako mambo mengine hayana mashiko kabisa. Anapozungumza habari ya Salma Kikwete kufanya kampeni, yule ni mjambe wa NEC wa Chama cha Mapinduzi na amezunguka nchi nzima kokinadi Chama chake, sasa hiyo dhambi iko wapi?

Mheshimiwa Spika, nawaona wengine wanazunguka na wachumba tu mchana kutwa wanazunguka na wachumba, wanakaa kwenye majukwaa na wachumba zao, wakimaliza kazi usiku burudani, hawa hamuwataji, lakini mnamtaja Salma ambaye anazunguka kama Mjumbe wa NEC nchi nzima kunadi Chama chake na kukipatia ushindi. Huo ni ufinyu kidogo wa fikra...

MJUMBE FULANI: Mtaje.

MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA: Sijui anaitwa Josephine sijui anaitwa nani sijui.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu pia katika hotuba hii imezungumwa vitu ambavyo si vya kweli. Nimpongeze sana yule mama, Mkurugenzi wa Benki ya Wanawake. Yule mama ni Simba, anajua kupigana, pamoja na kwamba Serikali haijatoa fedha nyingi kama walivyomwahidi maana bilioni mbili zilitoka mwanzoni, bilioni mbili zikafuata, baada ya pale zimefuata kidogo, baada ya pale zero zero mpaka leo lakini amejitahidi kuanzisha vituo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, amekwenda Mikoani pia siyo Dar es Salaam tu amekwenda Iringa, amekwenda Mbeya, amefika Songea na sasa hivi yuko Nyasa na ushahidi ni kwamba nyumba yangu mimi ndiyo sehemu ya Ofisi ya

Nakala ya Mtando (Online Document)

hiyo benki yao. Sasa hawa wanapozungumza kwamba hawaendi huko, ni aibu kweli! Unazungumza kitu bila utafiti, bila ya utafiti usiseme, usizungumze kabisa. Kwa hiyo, hii hotuba sijui kama ina mashiko. (Makof)

Mheshimiwa Spika, la pili, nikushukuru sana Mkurugenzi wa Benki ya Wanawake na leo hii ninapozungumza vijana mia moja hamsini wanajaza fomu za kupata mikopo ya pikipiki pale Nyasa, pale Mbambabay, hii ni kwa ajili ya juhudhi ya yule mama Chacha. Kwa hiyo, mama Chacha kama upo hapa ndani, kama upo nje nakushukuru sana. Baada ya hizi pikipiki mia moja hamsini, tutakuumba na nyingine tena mia moja hamsini ili vijana wote wafanye kazi wasikae vijiweni.

Mheshimiwa Spika, fedha wanazopata ni kidogo, naomba Serikali ijitahidi iweze kumwongezea fedha hizo ambazo Mheshimiwa Rais aliahidi mwenyewe kwamba kila mwaka watapewa bilioni mbili. Kwa hiyo, naomba miaka ile ambayo tayari imepita na hawajapata bilioni mbili wapewe, kwa kuwa ili iendeshwe kama benki na ijitegemee, lazima iwe na mtaji usiopungua bilioni kumi na tano sasa bilioni kumi na tano siyo mchezo. Kwa hiyo, naomba Serikali itimize ahadi yake. (Makof)

Mheshimiwa Spika, tatu, ni Halmashauri ile asilimia tano, kwa kweli kama Halmashauri zote zingetumia asilimia tano kuwapa akinamama, hakika wanawake hawahitaji mikopo mikubwa sana, ukimpa laki mbili atatengeneza milioni mbili baada ya miezi miwili, miezi mitatu, siyo kama sisi, maana hafikirii akimaliza pale akanywe pombe, anafikiria akimaliza pale akafanye kazi nyingine, tofauti ukimpa Komba akimaliza pale anafikiria kwenda kunywa pombe, kwenda kwenye mchepuko pengine, lakini akinamama hawaendi hivyo, akina mama wanaendeleza familia, ndiyo maana wanasema ukimwendeleza mwanamke, unaendeleza familia nzima na ukimwendeleza mwanamme unaendeleza mtu mmoja. Wanawake si mara nyingi kwenda kwenye michepuko. (Kicheko)

Mheshimiwa Spika, namba nne, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, kwa kweli naomba Serikali iangalie. Hakuna Chuo hata kimoja chenye gari la uhakika na vyuo hivi vingi vinaongozwa na akinamama, unawaonea huruma kabisa. Sasa Serikali nimeambiwa pale bandarini yako magari karibu mia tatu yaliyotaifishwa kwa ajili ya watu kukosa kulipa ushuru, basi kama magari mia tatu yale sehemu yake pelekeni kwenye vyuo hivi vya Maendeleo ya Wananchi vinavyoongozwa na akinamama ili maendeleo yafike sana kule vijijini.

Mheshimiwa Spika, halafu kuhusu ngoma. Ni kweli kuna ngoma kibaokata, sunsumia na zingine zingine. Zamani kwa mfano kibaokata ilikuwa inachezwa na akinamama, lakini leo akinamama sasa na mimi narudi kwenu, mnachukua vijana wadogo wadogo wa kiume, mnawafunga shanga,

Nakala ya Mtandao (Online Document)

mnawakatishakatisha vibaokata kule, ndiyo maana mashoga sasa wako wengi sana katika nchi yetu, acheni mchezo huu akinamama wakuchukua vijana wa kiume kuwachezesha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA: Aaaa! Ya kwanza hiyo au ya pili?

SPIKA: Ya pili hiyo.

MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (Makofii)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Omary Badwel, atafuatiwa na Mheshimiwa Rosweeter Kasikila!

MHE. OMARY A. BADWEL: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Spika, wengi tunafahamu namna ambavyo kina mama mbalimbali kule vijijini na mijini jinsi walivyokuwa na jitihada mbalimbali za kujiletea maendeleo ya kiuchumu, lakini akinamama wengi wanakwaza na utaratibu usiokuwepo wa mikopo ya kutosha. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nataka nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa hatua yake ya kuanzisha benki ya wanawake Tanzania. Ni mpango mzuri na sisi tunaupongeza, lakini wasiwasi wangu mkubwa kwamba benki hii imejikita sana mijini, sisi Wabunge wenye Majimbo ambayo asilimia mia moja ni vijijini tunaona tutachelewa sana kupata manufaa ya Benki hii ya Wanawake. Nitolee mfano sasa hii benki imeanza kujitanua hapa Dodoma imefungua vituo vyta kuwezesha akinamama kukopa na kupata ushauri wa ujasiriamali, lakini kati ya vituo kumi na moja vilivyofunguliwa Dodoma vyote viro hapa Dodoma mjini na Bahi iko hapa jirani, Kondoa iko hapa jirani, kwa nini vituo vyote hivi kumi na moja viende vikakae hapa Dodoma Mjini? (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wakati Mheshimiwa Waziri anajibu hoja hii, naomba aniambie ni vituo vingapi atapunguza hapa Dodoma Mjini ili apeleke Bahi angalau na wale akinamama wa Bahi waweze kufaidika na Benki hii ya Wanawake ambayo sasa imesogea hapa Dodoma na wamepeleka Kongwa, wamepeleka Mpwapwa, lakini Bahi naona haijafika.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili ni habari ya fedha ambazo zinatengwa na Halmashauri asilimia tano kwa wanawake na asilimia tano kwa vijana. Kama Halmashauri zetu zingekuwa serious kwa miaka mingi ambazo fedha hizi zimetengwa kwa mujibu wa Sheria, leo Halmashauri zingekuwa mbali sana katika kusaidia akinamama na vijana, lakini kwa kweli fedha hizi hazitengwi, Halmashauri zimesahau kabisa jambo hili. Nataka kujua Wizara inasema nini juu ya jambo hili? Sisi Wabunge tumepeiga kelele sana kule kwenye Wilaya zetu, lakini ni danadana na hata hizi fedha zikitengwa, upelekaji wake kwa akinamama ni mgumu sana, kumekuwa na urasimu mkubwa, kumekuwa na michakato mingi ambayo inamfanya mama huyu wa kijiji akate tamaa na asiweze kwenda kuukaribia huu mkopo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nione Wizara hapa inasema nini na pia katika kurahisisha kabisa suala la mikopo hii asilimia kumi kwa vijana na wanawake katika Halmashauri zetu. Ni lazima Wizara iwe na maneno ya kusema na kusimamia kikamilifu. Wakurugenzi na viongozi wengi wa Halmashauri wao wako katika miradi mikubwa mikubwa miradi ya maji, miradi ya barabara, miradi ya ujenzi, lakini miradi hii ya akinamama na vijana ya kuwaendeleza kiuchumi wameisahau na hapo hapo wanawadai wananchi kuchangia michango mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hivi utamchangishaje mwananchi kujenga Sekondari wakati hujamwezesha kiuchumi? Lakini leo Halmashauri zingekuwa makini, zingetoa hizi fedha akinamama na akinababa au vijana wangekopa, wangekuwa na uwezo mkubwa sasa wa kufanya kazi mbalimbali za kiuchumi na hata unapokwenda wala hakuchukii na anaweza kukupa mchango wake.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nichukue nafasi hii kutoa pongezi kwa zile NGOs ambazo kwa kweli zinafanya kazi nzuri ya kusaidia utoaji wa huduma kwa wananchi wetu mbalimbali. NGOs nydingi zimejitahidi sana, zinafanya kazi nzuri na zimechukua sehemu kubwa ya wajibu ambaeo ulikuwa ufanywe na Serikali, lakini wameendelea kuzifanya wao. Bahati nzuri mimi nimefanya kazi sana na NGO, watu mle ndani wako serious, wako busy, wako makini na wanatafuta fedha, wengi wao wanatafuta fedha kwa ajili ya kusaidia matatizo mbalimbali ya wananchi wanaowazunguka. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, niwapongeze wote kwa kweli na kwa kiwango kikubwa, nichukue nafasi kuipongeza NGO ya AFNET ambayo inafanya kazi karibu Mikoa nane katika nchi yetu na wanafanya kazi kubwa ya mapambano dhidi ya ukeketaji wa wasichana na watoto wa kike na wanawake. (Makofij)

Nampongeza sana Mkurugenzi wa NGO hii, Mama Sara Mwaga na timu yake kwa kufanya kazi nzuri iliyotukuka. Nami nafikiri ifike mahali lazima tuwe

Nakala ya Mtandao (Online Document)

tunatambua hizi juhudi za Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali, yanayofanya vizuri lazima tuyatambue na tufike mahali tuwe tunayapongeza. (Makofi)

Tunapongeza vitu mbalimbali, tunapongeza wafanyakazi bora, tunapongeza watu mbalimbali lakini tumesahau pia kujua kwamba hizi NGOs zinafanya kazi kubwa ya kusaidia kupambana na mambo mbalimbali ya kijamii katika maeneo yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kamati zile za UKIMWI zinafanya kazi kwenye Halmashauri zetu chini ya maendeleo ya Idara ya Jamii ambayo iko chini Wizara hii, nilikuwa na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, Kamati zile zinafanya kazi moja tu ya UKIMWI katika maeneo yale ya Wilaya, Kata na Vijiji, lakini tunasahau pia madawa ya kulevy ya yanayohusiana na bangi na mirungi ambayo pia imekuwa ni kikwazo kikubwa kwa vijana wetu. (Makofi)

Sasa nilidhani hizi Kamati ziongezewe jukumu; kama tulivyoshauri kwenye Kamati yetu ya UKIMWI kwamba ziongezewe jukumu pamoja na masuala ya UKIMWI, lakini pia ishughulike na masuala ya madawa ya kulevy ya hususan bangi. Serikali imekazania *heroin*, *cocaine*, madawa makubwa makubwa, wafanyabiashara wakubwa wakubwa, imesahau kwamba vijana wetu wanateketea kwenye Vijiji vyetu na Miji yetu kwa bangi na mirungi. (Makofi)

Kwa hiyo, lazima jambo hili, hata kama Kamati zile haizuisiki katika kukamata lakini zihusike katika uhamasishaji, upokeaji wa taarifa ili kuweza kujua hali halisi ya madawa ya kulevy katika maeneo hayo, kwa sababu maendeleo ya jamii hayawezi kuja kama vijana wakati mwingi wanafikiri kuvuta bangi au kutumia mirungi ndiyo sehemu ya maisha yao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti wangu wa Kamati aliwahi kuzungumza vizuri habari ya viroba. Viroba vinapunguza nguvu kubwa ya vijana wetu kufanya kazi. Leo hii mwanafunzi anakwenda na kiroba mfukoni, mkulima anakwenda na kiroba mfukoni, fundi seremala anakwenda na kiroba mfukoni; yote hii ni kwa sababu viroba vinauzwa holela. Maduka ya kuuza pipi, maduka ya kuuza nyanya yote yanauza viroba. Kila mahali panauza kiroba.

Hivi Serikali inasema nini juu ya jambo hili? Hatuwatakii mema vijana wetu kwa sababu wameona njia rahisi ni kiroba kimoja, amepata nishai, ndiyo anafikiri anaweza kufanya kazi akiwa ameshapata kiroba kimoja. (Makofi)

Kwa hiyo, nadhani Serikali ipige marufuku uuzaaji holela wa viroba; na hii itawasaidia sana vijana na akina mama kwenda kufanya kazi zao wakiwa na akili timamu, kuliko kuacha kama ambavyo ilikuwa. (Makofi)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. (Makof)

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita na Mheshimiwa Kasikila, atafuati*iiwa* na Mheshimiwa Modestus Kilufi.

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA: Mheshimiwa Spika, nami pia natoa shukrani zangu nyingi kwa kupata hii nafasi ili niweze kuchangia haya machache kwenye hii Wizara ya Maendeleo ya Jamii.

Kwanza, niipongeze Wizara ya Maendeleo ya Jamii kwamba katika maombi yao ya Shilingi bilioni 30.2 wameweza kutenga fedha za maendeleo Shilingi bilioni tisa lakini fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo, Shilingi bilioni nane, kinyume na Wizara nyingine ambazo utakuta matumizi mengineyo hela ni nyingi zaidi kuliko za maendeleo. Hongereni sana. (Makof)

Pia wameweza kufikiria fedha za ndani ni Shilingi bilioni saba lakini za nje Shilingi billioni mbili tu, tofauti na wengine ambao huwa wanategemea zaidi fedha za nje ambazo mara nyingi hazifiki.

Mheshimiwa Spika, sasa nzungumzie kwamba katika hizo fedha za maendeleo zinazoombwu, Shilingi bilioni tisa, nilikuwa nasisitiza kwamba zile five percent za vijana na five percent zinazotengwa kwa ajili ya wanawake, ziweze kufikishwa kwenye Halmashauri. Wakurugenzi, pesa hizi zitakapokuwa zimefika, wazitangaze! Zisiwe ni za kuhamisha na kutumia kwenye matumizi mengine halafu wahusika wanakuwa hawazipati. Zitangazwe na waelimishwe; ndiyo kazi za Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri zetu; kuwaelimisha wananchi kwamba pesa zipo na zitatumikaje.

Kama nilivyoongea *last time* kwamba pesa zipo, kama wanafikiriwa kupewa, wapewe kwanza mafunzo, kwa sababu kama watapewa pesa hizi bila mafunzo ndiyo utakuta wanunu magauni na kaptula tu. (Makof)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie kidogo kuhusu Benki ya Wanawake. Benki ya Wanawake naendelea kupongeza kwamba inatanua katika Mikoa mingine. Lakini mwaka uliopita niliomba kwamba Tawi Mkoo wa Rukwa lifunguliwe, ikichukuliwa kwamba Mkoo wa Rukwa ni Mkoo ulio pembezoni.

Mwaka 2013 niliomba kwamba mwaka huu na sisi Rukwa tuweze kufikiriwa. Lakini katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 28 imeandikwa, Vituo 29 ambavyo vimefunguliwa na vitanufaika na mkopo huu. Vituo hivi viko katika Mkoo wa Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena nipeleke ombi langu, kwamba basi kwa sababu Rukwa haikufikiriwa tena kupelekewa Tawi mwaka

Nakala ya Mtandao (Online Document)

huu, naomba mwakani 2015/2016 Tawi Mkoa wa Rukwa liweze kufunguliwa ili Wilaya ya Nkasi, Sumbawanga Vijiji, Sumbawanga Manispaa na Kalambo, ziweze kunufaika ili wale wanawake wanufaika na mikopo inayotokana na Tawi hili la Benki ili waweze kujinufaisha katika ujasiriamali na kuinua kipato chao. Wasiwe ni tegemezi kwa akina baba tu mpaka hata vitambaa vya kufunga kichwani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba hilo liweze kutekelezwa ili tuweze kufikiriwa na sisi Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, nzungumzie kuhusu elimu ya afya ya uzazi. Elimu ya Afya ya Uzazi, sielewi Serikali ina mpango gani thabiti wa kutoa elimu ya afya ya uzazi mashulenii, ili kuzuia mimba za utotoni zisizotakiwa. Kwa sababu mimba hizi ndiyo tunaona zinapelekea hata wanafunzi wasichana kusitisha masomo yao, pia zinapelekea sana utoaji wa mimba kiholela na kusababisha vifo kwa wingi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa tunazungumzia habari za *fivey fifty*. Lakini *fivey fifty* itakuwa ni ndoto endapo hatutadhibiti mimba za wasichana mashulenii na ikapelekea *dropout* kwa wingi sana. Itafika mahali Serikali inawatafuta wasichana wa kuingia kwenye *fivey fifty* lakini hawapo kwa sababu hawakusoma. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie kidogo ugatuaji wa madaraka kwa wananchi, ambalo ni sera nzuri na imekuwa ni jambo zuri sana. Tumekuwa tukishirikisha wananchi katika kutambua matatizo na fursa zilizoko kwenye maeneo yao EO and OD.

Sasa Vijiji na Kata na Halmashauri wanapoleta mipango na ikaletwa hapa bajeti na tukapitisha bajeti, pesa zinaporudi Halmashauri, tunaomba hata Kata nazo zipelekewe pesa ambazo zilikuwa zimetengwa kwenye mipango yao ya Kata, lakini kwenye mipango yao ya Vijiji ili wananchi wale waweze kutekeleza ile mipango ambayo walikuwa wameombea pesa hiso. Katika utekelezaji isiwe ni ngazi ya Halmashauri tu inayotekeliza, pia wananchi washirikishwe. Isiwe wananchi wanashirikishwa tu kwenye kutambua matatizo na fursa, lakini washirikishwe katika utekelezaji na hata katika ufuatiliaji, katika tathmini ili mwaka mwingine unaofuatia wajue ni wapi walipokosea waweze kutengeneza vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni kilio cha muda mrefu, wananchi wanashirikishwa kutafuta matatizo na kupanga lakini hawaonyeshwi hata pesa. Zile pesa zinaporudi huko ziwekwe kwenye mbao za matangazo ili wananchi wajue kile walichokiomba wamepewa chote au hawakupewa chote, au hawakupewa kabisa. (Makofi)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni kilio cha wananchi kwamba miradi wanayokuwa wameipanga au wameitambua inakuwa haitekelezwi na ukiuliza Serikali, inasema fedha hazikutosha. Mimi nilikuwa naona sasa tuchukue utaratibu mzuri wa kuboresha makusanyo ili Hazina iweze kupata fedha za kutosha na ili iweze kupeleka kwenye Halmashauri au kwenye Wizara husika kadri walivyokuwa wameomba. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, yangu machache ni hayo, naomba yachukuliwe na Wizara, lakini nauna mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. (Makofii)

SPIKA: Ahsante. Naomba nitambue kwanza wageni. Nilikuwa nimepanga baada ya kusema Wenyevitii niwatambue, nikawa nimepitiiwa. Kwa hiyo, naomba niwatambue wageni. Kwanza, wako wageni wa Mheshimiwa Sophia Simba, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ambao ni Wakuu wa Taasisi zake katika Ofisi yake, wanaongozwa na Mheshimiwa Anna Mayembe, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo. (Makofii)

Pia kuna wanafunzi 10 kutoka Chuo Kikuu Dodoma, wakiongozwa na Bi. Lucy Rutainura, na hawa naomba wasimame wote kama wapo. Okay, wako huku na huku, wamesambaa. Halafu kuna wanachuo wengine 31 kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe wakiongozwa na Spika wa Bunge la Chuo Kikuu cha Mzumbe. Huyo Spika kwanza asimame peke, yuko wapi huyo Spika? Ehe! Wengine wasimame sasa. Ahsante sana, wote ni akina mama. Tunaomba msome vizuri. Haya wanayosimulia Waheshimiwa Wabunge, ninyi msome kwani ndio ukombozi wetu sisi. Huyu Spika, anaitwa Mwashibanda Shibada. Ahsante sana, hongera Mheshimiwa Spika. (Makofii)

Tuna viongozi wawili kutoka UWT Morogoro, sijui wako wapi! Kuna viongozi wengine watano kutoka UWT Dodoma, naomba wasimame walipo. Halafu kuna wanafunzi 25 wa Chuo cha Ufundii cha Don Bosco Dodoma, wasimame walipo; ahsante sana, karibuni sana.

Halafu tuna wanafunzi wengine 150 kutoka Chuo cha Maendeleo ya Jamii, TRACDI. Naomba wasimame hawa, Maafisa wa Maendeleo ya Jamii. Ah, kweli, Wizara yenu! Hongera sana, mwendelee vizuri. Ahsante. (Makofii)

Kuna wanafunzi wengine 55 kutoka Chuo Kikuu cha St. John, naomba pia wasimame hapo walipo kama wamefika. Ahsanteni sana, karibuni sana. Tunaomba wanafunzi wote fanyeni kazi ya kusoma, mnaona tatizo letu ni watu wetu kusoma na tutaweza kuendesha mambo yetu vizuri kama nyie mnasoma vizuri. Ahsante sana. Niendelee na Mheshimiwa Modestus Kilufi. (Makofii)

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Spika,...

SPIKA: Samahani kidogo Mheshimiwa Kilufi.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niweke taarifa sawa kutokana na mchangiaji aliyejita, anasema kwamba *five percent* kwa ajili ya vijana na wanawake zinakuwa zinatoka Serikalini. Nataka niweke sawa hii taarifa kwamba *five percent* kwa ajili ya wanawake, *five percent* kwa ajili ya vijana inatoka kutokana na mapato ya ndani ya Halmashauri. *From own source* ya Halmashauri zetu. Ni wajibu wetu kama Madiwani kuhakikisha fedha zile zinatumika kama zinavyopaswa.

Kwa upande wa Serikali kinachotoka ni mchango wao wa Serikali ambapo Wizara hii ya Jinsia Wanawake na Watoto ilikuwa inatoa Shilingi milioni nane kipindi kilichopita. Baada ya kukaa na Kamati yetu ya LAAC tukakubaliana, sasa hivi wamepandisha mpaka Shilingi milioni 12. Hizo ndizo ambazo zinatoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, naomba niweke sawa katika hili. (*Makofii*)

SPIKA: Sasa lazima ueleze we nani, maana yake...

MBUNGE FULANI: Taarifa.

SPIKA: Si ujieleze, wewe nani?

SPIKA: Mimi sitaki taarifa. Mheshimiwa Rajab, jieleze wewe ni nani?

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge inashughulikia Hesabu za Serikali za Mitaa. (*Makofii*)

MHE. SYLVESTER M. MABUMBA: Taarifa Mheshimiwa Spika.

SPIKA: Mheshimiwa Mabumba.

MHE. SYLVESTER M. MABUMBA: Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa msemaji aliyejita. Maelekezo ya kutenga asilimia kumi yameelekezwa na Kamati yako ya TAMISEMI, siyo LAAC.

SPIKA: Sasa ngojeni kwanza tuelezane hapo, msianze kubishania vitu vidogo sana. maelekezo ya kwamba zile asilimia ziwekwe, ni ya siku nyingi sana. Aliyefanya hivyo, alikuwa Mama Anna Abdallah, wakati huo alikuwa Waziri wa TAMISEMI, isipokuwa utekelezaji wake ulikuwa haufanyiki vizuri. Sasa TAMISEMI ndiyo wanaongoza sekta; LAAC ndiyo wanaokagua hesabu. Kwa hiyo, wote mko sawa. (*Makofii*)

Tunaendelea. Mheshimiwa Kilufi, naomba uendelee na hotuba yako.

MHE. MODESTUS D. KILIFI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Naomba vilevile nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Ofisi ya Waziri Mkuu na TAMISEMI kwa kusitisha ushuru haramu uliokuwa unatolewa kwa wakulima wanaorudisha mazao yao kutoka shambani Wilayani Mbarali na mahali pengine; kwamba kama wanafanya hivyo waache mara moja na mageti yaliyomo ndani ya Wilaya yaliyotapakaa kila sehemu yaachwe bila kuwabungudhi wakulima, ushuru ni kwa wafanyabiashara na siyo kwa wakulima wanaorudisha mazao kutoka shambani. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niipongeze sana Wizara hii kwa jitihada nyingi ambazo wamekuwa wakifanya ili kuhakikisha kwamba huduma za jamii zinakwenda vizuri kwa akinamama na watoto. Lakini bajeti ya mwaka 2013/2014 ilikuwa ni Shilingi bilioni 25, lakini ukiangalia kwenye kutolewa, wamepewa hizi fedha kidogo sana ukilinganisha na mahitaji halisi ya Wizara hii. Ombi langu ni kwamba sasa Serikali ione umuhimu kutoa fedha za kutosha kwa Wizara hii ambayo ni kiungo muhimu kwa kuendeleza jamii ya Watanzania ili iweze kutimiza majukumu yake sawasawa.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka 2013/2014 wamepewa Shilingi bilioni 30. Fedha hizi kwa majukumu iliyonayo hazitoshi. Vilevile Halmashauri zinatakiwa zitoe asilimia 10, kwa maana asilimia tano kwa ajili ya vijana na asilimia tano kwa ajili ya akina mama, lakini hizi fedha zimekuwa hazitolewi kwa wakati. Halmashauri mara nyingi zimekuwa zikitoa fedha hizi lakini siyo kwa kupenda. Nini kinachofanya wasitenge? Nashauri, Mheshimiwa Waziri fuatilia ili kuhakikisha akina mama hawa ambao wanategemea sana fedha hizi kwa ajili ya biashara ndogo ndogo ili waweze kuinua vipato vyao waweze kulitumikia Taifa na kutunza watoto.

Mheshimiwa Spika, Azimio la Bunge la 993 (17) sehemu ya (1) cha sheria namba 21 ya mwaka 1961 kinahalalisha uhalali wa Wizara hii kusimamia vizuri majukumu yake kwa ajili ya ustawi wa Watanzania. Suala la Halmashauri kusaidia vikundi vyta akina mama na vijana siyo suala la hiari. Tumeshuhudia vijana ambao tumesema wajijiri, kwa maana ya kuendesha biashara ya boda boda, lakini boda boda hizi nyingi siyo za kwao ni za matajiri. Sasa kupitia Wizara hii, tunategemea hawa vijana hizi fedha zitolewe na Halmashauri ili waunde vikundi waweze kukopeshwa waendeshe biashara hii kwa maana ya faida yao wenyewe na siyo kutumikia matajiri. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nashawishika kushauri Wizara ijithidi kuhakikisha kwamba inasimamia vizuri mapato haya yanayotokana na mifuko ya vyanzo vyta Halmashauri ili kusudi fedha hizi ziweze kutolewa kwa vijana.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Vilevile Wizara ifanye jitihada kuhakikisha kwamba vijana wanaunda vikundi kushirikiana na wataalam walioko kwenye Halmashauri ili waweze kupewa utaratibu mzuri wa namna wa kupata mikopo hii kwa sababu wengi hawalewi wanapataje hiyo mikopo kutoka Halmashauri kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inalojukumu kubwa; wapo watoto yatima, wapo watoto wa Mitaani ambao wengine ni yatima hao hao; lakini wapo wajane wasio na uwezo, wapo wazee na wastaa fu ambao kwa kweli wanaendelea kuhangainika kwa kupata fedha hizi kwa shida sana na wakati mwengine kwa kiwango ambacho sasa kimepitwa na wakati; wapo walemavu; wote hawa ni haki yao katika Taifa hili; wana haki ya kuishi na kuenziwa na Serikali yao tukufu.

Mheshimiwa Spika, haifurahishi na haipendezi kuona watoto wa Mitaani wameachwa hivi hivi bila kuchukua hatua za kuhakikisha kwamba watoto hawa wanapewa utaratibu mzuri na kuishi kama Watanzania wengine wanavyoishi. Ni dhambi kuona watoto wa Mitaani wanaachwa bila kuangaliwa. Nilikuwa namshauri Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii afanye utaratibu wa kutambua watoto hawa bila kuziachia Halmashauri peke yake jukumu hili limekuwa ni kubwa, sasa hivi hawa watu wameongezeka kutokana na matatizo mbalimbali ambayo yamekuwa yakijitokeza nchini hasa ukizingatia maradhi haya ambayo yanaendelea kutuandama wananchi.

Mheshimiwa Spika, vilevile nawashukuru sana wote wanaojitoa kwa ajili ya kusaidia watoto, vijana na walemavu na hasa Mheshimiwa Rais kwa jitihada ambazo amekuwa akizifanya; vilevile Mheshimiwa Mama Salima Kikwete kwa kuitia Taasisi ya UWAMA ambaye na ye ye amekuwa akionyesha mfano mzuri wa kuigwa katika kuona umuhimu wa kuwaenzi hao watoto ambao wengi wamekuwa hawana mwelekeo.

Vilevile nawashukuru baadhi ya watu wenye mapenzi mema kama Mheshimiwa Reginald Mengi, mara nyingi tumeshuhudia akiwaenzi watoto hawa na walemavu kwa pamoja angalau kuwapa matumaini ya kwamba na wao wana haki ya kuishi kama watu wengi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto inayo...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante.

MHE. MODESTUS D. KILIFI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Muda hautoshi, naunga mkono hoja.

SPIKA: Nilitangaza kwamba kuna wanafunzi wa Chuo cha Don Bosco, naambiwa siyo wanafunzi, wao ni Wakufunzi, yaani Walimu na Wafanyakazi. Lakini karibuni na ahsanteni.

Sasa namwita Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, atafuatiwa na Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi.

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza, nakupongeza kwa kuleta ombi na kuweza kukubaliwa kuchangia sasa hizi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuleta agizo kuwa Halmashauri zichangie fedha kwa ajili ya kuendeleza wanawake. Jambo hilo ni zuri sana, lakini pia nataka kumwuliza Waziri, hizi rasilimali fedha atazipata wapi za kuendeleza wanawake hao? Kwani ukizingatia katika Halmashauri wanakusanya asilimia 35 tu. Kwa hiyo, namwomba Waziri kabla ya kutoa agizo ahakikishe kwanza hizi pesa zinapatikana wapi.

Pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuwa yuko karibu sana na Taasisi za kijamii, lakini naziomba na hizi Taasisi za Kijamii ziweze kuwa wazi hasa ukizingatia wako wengi Vijijiini wanasaidia wavuvi, wanasaidia wakulima, vitoe mapato yao kwa uhakika ili waweze kutengenezewa program Kitaifa, Kimkoa na Kiwilaya.

Mheshimiwa Spika, ni kweli mikopo mingi imetoka, lakini ukitazama Vijijiini haijaenda mikopo mingi, tukiacha mbali hiyo VICOBA. Mheshimiwa Waziri anaweza kuniambia mifuko mingapi ya mikopo iliyokwenda Vijijiini na wanawake wangapi ambao wamefaidika na hiyo mikopo?

Mheshimiwa Spika, kabla muda wangu haujawkisha naanza kusema kuhusu gazeti la leo la Uhuru. Gazeti la Uhuru, leo limemnukuu Mheshimiwa Nape Nnawiye akisema kuwa UKAWA ni sawa na Boko Haramu. Hii ni kauli chafu na ya uchochezi, haikubaliki na ninailaani kwa nguvu zangu zote. (Makof)

Mheshimiwa Spika, sijui hasa amefikiria nini kuifananisha UKAWA na Boko Haramu. Boko Haramu inawatesa wanawake; sasa hivi walishachukua wanawake mia mbili na zaidi huko Nigeria wamewapeleka mafichoni, wazee wao wako kwenye shida hawajui watoto wao watakula nini, wala wanalala vipi. Leo hii Nape Nnawiye amethubutu kusema kuwa UKAWA ni sawa na Boko Haramu!

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, nikiendelea kidogo, nitachangia kuhusu watoto wa Mitaani. Ni kweli Serikali inafanya jitihada, lakini bado ukiangalia unapofanya jitihada ya kuondoa tatizo hilo, huwa inapungua. Lakini idadi ya watoto wa Mitaani inakuwa imezidi. Ukitazama Dar es Salaam ni watoto 3,000, sasa wamefika mpaka watoto 7,000 Mitaani wanahangaika hovyo. Najua kwa kuwa mnafanya jitihada zenu kwa kupitia kila Halmashauri na kuandikisha na kuwarejesha kwa wazee wao na bado wanarudi, lakini nawambieni Serikali msichoke, hawa ni watoto wetu tutampelekea nani kama hatujawalea sisi wenyewe? Kwa hiyo, namwomba Waziri asichoke, maana nasikia Serikali imeshachoka, haijui la kufanya. Msichoke, mwendelee, kwa hili. Sijasema mmechoka kabisa; kwa hili mmechoka! Kwa hiyo, nawaomba mwendelee kuondoa tatizo hili la watoto wa Mitaani.

Mheshimiwa Spika, kidogo nizungumzie suala la ukeketaji. Juhudi zinafanywa na Serikali najua na Taasisi mbalimbali zinatoa elimu, lakini na sisi wanawake tuijunge pamoja tukiwa humu Bungeni na walioko nje tutoe elimu ya kutosha ili tatizo hili lisizidi kuendelea. Maana inasemekana takwimu za mwaka 2012 na mwaka 2013 katika watu walioketwa ni wengi wa mwaka 2013 kuliko wa mwaka 2012. Kwa hiyo, natoa wito kwa wanawake wote na wanaume wote wasishurutishwe kuoa wanawake walioketwa. Nao wawe mstari wa mbele kupita vita ukeketaji wa wanawake.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (Makofi)

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Tauhida Gallos Nyimbo, atafuatiwa na Mheshimiwa Fatuma Mikidadi.

MHE. TAUHIDA C. G. NYIMBO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia Wizara hii. Nichukue fursa hii kwanza kuwapongeza Mawaziri wote wawili kwa kazi na jitihada zao nzuri wanazozifanya katika Wizara hii. Tunashukuru kwa sababu wanajua wajibu wao kama wanawake na wanajua wajibu kama walezi. Kwa hiyo, tunaona jitihada zao katika kazi wanazozifanya.

Pia, nichukue fursa hii ya pekee kumshukuru na kumpongeza Mama Salma Kikwete kwa kazi nzuri anazozifanya katika Taifa letu la Tanzania. Ni mwanamke wa kupigiwa mfano, ni mwanamke anayestahili sifa, ni mwanamke wa kuwa gumzo katika Wanawake wenzake. Sisi tukiwa kama wanawake, tukiwa kama vijana hatuna jinsi, tunampongeza; kazi zake zinaonekana na za kuigwa.

Sisi kama wanawake tunachukua fursa hii kumpongeza. Tunajua sababu za watu kupiga kelele ni nini. Lakini Mama tunamtaka aendelee, afanye kazi. Taifa linajua na sisi vijana tunajua kama Mama Salma Kikwete anafanya kazi na

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kazi inaonekana. Wapo Viongozi wengi na wana wake zao lakini hatuwezi kumtolea mfano kwa kazi anazozifanya. Yeye anastahili sifa mionganoni mwetu kati ya wanawake wanaostahili sifa katika kazi wanazozifanya. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, nazungumza hili nikiwa kama shahidi. Niko ndani ya Kamati ya LAAC, tunapopita katika Ukaguzi katika Kamati yetu, tunakuta kazi zinazofanywa na Mama Salma. Tumekuta katika hospitali zinazofanya kazi, misaada anayopeleka Mama Salma kwa ajili ya wanawake ambao wanaokwenda kujifungua, lakini ukiacha hayo, tunaona vifaa mbalimbali kila leo akiwasaidia wanawake wenzetu katika hali ngumu walizokuwa nazo hasa Vijijini.

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze katika suala zima la pensheni ya Wazee katika Taifa letu. Mheshimiwa Waziri nakuomba, ukiwa kama mama suala hili limekuwa tatizo, lakini najua kwa sababu ya hali yetu iliyokuwepo ndani ya Tanzania. Naamini Serikali ina mikakati mizuri ya kujipanga juu ya suala zima la pensheni lakini bado hatujafikia, lakini naamini tuko katika maandalizi.

Namwomba Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, tuchukue mikakati ya makusudi katika kulinda wazee katika Taifa letu, hususan tuangalie wanawake wanaopata taabu katika Taifa letu. Nadhani tukiwa na mipango ya kutengeneza kila Halmashauri tukawa na nyumba ya kulelea Wazee, hususan wazee wanawake wanaokosa malezi na matunzo, kuna wazee bahati mbaya hawakujaliwa kupata watoto, kuna wanawake hawakujaliwa kuwa na watoto; wanapata shida na wananyanyasika na wengi wao ndiyo ambao tunawasikia wanaokufa.

Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri tunaomba katika mikakati yote wanayopanga mizuri, lakini hili walichukue walifanye kwa kuweka kipaumbele. Naamini hatutoshindwa kwa sababu tuna Halmashauri ya kutosha, Serikali ina mikakati mizuri na ninaamini tukiliingiza katika mikakati yetu, hili suala zima la kuweka nyumba za kulelea Wazee litafanikiwa.

Nichukue mfano kwa upande wa Zanzibar, Mheshimiwa Waziri mna wakati mzuri wa kuenda kuangalia Zanzibar. Zanzibar kuna nyumba za kulelea wazee. Wazee waliokuwa hawana watu wa kuwatunza kuna maeneo wanapelekwa. Leo utamkuta mzee yuko Kijijini, hana ndugu, hana familia, yuko peke yake, hatufurahii kama vijana kuona ndani ya Taifa letu kuna wazee namna ile wanashindwa kutunzwa.

Mheshimiwa Waziri naomba katika changamoto zako katika Uwaziri wako, lipe kipaumbele suala hili. Tuweke nyumba kila Halmashauri, kila Mkoo ikishindikana kila Halmashauri japo kila Mkoo tupate nyumba moja, wazee walelewe katika nyumba hizo. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala zima la mahabusu. Mheshimiwa Waziri naomba hili ulichukue, tena kwa umakini na ulifanyie kazi. Tumeona kazi kubwa unayoifanya ukiwa kama mwanamke Waziri unaye jitolea. Unapita Mkoo hadi Mkoo kuhamasisha wanawake, unapita Mkoo hadi Mkoo kuweka jithada wanawake wajikomboe katika maisha yao. Tunajua kazi yako unayoifanya, tunaiheshimu mama kazi yako unayoifanya.

Chukua fursa hii kati ya kazi zote unazozifanya, angalia mahabusu, watoto wanachanganywa, watu wazima na watoto; haikustahili. Tunajua Taifa letu likoje, lakini kuchanganywa mtoto ndani ya mahabusu siyo wakati mzuri. Vitendo vilivyoko kule wanavyofanyiwa watoto siyo vizuri. Watoto hawajifunzi maadili mazuri, baada ya kuweka kule wakitoka wajifunze wawe raia wazuri, wanakuja na mambo mabaya kutoka Gerezani.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la Benki. Mheshimiwa Waziri, tunakuomba sana, tunaomba angalu branch japo ndogo iwepo Zanzibar; japo kwa Mkoo wa Mjini Magharibi uwepo. Tunaiomba Benki hii ifunguliwe. Kwa niaba ya wanawake wote wa Zanzibar naomba nichukue fursa hii kuwasemea, wapate mikopo hii.

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba Serikali fedha wanazozitenga ndani ya Wizara hii ni kidogo hazitoshi kwa sababu Wizara hii ndiyo iliyobeba jamii yote! Vijana wamo humo, wazee wamo humo, watoto wamo humo, lakini ukiangalia bajeti yake ni ndogo. Mimi kwa leo nitakuwa mgumu kuunga mkono hoja kwa sababu pesa wanayotengewa Wizara ni ndogo, mambo ya kufanya ni mengi, kazi ni nyingi lakini fedha wanazoingiziwa ni kidogo.

Mheshimiwa Spika, kitu kinachotusikitisha sisi vijana hususan wanawake, wenzenetu wanapotoka hapa kwenda kuuzwa kwenye suala zima la ukahaba. Linatuma na Mheshimiwa...

(*Hapa kengele iliila kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji*)

MHE. TAUHIDA C. G. NYIMBO: Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Ngoja kwanza nikuulize swalii. Huungi mkono kwa sababu hela haitoshi au? Sasa ukimkatalia atafanyaje huyu? Tafuta Wizara nyingine ya kumgomea huyo na siyo huyu sasa. (*Kicheko*)

MHE. TAUHIDA C. G. NYIMBO: Mheshimiwa Spika, lengo langu, pesa hazitoshi. Majukumu ya Taifa anayo makubwa lakini fedha hana.

SPIKA: Basi, ukisema hivyo inatosha. Lakini ukimpinga huyu, basi tena unakuwa umemkatalia...

MHE. TAUHIDA C. G. NYIMBO: Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. (Kicheko)

SPIKA: Ahsante. Unajua *the logic is*, akisema haungi mkono, basi hata hizi ndogo potelea mbali huko, hazina haja. (Kicheko)

Sasa namwita Mheshimiwa Fatma Mikidadi akifuatiwa na Mheshimiwa Shibuda.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuushukuru Uongozi wa Taifa hili; Mheshimiwa Rais Hayati Mwalimu Julius K. Nyerere, Mheshimiwa Rais Mwinyi, Mheshimiwa Rais Mkapa, Mheshimiwa Rais Kikwete kwa kuendeleza mambo na maendeleo ya wanawake. Leo hii hatuwezi kuzungumza maendeleo ya wanawake bila kuwakumbuka Marais hawa. Kwa kweli wamefanya kazi kubwa sana ya kuendeleza wanawake, kiasi kwamba na sisi leo tupo hapa tunazungumzia masuala ya wanawake. Kwa kweli tunawashukuru sana.

Tunasema kwamba wanawake ni nguvu kazi na uzao wa nguvu kazi. Hatuwezi kuzungumzia mambo ya maendeleo bila kutaja wanawake kwa sababu wamefanya kazi kubwa sana katika kuendeleza uhuru wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, wanawake walikuwa katika mstari wa mbele kuendeleza uhuru wa nchi hii, kabla ya uhuru, baada ya uhuru na sasa tulivyo hivi katika mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa, wanawake kwa kweli wamekuwa katika mstari wa mbele katika kuendeleza juhudhi mbalimbali za nchi hii katika kupata uhuru, vilevile ulinzi na amani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo naomba niseme kwamba Katiba hii tuliyokuwa nayo sasa hivi ambayo tunataka kuitunga kama haitaendelea na kwisha kipindi hiki, tunaomba sana Mheshimiwa Rais Kikwete aweke kiraka cha 50 kwa 50. Aweke kiraka cha 50 kwa 50 kwa sababu hii Katiba tuliyonayo ukurasa wa 61 inaelezea kwamba wanawake watakuwa asilimia 30. Lakini kadri tunavyokwenda katika Katiba hii mpya tunayoendelea nayo, kama haitikuwa, tunamwomba Mheshimiwa Rais Kikwete aweke kiraka, badala ya kusema asilimia 30 tuseme asilimia 50 kwa 50 kwa wanawake. Aweke kiraka, akubali hivyo, pamoja na kwamba alisema hatakubali na kwamba tutaendelea na Katiba ya zamani.

Sisi wanawake wa Tanzania hii tunaomba abadilishe aseme 50 kwa 50 ukurasa wa 61, badala ya kusema asilimia 30.

Mheshimiwa Spika, nimesema kwamba uhuru wa nchi hii tulikuwa wote; wanawake kwa waume. Mwaka ule wa 54 kabla ya uhuru na mwaka ule tulio pata uhuru wa 61 na baada ya uhuru wa Vyama Vingi vya Kisiasa. Sasa tunaomba aendelee, asikwamishe. Aendelee na kutusaidia kwa kupata 50 kwa 50 kwa sababu nchi nyine zote ambazo tunazo katika mikutano mbalimbali ya wanawake, tayari wenzetu wameshafikia asilimia kadhaa. Wamepita asilimia 50.

Kwa mfano, Afrika ya Kusini wana asilimia 45, Rwanda wana asilimia 56, sisi Tanzania je? Azimio la mwisho, la nchi mbalimbali za Kiafrika, Azimio la Maputo namba 90 lilia zimia kwamba Afrika sasa wawepo katika maamuzi ya uongozi asilimia 50 kwa 50. Lakini Tanzania bado tupo katika asilimia 30. Tunaomba sana hilo liwekwe kwamba Serikali za Mitaa, Serikali za Miji, Serikali za Vijiji, Wabunge wawekwe 50 kwa 50 kutokana na maazimio ambayo yamewekwa katika Mikutano mbalimbali ya Wanawake ya Afrika.

Mheshimiwa Spika, hilo la kwanza. Wanawake tuna uwezo, wanawake tumeshakwenda taratibu, tumeanza na asilimia chache, tukaenda kidogo mbele, sasa hivi tuna asilimia 30. Tuna uwezo na tuna ukomavu, tunaomba tuwekwe sasa katika asilimia 50 kwa 50.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni CDCF. Pesa ambazo wanapewa Wabunge kwa ajili ya maendeleo ya wananchi kwa ajili ya kuchochoea maendeleo ya wananchi. Pesa zile na sisi wanawake tupewe, kwa sababu sisi wanawake vilevile tunawajibika kwa wananchi, tunawajibika kwa Serikali. Sasa iweje na sisi tunyimwe pesa zile. Tunaomba na sisi tupewe.

Mheshimiwa Spika, sisi tunakwenda katika Mikoa yote ya Tanzania. Mikoa ile kuna wanawake, wanaume, wanawanchi, Mikoa ile sisi tunawajibika. Sasa kwa nini tunyimwe zile pesa tuiswasaidie wananchi wale? Kwa sababu tunapokwenda katika Wilaya wananchi wanatuomba pesa za maendeleo, za shule, Zahati, wanawake katika vikundi mbalimbali, tunashindwa kuwapa, badala yake tunachukua pesa zetu binafsi tunawapa.

Mheshimiwa Spika, zile pesa za kichocheo cha maendeleo ya wananchi CDCF tupewe na sisi angalau kila Wilaya. Zile zile wanazopewa Wabunge, tuchotewe kiasi na sisi tuwasaidie wananchi wale badala ya kusema kwamba ah, ninyi siyo Wabunge wa Majimbo. Sisi siyo Wabunge wa Majimbo kwa nini wakati Serikali inaanini kwamba sisi ni Wabunge wa Tanzania? Sisi ni Wabunge wa Serikali hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali imekubali kwamba sisi ni Wabunge; kwa nini pesa zile na sisi tusigawiwe ili tuwasadie wananchi wenzetu, badala yake wanapewa wa Majimbo peke yake?

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha

kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante. Kengele imegonga.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (Makofi)

SPIKA: Okay, mwenye wajibu wa kubadilisha Katiba ni ninyi wenyewe kwa mujibu wa kifungu cha 98, siyo Rais. Mheshimiwa Shibuda! (Makofi)

MHE. JOHN S. MAGALLE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata fursa hii. Awali ya yote napenda kusema kwamba naunga mkono juhudzi za Wizara hii za kukusu maendeleo ya jamii na watoto.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hekima ya mwongozo huvutia kufuatwa na wasikilizaji au na waongozwa, naogopa kusikia ya kwamba Kamati za Ulinzi na Usalama sasa ndiyo zitakuwa nyenzo za kupambana na mazalia ya imani potofu na kuondoa imani potofu katika maeneo ya imani potofu.

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni ya kupambana na imani potofu, naishauri Serikali ijielekeze kuongeza huduma za afya katika maeneo ambayo yana imani kubwa za kutumia ramri kwamba ndiyo X-ray, na ndiyo clinic au ndiyo vipimo vya kutambua maradhi. Nasisitiza ya kwamba Serikali ijielekeze kuimarisha huduma hizo, hiyo ndiyo itakayoleta mageuzi na mapinduzi ya kifikra dhidi ya imani potofu.

Mheshimiwa Spika, Serikali tangu ianze kulalama na kurindima kuhusu mauaji ya imani potofu: Je, hadi leo, Wizara hii ambayo ni mtambuka, pamoja na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, wamekuwa na programs gani za kuondoa imani potofu katika maeneo ya kanda ya ziwa? Msikae tu mnapiga kelele na kushutumu kwamba kuna imani potofu, naomba mje na mkakati na mchakato. Naomba Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, pamoja na Wizara hii, leo mtutambulishie mna mchakato gani?

Je, Serikali hii ina mkazo gani wa kuinua huduma za lindo na usalama kwa akina mama wazazi katika hospitali, ambao wanajifungulia kwa Wakunga wa Jadi! Je, inapeleka huduma gani au Wizara hii, imekuwa ni sauti ya sikio sikivu na kelele ya kulaani au kupukutisha huduma potofu kwa njia zippi? Pale ambapo kuna maeneo hakuna hata darubini za kutambua kuna Malaria.

Mheshimiwa Spika, malengo ya ukombozi na wokovu kwa waathirika wa imani potofu katika Kanda ya Ziwa, hususan katika Wilaya kongwe kama Wilaya ya Maswa, naitaka Serikali ije ichambue mazalia yake ni nini? Bila kujua mazalia ya mbu, huwezi ukamaliza ugonjwa wa Malaria. Naomba Wizara hii, pamoja na

marafiki zake wa asasi mbalimbali, mhakikishe mnafunga safari ya kuja kwenye maeneo ya Kanda ya Ziwa. Napinga kabisa kusikia ya kwamba Jeshi la Polisi ndiyo litakuwa nyenzo ya kuondoa fikra potofu na kuleta mageuzi ya fikra.

Mheshimiwa Spika, janga la adui ujinga haliondolewi kwa mtutu wa bunduki. Sijawahi kuona kwamba kuna bunduki imetumika kwenda kuondoa ujinga kwa wanafunzi na wakazalisha vipaji vya elimu.

Sijawahi kuona hata siku moja! Sasa kuweka Jeshi la Ulinzi kwamba ndiyo liwe silaha au nyenzo za kuondoa imani potofu, ni kujidanganya sisi wenyewe. Jeshi la Ulinzi au Kamati za Ulinzi, sio wanasiasa, wala siyo Masheikh wala siyo Maaskofu, kwa hiyo, hawawezi kutoa elimu ya dini wala elimu ya kisiasa.

Namwomba Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara yake, wawe na mchakato wa kushiriksiha Wabunge, wawaimarishe Wabunge, akina mama; wanaweza wakachukua hata wanamkakati na kikosi kazi cha wanawake, Wabunge wanawake wa Bunge hili, wakaja katika maeneo yetu kuungana na akina mama wanawake wenzao kujenga elimu. Kuweni na mkakati huo, fedha hizo msipeleke kwenye Kamati za Ulinzi na Usalama, ni ulaji ambaa hauna faida na sijawahi kuona bunduki inaleta mageuzi ya kifikra.

Mheshimiwa Spika, Serikali Kuu naona haina dhamira njema ya kusaidia kuondolewa kwa matatizo ya Wizara hii ambayo ni makubwa sana kwa ustawi na maendeleo ya wanawake. Je, CCM, kuanzia Kamati za Siasa Wilaya, Mkoa na Taifa, na Kamati Kuu, hivi zimetengana na siasa zake za kuhakikisha zinaleta ukombozi na wokovu kwa wanawake? Kwa nini Wizara hii haina bajeti ya kutosha kama siasa bora za CCM zinapaswa kutekelezwa na Wizara hii? Au mmetengana? Kuna usaliti gani?

Mheshimiwa Spika, kuvunja imani ni rahisi, lakini kuirejesha ni vigumu sana. Bajeti ya Wizara hii ni huduma mgogoro na inanipa mawazo ya mgomo, kuamini ya kwamba kuna upatanifu wa siasa bora na utumishi bora.

Mheshimiwa Spika, wokovu kwa wanawake utategemea juhudzi za vitendo, siyo nadharia. Dua la kuku halimpati mwewe. Lini Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari sasa kuja ziara kuvuna mawazo na fikra?

Mheshimiwa Spika, imani potofu Maswa ambayo ni Wilaya kongwe, ina tatizo hilo vilevile. Lakini ni kwamba watu wengi walitoka katika Wilaya kongwe za kanda ya Ziwa ndiyo wameenea katika Mikao mbalimbali. Hitilafu ya imani potofu; naomba iandaliwe ziara maalum na Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri, mje mvune sababu ya mazalia, baada ya kuja kuvuna sababu ya mazalia, mzalishe mkakati na mchakato wa kikosi kazi cha kupambana. Maneno matupu, ni sawasawa na dua la kuku halimpati mwewe.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Naiomba Serikali sasa iache maneno mengi iwe na vitendo, na mdharau mwiba, huota tende. Nasikitika kusema kwamba kanda ya ziwa wamechoka na shutuma ambazo hazina suluhi.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri na asasi rafiki, pamoja na Mama Salima Kikwete, hebu sasa aandaeni mchakato, Mama Salma Kikwete, uache kumbukumbu ya kwamba umewatumikia wanawake wa Kanda ya Ziwa kuondokana na madhira ya dhuruma ambazo wanazipata kwa sababu hawapati huduma stahiki. Naomba mwaka wako huu wa mwisho uandae kikosi kazi ili kije kilete suluhi kwa ukombozi wa wanawake.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali pamoja na asasi zilitambulishé kuwa zina umakini gani wa kupambana na imani potofu? Naomba Wizara hii iwe msemaji mtambuka, na ninamwomba Mama Salma Kikwete, awe msemaji mtukufu wa kupambana madhila yanayowapata wanawake katika maeneo ya imani potofu. Aache kukaa sasa anasiliza maneno ambayo yana fikra mgogoro.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba Serikali...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Anna Abdallah!

MHE. ANNA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote naomba niwapongeze sana Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote katika Idara hii na Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Spika, utakuta kwamba Wizara wamepata takriban Shilingi bilioni 30 kuendesha Wizara hii, lakini katika mafungu yale ambayo tumekwisha yapitisha, kuna baadhi ya mafungu ni Idara moja tu ama kisehemu kimoja tu cha Wizara fulani, kinapata hizo Shilingi bilioni 30. Kwa kweli Idara hii ni muhimu sana na kazi yake ni mtambuka. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Jamii ni mtambuka! Sijui siku hizi, mambo tu yawe yamebadilika, lakini huko kama alivyokuwa anasema msemaji wa mwisho hapa, ilikuwa ni watu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, ndiyo wangekwenda kufanya tafiti za matatizo yanayotokea katika baadhi ya maeneo; kuua vikongwe, kukata vidole vya mtu, ya kufikiria kwamba utajiri

Nakala ya Mtandao (Online Document)

unatokana na hii; lazima kufanya tafiti za kina, zikaandikiwa ili kutafuta Serikali ifanye nini na mipago iweje.

Kwa kweli fedha hizi walizopewa Shilingi bilioni 30 kwa maendeleo na mishahara na nini ni fedha kidogo sana. Hasa kwa sababu katika nchi hii, katika sensa iliyopita, wanawake, ni zaidi ya nusu ya watu wote wa Tanzania. (Makofii)

Sasa wanawake walio wengi, bajeti yake ndogo. Ukimwendeleza mwanamke umeendeleza Taifa, umeendeleza familia, na mwanamke ndiyo mhimili; nasema mwanamke ni mhimili wa amani katika familia na katika nchi hii. (Makofii)

Watu wasije wakatuona sisi Wabunge labda ndio tunaosema sema huku barabara mtatutambua, patachimbika, lakini ndani ya familia zetu, mwanamke akianza kusema patachimbika, hapakaliki! (Makofii)

Mheshimiwa Spika, naomba katika programs zinazokuja, siyo tu kufundisha wafanyakazi, ni lazima kuwafikia akina mama pale walipo, na kuwafundisha mambo haya na kuwapa ule moyo kwamba wao ndio wahimili wa amani wa nchi hii na wala siyo Mikutano tu ya hadhara, ni sisi wanawake. Lakini inasikitisha, kwamba fedha wanazozipata, hata za huyo mfanyakazi wa kutembea kwenda huko kijijini, akakutana tu na akina mama wakazungumza mambo yanayofaa kufanya ndani ya familia ili familia iendelee, ni fedha kidogo sana. Kwa kweli hawataweza kufanya kazi. (Makofii)

Mimi mwenyewe niliyesimama hapa, tangu mwanzo, kazi yangu ya kwanza katika nchi hii niliyoifanya ni Idara ya Maendeleo ya Jamii. Mimi ni Bwana Maendeleo. Najua, kwamba Idara hii ilikuwa na kazi kubwa sana, tangu wakati wa ukoloni, kuhakikisha kwamba hata sera ndani ya Wizara za Serikali hazipingani. Kwa sababu yako mambo mengine yanafanya na Wizara moja, yanakinzana na Wizara nyingine na matokeo yake badala ya watu kuendelea, hawaendelei, ni kazi ya kutatua mizozo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, hii mizozo kwa kweli tunayoipata ndani ya jamii ni matokeo ya kutokuitumia vizuri Wizara hii, hasa Maendeleo ya Jamii ya namna ya kuwaweka watu pamoja na kuwafundisha namna Serikali za Mitaa zinavyoendelea, zinavyokwenda na namna ya kutatua mizozo katika familia ama katika jamii. Hii ni kazi kubwa sana. Hii ni kazi ambayo inaendana pia na Viongozi wa Dini. Ndani ya Serikali, mimi sioni Idara yoyote ambayo inaweza ikawa counterpart ya Viongozi wa Dini wanaoleta amani katika nchi. Counterpart wao ni Wizara hii, lakini utasikia hata Viongozi wa Dini wanapokutana kuzungumzia amani, wanakutana wenyewe tu. Wizara hii hata sijui kama inashiriksiwa! Wao ndio wataalam, wanaojua watu wanaendeleaje. Kwa nini watu wanafanya vile wanavyofanya sasa hivi, kuliko vile ilivyokuwa?

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, siyo vizuri kusema zamani tulikuwa tukifanya hivi, hapana. Kuna zama za zamani hizo, tulikotokea. Sasa tunakwenda katika sehemu tofauti kabisa, na watu wetu na vijana wetu, akina mama pia wako tofauti kuliko sisi wakati huo tulipokuwa vijana. (Makofii)

Haya yanapaswa akina mama hawa wapate nafasi ya kuona tofauti badala tu ya kulalamika, vijana wa siku hizi hawafanyi hivi, vijana wa siku hizi, wanawake wa siku hizi; jamani eeh! Msione kwamba hivi vitu vilikuwa hivi hivi; viliundwa, vinaelea lakini viliundwa. Sasa sisi hatuviundi vyta leo, huko havitaelea, vitazama. Taifa hili litazama kama hatutoi nafasi proper kabisa mahali ya kutosha kabisa kwa Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, hapa Maendeleo ya jamii siyo akina mama tu, hata akina baba ni maendeleo ya jamii. Kwa sababu hata matendo ya akina baba leo ukiyasikia, baba amemkata panga mkewe, sijui amemchoma mtoto moto; mama mtoto amechukua nyama kwenye chungu unamchoma moto. Haya ni matatizo yaliyo kwenye jamii ambayo tusipoyapatia ufumbuzi ni matatizo yataendelea. Mtoto aliyeswa na familia atakuwa na yeye na akili mbovu ya kutesa wenzake, kwa sababu hajui upendo. (Makofii)

Sasa, haya ni mambo makubwa sana. Mimi namshukuru sana Waziri, namsikia kila wakati anakemea, anasema akina mama habari za ukatili dhidi ya watoto na mimi nasikitika kwamba wanaofanya ukatili mwangi ni wanawake kwa watoto wao, hasa watoto wa kambo. Hili siyo jambo jema. Sasa haya, huko zamani tulikuwa hata na madarasa, kwenye hivi Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, ndipo tunapokutana na akina mama. Akina mama walikuwa na matatizo, nifanyeje, wanakuwenda kupewa maoni hayo. (Makofii)

Nashukuru na naunga mkono hoja hii, lakini nisisitize, fedha hizi hazitoshi kufanya kazi ya maana katika nchi. Ahsante. (Makofii)

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, naona nilipowatangaza wageni, Wizara haikuwa imeleta wale wa kuwatangaza. Kwa hiyo, yuko Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Wanawake, mlizungumzia hapa, Bibi Magreth Mataba Chacha; nadhani watakuwa kwenye maeneo yale ya kazi. (Makofii)

Yuko Mwenyekiti wa Bodi ya Taifa ya Uratibu wa NGOs, Bibi Rukia Masasi. Sijui wako wapi! Pia yupo Katibu Mkuu Baraza la Taifa la NGOs, Bwana Ismail Suleiman. (Makofii)

Halafu yuko UN Women, Bi Fortunata Temu; Mwakilishi wa USAID, Bi Rodurika Tarimo na yupo Mpishi wa Shirika la Elimu Kibaha, Dkt. Lucy Sisendi na Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya Wanawake, sasa huyu sijui ni miss

Nakala ya Mtandao (Online Document)

au nani, lakini anaitwa A. Ndarusa na yuko Mwakilishi wa *Save the Children Program Operation Director*, huyu Bwana John Kalage, aliko huko. (*Makofii*)

Halafu, matangazo ya kazi tena, kuna Mwenyekiti wa Tawi letu la Tanzania la *Common Wealth Parliamentary Association*, anaomba Wajumbe wafuatao wa Kamati ya Utendaji, anaanza; Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Profesa David Mwakusya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Mheshimiwa Zahara Ali Hamad, Mheshimiwa Highness Kiwia, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Zainabu Vullu na Mheshimiwa Lediane Mng'ong'o.

Wiki ijayo, sisi tunakuwa wenyeji wa Semina ya Kimataifa ya *Common Wealth Parliamentary Association*, inahusisha watu kutoka karibu nchi zote za *Common Wealth*. Sasa Tawi letu hili hapa ndiyo mwenyeji wa huo Mkutano. Kwa hiyo, inabidi wajiandae kupokea wageni hao na kuwaandaa watu watakaokuwa watoa mada katika Mkutano huo. Maana yake inabidi watoa mada wengi watoke katika nchi yetu hii. Kwa hiyo, tutakuwa na huo Mkutano karibu kwa muda wa siku nne, tano.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote wa Wizara na Maafisa walioandaa vizuri hotuba ya bajeeti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru Waziri kwa kuja kutuletea Wilayani Namtumbo na kutufungulia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Mputa. Juu ya yote naishukuru Serikali kwa maamuzi ya kutenga fedha kukarabati na kujenga majengo yale na sasa tuna Chuo.

Mheshimiwa Spika, lakini kama Mheshimiwa Waziri ulivyoona ndiyo Chuo kimeanzishwa baadhi ya majengo yaliyopo yanahitaji kukarabatiwa ili Chuo kiweze kufanya kazi ya ufundishaji katika maeneo yote yaliokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, hivyo naamini katika Bajeti ya Maendeleo ya *Training and Folk Development Collages* mtakuwa mmetenga fedha za kukikamilisha au kuendeleza pale mlipofikia Chuo cha Mputa.

Mheshimiwa Spika, nitashukuru sana kupata uhakika wa jambo hili.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kwa pongezi kwa Wizara yako na watendaji wote wa Wizara yako. Maendeleo yoyote ya binadamu kuanza kukua kiakili inaanza kwa mama. Malezi kwa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

watoto yanapatikana kwa wazazi. Kwa hiyo jitihada kubwa ni kutoa elimu kwa wazazi wote, mama na baba kwa kuwalea watoto vizuri ili kuondoa watoto wa mitaani.

Mheshimiwa Spika, kinachokosekana kwa watoto kuvuta dawa za kulevyia ni wazazi kuwalea watoto vibaya na wengine kuwatoroka watoto, malezi muhimu kwa watoto ni pamoja na elimu kwa watoto.

Wengi wa watoto wanaorandaranda mijini ni wale ambao hawakupelekwa shulenii. Kwa vile wanafunzi hawa wamekuwa wengi ni afadhali Serikali ichukue jukumu la kuanzisha shule za kuwapeleka watoto hawa wakasome kwani wakiachwa wataleta usumbufu baadaye kwani ndiyo watakuwa wezi baadaye.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara yako watembelee Wilaya za pembezoni ambazo bado wapo nyuma kimaendeleo. Kuna maeneo mengine ambayo mila zimetawala hata wanawake kuogopa kusema manyanyaso wanayopata kwa wanaume kwa sababu ya utawala wa mila iliyopitwa na wakati.

Taifa halitaendelea kama kuna baadhi ya maeneo ambayo wakinamama hawana uhuru wa kutoa mawazo hawana uhuru na ardhi, hawana uhuru na mali ya mumewe anapofariki. Kwenye maeneo mengine bado wanawake hawawezi kutoka kwenye mawazo bila wanawake kujitetea, uhuru haupatikani bila kudai kwa nguvu.

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri kwenye kipindi chake afike Wilaya ya Longido kuhamasisha wanawake wa jamii ya Kimasai ambao bado wanashiriki mila waweze kubadilika na wao kuwa kama wengine toka maeneo mengine. Nategemea ombi langu litakubaliwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia zote.

MHE. SYLVESTER M. MABUMBA: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ni tegemeo kubwa kwa ustawi wa Watanzania kwani wanawake na watoto ndiyo mhimili mkubwa kwa maendeleo ya Taifa letu. Bajeti ambayo kila mwaka inatengewa Wizara hii hairidhishi hivyo naiomba Serikali yangu iangalie upya bajeti hii ya mwaka 2014/2015.

Wizara inatakiwa kuratibu madawati yote yaliyoanzishwa kutetea haki za wanawake na watoto na ili madawati haya yaratibiwe vizuri lazima rasilimali watu na fedha ziwepo vinginevyo kwa mtindo wa bajeti kiduchu haitoweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Waziri, Mheshimiwa Sophia Simba na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana kwa mapenzi yao makubwa kwa nchi yetu na Watanzania wenzao, hata hivyo naiomba Serikali iwawezeshe kwa kuwapatia fedha za kutosha. Pia naomba Benki ya Wanawake iongezewe mtaji na ifungue matawi nchi nzima hasa kule Zanzibar.

Mwaka 2010 wakati wa kampeni tuliwaahidi wananchi wetu hasa wanawake wa Zanzibar kwamba Serikali zetu zimeamua kuanzisha Benki ya Wanawake ambayo itatoa mikopo nafuu na kuwawezesha wanawake kuwapa taaluma ambayo itawajengea uwezo kwa taaluma ya ujasiriamali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli kwamba Bunge lako Tukufu lilitunga sheria ya kulinda haki ya wanawake na watoto, lakini inaonekana usimamizi wa sheria hii unaonesha walakini kwani vitendo vya unyanyasaji bado vinatamalaki hapa nchini. Wanawake wengi na watoto wananyanyasika, naomba pia kuishauri Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano na ya Mapinduzi Zanzibar viimarishe vyombo vya ulinzi na usalama ili visimamie sheria ya kulinda haki za wanawake na watoto kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Spika, mwisho naiomba Serikali iimarishe Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Hili linawezekana sana iwapo Wizara hii itashirikiana kwa karibu na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa fedha nydingi zilizotengwa TAMISEMI kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 TAMISEMI imetengewa zaidi ya trilioni tano. Kiasi hiki cha fehda ni kikubwa iwapo kinaweza pia kutumika kwa ajili ya ustawi wa wanawake na watoto.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipee, nachukua fursa hii kuwapongeza sana Waziri, Mheshimiwa Sophia Simba (Mb) pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana.

Mheshimiwa Spika, naelekeza mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ni vyema sasa Chuo cha Ustawi wa Jamii cha Rungemba kipandishwe hadhi na kuanza kutoa Shahada badala ya Stashahada. Sisi wananchi wa Kijiji cha Rungemba tumekubali kuwapa ardhii Chuo hiki tukiwa na matumaini ya Serikali kusikia kilio chetu cha muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, tulifurahi sana Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Kamati walipoamua kwa makusudi kuja kukitembelea Chuo hiki na kuona maendeleo na changamoto zake. Lakini pamoja na ziara hii katika bajeti hii

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Chuo hiki hakijatengewa fedha zozote, mimi kama Mbunge tumehakikisha umeme unawaka na sasa upo.

Mheshimiwa Spika, ni vyema sasa Benki ya Wanawake ikashuka vijijiini kuliko kuendelea kuwa kwenye miji mikubwa kama ilivyo sasa, mijini tayari kuna mabenki mengi.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Wizara hii ipate nafasi ya kusimamaia na kujua fedha zote zinazotakiwa wapewe 10% kwa ajili ya akinamama na vijana kuliko ilivyo sasa ambapo fedha hizi hazifiki kwa walengwa kwani maafisa wengi wa Halmashauri kuwa wanazichukua.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja.

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nampongeza Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, naanza na watoto wa mitaani. Kundi hili linaendelea kukua leo hadi leo nchini Tanzania kutokana na sababu mbalimbali, nina taarifa zisizo rasmi kuwa katika Mkoa wa Iringa, tatizo hili linazidi kupungua na kuelekea kuisha kabisa, je, tetesi hizi ni kweli? Kama ni kweli kwa nini tusiende kujifunza kwa vipi wenzetu wamefanikiwa na kwa mbinu zipi?

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu watoto wa majumbani (*house girl*). Kundi hili pia ni kubwa hapa nchini. Utafiti umefanyika na NGOs mbalimbali kuwa elimu kuhusu wasichana wa kundi hili ikitolewa vizuri mabinti hawa huweza kutulia majumbani mwao na kufanya shughuli za maendeleo wakiwa nyumbani wanakotoka hii ni pamoja na Mkoa wa Iringa. Mkoa huu ulikuwa unaongoza kwa ma-house girls kutapakaa nchi nzima kama ajira rasmi kwao.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwa nini elimu hii isibebewe bango nchi nzima kwa kuyaelimisha makundi haya madhara ya ajira hii nje ya Mikoa yao?

Mheshimiwa Spika, kuna ukatili mkubwa hufanyika juu ya watoto aidha kwa kupigwa viboko, kuchomwa moto sehemu mbalimbali mwilini, kumwagiwa maji ya moto na kadhalika. Ushauri wangu kwa wanayoyafanya haya kwa nini Serikali isiwaadhibu watu wazima hawa kama wabakaji wanaofungwa miaka 30 au kufungwa maisha?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara hii hupewa fedha kidogo kwa kuwa ni Wizara mtambuka nashauri kwa kila Wizara ambayo inaguswa na Wizara hii ziwe na taratibu kuchangia kwa asilimia fulani katika Wizara hii kwa ushauri kupelekwa katika Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu unyanyasaji wa watoto na wanawake. Kadri siku zinavyozidi kupita matukio ya kutisha ya unyanyasaji wa watoto na wanawake yanazidi kutamalaki katika nchi yetu. Watoto wadogo wamekuwa wakilawitiwa, kubakwa, kuchomwa moto na wazazi/walezi wao na kuwasababishia matatizo makubwa ya kiafya, kisaikolojia na hata vifo. Wanawake wamekuwa wakinyanyaswa, kupigwa, kudhalilishwa na hata kuuawa. Ni muda muafaka sasa kwa Wizara kuandaa mkakati wa makusudi wa kutoa elimu kwa wananchi na rika yote na kutunga sheria ngumu zaidi ili kuwabana watu wote wanaohusika na vitendo hivi vya kikatili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukeketaji wa watoto wa kike. Pamoja na Serikali kutoa elimu na kukemea suala la ukeketaji wa watoto wa kike, bado suala hili ni kubwa katika Mikoa ya Singida, Dodoma, Manyara Mara, Arusha na kadhalika na hasa baada ya mangariba kubadili mtindo wa kukeketa watoto wachanga wenye umri wa wiki moja mpaka mbili, hivyo kukwepa mkono wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Serikali sasa ibadili mtindo wa kulazimisha Mikoa hii kuachana na jambo hilo kwa nguvu, ila itambue kwamba suala hili ni la kimila hivyo busara itumike kutatua tatizo hili kwa kuanza na kuwaelewesha wananchi kwamba si kila mila ina manufaa kwa wakati huu, bali kuna mila zingine zina madhara ya kiafya. Serikali isitumie nguvu kuzimisha mila hii ambayo ni potofu kuachwa, bali itumie njia ya majadiliano ya kirafiki.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu Benki ya Wanawake. Kutokana na malalamiko ya kila mara kwamba Benki hii ipo Dar es Salaam tu na haina matawi katika Mikoa mingine, suala hili ni tatizo kubwa kwa wanawake wote ambaeo wanahitaji huduma ya benki hii. Ni wakati sasa Wizara kuwa na umuhimu wa kupanua wigo wa kuanzisha matawi katika Mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani ili kuepukana na dhana kwamba benki hii inawafaidisha wake wa viongozi na si wahitaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la watoto wa mitaani ni aibu kwa nchi yetu kuona watoto wanakosa matunzo toka kwa wazazi wao kwamba ni wa mitaani.

Ni kwa nini tunawaita hawa watoto ni wa mitaani kwa maana hawana wazazi, hawana baba na mama? Sheria kali zitungwe kuwabana wanawake

Nakala ya Mtandao (Online Document)

na wanaume wanaotelekeza watoto wao baada ya kuwazaa. Si baba tu ambaye ndiye anapaswa kulaumiwa, hata mama/mwanamke naye anachangia kuwa kikwazo kikubwa kuzalisha watoto wa mitaani.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la haki ya wasichana wanaojifungua kuendelea na masomo. Kuna usemi unaosema ukimuelimisha mwanamke umeelimisha watu wote, ila ukimuelimisha mwanaume, umeelimisha mtu mmoja.

Elimu kwa mtoto wa kike ni jambo la msingi kuliko ambavyo tunaweza kufikiria. Msichana anapopata mimba kwa bahati mbaya akiwa bado anasoma, si jambo la busara kumkatisha masomo mtoto huyu, maana kwa kufanya hivyo unampa mateso kwanza ya kisaikolojia na vilevile ya kiuchumi na kijamii jambo jema ni kumrudisha mtoto huyu shulenili aendelee na masomo kama wanavyofanya wenzetu Zanzibar, Ghana, Kenya, Afrika Kusini na nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, adhabu ya kupata mimba utotoni ni kubwa na kumuongezea nyingine ya kumnyima elimu ni kumfanya afe kabla ya muda wake, ni kwa nini sheria ya kuwarudisha wasichana wanaopata mimba wakiwa shulenili hailetwi na kuanza kutumika mapema iwezekanavyo? Naishauri Serikali kuona umuhimu wa jambo hilo ili kuwa Taifa lililoelimika na kuwafanya wanawake wasiendelee kubaki nyuma kielimu na hata kutoka vyombo vya maamuzi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. GREGORY G. TEU: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri mnayofanya. Kupitia kwako, naishukuru Wizara kwa kuanzisha huduma za kibenki kwa kufungua Tawi la Benki ya Wanawake Tanzania katika eneo la Jimbo la Mpwapwa, ikiwa ni kituo kimojawapo cha kutolea mikopo na mafunzo kwa wajasiriamali.

Mheshimiwa Spika, ombi langu Wizara itatatu lini uhaba wa wakufunzi wa kada mbalimbali katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kikiwepo cha Maendeleo ya Wananchi (Chisalu – Jimbo la Mpwapwa). Vilevile itoe utaratibu/mwongozo unaojumuisha utoaji wa malipo ya ada ya mafunzo yanayotolewa vyuoni, kikiwemo Chuo cha Chisalu - Mpwapwa, kitapewa nafasi ya ukarabati na kutoa mafunzo ya VETA zaidi na kupewa hadhi ya VETA. Wizara iseme haya ili iweze kusikika.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. MARIAM S. MFAKI: Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuongeza bajeti ya Wizara hii ili kuwawezesha watumishi wa Wizara hii kufanya kazi kwa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Benki ya Wanawake tunaomba Serikali ieleteze kwa nini haipeleki fedha alizoahidi Mheshimiwa Rais kutoa ili kuongeza mtaji wa Benki hii. Naomba Serikali itimize ahadi hiyo ili wanawake wafaidike na waweze kupunguza matatizo waliyonayo.

Mheshimiwa Spika, pia nashauri Benki hii iweze kufungua matawi katika Wilaya ili kuwarahisishia wananchi wake kufika katika Benki hizo kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la watoto wa mitaani, kundi hili la watoto linazidi kuongezeka, tunaomba lianzishwe dawati litakaloshughulikia tatizo hili kupunguza watoto hawa. Suala hili ni aibu na linasikitisha.

Mheshimiwa Spika, suala la ajira tunaomba Serikali iwaajiri vijana waliomaliza Vyuo ili kuongeza watumishi katika Wizara hii na waweze kusambazwa kila Kata ili kuelimisha wanawake juu ya ujasiriamali.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara hii iwe na mtiririko wa utumishi katika ngazi ya Wizara, Mkoa, Wilaya na Kata badala ya watumishi hawa kuwa chini Halmashauri sababu ni kwamba Halmashauri imerundikiwa idara nyingi na matokeo yake husahauliwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu NGOs tunaomba NGOs hizi zidhibitiwe katika utendaji wao. Fedha wanazopata Serikali itume wakaguzi, NGOs zikaguliwe na taarifa zitolewe kwenye vikao vya kisheria vya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Waziri na watendaji wake kwa kazi nzuri wanazofanya katika Wizara hii.

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Spika, ili kuchangia kwa ukamilifu nimeona nichangie kwa njia ya dondo (bullet points) masuala ya kijinsia watu wengi wanaelewa ni mambo ya wanawake lakini jinsia (gender) maana yake ni kike na kiume kwa hivyo suala ni maisha ya jamii ya kike na kiume na watoto wao (wholistic approach), siyo wanawake na watoto.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu sera iwe jinsi ya ukuzaji wa jamii kwa jumla wanawake wahuishwe.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kuhusu uratibu wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali, kuna Mashirika mengi ambapo shughuli zake hazijulikani naishauri Serikali iwe macho juu ya taasisi hizi. Kuna kuingiliana kazi kati ya RITA na kitengo cha Wizarani katika kusimamia shughuli za NGO hasa vituo vya watoto.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Maendeleo ya Tango - Mbulu awali kituo hiki kilikuwa *Folk Development Centre*, Chuo kina ekari 600 ya ardhi na majengo ya kutosha kwa ajili ya Chuo kuwa cha kutoa Stashahada lakini kutokana na ukosefu wa bajeti Chuo kimekuwa Mahakama. Naomba kauli ya Serikali kuhusu Chuo hiki.

Mheshimiwa Spika, suala la watoto wa mitaani Mbulu, kwa kuwa hakuna kituo Wilayani Mbulu tunaomba Wizara iongeze fedha kwenye Halmashauri ya Wilaya ili kituo kianzishwe. Bajeti ya shilingi bilioni 30 ni ndogo sana, iongezwe.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu nampongeza Mheshimiwa Pindi Chana kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ni Wizara muhimu sana katika jamii yetu. Ni Wizara inayohusika na maendeleo ya jamii nzima ya Tanzania lakini hata hivyo Wizara hii haijapewa kipaumbele na Serikali kwa kutengewa fedha za kutosha ili kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha fedha kilichotengwa kwa mwaka 2014/2015 cha shilingi 9,017,544,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo kitolewe kwa wakati ili miradi ya maendeleo ya Wizara hii itekelezwe kwa wakati kwa manufaa ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, suala la watoto wa mitaani au wanaoishi katika mazingira magumu ni tatizo ambalo bado halionyeshi kupungua je, tatizo ni nini? Wizara inafanya nini ili kupunguza ukuaji wa tatizo hili?

Mheshimiwa Spika, mimba za utotoni hazijapungua, wanafunzi wengi hasa waishio vijiji ambao shule zipo mbali wanaathirika sana na tatizo hili. Wizara ya Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu itafute jinsi ya kupunguza tatizo hili kwa kuhakikisha wale wote wanaowapachika mimba wasichana wenye umri wa kwenda shule wanachukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, vituo vya kulea watoto wa mazingira magumu, vingi viro katika hali isiyoridhisha, hakuna walezi wa kutosha, watoto wanaathirika kisaikolojia kwani mazingira wanayoishi ni yenye hali mbaya, Serikali itenye fedha za kutosha kuendeleza watoto katika hali ya usawa.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache naomba kuwasilisha.

MHE. ASHA MSHIMBA JECHA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, naipongeza Wizara hii kwa kutekeleza majukumu yake ya kila siku na kuwa kituo muhimu kwa maendeleo ya wanawake na watoto.

Mheshimiwa Spika, watoto walio katika mazingira magumu ni kundi kubwa na linaendelea kukua siku hadi siku, naiomba Serikali kupitia Wizara zote za Afya, Kilimo, Elimu, Tawala za Mikoa na kadhalika kuwa na mipango ya pamoja ya kulitambua kundi hilo kitakwimu, maeneo walimu hali zao za kijamii (wana wazazi au laa) na baadaye kila Mkoa upange mpango mkakati katika muda mfupi wa kati na muda mrefu wa kuwaendeleza watoto hawa.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha ubakaji na ulawiti dhidi ya watoto, nalaani vitendo vya baadhi ya wanaume, umefika wakati wa kuungana pamoja na wanawake na wanaume kupiga vita vitendo hivi vya unyanyasaji wa watoto. Baya zaidi unyanyasaji huu hatimaye ni kuua kizazi na maendeleo ya Taifa kudumaa.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika wanawake tupaze sauti zetu kuwasema na kuwafichua wale wote wanaoshiriki unyanyasaji wa wanawake na watoto.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Wanawake inafanya kazi nzuri ya kuwashudumia wanawake na wanaume kwa kutoa mikopo na hata kusaidia jamii. Tunaomba huduma hizi ziwafikie wanawake wengi zaidi mpaka Zanzibar.

Kuhusu ajira za watoto tunaiomba Wizara kwa nafasi kukemea ajira hizi kwani umezuka mtindo watoto kutumikishwa majumbani na kukosa haki zao za msingi kama elimu, afya kushirikishwa na kadhalika na kupewa chakula tu ndiyo malipo yao na inapobidi kudai malipo hufukuzwa na kuondoka bila malipo yoyote na hatimaye kuzurura mitaani mijini na wengine kunyanyasika kwa kubakwa na hata kupata UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, elimu itolewe kwa jamii kutokukubali watoto kuwatelekeza kwa kufanyishwa kazi ngumu nje ya familia na ndani ya familia.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake ulianzishwa kutokana na Azimio la Bunge mwaka 1993 wenye lengo la kuwawezesha wanawake kujiiamarisha na kujikwamua kiuchumi. Mwongozo unaongoza mfuko huu hauendani na hali halisi ya sasa, kupitia Bunge hili niliuliza swali la lini mwongozo huo utafanyiwa mabadiliko na tathimini ili uendane na hali halisi ya sasa. Hata hivyo majibu yalikuwa ni tathimini ilifanyika mwaka 2006

Nakala ya Mtandao (Online Document)

ili kuona ufanisi wa mfuko huu. Je, Serikali imefikia hatua gani katika tathmini ifanyike sasa ni takribani miaka nane, je, Wizara haioni tathmini hiyo itakuwa imepitwa na wakati? Je, nini mafanikio ya mfuko huo?

Mheshimiwa Spika, Halmashauri nyingi nchini zimekuwa hazitengi fedha asalimia tano (5%) ya mapato yake kwa Mifuko ya Wanawake na Vijana na si kwamba Halmashauri hazitoki bali hali halisi ya kimapato kwa Halmashauri hapa nchini inajulikana, hata hivyo fedha za mapato ya ndani katika Halmashauri zetu hapa nchini huelekezwa zaidi katika miradi ya afya, maji, barabara na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuendelea kutoa msisitizo kwa Halmashauri zitenge fedha katika mifuko hiyo ni jambo linalopaswa kutazamwa kwa upya kutokana na hali halisi ya kimapato katika Halmashuri zetu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo nashauri swala hili liachiwe Serikali kuu kutenga fedha katika mifuko hiyo na si Halmashuri za Wilaya pekee.

Mheshimiwa Spika, uratibu wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali, kumekuwa na ongezeko kubwa la Mashirika haya hapa nchini kwa mujibu wa taarifa ya Wizara, hata hivyo Mashirika hayo kwa wingi wake baadhi hazipo wazi kwa wanayolenga kuyafanya katika jamii ya Watanzania, suala la uratibu wa Mashirika haya ni dhaifu sana kwa kuwa tumeona jinsi kulivyo na NGO's ambazo henzieleweki pamoja na kuwa Bodi ya Uratibu wa NGO's bado Bodi hii haitekelezi wajibu wake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha NGO's zote zinatekeleza yote yaliyokusudiwa kwa mujibu wa uanzishwaji wake? Je, nini mkakati wa kufuatilia na kuzifuta NGO's zenye utata na zilizokwenda kinyume na uanzishwaji wake?

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii na mimi nitoe mchango wangu katika Wizara hii nyeti ambayo vijana wetu na mama zetu wanahusika nayo.

Mheshimiwa Spika, mimi napenda kuchukua nafasi hii nichangie hasa kwa watoto wa mitaani na hasa wale watoto walio Dar es Salaam ambao kazi yao ni kuza maji na juice pale mjini, hivi vijana wale ambao ndani ya ujana wao hawasomi wala hawatayarishwi kwa maisha ya baadaye, wanategemea baada ya kuzeeka wataweza kumudu maisha yao ya uzeeni? Ni kwa kiasi gani wataweza kuweka akiba ili waweze kujenga, kuo na kuishi maisha yaliyo bora?

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, ni vyema vijana hawa sasa ni lazima kuwawekea mpango maalum kwa ajili ya maisha yao ya baadaye, wawekwe katika makambi na wapewe elimu ya ujasiriamali kwa muda ambao unaendana na umri wao, vinginevyo ni dhahiri kwamba tutakuwa tunajenga Taifa la wazururaji na wahuni.

Mheshimiwa Spika, kuna mmong'onyoko mkubwa wa maadili ndani ya nchi yetu, na hili kwa sasa ndiyo linaonekana ndiyo ustaarabu. Ngoma, muziki na hata maonyesho yanayofanywa hapa nchini, wanawake na watoto wanafanywa ndiyo chombo, kivutio kwa watazamaji je, haya hayaonekani kuwa ni kudhalilisha jamii yetu? Na haya si maadili yetu? Na hata nyimbo za sasa zinazoimbwa hazina maadili je, ile "board of sensor" sasa ina kazi gani?

Mheshimiwa Spika, ni wakati sasa kwa Wizara hii kuchukua hatua za haraka kuona hali hii na hata jamii inavyopotea na nini kifanyike kwa haraka. Hata vifo hivi vya walemavu wa ngozi na vikongwe ni mmong'onyoko wa maadili tu. Hivyo ni lazima sasa kusimama kwa pamoja kuchukua hatua za dhati kwa suala hili ambalo jamii inapotea. Wakati wa maneno umekwisha na vitendo vitawale katika hali ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la watoto yatima ndani ya nchi yetu linaongezeka kwa kasi sana na hatua za dharura zinahitajika ili watoto hawa wapate huduma zinazostahili ili watoto hawa wajisikie kama watoto wenzao. Aidha, kinga ni bora kuliko tiba kwani ni lazima vile viashiria vyote vinavyofanya kuongezeka kwa watoto yatima vidhibitiwe mapema kuliko kuona watoto tu. Tufanye kazi ya kuwalea watoto hawa kwa moyo wetu wote ili wawe viongozi bora na watendaji wazuri katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kuwashukuru wale wote wanaochangia kwa namna moja au nyingine wanaowalea watoto wa mitaani kwa moyo wao wa kujitolea na huruma waliyonayo kwa Taifa la kesho. Ni vyema vituo vile vikapewa upendeleo maalum na Mheshimiwa Waziri bajeti ijayo ikawa na fungu la vituo hivi ili wale wanaowalea watoto hawa wawe na uhakika wa maisha kwa vijana wale badala ya kusubiri hisani za wenye uwezo, hii itawapunguzia mzigo wa kufikiria na kutafuta na badala yake watajikita zaidi katika kuwashughulikia watoto wale.

Mheshimiwa Spika, mcheza kwa hutunzwa. Ahsante sana.

MHE. LOLESTIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Sophia Simba (Mb) kwa hotuba nzuri. Pia nampongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kama lilivyo jina la Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Wizara hii inahusu maendeleo ya jamii kwa ujumla wake. Hii ina maana kwamba bila ya utekelezaji katika Wizara hii hakuna maendeleo. Hivyo ninapenda kuishauri Serikali iongeze bajeti katika Wizara hii. Tukiangalia katika Halmashauri zetu kuna upungufu mkubwa sana wa Maafisa Maendeleo ya Jamii katika ngazi za Kata na ngazi za Vijiji, nikitolea mfano katika Jimbo la Busanda Vijiji vyote 80 havina Maafisa Maendeleo ya Jamii. Je, maendeleo yatakuja vipi bila kuwa na watu waliosomea utaalami wa maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, hivyo niiombe Serikali iajiri wataalamu wa maendeleo ya jamii ili kuinua hali ya maendeleo katika vijiji vyetu.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili katika Mkoa wa Geita pamoja na Wilaya zake hatuna Chuo cha Maendeleo ya Jamii wala Chuo cha VETA, katika hotuba nimeona wenzetu kwenye mikoa mingine yenyu vyuo vya maendeleo wanavyofaidika na mafunzo mbalimbali. Naomba Serikali itujengee Chuo cha VETA/Chuo cha Maendeleo kama sera ya Taifa inavyosema kwamba kila Wilaya tuwe na Chuo cha VETA/Chuo cha Maendeleo ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ninaomba Serikali iwekeze katika maeneo ya uchimbaji madini ambako watoto wengi wanakabiliana na changamoto mbalimbli zikiwemo ajira za watoto kwenye migodi ya wachimbaji wadogo. Kuwepo na watoto wengi wanaoishi katika mazingira magumu na hatarishi, hii ni kutokana na wingi wa watu wakati shughuli za uchimbaji zinapopamba moto na baada ya muda watu huondoka mara uzalishaji unapopungua wakati huo watoto huzaliwa, wazazi wa kiume huondoka kwenda kutafuta madini sehemu nyininge, mwisho wa siku watoto wanaachwa bila malezi yoyote. Ninayo mifano hai katika Wilaya ya Geita kwenye maeneo ya Nyarugusu, Rwanagasa, Kaseme na sehemu zote zinazojishughulisha na uchimbaji mdogo wa madini.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo maelezo ninaomba Serikali iwekeze kwa kuongeza bajeti katika Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba hii na kuwasilisha kwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na tabia ya baadhi ya watu kwa kutumia NGOs zao kukusanya watoto yatima kutoka vijiji kwa maelezo kwamba wanakwenda kuwalea, matokeo yake watoto wanawekwa kwenye vituo ambavyo sio salama kwao, mazingira mabovu, wanakosa huduma zote

Nakala ya Mtandao (Online Document)

muhimu ikiwepo elimu, watoto wanalala chini. Serikali itueleze ni uchunguzi gani unafanyika kwa vituo vinavyoandaliwa kulea watoto kuona uwezo wa NGO na mazingira ya kituo ili watoto wasiteseke?.

Mheshimiwa Spika, matukio mengi yameendelea kuongezeka ya mauaji na manyanyaso ya watoto nchini yanayofanywa na wazazi, walezi na hata walimu. Kwa kweli mzazi/mlezi anampiga mtoto vibaya kiasi cha kumuumiza na hata kumletea umauti inaumiza sana na watoto wanachomwa mikono, wanabanikwa kwenye majiko ya mkaa, wanafungiwa ndani kwa zaidi ya wiki huku wamefungwa *chain*.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali itoe elimu zaidi kwa jamii kuondoa matukio hayo. Pia hatua kali zitolewe kwa wote wanaobainika kufanya unyama wowote kwa watoto ili kutoa fundisho.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Wanawake wa Wilaya pamoja na kuwa Halmashauri hawatengi ile asilimia tano (5%) kutunisha hata kile kinachotengwa na Serikali hakiendi kule ili wanawake waweze kukopeshwa. Tatizo la mfuko huu pia unatolewa kwa upendeleo kwa wanawake kwa kuangalia itikadi za vyama vyao. Wanawake wa CCM wanaonekana kama wao ndiyo wanaostahili, huku wanawake wa vyama vingine wakinyimwa fursa hiyo. Kwa kuwa mfuko ni wa wanawake utolewe kwa wanawake bila upendeleo wowote.

Mheshimiwa Spika, tatizo la watoto wa mitaani linazidi kuongezeka, tena ni bahati mbaya sana kwa baadhi ya Mikoa wazazi wanawatumia watoto wadogo wamebeba wadogo zao migongoni wazunguke kwenye magari kuomba. Hatua zichukuliwe kwa wazazi hawa wanaowatumia watoto kama vitega uchumi vya familia zao huku watoto wakikosa fursa ya malezi bora na elimu. Kwa wale watoto yatima na waliofukuzwa na walezi wao/kutekelezwa na hivyo kwenda mitaani Serikali ije na mkakati makini wa kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, nimeshauri miaka yote hapa Bungeni Serikali ijenge kituo maalum cha kuwashifadhi watoto hawa. Kituo hiki kiwe ni cha mafunzo kwa kuweka ufundi wa aina mbalimbali ili wafundishwe baada ya kupata ufundi watatoka kwenye kituo, watakwendwa kujitegemea kwa kutumia ujuzi wanaopewa pia wataweza kutumia nguvu zao kuzalisha ile bustani za mboga, ufugaji, ushonaji na hivyo kuinua uchumi.

Mheshimiwa Spika, mauaji ya albino na vikongwe/wazee yanatilia aibu Taifa letu. Serikali ilifanikiwa sana kupunguza mauaji haya miaka mitatu iliyopita baada ya kuanzishwa kwa Mahakama Maalum ya kushughulikia kesi za mauaji haya. Pia kitendo cha kufuatilia waganga wa kienyeji na kuwafutia leseni wale waliogundulika kuhusika kwenye masuala ya mauaji haya.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Serikali izidi kuwabana waganga wa kienyeji na kuwatangaza kwenye vyombo vya habari wazi kabisa ili wengine waone na hivyo kuasi maasi hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali iweke nia ya dhati ya kuipatia Wizara hii fedha za kutosha kutekeleza majukumu yake yaliyopangwa.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Spika, katika kuchangia katika hotuba ya Wizara hii niulize swalii.

Kwanza, ilishapitishwa sheria kuwa kila Halmashauri ya Wilaya ichangie asilimia tano (5%) katika mfuko wa akina mama.

Katika bajeti yake kwa nini maamuzi haya hayasimamiwi? Kwa nini Serikali haichukui hatua thabiti kwa Halmashauri ambazo hazichangii? Na hata zinazochangia hazifiki malengo yake? Serikali inachukua hatua gani?

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali isichukue hatua ya kuagiza Halmashauri zote nchini ziamuliwe na Serikali kulipa madeni yote ya nyuma kuliko kuendelea kulalamika kila siku kukicha, Serikali ichukue hatua sasa. Wakati ndiyo huu, tuache maneno, tuchukue hatua.

Mheshimiwa Spika, swalii langu naomba kujua hivi maendeleo ya wanawake ni wanawake wa mijini tu? Naishauri Serikali ielekeze nguvu zake kwa akina mama wa vijijini, wanawake wa vijijini wapo nyuma sana Serikali haiwasaidii kuwapelekea fedha za mikopo japo wanafanya kazi sana.

Mheshimiwa Spika, lingine pelekeni elimu kwa akina mama wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu watoto yatima, Serikali iweke mtandao wa kutosha kuwatambua watoto yatima waliopo vijijini ili iweze kuwasidia kiafya, kielimu naona nguvu nyingi zinaelekezwa mijini tu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hotuba ya Msemaji Mkuu Kambi Rasmi ya Upinzani, upungufu na changamoto za Wizara hii zimeelezwa kinaganaga.

Mheshimiwa Spika, naungana na wachangiaji wengi wasioridhishwa na kiasi kidogo cha fedha kilichotengwa hakitoshi kabisa kwa mahitaji ya Wizara hii muhimu inayohusika na maendeleo ya jamii, jinsia na watoto. Inashangaza kwamba Wizara muhimu kama hii haikuingizwa kwenye utaratibu wa Matokeo Makubwa Sasa. Hivi bila kuwaandaa wananchi na kuwawezesha kuna maendeleo gani yanayoweza kutokea vijijini na mijini? Yatakuwa hafifu kweli.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kwa hiyo Serikali iangalie namna ya kuipa uzito Wizara hii kwa kuipa fedha ya kutosha kulingana na mahitaji yake.

Mheshimiwa Spika, mambo mengine ambayo ningependa kuchangia ni haya yafuatayo:

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu fursa sawa za kijinsia. Bado changamoto kubwa inayowakabili wanawake nchini ni kuwa na fursa sawa na wanaume hasa kuhusiana na upatikanaji wa elimu. Bado mfumo dume unawakandamiza wasichana wanaosoma shule (hasa za msingi na sekondari). Bado kuna watu wasiothamini haki ya mtoto wa kike kupata elimu, bado kuna wasichana wengi wanaoacha kuendelea na masomo kwa sababu mbalimbali ikiwemo mimba zisizotarajiwa, Wizara ina mkakati gani kumsaidia mtoto wa kike ilia pate fursa sawa na mtoto wa kiume kupata elimu?

Pili ni kuhusu watoto wa mitaani kuongezeka. Tatizo hili linazidi kuongezeka kila uchao na linaonekana ni kubwa zaidi katika maji na miji mikubwa kama Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Arusha, Dodoma, na kadhalika, Serikali ina mkakati gani kukabiliana na tatizo hili?

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuhusu kutotumika kwa wataalam wa maendeleo. Wataalam wanaozalishwa na Vyuvo vya Maendeleo ya Jamii hawatumwi kikamilifu kuhamasisha maendeleo vijijini kutokana na bajeti kuwa finyu. Katika Halmashauri yangu kwa mfano, watalaam wa maendeleo wanatumia muda wao mwangi wakiwa ofisini tu kwa sababu hawana fedha ya kutosha, kwa hiyo hakuna chochote cha maana kinachofanyika katika kuhamisha maendeleo ya jamii vijijini.

Mwisho ni kuhusu ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Wizara ina mkakati gani wa uhakika na endelevu kuhusu utokomezaji wa ukatili dhidi ya wanawake na watoto? Tatizo hii ni kubwa na linapaswa kuandaliwa mkakati maalum.

Mheshimiwa Spika, maswali ya mwisho, naomba Waziri ajibu maswali ya mwisho yafuatayo:-

Kwanza, je, taarifa ya hali ya jinsia nchini ipo tayari? Kama ipo tayari inapatikana wapi?

Mheshimiwa Spika, pili ni Halmashauri ngapi hutoa asilimia tano (5%) ya mapato yao kwa ajili ya mfuko wa wanawake na zile ambazo hazitoi huchukuliwa hatua gani?

MHE. KULUTHUM J. MCHUCHULI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nachukua fursa hii kwapa pole Mheshimiwa Waziri, mMama Sophia Simba, Naibu Waziri na watendaji wote kwa kuwa wanafanya kazi kubwa sana lakini Serikali imeendelea kuinyima fedha Wizara hii hali ya kuwa wanafahamu hii ni Wizara mtambuka.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na wimbi kubwa la mauaji ya kikatili ya wanawake katika siku hizi za karibuni hasa katika Mikoa ya Mara na hata jana ameuawa mwanamke mwingine katika Mkoa wa Mwanza. Je, Serikali imeshindwa kabisa kudhibiti vitendo hivi vya kikatili vya mauaji dhidi ya wanawake? Nini hatma ya wanawake katika kuijendeleza kiuchumi kwa kuwa wakinamama hawa wanauliwa wakati wakiwa shambani?

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anasoma hotuba yake hapa Bungeni ya mwaka 2014/2015 katika ukurasa wa 28 alisema kuwa hadi kufikia Desemba, 2013 Mfuko wa Wanawake umetoa mikopo kwa wanawake wajasiriamali 500,000 nchini takribani shilingi bilioni 5.44 zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya mikopo, lakini katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mama yangu Sophia Simba ukurasa wa 15 anaeleza kuwa kati ya mwaka 2011/2012 - 2013/2014 Wizara imekopesha jumla ya shilingi milioni 612 na huu ndio ukweli ninaouamini.

Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu amezitoa wapi na amepeleka hizo bilioni 5.44 katika Halmashauri zifi hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, tunamtaka Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Waziri wa Uwekezaji na Uvezeshaji atupe maelezo kamili juu ya matumizi ya shilingi bilioni 5.44 ambazo zinazosemekana zimepelekwa kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake. Je, mfuko unaosimamiwa na Mheshimiwa Waziri Nagu ni tofauti na mfuko unaosimamiwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto?

MHE. NAMELOK E. M. SOKOINE: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii yenye changamoto nyingi.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara iangalie ni kwa namna gani watatunga sheria ambazo zitawasaidia wanawake hawa hasa manyanyaso wanayoyapata ndani ya ndoa, mfano inapotokea mwanamke akijifungua mtoto mwenye ulemavu mwanamke anabaguliwa na kuonekana yeye ndio tatizo na wengine hupigwa hadi kuuwa na la kusikitisha baada ya muda mwanaume anaachiwa, haki ya mwanamke ipo wapi?

Mheshimiwa Spika, takwimu hazingopi, utafiti wa mwaka 2010 unaohusu afya na takwimu za uzazi, vifo na maradhi uliofanywa na Serikali pamoja na utafiti wa matendo ya kikatili dhidi ya watoto wa mwaka 2011 unaonyesha

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kuwa asilimia 45 ya wanawake wametendewa ukatili wa kijinsia. Ukatili dhidi ya wanawake majumbani huendelea kuongezeka ambapo takwimu mbalimbali na utafiti zinaonyesha kuwa kati ya wanawake watatu, wawili wanatendewa ukatili wa kijinsia na waume zao.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara iendelee kuangalia sheria zote kandamizi ambazo zinawanyanya wanawake na watoto.

Mheshimiwa Spika, pongezi za pekee kwa Benki ya Wanawake licha ya fedha kidogo walizonazo wanaweza kufungua matawi maeneo mbalimbali, hii inaonesha kwamba wanawake tunaweza, na hii inaonesha kuwa ukimuelimisha mwanamke umeendeleza Taifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Spika, wanawake ni 51% ya idadi ya watu milioni 45 ya Tanzania. Wanawake wengi sasa hivi ndiyo breaderner katika familia zao, wanawake wa nchi hii ndiyo wanafanya kampeni zaidi katika chaguzi mbalimbali nchini *regardless of itikadi za vyama vya siasa*.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaunga mkono wazo la wanawake kupata 50% katika ngazi zote za uongozi nchini. Inasikitisha bajeti ya Wizara hii ni ndogo kuliko Wizara nyingine, mfumo dume ambao Serikali unaupiga vita unajidhihirisha hapa. Nashauri Serikali iongeze bajeti ya Wizara hii. Wizara hii ndiyo inasimamia makundi mbalimbali hasa watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ni muhimu katika maendeleo ya jamii. Jamii kubwa inaweza kuijendeleza katika vyuo hivi hasa katika fani mbalimbali yanayofaidisha jamii. Zipo fani za upishi, kilimo, kushona na kadhalika.

Nashauri Serikali iweke mkakati wa kuwa na uongozi bora katika vyuo hivi ili vifaidishe jamii inayovizunguka na hata kutoka maeneo mengine nchini. Vipo vyuo vya Maendeleo ya Jamii vinafanya vizuri sana, lakini vipo vingine vimebaki na majengo tu, hakuna uongozi bora, hakuna wanafunzi wa kutosha na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri za Wilaya zote nchini zina Idara ya Maendeleo ya Jamii ambazo zinashughulikia na kutoa mikopo kwa wanawake na vijana katika Halmashauri nyingine, fedha hizi zimekuwa za msaada sana kwa vikundi pengine kwa sababu kuna bajeti za kutosha katika idara hizo. Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya kwa njia moja au nyingine wahuishwe katika ku-monitor na ku-evaluate vyuo vilivyopo katika Wilaya zao ili kutoa

taarifa na kushauri mikakati bora itakayofaa kuendeleza chuo kilichopo katika Wilaya zao. Pengine certificates zinazotolewa na vyo hivi ziboreshweli graduate anayetoka katika chuo hiki aweze kutumia kuingia Chuo Kikuu (Vyo Vikuu siku hizi vimeanzisha system ya certificates/foundation courses, ili ku-bridge the gap kwa wale wanafunzi ambao hawakumaliza A-level au kama alimaliza A-level hakupata credits za kuweza kuingia University).

Mheshimiwa Spika, Serikali ipige marufuku uvaaji wa nguo fupi (sana), nguo za kuonyesha maungo yao, ndoa za jinsia moja, suruali zinashushwa mpaka makalioni. Tusione haya, mila na desturi zetu budi tuzidumishe, maadili ya vijana wetu yanaendelea kuperomoka. Serikali ipite ndanguro zote kuokoa maisha ya watoto wetu na izifunge.

Mheshimiwa Spika, pia ipo haja ya kufanya mikutano ya hadhara nchini kuwakumbusha wazazi jukumu lao la kulea watoto wao, ipo haja kila mzazi ahakikishe mtoto wake ana more years in school ili kuondoa ndoa za utotonii, mimba za utotonii na mtoto wa kike akipata elimu familia nzima inafaidika. Mtoto wa kike akipata elimu ana uwezo wa kupanga uzazi atakapoamua kuzaa na hivyo kuwa na familia ndogo kutegemea na kipato.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwenye Wizara hii kwa kifupi sana kwani mawazo mazuri na mengi yameshasemwa katika hotuba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ni juu ya hali mbaya ya Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Tarime ambacho kipo katika hali mbaya sana na nimekuwa nikilizungumzia hili kwa muda mrefu sana na Mheshimiwa Sophia Simba mwaka 2012 alitembelea chuo kile na kuahidi kupeleka fedha ili kulipa madeni ya umeme, maji na wazabuni wengine.

Mheshimiwa Spika, Chuo hiki kimechakaa na hakina hadhi hata ya kuwa chuo wala shule ya msingi kuanzia madarasa, mabweni, maabara hamna kabisa, maktaba hamna, vifaa vya kufundishia hamna, vitabu hamna, upungufu wa walimu na kuna walimu waliojitelea lakini hawalipwi, kiufupi Wizara/Serikali haipo tayari kuboresha miundombinu ya chuo kile cha TPDC - Tarime na ikumbukwe kuwa chuo kile kinachukua vijana toka Wilaya zingine za Mkoa wa Mara kama Ranya, Serengeti, Musoma na Butiama.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali inatambua Wilaya hizi hazina Vyuo vya Ufundii (VETA) hivyo wanategemea vyuo hivyo, sasa kwa nini Serikali inashindwa kuboresha chuo hiki na kupeleka bajeti ya chuo kwa muda muafaka na

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kuhakikisha ile ahadi ya kulipa madeni na kuboresha miundombinu aliyoitaoa Waziri inatekelezwa mara moja. Naomba majibu ya kina kwenye hili.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu unyanyasaji wa wanawake katika jamii. Tumeshuhudia mauaji ya wanawake wakulima na hasa hili la mauaji ya kina mama wa Butiama, hii inarudisha nyuma maendeleo ya wanawake. Wale kinamama wanashindwa kwenda kisimani/wala mashambani na ikumbukwe kule kwetu mwanaume huoa zaidi ya wanawake wawili, hivyo kauli ya kuwa waenda shambani na waume zao, hii haikubaliki kabisa, Wizara itoe majibu mbadala ni kwa nini imeshindwa kuchukua hatua kwa takribani mwaka sasa tangu mwaka jana.

Pia Wilayani Tarime kuna manyanyaso makubwa kwa wanawake, tumeshuhudia wanawake wamekatwa mikono kama yule Dada Gati lakini Wizara haikutoa kauli, pia yule mwanamke wa Bunda aliyeburuzwa kwenye lami na mume wake na Mheshimiwa Sophia Simba analijua hili suala maana alienda hadi kumuona, je, huyu baba amechukuliwa hatua gani? Naomba majibu pia kwa suala la kuozeshwa watoto wa kike na kubakwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni juu ya watoto wa kike waliotekwa huko Nigeria na kikundi kinachoitwa Boko Haram. Nashangaa Serikali yetu haitoi tamko lolote lile kukeme kitendo kile. Maana hata hapa kwetu tuna watu wanaoteseka sana na kufanyiwa vitendo kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho ningependa kujua ni hatua gani zinachukuliwa kwa wale wote wanaume/wanawake ambao wanajua wana maradhi ya ugonjwa wa UKIMWI lakini wanachukulia fursa ya umaskini kwa Watanzania na kuwarubuni na kushiriki ngono ambayo hupelekea maambukizi ya UKIMWI. Hii ni tabia mbaya na haikubaliki katika ulimwengu huu na ni kinyume na haki za binadamu, sababu hupelekea gonjwa na kifo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. JUMA SURURU JUMA: Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja hotuba ya bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Benki ya Wanawake Tanzania naipongeza Serikali kwa kutekeleza kwa vitendo katika huduma hii ya Benki ya Wanawake Tanzania, hata hivyo nimeona benki imefungua vituo vingi vya benki hiyo vinavyotoa mikopo na mafunzo ya wajasiriamali, lakini kwa kuwa ni Benki ya Tanzania nzima, je, ni lini vituo hivyo vitafunguliwa Zanzibar?

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uzururaji wa watoto barabarani na mitaani, ni kipindi kirefu watoto wengi wamekuwa wakizurura mitaani na idadi

Nakala ya Mtando (Online Document)

inaongezeka, suala ambalo ni hatari kwa Taifa letu. Sasa ili kuondoa tatizo hili lenye kutia aibu kwa Tanzania je, Wizara imepanga mkakati gani katika kuliondoa tatizo hili na je, Wizara itawaambia nini Watanzania kwa zile familia zinazotelekeza watoto hao?

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa sana Waziri Sophia Simba, nichukue fursa hii nikupongeze kwa kazi nzuri sana unayofanya katika mazingira magumu sana. Aidha nikupongeze kwa hotuba yako yenyeye kuonyesha kukata tamaa.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru na kumpongeza Rais, Mheshimiwa Jakaya Kikwete kwa kumteua Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana kuwa Naibu Waziri, hakika anastahili na ni imani yangu ya kwamba kwa pamoja ninyi wapambanaji mtaendelea kufanya kazi kwa nguvu.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Katibu Mkuu Mama Anna Maembe, Naibu Katibu Mkuu Mama Milao na watendaji wote wa Wizara wa Wizarani, Mikoani na Wilayani.

Maoni yangu, nikiri kuwa mimi ni Afisa Maendeleo ya Jamii tangu mwaka 1978 na hata dakika moja sitaacha fani yangu. Lakini nimekuwa nikiona maendeleo ya jamii ikijikongoja ni lini tutatumia sekta hii ipasavyo?

Tumeona mikakati, mipango, miradi mbalimbali ikiendelea bila ufahamu wa wananchi, mikakati hafifu iliyotumika hatimaye utekelezaji umeshindikana, yangefanywa na Maafisa Maendeleo ya Jamii pangekuwa na mafanikio. Kwa nini basi hamfanyi makusudi mazima kuelimisha na kuwezesha sekta zote kuelewa umuhimu wa hawa watu?

Mheshimiwa Spika, pana pendekezo kuwa paanzishwe Baraza la Wanawake ambalo linalekeea kuzaa matunda na hata kuingizwa kwenye Katiba. Hamuoni kuwa Wizara ya Jinsia imeonyesha upungufu sana hadi kuonekana kuanzisha Baraza hilo.

Nina hakika likianza Idara ya Jinsia itakosa mwelekeo, acheni kufanya *business as usual*, na kutegemea semina, mikutano na conferences na kutegemea wafadhili mambo ni mengi ukatili wa wanawake wa kutisha unaendelea, watoto wanadhalilishwa, hakuna *action* wala matamko. Kama vipi chukueni maamuzi magumu ya kuondoa hiyo mizigo muweke watu amba wana weledi na uelewa wa mambo haya. Tunaumia sisi Maafisa Maendeleo ya Jamii proper kuona sekta imelala.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko toka kwa wafadhili kuwa Wizara utendaji umezorota, miradi mingi, mikakati mingi haiendi, *please elezeni tatizo tuchangie*. Tatizo la fedha linatokana na mikakati sifuri na uzito kwa kufanya mambo kwa mazoea.

Mheshimiwa Spika, Maafisa Maendeleo ya Jamii Wilayani hawana vitendea kazi, magari, fedha kwa kweli ni kama yatima kwenye Halmashauri na nyakati nyingine hawaeleweki shughuli zao. Kwa vile bajeti ya Serikali ni ndogo sana, basi hizo fedha za wafadhili zitumieni kwa *activities* huko, wasaidiwe kuandika *proposals* na mafunzo.

Mheshimiwa Spika, asilimia tano (5%) ya kwenda kwa akina mama isimamieni, kwani maeneo mengi hazipelekwi, lakini vilevile muwawezeshe ma-CDO/CDA'S kuhamasisha akina mama na vikundi vyao kuanzisha miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mwisho tutumieni Maafisa Maendeleo ya Jamii proper tuliostaafu, anzisheni Baraza hilo, litawasaidia na kuwashauri. Mungu awabariki.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu na namshukuru Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi nitoe ushauri katika maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maendeleo ya Jamii ni miongoni mwa Wizara inayopewa fedha kidogo wakati Wizara hii ni Wizara ya Maendeleo, ni Wizara mtambuka. Kwanza Wizara hii ndiyo inayohamasisha maendeleo ya wananchi na pili, kuhamasisha vikundi vya maendeleo, kulea wazee na inashughulikia masuala ya watoto. Ningependa kujua Serikali ina mpango gani wa kuongeza fedha kwa ajili utekelezaji wa kazi za Wizara?

Mheshimiwa Spika, kuhusu mauaji ya wanawake hasa Butiama, wanawake wamekuwa wakiuawa, ningependa kujua ni hatua gani zimechukuliwa juu ya matukio hayo, pia ningependa kujua je, Serikali na jamii wamejipangaje katika kukabiliana na hali hiyo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, naishukuru Serikali kwa kutenga fedha shilingi bilioni mbili kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo. Naiomba Serikali itoe fedha ili kukamilisha deni hilo lililobaki kabla ya mwaka wa fedha haujaisha.

Mheshimiwa Spika, vilevile naishauri Serikali itenye fedha zingine za kutosha kwa ajili ya kuimarisha vikundi vya kiuchumi. Pia ningependa kusikia kauli ya Serikali ya fedha zilizotengwa za Mfuko wa Maendeleo zinatoka lini bilioni mbili?

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kuhusu asilimia ya mapato ya Halmashauri, naomba kusikia kauli ya Serikali kwa Halmashauri zilizoshindwa na zitakazoshindwa kutenga asilimia 10% ya wanawake na vijana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu watoto wa mitaani, ningependa kujua Serikali ina mkakati gani kupunguza tatizo la watoto wa mitaani.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali itenye fedha za kutosha kwa ajili ya ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo na fedha za kuendeshea Vyuo hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Benki ya Wanawake, nampongeza Mkurugenzi wa Benki ya Wanawake na Bodi kwa kazi nzuri wanayofanya ya kuifanya benki ikuwe siku hadi siku kwa kuanzisha tawi la pili Kariakoo Dar es Salaam na vituo vya kutolea mikopo na mafunzo kwa wajasiriamali na kufungua matawi Mwanza na Dodoma. Naishukuru Serikali kuendelea kutoa ruzuku.

Mheshimiwa Spika, ombi langu naomba Benki ifungue vituo vya mafunzo na kutolea mikopo katika kila Mkoa kwani manufaa ya benki hii yawafikie wanawake wengi hasa wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, pia masharti ya kutoa mikopo katika Benki ya Wanawake yaangaliwe upya ili kukidhi malengo na madhumuni ya kuwakomboa wanawake hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ni Wizara nyeti sana kwa sababu iwapo ingeendelezwa kwa kupata bajeti ipasavyo ingeweza kuinua maisha ya jamii na kuwezesha jamii kuchangia maendeleo ya nchi. Hii ingebadili kabisa maisha ya jamii na kuweza kumudu mahitaji yao na ni nyenzo muhimu ambayo ingeleta maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imekuwa inapewa bajeti ndogo sana pamoja na ukweli kwamba imekuwa ikifanya mengi kwa jamii. Ni kwa nini sasa Serikali isiwezeshe zaidi Wizara hii?

Mheshimiwa Spika, kila Halmashauri inatakiwa kutoa asilimia tano (5%) kwa maendeleo ya wanawake na asilimia tano (5%) kwa vijana kwa mapato ya ndani ya Manispaa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo ni Manispaa chache zinazotoa hizo asilimia tano (5%) za wanawake na vijana, kwa kudhani kuwa suala hilo siyo muhimu. Fedha hizo Halmashauri nyingi wanaona ni nyingi na hivyo kumega nyingine na kuzipeleka kwenye mahitaji mengine.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa maendeleo ya jamii, ni kwa nini hii asilimia kumi (10%) ya makusanyo ya ndani ya Manispaa zisipelekwe katika Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii ili fedha hizo zihakikishwe zinalipwa na vilevile zitahakikiwa kuhakikisha zinatumika kwa walengwa mahsusii.

Mheshimiwa Spika, uktili kwa wanawake na watoto umezidi na ni dhahiri waathirika hao wakiwemo na wazee wanaume, je, Serikali ina mpango gani wa kukomesha mauaji ya wazee hawa kwa sababu mbalimbali ikiwemo ya ushirikina, ni kwa nini pamoja na elimu endelevu, adhabu kali isitolewe kwa wahusika?

Mheshimiwa Spika, wasichana wengi wamekuwa victims wa mimba za utotoni hasa wale wanaochaguliwa kuijunga na sekondari. Sekondari nyingi vijijini zipo mbali sana na makazi ya watu hivyo inalazimu wasichana kutembea umbali mrefu lakini pia wazazi wengine huamua kuwapangia watoto hao wa kike vyumba karibu na shule hizo. Matokeo yake wasichana hubakwa, hujamiiiana na watoto wa kiume, lakini pia kuwekwa kinyumba na wanaume wakubwa. Watoto hao hupata mimba kirahisi na kukatisha masomo yao. Wazazi nao huona hiyo ni aibu na wengi wanaamua kuwaoza na kuwatumbukiza watoto hao kwenye dimbwi la ujinga na umaskini. Je, ni kwa nini Serikali isijenge hosteli kwa ajili ya watoto hao?

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya ina Ustawi wa Jamii wakati Wizara hii ina maendeleo ya jamii lakini Ustawi na Maendeleo ya Jamii, ni mambo yaliyohusiana kwa karibu sana na mambo yale yanahu kundi la watu hao hao. Je, ni kwa nini kazi hizo zisiunganishwe ili ziweze kuendelezwa kwa pamoja? Hii itasaidia Serikali kuchanganya nguvu zinazotawanywa fedha hizo kwenye Wizara mbili badala yake fedha zote ziende mahali pamoja.

Mheshimiwa Spika, mwisho natoa wito kwa Serikali kusoma michango ili kuona yanayoweza kuchukuliwa na kufanyiwa kazi kwa ustawi wa jamii ya Watanzania.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kuhusu unyanyasaji wa watoto. Vitendo hivi vyta unyanyasaji wa watoto vimekithiri kwa kiasi kikubwa na bado Serikali haijaweza kuyadhibiti.

Mheshimiwa Spika, kuna watu wengi wanabaka watoto, wanalawiti watoto lakini inapopelekwa kesi Mahakamani mara nyingi kesi hizi zinakosa ushahidi wa kutosha na hawa wanaofanya vitendo hivi wanaachiwa huru. Hili naiomba Serikali ione kuwa ni tatizo kubwa ambalo linaathiri kizazi chetu. Serikali itoe taaluma kwa wazazi pale inapotokea mtoto kubakwa au kulawitiwa basi wazazi wasiwafishe hawa watoto mpaka wafikishwe Polisi ili wapelekwe

hospitali upatikane ushahidi. Pale anapopelekwa bado mbegu zile zinaonekana pale anapopelekwa na kupimwa hospitali ushahidi unapatikana.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ndiyo linalosababisha kesi hizi kukosekana ushahidi na wahalifu hawa kuachiwa huru na kuendelea na kazi yao ya kudhalilisha watoto.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia kuhusu akinamama wengi wanavyoteseka ndani ya majumba yetu kwa kupigwa na kunyanyaswa na wanaume. Wanawake wengi sana wanafanyiwa ukatili wa kijinsia kwa sababu hawawezi kuondoka pale kwa sababu ya uwezo mdogo wa kuendesha familia hawawezi kuwaacha watoto na pia akiwachukua hawezi kuwashughulikia. Matokeo yake anaendelea kuteseka.

MHE. HAMOUD ABUU JUMAA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwangi wa rehema kwa kunipa fursa hii ya upendeleo ili nami nichangie hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ya mwaka 2014/2015. Vilevile nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalamu wake kwa kundaa bajeti nzuri inayokuja kukabiliana na changamoto zinazozikabili sekta hizi. Mpango huu wa Serikali unaendana kabisa na llani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la sekta ya maendeleo ya jamii ni kuchukua hatua zinazowawezesha watu kutambua uwezo walionao na kubaini matatizo na uwezo wao wa kutumia rasilimali zilizopo kujitatalia matatizo hayo, kujipatia na kujongeza kipato na kujiletea maisha bora zaidi na hivyo kujiletea maendeleo wenyewe, na kuweka mazingira muafaka yatakayowawezesha wanawake na wanaume kutekeleza makujumu yao katika jamii kwa kuzingatia mahitaji ya kijinsia.

Aidha lengo lingine ni kuongeza ushirikishwaji wa wanawake na vijana katika shughuli za maendeleo, hatimaye kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania. Kazi zinazotekeliza na sekta ya maendeleo ya jamii katika maeneo mbalimbali nchini ni pamoja na:-

Kwanza, kujenga uelewa wa wananchi ili aweze kushiriki shughuli mbalimbali za kujiletea maendeleo yao kwa njia ya kujitegemea na kuwasaidia kupanga mipango inayotekelzeka.

Pili, kuhamasisha wananchi kuujinga katika vikundi vyta kijamii na SACCOS ili kuanzisha na kutekeleza shughuli za uzalishaji mali zenye kuchangia kuinua hali zao za maisha, pamoja na utoaji wa mikopo ya kiuchumi kwa wanawake kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii wa Wanawake.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Tatu, kusaidia jamii jinsi ya kuondokana na mila potofu zinazochangia kuzorotesha maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kila Halmashauri katika mikoa yetu hapa nchini ina dawati la jinsia na kwa kuzingatia msimamo wa nchi yetu kuhusu usawa wa kijinsia Halmashauri zote zimekuwa na msimamo wa kutekeleza maazimo mbalimbali ambayo Serikali imekuwa ikisaini mikataba yake, mfano azimio la haki za binadamu la mwaka 1948 la kuondoa aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake (CEDAW 1979) pamoja na maazimio mbalimbali yanayohusu haki za wanawake na watoto. Madawati haya yamekuwa chachu ya kuleta usawa katika utendaji kazi na umiliki wa rasilimami katika jamii ikiwa ni pamoja na kuachana na mila potofu zinazosababisha wanawake kuonewa na kupuuzwa kutokana na kutokuwa na kauli ya kumili mali.

Mheshimiwa Spika, zipo changamoto mbalimbali zinazosababisha vikwazo mbalimbali katika utekelezaji wa kazi za idara kama ifuatavyo:-

- (i) Tatizo la usafiri kwa watumishi walio kwenye Kata pamoja na Halmashauri nyingi kukosa vyombo vyafurahishe.
- (ii) Tatizo la makazi kwa watumishi waishio kwenye Kata.
- (iii) Tatizo la vitendea kazi.
- (iv) Ukozefu wa ofisi kwa watumishi katika Kata.
- (v) Fedha za matumizi ya kawaida zinazoletwa na Serikali kufanya kazi ni kidogo kwa ajili ya kazi za Idara ya Maendeleo ya Jamii.
- (vi) Mashirika yasiyo ya Kiserikali kutotoa taarifa zao za utendaji kazi kwa wakati

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizo nilizozitaja hapo juu, kuna njia ya kukabiliana nazo ili kuleta tija katika sekta hii nzima, nazo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Wizara ishirikiane na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kusaidia kutoa vyombo vyafurahishe kwa watumishi wa Maendeleo ya Jamii katika ngazi zote Wilayani na kwenye Kata.
- (ii) Watumishi wa Sekta ya Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na wananchi wanatoa hamasa kwa wananchi waweze kujitolea kuwajengea nyumba watumishi wao wa sekta zote.

- (iii) Wakurugenzi wa Halmashauri wanahimizwa kuchangia katika OC ya Idara ya Maendeleo ya Jamii ili kuifanya Idara hii iweze kufanya kazi zake vizuri.
- (iv) Mkoa na Halmashauri zinafanya jitihada ya kuwawezesha watumishi wa Maendeleo ya Jamii kuwafikia walengwa.
- (v) Mashirika yasiyo ya Kiserikali yamekumbushwa kuwasilisha taarifa za kazi zao katika mamlaka ya Serikali za Mitaa.
- (vi) Uanzishaji wa mitando ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya Mkoa na Wilaya imesaidia kusukuma utendaji wa kazi za mashirika hayo.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Kibaha Vijiji matatizo haya pia yapo na kusema kweli tumekuwa tukikabiliana na changamoto nyingi sana kutokana na matatizo haya, tukianzia na suala zima la watoto wa mitaani tumekuwa tukikabiliana na changamoto hiyo kwa miaka mingi sana na mpaka hivi sasa bado watoto hawa wamekuwa wakizidi kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara kuchukua juhudzi za wazi na za haraka kabisa ili kuweza kutatua tatizo hili kwani watoto na vijana hawa ni Taifa la kesho hivyo basi tukiwaacha wazagae mtaani bila kupata elimu na kuwaendeleza tutakuwa tunapoteza viongozi wa kesho.

Katika bajeti ya mwaka jana niliishauri Serikali kuanzisha vituo vya kuwalelea watoto hawa Jimboni kwangu ili kuwatunza na kuwapa maadili yaliyokuwa bora tofauti na sasa hivi kwani huzagaa hovyo mitaani na kujifunza mambo yasiyokuwa ya maadili kulingana na umri waliokuwa nao.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi narudia tena kusema naomba kuleta tena kwa Serikali ombi langu ili walifanyie kazi tuweze kuokoa kizazi hiki ambacho ni Taifa la kesho. Kwa kuwa sisi bado tuna maeneo mengi na mazuri ya wazi hivyo haitakuwa shida kupata eneo kwa ajili ya kujenga kituo hicho.

Vilevile tumekuwa tukikabiliwa na tatizo la wazee wasiojiweza na wao pia wanastahili kuhudumiwa, wazee hawa hali zao sio za kuridhisha kwani wamekuwa wanakosa hata mlo wa kawaida unaohitajika kwa binadamu, wakiwekwa mahali na kupatiwa huduma basi wazee hawa wataondokana na adha hii wanayoipata hivi sasa. Kupitia maombi haya kwa Serikali, nawashauri watumie vyanzo mbalimbali kuweza kupata fedha na kuja kuwasaidia wananchi wetu na kuwaondoa na adha hii ambayo hakuna kati yetu anayependa kuwaona wazee hawa, vijana ama watoto wa mitaani wakipata shida na kuishi katika mazingira magumu wanayokabiliana nayo hivi sasa.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, yanahitajika mafunzo yanayoungasha utashi wa kisiasa kwa kuzingatia masuala ya jinsia na usawa Serikalini ili kupunguza mapengo yaliyopo, inabidi kuwekeza fedha na rasilimali anuai. Nadharia iliyopo kwenye sera inaweza kutekelezeka endapo kutakuwa na uvezeshaji wa rasilimali na fedha ili kuhakikisha huduma za kijamii zinatekelezwa kwa kuzingata mahitaji ya makundi yote yaani wanawake na wanaume.

Aidha, mara nyingi mahitaji ya makundi la wanawake yamekuwa yakisahaulika jambo ambalo linaonesha kuna kila sababu ya kuwawezesha watendaji Wizara husika kiuchambuzi wa sera na bajeti kwa mlengo wa kijinsia na kuainisha mapungufu kama hayo ili yaweze kufanyiwa kazi. Kundi la wanawake bado limekuwa na changamoto hasa katika huduma za afya, elimu na nyinginezo ambazo zinaongeza mzigo kwa wanawake.

Naiomba Serikali kuongeza uwekezaji katika kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia na kuongeza idadi ya wanawake katika vyombo vya uamuzi ili kuleta usawa wa kijinsia. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ndiyo Wizara yenye dhamana katika usimamizi wa masuala ya kijinsia kwa Taifa letu na usimamizi wa sera ya jinsi na uratibu wa vitengo vyote vya jinsia, hivyo ni muhimu kwa watendaji wake kuwa na uelewa wa kutosha, uwezo wa kirasilimali na rasilimali watu ili watendaji hao waweze kufanya ufuatiliaji wa kutosha katika utekelezaji wa masuala anuai kwenye bajeti.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko yoyote ya kijamii ni mchakato na miaka yote hii toka tupate uhuru ni mingi, tungetarajia tuwe tumepiga hatua kubwa zaidi, lakini kwanza ni vizuri kutambua juhudzi zilizofanywa zimeanza kuzaa matunda kwenye maeneo mengi, miaka yote hii iliyopita hata dhana ya jinsia haikuwepo kwenye mazungumzo yetu hata dhana ya mfumo dume ilikuwa haipo, lakini kwa sasa wanawake na wanaume wanakaa pamoja na kuzungumzia masuala hayo. Ni jambo la kujivunia katika historia ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejitahidi sana katika upangaji na utekelezaji wa bajeti maeneo anuai ili kuhakikisha makundi yote yananufaika na rasilimali za Taifa, hatuna budi kuipongeza kwa hilo. Ila kuna hali ya unyanyasaji wa kijinsia katika baadhi ya maeneo licha ya juhudzi za kupambana na vitendo hivyo ambavyo havikubaliki kabisa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali indelee na mkakati wa utoaji wa elimu ya uelewa juu ya masuala ya haki, kwani jamii ikielewa vitendo kama hivyo vitakoma mara moja na kubaki kuwa historia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, suala ya ukatili wa kijinsia licha ya juhudini kubwa za Serikali za kuhakikisha inakomesha ukatili huu bado kuna vitendo vingi vya kikatili vimekuwa vikiripotiwa kwa mfano mauaji ya vikongwe, ukatili kwa walemaru wa ngozi (albino), mauaji ya wanawake katika mikoa mbalimbali ikiwemo Mkoa wa Mara. Je, Serikali ina mipango na mikakati ipi kuhakikisha vitendo hivi vinakomeshwa?

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ni vyema Serikali kupitia Wizara hii ikafuatilia kwa ukaribu kuhakikisha kwa asilimia tano (5%) inayotakiwa kutengwa kwa ajili ya kuwawezesha wanawake kiuchumi inapatikana na pia kuweka mkazo kwa wanawake wengi waliopo vijiji.

Mheshimiwa Spika, Benki za Wanawake nashauri kwamba matawi yaanzishwe mikoani kwa kuweka madirisha kupitia Benki za Posta ambazo zinapatikana karibu katika mikoa yote ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, katika eneo hili Serikali kupitia Wizara hii katika bajeti yake ya mwaka 2013/2014 iliahidi kukifufua Chuo cha Maendeleo cha Msaginya Kilichopo Mkoani Katavi kwa kuanzisha pia kozi zingine kama masomo ya upishi na mengineyo kama ufugaji wa nyuki kwa ajili ya kuzalisha asali na kuweza kujikwamua kiuchumi kuanzia ngazi ya familia hadi Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, je, mpaka sasa hali ya Wizara ikoje? Je, Serikali inasema nini katika hili?

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake atueleze wananchi wa Katavi tutegemee nini katika hili.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. PHILIPA G. MTURANO: Mheshimiwa Spika, Wizara hii inashughulikia maeneo mengi sana ambayo yanagusa mtu moja kwa moja na mazingira yanayomzunguka.

Mheshimiwa Spika, mengi yamezungumzwa kuhusu Wizara hii lakini kama Serikali haitaona umuhimu wa kuipatia Wizara hii pesa ya kutosha hakuna kitakachofanyika.

Mheshimiwa Spika, majengo ya Vyuo vya Maendeleo yamechakaa kiasi cha kutishia uhai wa wanayoyatumia. Maeneo mengi hayopo sawa kwa ajili ya

Nakala ya Mtandao (Online Document)

ufinyu wa bajeti. Tunaitaka Serikali iitizame kwa jicho la pekee Wizara hii ili kazi iweze kufanyika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, suala ya ukatili wa wanawake, watoto na walemavu bado ni tatizo kubwa katika nchi hii, Serikali ifanye operesheni maalum kubaini watu wanaofanya vitendo hivi na kuwafikisha katika vyombo vyaa sheria na Wizara husika ifuatilie kuona haki imetendeka.

Mheshimiwa Spika, pia tatizo la utumikishwaji kazi ngumu watoto wadogo bado lipo na limekuwa tatizo sugu. Serikali ilichukue hili kwa kumaanisha kwani wanateseka majumbani na migodini.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa Serikali ione umuhimu wa Wizara hii ipate fedha ya kutosha ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi kama Wizara nytingine.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Spika, ninapenda kumpongeza Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Mheshimiwa Sophia Simba (Mb) pamoja na Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana na Katibu Mkuu na Maafisa wote na wafanyakazi wa Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hotuba hii kwa kutoa rai kwa kuwa Wizara hii ni mtambuka hususan katika masuala ya jinsia na watoto basi wafuatilie na kushinikiza kwa nguvu zaidi na ikibidi kuwa na sheria inayoibana Serikali kwa maana ya Wizara na taasisi kuajiri na kuanzisha dawati la jinsia ambalo litakuwa linafanya kazi kwa karibu sana na kuwatumia kutekeleza au kusimamia utekelezaji wa miradi husika katika Wizara na taasisi hizo.

Mheshimiwa Spika, Wizara iboreshe mfumo wa kutoa Maafisa Maendeleo wengi kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hizi wakichangiwa na kila Wizara na taasisi katika yale maeneo yanayohusu sekta hii. Hii itahakikisha kuwa maendeleo ya kila sekta yanatekelezwa kwa kuzingatia usawa wa jinsia huku wakichangia kibajeti na ujuzi kwa matumizi ya maafisa hawa wa maendeleo ambaa wengi wapo vijijini na mijini kwenye ngazi ya Kata na Halmashauri.

Maafisa Maendeleo wafanye kazi na Maafisa Ugani na Maafisa Biashara, Afya, Elimu, Wahandisi, Wanyamapori, Kilimo, Mavuvi, Wafugaji na kila sekta kuhakikisha kuwa masuala ya jinsia yanazingatiwa kuanzia ngazi ya kupanga mipango, utekelezaji na kwenye ufuatiliaji na tathmini. Gharama zote zitachangiwa na sekta husika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni mategemeo yetu kuwa tutaona Wizara hii ikianzisha Idara au ikijumuisha kwenye Idara ya Jinsia. Afisa atakayeratibu Maafisa Jinsia katika kila Wizara na taasisi ya Serikali na kutengeneza mpango

Nakala ya Mtandao (Online Document)

mkakati wa kitaifa unaoanisha shughuli zote zinazotajwa hapo juu kwa mtazamo wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Wanawake ilipata bahati ya kupata mtaji wa kuianzisha lakini hata kwa fedha hizo Benki haijatumia ubunifu kujizalishia mapato zaidi ili hali benki binafsi kama Benki ya Maendeeo iliyoenda kwenye soko la hisa kupata fedha ya kutosha kuijendesha. Uongozi wa Benki hii uangalie jinsi gani wataweza kufanya hivyo ili waweze kueneza huduma hii muhimu kwa wanawake.

Mheshimiwa Spika, suala la uzazi wa mpango na elimu ya uzazi kwa vijana isimamiwe chini ya mfumo huo tajwa hapo juu. Nepal, Pakistan na India hata Ethiopia wana modeli nzuri ya kuigwa unaosaidiwa na UNDP.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa tayari kushirikiana na Wizara kutoa uzoefu wangu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, pia Katibu Mkuu kwa kuijendesha vyema Wizara hiyo japo bajeti/fedha wanazopewa ni ndogo sana kulingana na majukumu walijonayo katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengi mazuri yanayofanywa na Wizara hii lakini zipo changamoto zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa watoto wa mitaani na wakubwa wanaomba omnia mitaani, tatizo linazidi kuongezeka siku hadi siku katika maeneo ya mijini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ni vyema sasa ikatoa tamko kwa wazazi wanaoachia watoto hovyo mitaani wachukuliwe hatua za kisheria. Sababu za kushauri hivyo ni utafiti niliofanya si watoto wote wana matatizo, bali ni utovu wa nidhamu tu. Watoto hao wana wazazi wao isipokuwa wanakataa kwenda shule tu.

Mheshimiwa Spika, watu wazima wanaoomba mitaani hali kadhalika na wao pia si wote wana matatizo kwani walio wengi wamegeuza hiyo ni ajira na wanadiriki hata kupeana fedha wanazoomba kwa kucheza michezo. Je, ni kweli watu hawa wana shida ya kweli?

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto lakini napenda nitoe shukrani kwa Halmashauri yangu ya Manispaa ya Temeke kwa kutekeleza mpango wa Serikali wa kutoa asilimia tamo (5%) ya mapato yake kwa maendeleo ya wanawake na vijana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja, nawasilisha.

MHE. MARGARET A. MKANGA: Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa viongozi wa Wizara hii ikiongozwa na Mheshimiwa Sofia Simba, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu wake, Wakurugenzi na watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, kwanza niunge mkono hoja na mchango wangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Benki ya Wanawake ni jambo la heri kwa wanawake wote Tanzania ila changamoto ni uhaba wa mitaji. Ni vyema sasa Wizara na Kamati husika kuhimiza Kamati ya Bajeti kuishauri Hazina kutimiza maagizo ya Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete kutoa fedha alizoelekeza ili kuiwezesha Benki hii kutanua shughuli zake kibiashara.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu kupuuzwa kwa taaluma ya Maendeleo ya Jamii, inasikitisha kuona kwamba kwa wakati wa sasa kazi/majukumu ya Maafisa Maendeleo ya Jamii henzieleweki katika Halmashauri zetu au Kata na kadhalika. Imekuwa ni jambo la kawaida kukuta maafisa hawa wanapangiwa kazi ya kukusanya ushuru kitu ambacho ni kinyume kabisa. Mkusanya ushuru si rafiki wa wafanyabiashara na Maafisa Maendeleo anapaswa kuwa rafiki wa wananchi wakiwijibika kuelekeza jamii, kuelimisha jamii kuhusu programu na miradi mbalimbali, kufanya utafiti wa masuala ya kijamii kwa mfano sababu za madanguro na kadhalika. Hivyo inaelekea hata viongozi hawa hawafahamu umuhimu/kazi za Maafisa Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, nashauri elimu itolewe kwa wananchi kuhusu umuhimu wa taaluma hii kwani Maafisa Maendeleo ni kama wasafisha njia za maendeleo, yafaa wathaminiwe kwa kupangiwa majukumu yanayowahusu.

Mheshimiwa Spika, tatu, pamoja na kwamba kisera suala la watu wenye ulemavu lipo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii lakini wenye ulemavu hao wanapaswa kuendelezwa kama wanajamii wengine katika masuala yote ya maisha. Hata hivyo sikuona maelezo yoyote kuhusu suala la wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu nawasilisha na kuunga tena mkono hoja.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara hii kuhusu mpango wa bajeti yake ya mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ije na mkakati maalum wa kupunguza idadi kubwa ya watoto ombaomba mitaani. Mfano ni hapa hapa Mji wa Dodoma karibu kila mtaa watoto wenyewe umri wa kati ya miaka 5 – 10 wanapita wakiomba omba. Huu ni mji mmoja tu nchini, wawekwe katika makazi maalimu hususan mayatima. Aidha wazazi wanaotelekeza watoto wao wachukuliwe hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani wa kuboresha Vyuo vya Maendeleo vilivyo chini ya Taasisi za kidini? Vyuo hivi vinahitaji msaada wa Serikali kwa kuwa vinapokea idadi kubwa ya watoto waliohitimu shule za msingi kuwajengea stadi mbalimbali, mfano ni Chuo cha Maendeleo ya Biblia cha Sanjaranda, Wilayani Manyoni Mkoa wa Singida. Aidha, nawakaribisha Waziri na Naibu Waziri wake watembelee Chuo hiki muhimu wajionee shughuli zake. Hapo nyuma kiliwahi kufadhiliwa na DANIDA lakini sasa hivi kimekosa msaada wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, Wizara ije na mpango maalum wa kupanua huduma za Benki ya Wanawake Tanzania ili kuwafikia wanawake wengi zaidi. Ikiwezekana mpango mkakati huo uwe kwa Mkoa nchini kuanzia Singida ambako ni katikati ya nchi na karibu na wanawake wote ni wana CCM na wana vikundi vingi vya ushirika.

Mheshimiwa Spika, suala la ukatili kwa akina mama ukabiliwe na Serikali maana limendelea kujitokeza hasa Mkoa wa Mara na Rukwa. Muswada uletwe Bungeni ili kupendekeza kutungwa kwa sheria kali za kuwadhibiti watu hawa wakatili wasiopenda kuendana na wakati. Ni aibu kuwa na watu wakatili karne hii ya 21.

Aidha sheria kali nazo zitungwe kukabiliana na tatizo la albino (walemavu wa ngozi). Washirikina wote watungiwe sheria kali za kuwatokomeza, wahanga wengi wa masangoma ni wanawake na watoto. Wizara hii ije na mikakati ya kuwadhibiti watu hawa wabaya.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. KHATIB SAIDI HAJI: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mchango wangu katika hoja hii muhimu kwa mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari hususan magazeti yanaongoza katika udhalilishaji wa wanawake katika nchi yetu. Kuna magazeti kadhaa ambayo kwa sasa ni maarufu kwa kuanika picha chafu za udhalilishaji wa akina

Nakala ya Mtandao (Online Document)

mama. Magazeti haya maarufu kama Ijumaa, Kiu, Risasi na kadhalika ambayo sasa ni maarufu yanaitwa magazeti ya udaku hayastahili kuwepo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inajua mambo haya machafu na Wabunge mara kadhaa tumekuwa tukilalamika kuwa magazeti haya lakini hakuonekani juhudhi na hatua za dhati za kukabiliana na tatizo hili. Naomba Serikali ichukue hatua sasa, haijachelewa.

Mheshimiwa Spika, suala la mauaji ya albino, napenda kutambua juhudzi za Serikali juu ya kukabiliana na janga hili kubwa la Taifa. Hata hivyo bado tatizo la mauaji ya albino linaendelea, kuwaresa Watanzania. Naomba sasa Serikali iongeze juhudzi za kuwalinda watu hawa kwa kuwasajili nchini kote na kuwatumbua kila maeneo wanayoishi ili iwe rahisi kuwashirikisha hata Serikali za Vijiji kupitia Polisi Jamii na sungusungu kusaidi kuwalinda albino.

Mheshimiwa Spika, tatizo la watoto wa mitaani limezidi kuongezeka katika nchi yetu, juhudzi halisi za kuondoa tatizo hili bado hazionekani, matokeo yake ni ongezeko la Taifa lisilo na maadili, tuelewe kwamba kukosa malezi bora kwa watoto ni matayarisho makubwa kwa Taifa la watu wakorofi. Masalia ya majambai, vibaka na wavuta bangi na dawa za kulevyia hupatikana kutokana na kada hii ya watoto wa mitaani. Ni wajibu wa jamii na Serikali tushirikiane kukabiliana na janga hili kubwa ambalo ukuaji wake hasa katika miji mikubwa katika nchi yetu lipungue hasa katika miji ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Mbeya, Tanga na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. PEREIRA A. SILIMA: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hoja hii. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa hotuba nzuri iliyoweka hadharani maendeleo lakini pia changamoto ya sekta ya jamii.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la watoto wa mitaani ni tatizo linalotia aibu na kulidhalilisha Taifa. Naelewa kwamba jibu la suala hili ni kuwa na familia imara na zenye maadili lakini pia naelewa nafasi ya Serikali ya kurekebisha haki hii. Naelewa kwamba Serikali inayo mikakati ya kutatua tatizo hili lakini naomba nikiri kwamba mingi ya mikakati hii haijaza matunda na naomba Serikali iendelee kujipanga ili tatizo hili lisiendelee kukua.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukatili wa kijinsia (GBV) wanawake wengi wamepata tatizo la kufanyiwa ukatili wakiwa kwenye ndoa zao na au kwenye

Nakala ya Mtandao (Online Document)

mahuiano mengine. Jambo hili ni kubwa na madhara yake ni makubwa katika jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, elimu inahitajika kukithirishwa ili jamii ielewe haki za kila kundi na kuzisimamia ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukeketaji mwaka 2012 mwezi wa Novemba nilialikwa na aliyekuwa Naibu Waziri (Mheshimiwa Ummy Mwalimu) kuungana naye huko Tarime kwa lengo la kuendeleza elimu ya kuacha ukeketaji wa watoto.

Mheshimiwa Spika, siku mbili nilizotumia kwenye Wilaya ya Tarime nilijiona uonevu mkubwa wa wasichana. Kubwa zaidi niliona wazee wa maeneo haya wakifanya sherehe bila woga wowote na naelewa kwamba kampeni hii ni ngumu lakini ni ya lazima.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. SAID M. MTANDA: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kuwapongeza kwa kazi.

Mheshimiwa Spika, nataka kufahamu ni lini watumishi wa Chuo cha Wananchi Chilala watalipwa fedha zao za malimbikizo. Je, wanaodai, wanadai shilingi ngapi na lini fedha hizo zitalipwa, orodha ya wanaodai ni Ndugu Regimius Komba shilingi 23,663,324/= na Ndugu M. G. Vara shilingi 9,319,575/= na jumla shilingi 32,981,720/=.

Mheshimiwa Spika, tatizo la uchakavu wa Chuo cha Chilala, Chuo kipo katika hali mbaya sana, majengo yake yana nyufa, je, kuna mpango gani wa kufanya ukarabati mkubwa kwa Chuo hiki.

Mheshimiwa Spika, suala la kutokuwa na gari Chuo kinaendesha kozi ya ufundu umeme wa magari bila kuwa na gari, je, Serikali ipo tayari kukipa Chuo gari dogo aina ya Noah ili wanafunzi wajifunze kwa vitendo? Nawasilisha.

MHE. JOHN J. MYIKA: Mheshimiwa Spika, maendeleo ya jamii yanapaswa kuongozwa na dira bora yenyе kutambua dhamira yake katika kuleta ustawi wa wananchi na ukuaji wa uchumi wa nchi. Aidha, maendeleo hayo yanapaswa kuzingatia usawa wa kijinsia na uendelevu wa kizazi cha sasa na cha baadaye kupitia makazi bora ya watoto. Suala la watoto na maisha yao ni muhimu kwa Taifa letu kwa kuzingatia kwamba nchi yetu ina watoto wengi kuliko vijana na wazee katika piramidi la idadi ya watu.

Hata hivyo Sehemu "B" ya hotuba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto inayohusu mapitio ya utekelezaji wa llani ya Uchaguzi ya CCM

Nakala ya Mtandao (Online Document)

ya mwaka 2010 kwa kipindi cha Januari, 2011 hadi Machi 2014 yanadhihirisha udhaifu mkubwa wa kushindwa kutekeleza ahadi kwa ukamilifu na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, aya ya 10 na 11 juu ya ajira na uwezesajji wa wananchi inaonyesha kasi ndogo ya kuimarisha na kupanua mafunzo ya vyuo vya maendeleo ya wananchi ili viweze kupokea vijana wengi zaidi na kuwapatia mafunzo ya stadi za maarifa ya kisasa katika fani za kilimo, biashara, ufundi na ujasiriamali. Hivyo katika mwaka 2014/2015 Wizara iongezwe bajeti ili iweze kukamilisha upanuzi wa miundombinu kwenye vyuo vyake.

Aidha wakati hatua hizo zikisubiriwa naomba kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam kwa kuwa Wizara haina Vyuo vya Maendeleo ya Jamii wala vya Maendeleo ya Wananchi, Wizara ianzishe kituo cha mafunzo au walau ishirikiane na vyuo vingine vya umma au kutumia majengo ya umma mathalani ya shule au ya Shirika la Maendeleo Dar es Salaam (DDC) kuanzisha mpango maalum ya mafunzo ya vijana wengi kwa muda mfupi, kuwaongezea stadi zenye kupunguza ukosefu wa ajira. Nipo tayari kutoa ushirikiano kwa Wizara kufanikisha azma hiyo kwa upande wa Jimbo la Ubungo.

Mheshimiwa Spika, katika aya ya 12 na 13 juu ya kuyaendeleza makundi mbalimbali kwa upande wa watoto, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto itoe maelezo ya kwa nini imechelewesha kukamilisha sera ya malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto. Aidha, Serikali ieleze lini sera hiyo itapitishwa? Mara baada ya sera hiyo kuitishwa Serikali irejee pia Sheria ya Mtoto na kuandaa mpango maalum wa malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto kwanza na kuiwakilisha Bungeni. Aidha katika kufanya hivyo Serikali ieleze iwapo itazingatie ajenda ya watoto (*Children's Agenda*) ambayo viongozi mbalimbali tulisaini mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Jamii yatachochewa kukiwa na demokrasia na madaraka ya umma kazi hii inaweza kufanya kwa kuambiwa na Serikali zenye kuongozwa kidemokrasia na kutoa madaraka kwa umma kuanzia kwenye ngazi za Serikali za Vitongoji, Vijiji na Mitaa, kwenye Kamati za Maendeleo ya Kata na haki katika Halmashauri za Wilaya. Hata hivyo kumekuwa na udhaifu katika utekelezaji wa dhana na dhima hii katika maeneo mengi nchini na hivyo kukwamisha dira ya kuwa na jamii yenye maendeleo. Aidha wadau wengine muhimu wa kuwezesha demokrasia na madaraka ya wananchi na kuchangia katika maendeleo ya jamii yenye usawa wa kijinsia na ustawi wa watoto ni Mashirika yasiyo ya Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Serikali inajitazama zaidi kama kiranja dhidi ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali badala ya kuyawezesha kisheria na kitaasisi kujisimamia na kushiriki katika maendeleo ya jamii. Sheria ya NGOs Na. 24 ya

Nakala ya Mtando (Online Document)

mwaka 2002 na hata Marekebisho yake ya mwaka 2005 hayajaweza kutengeneza muundo bora na kuweka mfumo bora wa kufanikisha azima hiyo.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NACONGO) kwa muundo na mfumo wake wa sasa nalo halitaweza dhima na dira kutimizwa ikiwa mabadiliko ya msingi hayatafanyika. Aidha utegemezi wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali usitazame tu kwamba ni tatizo la Mashirika yasiyo ya Kiserikali bali mfumo mzima wa kushughulikia sekta hiyo. Ni hatari kwa wananchi na nchi kwa Serikali kuachia utegemezi wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali kwa fedha za nje kuendelea. Ni muhimu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ikaongeza jitihada za kufanya yafuatayo kupunguza utegemezi wa fedha za nje wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali nchini:-

Mosi, Maafisa wa Maendeleo ya Jamii wasihusike tu kwenye kusajili Mashirika na kupokea taarifa za utendaji bali waelimishwe vilevile wananchi umuhimu wa Mashirika hayo na mchango wake katika maendeleo ili wanachama na wananchi wenyewe uwezo waweze kuchangia kuwezesha mashirika kujitegemea.

Pili, Serikali badala ya kuingia gharama kubwa za fedha za umma kwenye kandarasi kwa makampuni ya nje au ndani yenye kutaka faida kubwa itoe kazi kwa NGOs zenyeye kutekeleza miradi kwa gharama nafuu kwa kuwa hazitegemei faida.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuanzishwe mfuko wa kutoa ruzuku kwa NGOs – utegemezi wa mifuko ya NGOs kama Foundation For Civil Society (FCS) pamoja na kazi nzuri havitoshi.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya jamii yanaweza vilevile kuchochewa kwa kutoa msukumo katika kazi za kuijendeleza makundi mbalimbali katika Jumuiya ya Taifa kwa ujumla. Kundi la kwanza linalopaswa kupewa mkazo katika kutekeleza azma hiyo linapaswa kwa kundi la wanawake. Hata hivyo katika aya ya 14, 15 na ile inaonyesha kwamba bado kuna udhaifu katika kuweka mstari wa mbele mipango ya kuwezesha wanawake.

Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake unatengewa fedha kidogo, bilioni mbili tu kwa nchi nzima na hata hizo kidogo hazitolewi kwa ukamilifu kwa kuzingatia kuwa katika mwaka wa fedha 2013/2014 taarifa zinaeleza kwamba zinatolewa shilingi milioni 500 tu. Hivyo Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto itoe maelezo ni sababu zippi zingefanya fedha hizo kutokutolewa kwa ukamilifu?

Aidha, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ieleze ni jitihada gani kupitia Maafisa wa Maendeleo ya Jamii katika kila Kata na kupitia Waziri

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kwenye Baraza la Wananchi imefanya kuhakikisha kila Halmashauri nchini imetenga 10% ya mapato ya ndani kwa mikopo ya wanawake na 10% ya mikopo ya vijana kwenye mapato ya ndani kwa ajili ya vijana.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wangu toka mwaka 2011 nimefuatilia kwenye Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Kinondoni na kiwango cha fedha kuongezwa kutoka milioni 20 za zamani mpaka milioni 200 za mwaka 2013/2014 na sasa takribani milioni 300 kwa makadirio ya mwaka wa fedha 2014/2015. Hata hivyo kiwango hicho bado hakijafikia asilimia kumi (10%). Hivyo Wizara ishirikiane nasi kuifuatilia Manispaa ya Kinondoni

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono pia Kinondoni Youth SACCOS iweze kuwa chombo cha kuwaratibu vijana juu ya fedha za upande wa Serikali Kuu kwa kuwa kwa sasa fedha za Halmashauri zinapitia Commercial Bank (DCB) zamani Dar es Salaam Community Bank).

Nashukuru na kupongeza kwamba pendelezo mlilotoa mlipotembelea Benki ya Wanawake (TWB) ya kuanzisha kituo katika Jimbo la Ubungo. Tumekuwa tukiunganisha wanawake na vijana kuwapa mafunzo ya ujasiriamali na kutumia fursa za Benki ya DCB na Benki nyingine, niko tayari kushirikiana na Wizara na TWB kuhamasisha wanawake na vijana kutumia fursa za Benki hiyo katika vituo vipyta tayari ofisi ya Mbunge Ubungo ilishafika TWB makao makuu kufuatilia suala hili, ningomba majibu katika majumuisho ni lini TWB ipo tayari?

MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hivi sasa katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii wahitimu wanaongezeka mwaka hadi mwaka, hivyo mwelekeo mkubwa kuweka na shughuli za ujasiriamali ili vijana wakimaliza wawe na uwezo wa kuijendeleza kimaisha kwa kila siku. Sio rahisi kutokana na Serikali kuwa na mzigo mkubwa kuweza kuwapatia ajira wahitimu wote wa Vyuo hivi vya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa vijana hivi sasa lazima pawe na msisitizo wa maadili mazuri hivyo katika vyuo inawajibika kupata nyakati kila mara kusisitiza maadili mazuri ili jamii kujengeka.

Mheshimiwa Spika, Benki zinawajibu kusambazwa kila sehemu za Mikoa, Wilaya, Majimbo ili wananchi waweze kufaidika kutumia katika Benki hizo. Kwa kweli funzo la jamii kuweza kutunza fedha itasaidia ndani ya jamii, funzo kubwa katika Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake itasaidia sana.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto inawajibika kuongezewa fedha kutokana na huduma zilivyokuwa nyingi na yale yanayokusudiwa kutendeka yanazorota na kutokufikia kiwango kinacholengwa. Lakini hata hivyo tatizo kubwa ambalo linajitokeza ni ucheleweshaji wa fedha ambazo hazifiki fedha kwa wakati uliopangwa.

MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR: Mheshimiwa Spika, kutokana na mauaji ya walemaru wa ngozi, hofu imetanda kwenye familia zenyé watu wenye ulemarú wa ngozi hasa watoto. Wazazi wengi wamewapeleka watoto hao kwenye kambi au shule za boarding na kuwatelekeza bila kwenda kuwaona. Kuna shule ipo Shinyanga inaitwa Buhangija, kuna watoto wapo pale bila kwenda likizo maana wazazi wamewatelekeza.

Mheshimiwa Spika, Wizara ifuatilie kwa kina tatizo hili pale Shinyanga.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa mchango ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi nchini vyuo hivi ni muhimu sana kwani vinawasaidia sana wananchi hasa wenye uwemo mdogo, hata hivyo vinakabiliwa na changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na ukosefu mkubwa wa walimu, usafiri na fedha za kuendeshea hali hii inaenda kinyume na azma ya Serikali ya kuviboresha na kuviwezesha kutoa mafunzo ya VETA.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Maendeleo cha Wananchi cha Chala kina walimu wawili tu, workshop jengo limeanguka, usafiri unaotumika ni pikipiki tu, hakuna hadhi kabisa za uendeshaji, tunaomba tusaidiwe kwani kipo kwenye mpango wa maboresho.

Mheshimiwa Spika, nataka maelezo ni lini sasa chuo hiki kitapelekewa walimu wa kutosha na usafiri na changamoto zilizotajwa hapo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikopo kwa vijana na wanawake Halmashauri zetu zinakwepa kwa kiasi kikubwa kuwajibika kutoa fedha ambazo kisheria wanatakiwa kupeleka kwa vijana na wanawake na pale wasipopeleka hakuna hatua zozote zinazotolewa na kwa msingi huo kuzorotesha kabisa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa makundi haya mawili ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, pendekeso langu ni kwa Halmashauri zilazimishwe kutoa fedha kwa lazima na iwe ni kigezo cha kuwapatia fedha za miradi/matumizi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mauaji ya albino/wanawake wazee, jambo hili linaweza kukomeshwa kabisa likabaki historia nchini, nachelea kusema dhamira

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kamilifu bado. Naomba hatua thabiti zichukuliwe kukomesha kabisa. Albino ni watu, wanawake wazee ni watu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu watoto wa mitaani nashauri kuwa tatizo hili kama litapewa umuhimu muda mfupi linaweza kuisha. Nashauri Serikali kukabiliana kwa dhati kwa kutenga fedha na kuanzisha maeneo machache ya kulelea watoto hawa yenyé mtazamo wa uzalishaji kama vile kuanzisha Skimu za Kilimo cha Umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu dawa za kulevyia kadhalika ni tatizo ambalo tukiwa serious linaweza kupungua kuliko liliyvo sasa.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, nianze na kuwapongeza Waziri, Mheshimiwa Sophia Simba, Naibu Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana na watendaji wote wa Wizara hii kwa kufanya kazi nzuri kwenye mazingira magumu. Wizara hii ni muhimu sana sababu inashughulika na maendeleo ya wanawake, wanaume na watoto lakini siku zote imekuwa ikitengewa bajeti ndogo sana na fedha za maendeleo hawapatiwi kwa wakati au hawapati zote.

Mheshimiwa Spika, nalaani mauaji ya wanawake, niungane na wote waliolaani mauaji ya wanawake waliouwawa kule Mara pia yale ya vikongwe. Haya mauaji yamekuwa yaitokea kila mara, je, Serikali imeweka mikakati gani ya kudumu ya kuzuia mauaji au kukomesha kabisa?

Mheshimiwa Spika, pia nalaani vikali matendo ya ubakaji na ulawiti kwa watoto, vitendo hivi vimekuwa vikiongezeka kila siku hadi katika Mkoa wetu wa Iringa na Tanzania nzima na vitendo hivi vimekuwa vikiwaathiri watoto kisaikolojia, ni sawa na kesi ya mauaji watoto, wanaambukizwa hata UKIMWI, lakini hukumu za kesi zake zinachukua muda mrefu wakati wengine wanashikwa na vidhibiti kabisa. Wizara hii ina mkakati gani kuingilia suala hili?

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Benki ya Wanawake, niipongeze Wizara kupitia Benki ya Wanawake na Mkurugenzi Magreth Chacha kwa kufungua kituo cha kutoa mikopo katika Mkoa wetu wa Iringa. Tunaiomba Serikali iweke mkakati wa kufungua matawi ili benki iweze kuwafikia hata akina mama waliopo vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sheria ya kutenga 5% katika Halmashauri inasikitisha sana kuona bado kuna baadhi ya Halmashauri hazijaanza kutenga fedha hizo kwa ajili ya kina mama na vijana. Je, Halmashauri ambazo hazitengi fedha hizo zinachukuliwa hatua gani na tuambiwe ni chombo gani kinachoratibu fedha hizo kuhakikisha zinawafikia walengwa?

Mheshimiwa Spika, suala la Maafisa Maendeleo, kumekuwa na tatizo kubwa sana la Maafisa Maendeleo katika kata zetu, ni utaratibu gani unatumika katika kuwapeleka maafisa hao? Kwa nini Halmashauri zisipatiwe vibali vyaa kuwaajiri hawa Maafisa?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vyuo vya Maendeleo na Ustawi wa Jamii na bajeti finyu Mkoa wetu wa Iringa una Chuo cha Maendeleo cha Rungemba na Chuo cha Ustawi wa Jamii cha Ruaha, vyuo hivi viro katika hali ngumu sana katika miundombinu na tunaomba vyuo hivi vipatiwe kipaumbele kwa sababu vinasaidia sana katika kuelimisha jamii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuwapongeza Waziri, Mheshimiwa Sophia Simba pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana kwa kuongoza Wizara hii ambayo hata bajeti yake ni ndogo na haitoki yote pia. Hii ni hatari kwa Wizara hii, kwani inashindwa kutekeleza majukumu yake. Hivyo nawapa pole na ninawatia moyo mkaze buti kwani jamii inawategemea.

Mheshimiwa Spika, napenda Mheshimiwa Waziri aniambie kwa nini katika Halmashauri zetu wanapotenga asilimia tano (5%) Wabunge wa Viti Maalum hawashirikishwi kuamini utengaji huu kama kweli unafanyika na hata kuhakiki kama kweli wanaopewa ni kweli wahusika. Mheshimiwa Waziri unasema nini kuhusu Wabunge hawa wanawake kutokushirikishwa kabisa?

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kutoa ushauri kuwa na Muswada wa kuzuia vijana kuvali suruali chini ya makalio na wasichana kuvali matiti nje. Mheshimiwa Waziri naomba Muswada huu uandaliwe ili kurejesha heshima na utamaduni wetu wa Tanzania, kwa mfano, jirani zetu Kenya wamefanikiwa kwa suruali ambayo inajita "KK", Uganda pia imefanikiwa kupitisha sheria ya kuzuia vimini na mpango huu utafanikiwa kwani wamelivalia njuga. Tukiwa na nia hata sisi tutashinda.

Mheshimiwa Spika, napenda kumuuliza Waziri ana mpango gani endelevu kuhusu watoto wa mitaani kwani watoto hawa wamekuwa kero katika miji mikubwa kama Mwanza, Dar es Salaam, Arusha, Mbeya na miji mingine mingi. Hii ni aibu kwa wageni wajao nchini pia ni kero.

Mheshimiwa Spika, mauaji ya wanawake katika Mkoa wa Mara yamekuwa ni tishio sana kila kukicha wanawake wanauliwa, Mheshimiwa Waziri wauaji ni wanaume ni vyema sasa tukaandaa maandamano makubwa na

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kugomea kazi za mashambani na uchotaji wa maji visimani ili kazi hizi zifanywe na wanaume sasa ili kunusuru maisha yetu.

Mheshimiwa Spika, ni lazima sasa Serikali iangalie kuipatia fedha Wizara hii ili iache kuwa ombaomba inapotaka kufanya shughuli zake katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri mshike mkono Waziri wako ili muikwamue Wizara hii, kwani inaonekana kama ipo kwa bahati mbaya. Ni imani yangu mkishikamana mtafanikiwa nasi tutafanikiwa kabisa, msife moyo. Ahsante.

MHE. ELIZABETH N. BATENGA: Mheshimiwa Spika Wizara ya Maendeleo ya Jamii ni muhimu kwa kuwa ni mtambuka katika nyanja nyingi, watumishi wa maendeleo ya jamii pamoja na kuwa ni wachache pia hawatumwi kikamilifu na ipasavyo kutokana na rasilimali fedha kidogo inayotolewa, aidha Halmashauri za Wilaya kutojua umuhimu wao. Hawana nyezo za kufanya kazi.

Mtumishi wa maendeleo ni mtafiti kuhusu matatizo mbalimbali, ni muelimishaji na hatimaye kutathimini, hivyo ni msaada mkubwa kwa jamii mahali alipo. Matatizo mengi yanayokabili jamii zetu na hata familia hayafanyiwi utafiti na jamii kuelimishwa jinsi ya kuyatatua. Ni lazima kama tunataka Wizara hii (watumishi) ifanye kazi kwa mafanikio rasilimali fedha iongezwe lakini pia watumishi waongezwe ili angalau kila kijiji/mtaa awepo mtumishi.

Mheshimiwa Spika, Serikali/Wizara lazima iweke mkazo kwa jamii kuzingatia maadili hivyo wazazi wawe makini katika malezi ili kupunguza kumomonyoka kwa maadili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza sana Wizara kwa kazi nzuri inayofanya hadi kupelekea ongezeko la bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Pamoja na kwamba bado fedha ni ndogo lakini ongezeko la fedha za ndani kwa matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo zinatia moyo. Tuombe heri ili kwa siku zijazo maboresho haya yaendeleee.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa jitihada za kutoa mafunzo katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na pia kutoa mikopo mingi kupitia Benki ya Wanawake.

Mheshimiwa Spika, nina ushauri ufuatao, kwanza Wizara iendelee kuhamasisha wanawake wengi zaidi kuijunga na Vyuo vya Maendeleo ya

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Wananchi kwani idadi yao hairidhishi. Naomba pia mada zinazohusu uwajibikaji na maadili zifundishwe ikiwa ni pamoja na kuepukana na ulevi wa aina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa inaweza kuchukua muda mrefu kwa Benki ya Wanawake kufika kila Mkoa naishauri Wizara ijaribu kufanya utaratibu wa kupitishia huduma zake kwenye taasisi nyingine, kwa mfano katika Wilaya ya Tandahimba kule Mtwara ipo Benki ya Wananchi, napendakeza Wizara ipeleke huduma Mtwara kupitia Benki ya Wananchi Tandahimba.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Igala tunaomba Chuo cha Maendeleo ya Jamii katika Jimbo letu ili vijana wa jinsia zote wapate mafunzo ya mbini na uwezo wa kujikimu na kujitegemea. Jimbo la Igala ni la mwisho kimaendeleo nchini Tanzania (taarifa ya maendeleo ya matumizi ya chandaria kimoja kila Mtanzania Prof. Jeffery Sykes- mchumi, uchumi wa Afya, Harvard university Marekani) imetajwa Wilaya ya Uyui lakini ni Jimbo la Igala kwani Tabora Kaskazini kuna mradi wa UNDP wa Mbola Milleniuam Village una workshop, shule ya msingi, sekondari, visima, zahanati na wanatoa pembejeo za kilimo na wana trekta.

Mheshimiwa Spika, Tawi la Benki ya Wanawake Tanzania mwakani wajenge kituo angalau Tabora ili Igala nayo ifaidike kwa mikopo ya akina mama na waweze kupata mitaji ya vikundi na mmoja mmoja katika biashara, kilimo na hata ufugaji samaki kwa mabwawa. Elimu ni muhimu wapate mafunzo ya ujasiriamali ili mitaji waweze kuikuza kwa ufanisi zaidi na iwe endelevu.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu watu wenye ulemavu ni jukumu la Serikali la kuwalinda, kuwahudumia, kuwaendeleza na kuhakikisha wanapata elimu. Bado katika mashule yetu, maofisi na sehemu nyingi bado miundombinu siyo rafiki wa watu wenye ulemavu hata vyoo siyo rafiki. Ningependa kupata majibu kulikuwepo na agizo la kupiga kura ya kutambua wahalifu wanaouwa watu wenye ulemavu wa ngozi (albino) umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, kipindi cha Bunge Maalum katika televisheni ya Taifa - TBC kilikuwa na mkalimani aliyeeweza kuwasaidia walemavu wasiosikia kuweza

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kufuatilia Vipindi vya Bunge lakini sasa hivi huduma hiyo haipo. Je, kumetokea nini?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 sheria hii ni kandamizi, zaidi inawakandamiza watoto/wanawake, watoto wanaruhusiwa kuolewa wakiwa watoto. Ni zaidi ya miaka mitano tumekuwa tukipigia kelele sheria hii irekebishwe mpaka leo hii bado. Je, ni sababu zipi zinazochelawesha marekebisho ya Sheria ya Ndoa ambayo inahalalisha ndoa za utotoni italetwa hapa Bungeni? Tunaomba *time frame* ni lini?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mashirika yasiyo ya Kiserikali kuna mashirika mengi yaliyosajiliwa mengi yakiwa ni ya kulea watoto wanaoishi katika mazingira magumu ikiwa ni pamoja na watoto yatima, inabidi Serikali iyakague mashirika haya sababu mengi ni matapeli, wanapata fedha kutoka nje lakini baadhi yao hawatoi huduma zinazostahili mfano, ni kituo cha mkombozi kilichopo Moshi. Badala ya kuwasaidia watoto hawa pamekuwa ndiyo kituo cha watoto wenye uovu mkubwa na tishio kwa jamii. Ningependa kujua kuwa shirika liitwalo Sisi kwa Sisi lililokuwa lina-promote ushoga, je, Serikali halifahamu hili? Na kama wanafahamu ilikuwaje wapate usajili wakati nchi yetu tunapiga vita ushoga? Naomba jibu

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuperomoka kwa maadili nchini imekuwa ni kawaida kwa vijana wetu kuvaa nguo zenyenye kuonyesha maumbile yao hata watu wazima wanafanya hivyo. Na hii mitandao ndiyo inayochangia zaidi kwa kusambaza picha chafu. Ni muda muafaka sasa kwa Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano waweze kufuatilia wote wenye kusambaza picha hizo wakamatwe, watajwe hadharani na wapewe adhabu ya juu na kifungo hii kwa kiasi kikubwa kitapunguza uhalifu huu.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hotuba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, napenda kumsisitiza Waziri atembelee Chuo cha Maendeleo Wilaya ya Kilombero kilichopo Ifakara ili akajionee mwenyewe matatizo yaliyopo na kuyapatia ufumbuzi. Ni miaka takribani mitatu mfululizo nachangia mapungufu ya Chuo hicho ambacho ni mkombozi kwa wanawake lakini Wizara haijafuatilia hadi leo.

Mheshimiwa Spika, suala la unyanyasaji wa watoto wa kike na kiume, watoto wa kiume kufanyiwa vitendo vya ukatili na kulawitiwa ama mashulen, na ndugu ama kwa kudanganywa na watu wazima mitaani. Wizara ina mikakati gani ya kukomesha vitendo hivyo? Imefikia wakati sasa kuwe na makongamano katika ngazi mbalimbali vijiji na mashulen kueleza vitendo hivyo. Pia kuwepo na dawati la jinsia mashulen na ofisi ya kijiji ili kuwapa nafasi

Nakala ya Mtandao (Online Document)

watoto wanaofanyiwa vitendo vya ukatili kupeleka taarifa na kuchukua hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, kasi ya watoto kulawitiwa ni kubwa na likiachwa ilivyo hapo baadaye Taifa litakuwa na mashoga wengi na wataanza kudai haki zao kwani hawataweza kujibadili tena kuwa na maisha ya kawaida, tulinusuru Taifa chonde chonde.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii kwa umuhimu wake inahitaji mjadala wa Kitaifa, Wizara hii ni nyeti kwa wananchi, lakini wananchi wengi wanadhani ni kwa wanawake na watoto tu na ndiyo maana Maafisa wa Ustawi ngazi ya Wilaya na Kata na kwingineko hawapo, hata wakiwepo hawatengewi bajeti wala hawana vitendea kazi. Nashauri kuwe na kongamano la kupata uelewa.

Mheshimiwa Spika, ipo haja ya kuwepo na sheria inayosimamiwa vyema na watoto waelimishwe kuzielewa ili wadai haki zao.

Mheshimiwa Spika, uvezeshaji wa wanawake kwa kupeleka vituo vya ukopeshaji, ningependa kujua ni lini Wizara itaelekeza Benki ya Wanawake ikafungue tawi Morogoro, pia vituo vya mikopo katika Wilaya ya Kilombero, karibu sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mauaji ya wanawake wenyewe ulemavu unaoendelea nchini, ni vyema Serikali ikachukua hatua madhubuti ya kuelimisha kukomesha mauaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali ichukue hatua madhubuti ya kukomesha mauaji ya wanawake Wilaya ya Musoma Vijijiini yaliyotokea mfululizo kwa wanawake waliokuwa wako shambani kutafuta chakula kwa ajili ya watoto/familia, inasikitisha sana. Wizara ishirikiane na Wizara ya Mambo ya Ndani iweke ulinzi kama Kanda Maalum kwa Polisi kukomesha mauaji hayo.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ipewe bajeti ya kutosha ili ikatekeleze majukumu yake ipasavyo.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wale wachangiaji niliokuwa nao wamekwisha. Kwa hiyo, nawapa nafasi Wizara kuandaa majibu yao. Saa 10.00 tukija wataanza kujibu. Kwa hiyo, nawashawishi muweze kuwahi kusikia yale mliyokuwa mnasema, mjibiwe. Mara nyingi unakuta wanakuwa watu watatu au wanne tu. Sasa Mawaziri wanaieleza tu Hansard. Kwa hiyo, tukirudi saa 10.00 wanajibu hoja zinazostahili.

Nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

(Saa 6.38 mchana Bunge lilahirishwa hadi Saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, asubuhi wale walioomba kuchangia walikwisha kwenye orodha yao yote. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri atatumia dakika 35; yaani hawa wana saa yao, Waziri ana saa moja, mchangiaji dakika 15 lakini wanaweza kugawana muda wao kadiri wanavyotaka kufanya. Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO:

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa fursa hii. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema hivyo kuwemo katika Bunge hili Tukufu na kuchangia hoja iliwasilishwa hapa Bungeni leo tarehe 17 mwezi wa Tano.

Pili, nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kunitua kuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia Watoto. Pia nimshukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu ambao ni hakika wamechangia katika uteuzi wangu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Sophia Simba, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa jinsi alivyopokea kwa upendo na kunipa ushirikiano wa hali ya juu tangu nimeteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuishukuru na kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii kwa michango, ushauri, maoni, wanayotupa; tunaahidi kuwa tutazingatia maoni, maelekezo na ushauri wao katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, sasa naomba nitamke rasmi kwamba naunga hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa nichangie hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto, aliyoiwasilisha leo hapa Bunge kwa kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge. Majibu yangu yatalenga hoja zilizoelekezwa kwenye maeneo yafuatayo:-

Vyuo vya Maendeleo ya Jamii (CDTs) na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs) na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) na masuala kuhusu Maafisa Maendeleo ya Jamii.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kwa kweli vilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 kwa kurithi majengo mbalimbali yakiwepo Vijijini na maeneo mengine.

Vyuo vilivyojengwa kwa fedha za Maendeleo ya Jamii ni Vyuo vinne tu nchini, ambavyo viko Sengerema, Bigwa, Handeni na Ngara. Ilipofika mwaka 1987 Tume ya Nsekela iliundwa na Tume ilielekeza kwamba Vyuo hivi viende Wizara ya Maendeleo ya Jamii.

Kwa hiyo, Vyuo hivi vimerithiwa na viko takriban 55, na ndiyo maana Wabunge wengi wanavyosema kwamba Vyuo hivi vinahitaji maboresho, hiyo ni kweli kwa sababu tumerithi yale majiengo toka mwaka 1975. Vyuo vilivyojengwa per-se ni vinne tu. Kwa hiyo, tunaposema Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vinahitaji ukarabati, tunahitaji maboresho, hilo ni jambo ambalo Wizara inalizingatia.

Mheshimiwa Spika, tumetembelea maeneo mengi ya Vyuo na pia tunaungana na mialiko mbalimbali ya michango ya Wabunge kwa maandishi kwamba tutembelee maeneo ya Vyuo vyao. Baadhi ya Wabunge waliosema tutembelee ni pamoja na Mheshimiwa Lwanji, Mheshimiwa Lekule Laizer na Mheshimiwa Said Mtanda na wengine.

Mheshimiwa Spika, Vyuo hivi ndivyo vinavyozalisha Maafisa Maendeleo ya Jamii nchini, hivyo ni kimbilio la wananchi na tegemeo kubwa na vinatoa stadi za maisha na maisha bora kwa kila Mtanzania na Matokeo Makubwa Sasa. Hivyo siyo kweli kwamba Serikali ya CCM inawahadaa wananchi bali kwa kupitia vyuo hivi imekuwa ni kimbilio kubwa.

Ushahidi umeonesha hadi sasa watoto 146,383 wame-graduate tangu mwaka 2010/2011, 2011/2012, 2013 hadi 2014, yaani kwa muda wa kipindi cha miaka mitatu. Naomba Waheshimiwa Wabunge mwangalie jedwali namba moja, hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Spika, katika maisha lazima tuwe na malengo, (*vision*); *Millennium Development Goals*.

Serikali ya CCM huweka mipango mizuri ya kibajeti na kifedha, lakini tatizo ni kwa wanaokwepa kodi. Serikali ya CCM ndiyo pekee inayomjua Mtanzania alikotoka, alipo, na anapokwenda, na haina nia ya kuwahadaa wananchi bali kuwapa maisha bora kwani hata ada za Vyuo hivi huwa ni ndogo sana ukilinganisha na wananchi ambao wanalipa ada kwenye Vyuo vya binafsi. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya CCM kwa nia njema kwa wananchi wa Tanzania.

Naomba nimnukuu Mzee Nelson Mandela alipotembelea mara ya mwisho nchini Tanzania, alisema maneno ya Kiingereza kutokana na Vyuo hivi

Nakala ya Mtandao (Online Document)

vyo FDCs alisema kwamba Serikali hii ya CCM inafanya kazi na alitumia maneno akasema, *Long Live CCM. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zilikuwepo hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge waliozungumzia kuhusu mashirika yasiyo ya kiserikali. Naomba niwatambue Wabunge 18 na majina yao nitaomba yaingie kwenye Hansard kama jinsi ambavyo walichangia.

Hoja ya kwanza ilikuwa inahusu taarifa ya mchango wa NGOs kuwasilishwa Bungeni. Ushauri wa Kambi ya Upinzani Bungeni kuhusu uwasilishwa ji wa taarifa ya michango wa NGOs nchini kwa kweli umepokelewa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja inayohusu masuala ya marekebisho ya Sheria ya NGOs namba 24 ya mwaka 2002.

Kuhusu hoja hii, siyo kweli kwamba Sheria ya NGOs Na. 24 ya mwaka 2002 kama ilivyorekebishwa ilipitishwa kwa nguvu kwani taratibu zote za utungaji wa sheria zilizingatiwa ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha wadau mbalimbali na kupitishwa na Bunge. Kwa sasa Serikali iko katika mchakato wa kuifanyia mapitio ya Sera ya Taifa ya NGOs ya mwaka 2001 ili kuwezesha marekebisho ya Sheria ya NGOs kwa lengo la kuboresha mazingira ya utendaji na mchango wa NGOs nchini.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja pia inayozungumzia mkakati wa Wizara juu ya kuhakikisha NGOs zinatekeleza majukumu yaliyokusudiwa kwa mujibu wa uanzishwaji wake. Kuhusu mwingiliano wa kiutendaji na kimajukumu baina ya Idara ya Uratibu wa NGOs na RITA; kuhusu usajili wa kufutwa kwa Shirika la Tanzania, Sisi kwa Sisi; kuhusu muundo wa Mabaraza ya Taifa ya NGOs kuiwezesha NGOs kujisimamia na kushiriki katika maendeleo ya Jamii kwa kuwa huru na NGOs kuingiliwa na Serikali. Kulikuwa na hoja pia kuhusu NGOs kuwa tegemezi kwa wafadhili toka nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hoja zote hizo, naomba kusema, pia kulikuwa na hoja inayohusu Shirika la WAMA kujihusisha na masuala ya siasa.

Kuhusu WAMA kujihusisha na siasa katika uchaguzi wa mwaka 2010 Wizara haijapata ushahidi wowote kuhusu suala hilo, bali Mheshimiwa Mama Salma Kikwete alishiriki binafsi katika masuala ya kampeni kama mke wa Mheshimiwa Rais na siyo kama Shirika la WAMA. Ndiyo maana tunasema Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto haijapata ushahidi, bali alishiriki kama mwananchi, kama *individual*.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimwia Spika, kuhusu mikakati ya Wizara kuhakikisha NGOs zinatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa malengo ni kwamba NGOs czinatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa malengo yaliyoanzishwa katika mashirika haya, na ni pamoja na Maafisa Maendeleo ya Jamii wa ngazi za Wilaya na Mikoa walioteuliwa kuwa Wasajili Wasaidizi ili kuyafuutilia mashirika hayo katika Serikali za Mitaa na ngazi za Mikoa, kwamba hawa Maafisa wanazifuutilia zile NGOs kule kule katika Serikali za Mitaa.

Pia Baraza la Taifa la NGOs limeandaa Kanuni za Maadili ya NGOs na lipo katika hatua za uundaji wa Kamati za Maadili za NGOs katika ngazi mbalimbali. Pia kuna kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji wa NGOs nchini; na vile vile Wizara kupitia Sheria ya NGOs namba 24 ya mwaka 2002 imeweka utaratibu wa NGOs kuwasilisha taarifa za mwaka za fedha zilizokaguliwa na kazi za NGOs kwa msajili wa NGOs.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hakuna mwingiliano wa kimajukumu na kiutendaji baina ya Idara ya Uratibu wa NGOs nchini ya Wizara yangu, yaani Maendeleo ya Jamii na RITA chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa kuwa kila mamlaka ina majukumu yake kisheria.

Aidha, naomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa usajili wa Makao ya Watoto hufanyika chini ya Idara ya Ustawi wa Jamii nchini, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Kuhusu Shirika la Tanzania Sisi kwa Sisi, lilisajiliwa mwaka 2011 kama Shirika la Kutetea Haki za Binaadamu na Masuala ya UKIMWI na Virusi vya UKIMWI. Hata hivyo, uchunguzi uliofanywa na Wizara ulibaini kuwa Shirika hilo lilikua likijishughulisha na uhamasishaji wa Ushoga, kinyume na malengo ya usajili wake. Kutowana na hilo, Serikali ilifuta usajili wake kwa kuwa kufanya hivyo ni kinyume cha Sheria za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuna Wabunge walihoji kuhusu muundo wa Baraza la Taifa la NGOs. Kwa mujibu wa Sheria ya NGOs namba 24 ya mwaka 2002 muundo uliopo unatoa uhuru kwa mashirika haya kushiriki katika maendeleo pasipo kuingiliwa na Serikali wala chombo kingine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushauri wa kuondokana na utegemezi wa NGOs kwa wafadhili kutoka nje ya nchi, Wizara ilifanya marekebisho ya Sheria ya NGOs mwaka 2005 kuruhusu NGOs kuanzisha na kuendesha miradi kutengeneza faida ili kuondokana na utegemezi wa aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia zilikuwepo hoja mbalimbali zinazohusu Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kulikuwa na hoja ambayo inasema, Muswada wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii, Tengeru kuijidesha chenyewe umefikia wapi? Kama Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ilivyoainisha kwenye Taarifa yake, Muswada huo umewasilishwa Bungeni, ukisubiri kuwasilishwa rasmi na Waziri mwenye dhamana pindi Bunge litakapopanga ili Chuo cha Maendeleo ya Jamii, Tengeru kiweze kuwa Chuo kitakachojitegemea.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja inahusu mgogoro wa ardhi kati ya Chuo cha Maendeleo ya Jamii, Rungemba na wananchi. Ni kwamba katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii, Rungemba eneo la ekari 10 ambalo Serikali ililirithi kutoka kwa mmiliki wake, Marehemu Marion Chesham, Lady Chesham, mpaka sasa halina mgogoro wowote na hati miliki ya eneo hilo namba 22437 ipo.

Mwaka 1989 Chuo kiliomba kuongezewa ardhi zaidi kutoka kijiji cha Rungemba na kijiji cha Kitelewasi. Eneo la Chuo ambalo limeshapimwa ni hekta 2063. Namba ya ramani ya eneo hilo ni 31195. Mgogoro uliopo sasa ni mgogoro kati ya eneo lililotolewa na kijiji cha Rungemba. Hata hivyo, mgogoro huo upo katika hatua za mwisho za usuluhishi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukarabati, ni kwamba Ukarabati wa majengo na miundombinu ya Chuo cha Maendeleo ya Jamii, Rungemba unaendelea. Pia kulikuwa kuna hoja kwamba kuna upungufu wa fedha zinazotolewa kwenye ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Jibu ni kwamba, ukarabati wa majengo na miundombinu ya Chuo cha Maendeleo ya Jamii, Rungemba unaendekea kufanyika kwa awamu. Katika kipindi kilichopita, Wizara yangu ilikarabati mabafu na Vyoo vya Wanachuo. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara itaendelea kukarabati maeneo mengine kulingana na upatikanaji wa fedha ambazo Waheshimiwa Wabunge leo tutakuja kuwaomba. Aidha, Wizara yangu imeshaingiza umeme wa gridi ya Taifa katika Chuo hiki.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya wahitimu wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii wanaongezeka mwaka hadi mwaka; kwa kuwa siyo rahisi kuwaajiri wote, hivyo wahamishwe kujihusisha na shughuli za ujasiriamali. Jibu ni kwamba, tunaendelea kuwasiliana na TAMISEMI ili wakihitimu, ikiwezekana waajiriwe moja kwa moja kama Waalimu. Kwa hiyo, hiyo ni rai ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii kuomba TAMISEMI waweeze kuwachukua Maafisa Maendeleo ya Jamii moja kwa moja kutoka kwenye Vyuo vyetu vya kitaaluma.

Pia wanafushwa ujasiriamali na baadhi yao wanajajiri, na wengine wanaajiriwa na NGOs na sekta binafsi na wanahamasishwa kujunga katika vikundi ili wakopeshwe.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba Wizara iboreshe taaluma inayotolewa na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ili wahitimu wanaotoka katika Vyuo hivi waweze kutumia vyeti vyao kuingia Chuoni. Wizara imefanikiwa kudurusu mitaala ya wanafunzi katika Vyuo vyake. Mitaala iliyodurusiwa imeboreshwa na kuzingatia mwongozo wa Baraza la Itifaki la Mafunzo ya Ufundı, NACTE, ambalo linasimamia ubora wa mafunzo yanayotolewa katika Vyuo vyote. Hali hii inawezesha wahitimu wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii kuweza kuijunga na vyuo vingine vya elimu ya juu kulingana na ufaulu wao.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba Jimbo la Igala lipatiwe Chuo cha Maendeleo ya Jamii ili vijana wa jinsia zote wapate mafunzo ya mbinu na uwezo wa kujikimu pamoja na kujitegemea. Wizara imepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Igala kuwa hakuna Chuo cha Maendeleo ya Jamii katika Jimbo la Igala, Wizara itaendelea kushauriana na eneo husika kuangalia uwezekano huo kulingana na upatikanaji wa rasilimali na kuendelea kuomba mchango wa wananchi katika uanzishwaji wa Vyuo hivi, kwa sababu Vyuo hivi vya Maendeleo ya Wananchi ni Vyuo vya Wananchi wenyewe katika eneo husika.

Katika maeneo yote, Wakurugenzi ndio wamekuwa Wenyeviti wa Bodi za Vyuo hivi, na hata kozi zinazotolewa katika vyuo hivi kimsingi, inategemea na eneo. Kama ni eneo ambalo shughuli nyingi ni za kilimo, basi wanatoa kozi za kilimo; kama ni eneo la ufugaji, wanatoa kozi za ufugaji au uvuvi au ufundı wa magari, ufundı wa umeme majumbani, useremala, uashi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lingie ni kuhusu Chuo cha Maendeleo ya Jamii, Rungembä kipandishwe hadhi kuanza kutoa Shahada badala ya Stashahada. Wizara itazingatia ushauri huu baada ya kukiwezesha Chuo kutimiza vigezo. Maana ili kipandishwe hadhi, lazima kuwe na vigezo, vimekidhi? Kwa hiyo, Wizara itaangalia kukiwezesha ili Chuo hiki kiweze kutimiza vigezo vya kuanzisha mafunzo hayo kufuatana na mwongozo wa Baraza la Ithibati la Mafunzo ya Ufundı (NACTE).

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba Serikali iweke mkakati wa Uongozi bora katika Vyuo vya Maendeleo Jamii ili vifundishe Jamii inayovizunguka. Jibu ni kwamba, Wizara illanda mpango mkakati wa utoaji wa mafunzo mbalimbali yakiwemo ya uongozi bora katika jamii inayozunguka Vyuo. Katika mpango huo, kila Chuo kimeainisha Vijiji vinne kwa ajili ya utoaji wa mafunzo hayo. Kwa mfano, Chuo cha Tengeru kimekuwa kikitoa mafunzo hayo katika Vijiji vya King'ori, Marewu, Nambala na Kikwe vilivyo katika Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru.

Mheshimiwa Spika, sasa nijikite katika hoja ya upungufu wa Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Kata. Sera ya Maendeleo ya Jamii inaelekeza

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kwamba kila Kata iwe na Mtaalam wa Maendeleo ya Jamii. Mpaka sasa ni asilimia 39 tu ya Kata zote 3,339 ndizo zenyé wataalam hawa. Jumla ya Kata 1,045, sawa na asilimia 61 kwa kweli hazina wataalam wa Maendeleo ya Jamii. Wizara inaendelea kuishauri Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI kutenga fedha za kutosha ili waweze kuajiriwa. Aidha, Wizara yangu inaendelea kuzalisha wastani wa wataalam wa Maendeleo ya Jamii 2,800 kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umuhimu wa sekta nyingine kuwatumia wataalam wa maendeleo ya Jamii katika kuelimisha na kuhamasisha utekelezaji wa mipango ya Maendeleo ya Jamii, Serikali imekuwa ikitenga fedha kuanzia mwaka 2009/2009 ili kuiwezesha Idara ya Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri kufanya kazi zake kwa ufanisi. Serikali kupitia TAMISEMI, inaendelea kuhimiza Halmashauri kutenga fedha za kutosha na kuwapatia vitendea kazi na vyombo vyá usafiri ili waweze kuhamasisha jamii kushiriki kikamilifu katika programs za maendeleo.

Aidha, Wizara yangu imepokea ushauri wa kupokea Baraza la ushauri la Wazee wastaafu wa Maendeleo ya Jamii. Aidha, Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi yakiwemo masuala ya uandishi wa Miradi, ili kuwajengea uwezo zaidi. Pia Wizara inaomba, katika masuala mbalimbali, katika Halmashauri zetu na maeneo mengine, Maafisa Maendeleo ya Jamii Hawa wawe wanatumika. Kwa maana wao ndio waliosomea masuala ya maendeleo ya jamii; iwe ni kwenye ujenzi, iwe ni kwenye masuala ya elimu, masuala ya afya, ni muhimu kushirikisha Maafisa Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba, Sekta ya Maendeleo ya Jamii, imekuwa ikijikongoja. Lini tutaitumia sekta hii ipasavyo? Sekta hii kwa kweli haijikongoji. Sekta ya Maendeleo ya Jamii, ina watumishi katika ngazi za Wizara, Mikoa, Halmashauri hadi katika Kata. Kwa hiyo, ni muhimu tukawatumia watumishi hawa. Sekta hii itatumika ipasavyo pale itakapoweza kushirikishwa na wadau mbali mbali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, ninaomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi, kutoa ufanuzi wa baadhi ya maeneo ya hoja zilizoteolewa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofí*)

SPIKA: Ahsante. Sasa nitamuita...

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofí/Kicheko*)

SPIKA: Wewe unafikiri atapinga! Mheshimiwa mtoa hoja, unazo dakika 45.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja nilioiwasilisha asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipogneza sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, kwa kuisimamia Wizara yangu kwa umakini mkubwa.

Naishukuru Kamati kwa jitihada zao za kuiwezesha Wizara kuongeza Bajeti ya Serikali, ingawa bado ni finyu, ukilinganisha na majukumu ya Wizara. Pia naipongeza sana hotuba ya Kambi ya Upinzani na ninaahidi kwamba Wizara yetu itajibu zile hoja na itafanya kazi yale maoni mazuri ambayo wametupatia. Wizara kwa upande wake inachukua hatua mbali mbali za kupambana na ufinyu wa Bajeti. Moja ya hatua hiyo ni kuandika maandiko ya miradi na kuwasilisha Serikali na kwa wabia wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, jumla ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja yangu ni 58, na kati yao 17 wamechangia kwa kuongea na 44 wamechangia kwa maandishi. Katika michango iliyotolewa, iko inayotoa ushauri wa kutusaidia na mengine ni maswali ambayo nitajaribu kuyajibu hapa.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea zaidi, naomba nichukue nafasi hii, kwa masikitiko makubwa Wizara yangu inalaani sana viendo vyta ukatili wanavyofanyiwa Wanawake, Watoto wa kike na wakiume na katika maeneo mengi, wanawake wanawatendea ukatili wanaume, lakini hasa ukatili mkubwa wanaofanyiwa wanawake hususan katika Kanda ya Ziwa. Tuna laani kabisa vitendo hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue fursa hii kuungana na wapenda haki wote duniani kulaani kwa nguvu zote, kitendo cha utekeaji wa wasichana zaidi ya 200 huko Nigeria, kilichofanywa na kikundi cha Boko Haram. Natoa wito kwa wapenda haki wote duniani kuendelea kufanya kila juhud ili wasichana hawa waweze kuachiliwa haraka iwezekanavyo na bila ya masharti yoyote.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa unyenyekevu na heshima kubwa niwashukuru Wabunge wa Bunge hili, pamoja na Wajumbe wa Bunge la Katiba, pamoja na ndugu jamaa na marafiki ambao walinifariji wakati wa kipindi kigumu cha msiba wa mtoto wangu mpandwa Lyford.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, ningependa niseme machache kuhusu WAMA. Leo nimesikitika sana ilipoonekana kama WAMA inafanya kazi ambazo siyo zake. WAMA imeandikishwa kisheria na ina majukumu yake na inayafanya majukumu kwa uadili fu sana. (Makofi)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mama Salma Kikwete – Mwenyekiti wa WAMA, amekuwa akifanya shughuli zake kwa kiwango kikubwa sana. Nashangaa sana leo kuona kuna watu wanahoji walipomwona amekwenda kumsaidia mume wake kwenye campaign. Nyie wote hapa mkiwa kwenye campaign zenu wake zenu hawalali, lakini ye ye mmeona mseme.

Mheshimiwa Spika, nataka niondoe ile kejeli kwa kutaja mambo machache tu ambayo WAMA ambayo iko registered chini ya NGO, imekuwa ikiyafanya.

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti wa WAMA Mama Salma Kikwete, amefanya kazi kubwa sana kwenye fani ya Elimu ya Mtoto wa Kike na Mapambano ya Kupunguza Mimba Mashulen. Katika maeneo aliyoyafanya, kwa kweli Mikoa ile mimba za utotoni zimepungua. Mama huyu amekuwa mstari wa mbele katika campaign za chanzo mbalimbali, ameweza kuwawezesha wanawake kiuchumi mpaka sasa idadi tuliyokuwanayo wanazidi wanaweke 60,000. (Makof)

Kutokana na kazi nzuri anazosifanya. Ningelipenda mjue, kuna Chama cha Wanawake wa Marais, inayoitwa Jumuiya ya Wake wa Marais Duniani. Katika Chama hicho, Mama Salma Kikwete, ye ye ni Vice Chairperson wa Jumuiya hiyo kwa upande wa Horn ya Afrika, nchi 11 za za Afrika. Yeye ni Vice President, na amepata kutokana na michango yake. Akienda katika nchi za Kimataifa wana-recognize kazi nzuri ambayo ameifanya. Hiyo organization inaitwa *Organization of African First Ladies Against Aids*. Kwa hiyo, mnaweza mkaingia kwenye mtandao mkaona, badala ya kuzungumza tu hapa. (Makof)

Mheshimiwa Spika, Mama Salma ameishapata awards nyingi huko duniani, pamoja na hapa nyumbani tumekuwa tukimpattia tuzo; lakini mimi nitasema zile za nje. Miongoni mwa tuzo hizo, mojawapo amepata MDG – Woman Achievement Awards; ameisaidia Tanzania ku-achieve kwenye MDG goals. Lakini pia amepata Award ya Global Inspirations Leadership Award, aliyoipata kule New York, kwa kazi nzuri ya campaign anayoifanya; Campaign ya chanjo na campaign ya chanjo ya cervical cancer, ambayo Mama Salma yuko mstari wa mbele. Lakini ili nisipoteze muda na nyinyi ni wasomi wazuri, mkitaka taarifa zaidi, naomba mtembele Web Site ya WAMA, www.wamafoundation.org.tz. Au kama mnaona taabu mnaweza mka-Google tu mkapaa WAMA Foundation, mambo yote yako pale.

Nadhani baada ya hapo, tutakubaliana kwamba kazi inafanyika. Lakini siku ya campaign mama akika nyumbani baba itakuwaje? (Makof)

Mheshimia Spika, naomba sasa nijibu hoja za Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii. Walihoji Serikali irudishe mfumo wa zamani wa fedha za

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, kulipwa katika Hazina ndogo. Badala ya kutumia mfumo wa sasa wa kupeleka kwenye retention.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa upande wake na sisi tumekuwa concern, kwa vile zile pesa za retention hazifiki, au zinakuja kidogo sana, kwa hiyo, kwenye Vyuo kunakuwa na matatizo ya kununua vitu vya muhimu sana. Kwa hiyo Wizara imekaa kikao na Hazina na kujadili kuhusu kutumia fedha zote zinazokusanywa na Vyuo kupitia Hazina Ndogo. Wizara pia imeiandikia barua Hazina ikiomba kutumia utaratibu wa malipo kupitia Hazina ndogo. Wizara bado inasubiri majibu kutoka Hazina, na Hazina itakapotoa idhini hiyo, utaratibu huo utafuatwa kama inavyopendekezwa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya kudumu imezungumzia Serikali kuainisha vyanzo vya mapato nakupunguza matumizi yasiyo ya lazima ili kuweza kutenga fedha za ndani kwa ajili miradi ya maendeleo na siyo kama ilivyo sasa ambapo fedha nyingi za Miradi ya Maendeleo zinategemea fedha za nje ambazo upatikanaji wake umekuwa siyo wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2014/2015, Wizara imetengewa Shilingi bilioni saba, fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ikilinganishwa na Sh. 2,017,544,000/= ambazo ni fedha za nje za Maendeleo. Hali hii inaonyesha azma ya Serikali ya kuanza kutotegemea zaidi fedha za nje. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kambi ya Upinzani yamesemwa mengi, mengine nitayajibu wakati nikijibu na hoja nyingine. Lingine lilihusu Serikali ieletee kwa nini imeendelea kutoa kiwango kidogo cha fedha kwa ajili ya kukarabati majengo na miundombinu katika Vyuo ambavyo bado ni chakavu.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, Serikali imeviingiza vvyuo hivyo katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Serikali itaendelea kuvitengea Vyuo hivyo fedha kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi wamehoji kuhusu Bajeti, na nikiwataja wako Wabunge 19. Walisema Wizara haijapewa kipaumbele na Serikali kwa kutengewa fedha za kutosha. Sisi tunashukuru kwa Wabunge kuonyesha kuwa Bajeti haitoshi. Hata hivyo mwaka 2014/2015 Serikali imeongeza bajeti ya Wizara kwa asilimia 16, na mtaona kwenye vifungu kwamba tumeongeza ongeza, kutohakana na nyongeza hii. Wizara itaendelea kuwasiliana na Hazina kuhusu kuongezewa fedha.

Mheshimiwa Spika, aliyechangia kuhusu masuala ya fedha ni mmoja, yeye amezungumzia fedha. Alisema fedha nyingi zimetengwa katika Kasma ya

Nakala ya Mtando (Online Document)

Travel in Country, fedha ambazo haziwezi kuleta mabadiliko nchini. Fedha hizo zipunguzwe na kuzipeleka kwenye maendeleo.

Mheshimiwa Spika, fedha zimetengwa kuwezesha Wizara kutekeleza majikumu yake ya uhamasishaji, kwenda kuwezesha jamii katika masuala ya maendeleo, kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Sera za Wizara, kutoa elimu kwa wananchi kuhusu ukatili wa kijinsia. Kutoa mafunzo ya ukufunzi kwa Maafisa wa Mendeoeo ya Jamii 50 na kufanya maadhimisho mbalimbali kutokana na ufinyu wa Bajeti katika miaka ya nyuma. Wizara ilikuwa inashindwa kutekeleza majukumu yake yote haya. Dhana ya Maendeleo ya Jamii, maana yake kufanya kazi na wananchi. Huwezi kumfikia mwananchi kule Kasulu, au Katavi, kwa kutembea kwa miguu. Kwa hiyo, ndiyo maana tumewe ka Kasma ya *Travel in Country*. Sisi tuko na wananchi grass root. (Makof)

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Jamii, maana yake unafanya kazi na wananchi. Jamii lazima ifikiwe. Siyo wote wana TV, ingelikuwa wote wana TV na Radio, pengine ingekuwa rahisi, lakini ni lazima tuwafikie.

Mheshimiwa Spika, suala zito sana ambalo linawasikitisha Wabuge na sisi wenyewe na wananchi kwa ujumla ni kuhusu watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi. Mfumo wa udhibiti takwimu na taarifa ni dhaifu, hili limezungumzwa hata kwenye taarifa ya Mkaguzi Mkuu na kutegemea Wafadhili katika kushughulikia matatizo ya watoto badala ya Serikali na kutokuwepo utaratibu wa kutosha katika utoaji wa huduma. Waheshimiwa Wabunge 20 wamechangia, Lakini majibu yake naomba nijibu kama hivi ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuhamasisha na kutoa elimu ya familia ili zisimamie malezi ya watoto. Waheshimiwa Wabunge, masuala ya watoto ni masuala ya familia. Serikali inaingilia pale ambapo hapana budi. Pengine wazazi hawapo; mtoto hata akifiwa na wazazi wake, walezi wapo. Jamii inatakiwa irudi kwenye maadili ya Tanzania. Lakini Serikali bado inafuatilia masuala hayo pamoja na kwamba ni jukumu la familia.

Mheshimiwa Spika, tuna mpango wa pili wa kusaidia watoto walio katika mazingira hatarishi, ambao Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto ni mdau na anashirikiana na wadau wengine. Napenda ieleweke kwamba masuala ya watoto ni mtambuka. Mtoto huyu anashughulikiwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, anashughulikiwa na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Afya, anashughulikiwa na Elimu, anashughulikiwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, anashughulikiwa mtoto huyu na Sheria, anashughulikiwa hata na Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika. Kwa hiyo tunayo Task Force kubwa ambayo inawahusu wote, kila mtu ana majukumu yake.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, katika ngazi ya Kata, Maafisa wa Maendeleo ya Jamii ni wahamasishaji na watekelezaji wa Mpango huu. Huu mpango Afisa Ustawi wa Jamii kule kwenye Kata anajua kazi yake; na Afisa wa Maendeleo ya Jamii anajua.

Waheshimiwa Wabunge ni jukumu letu tunapopitisha fedha kwenye Halmashauri zetu, tuhakikishe Idara ya Maendeleo ya Jamii, Idara ya Ustawi wa Jamii, wanapata fedha za kutosha kwenda kupeleka hizi taarifa kwa wananchi na jamii. Lakini ilivyo sasa hivi, hizi Idara mbili ambazo zinahusiana moja kwa moja na watoto, hazitengewi fungu la kufanya kazi hii, wala hazipewi nyenzo za kufanya kazi kama vile magari au pipipiki. Aidha, Halmashauri za Wilaya kuititia mafunzo ya elimu ya familia, wameandaa mipango kazi itakayotumia fedha kutoka katika makusanyo ya Wilaya ili kutekeleza. Kwa hiyo, tunawategemea Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani Wizara ya Maendeleo ya Jamii iweze kushughulikia mtoto ambaye anadhalilishwa, yuko kule Nyasa, wakati Halmashauri iko pale na Afisa wa Maendeleo ya Jamii yuko pale. Hili ni jukumu letu. Nawaombeni sana, Sera ya Maendeleoya Mtoto imedurusiwa na mkakati kuandaliwa ili kuelekeza familia jamii na Serikali kutimiza wajibu wa kutunza watoto. Tunashirikiana na TAMISEMI na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuititia Idara ya Ustawi wa Jamii, katika kuhakikisha kwamba watoto wanapata huduma kulingana na rasilimali walizonazo.

Mheshimiwa Spika, kitini cha Elimu ya Malezi kwa familia kuhusu kuzuia ukatili dhidi ya watoto kimeandaliwa na mafunzo kutolewa kwa wadau kutoka kwa Halmashauri za Wilaya na baadhi ya Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, hivi vyote, ili kutekeleza hiki kitini kiwafikie, ni lazima Maafisa wetu waende huko kwenye Halmashauri watoe elimu.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo imetolewa, ni mimba za utotoni ambayo imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi. Jibu lake ni kwamba katika kupunguza mimba za utotoni, Serikali imeendelea kuhamasisha jamii kuititia Maafisa Maendeleo ya Jamii, kuondoa mila zenyе kuleta madhara kwa watoto na wasichana. Aidha, Serikali imeendelea kuhamasisha wadau mbalimbali kujenga mabweni katika Shule za Kutwa nchini ili kuwakinga watoto na mwingilio mkubwa wa watu ambaa unapelekea mimba hizo.

Aidha, Mikataba mbalimbali ya Kimataifa kuhusu haki na ustawi wa mtoto na Sheria ya Mtoto Namba 21 ya mwaka 2009 inatoa adhabu kwa yejote anayepatikana na hatia ya kuwapa ujauzito watoto.

Hili linahitaji pia ushirikiano mkubwa wa jamii. Tunaficha! Mtoto amepewa mimba, badala ya kwenda kutoa taarifa kwenye vyombo vya sheria

Nakala ya Mtando (Online Document)

achukuliwe hatua, basi tunamaliza hapo hapo waoane. Sasa tunavyofanya vile na mtoto mwingine naye anafanya kwa sababu anaona hakuna litakalofanyika. Lakini hili ni kosa na ni lazima kutoa taarifa Polisi ili jamii ijue kwamba vitendo hivi siyo vizuri. Tutaweza kuvimaliza kwa njia hiyo tu, lakini kama jamii itaendelea kufichaficha mambo haya, yatakuwa yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo tunatakiwa kufanya ni kuhakikisha kwamba wazazi wanawapa elimu watoto wao ya afya ya uzazi. Ni vema kuongea na mtoto aelewe kwamba akifanya tendo fulani atapata mimba. Zile siku za kumuonea aibu mtoto wako usimwambie ukweli zimepita jamani, tupo kwenye karne nyingine, akina mama ongeeni na watoto wenu wa kike na akina baba waongee na watoto wao wa kiume kwa sababu wengi sana wanapata mimba kutokana na kutokujua, wengi sana! (Makofij)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja juu ya jukumu la kuwalinda na kuwahudumia watu wenyewe ulemavu. Hoja hii imechangiwa na Waheshimiwa wengi, Kambi ya Upinzani na wengine wengi, nashukuru kwani ni jukumu kubwa sana hili na la muhimu.

Mheshimiwa Spika, jukumu la kulinda na kuwahudumia watu wenyewe ulemavu kwa kuwaendeleza, kuwalinda na kuhakikisha kuwa hawabaguliwi na wanapewa hadhi sawa limeendelea kushughulikiwa na Serikali kwa kuwa na Sera ya Maendeleo ya Wazee iliyopo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Wizara yangu kwa upande wake imeendelea kuhamasisha jamii kuondokana na mila na desturi zinazowabagua watu wenyewe ulemavu na kuwaona kuwa wana haki sawa na binadamu wengine ikiwepo haki ya kupatiwa elimu. Suala hili litazungumziwa kwa urefu na mapana zaidi itakapokuja Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Spika, ukatili dhidi ya watoto, hili pia limechangiwa kwa masikitiko makubwa na Waheshimiwa Wabunge wengi tu, Wabunge 13 wamelzungumzia katika michango yao ya maandishi na kwa kuzungumza. Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ya watoto tulianaa na sasa tunatekeleza mpango kazi shirikishi wa mwitikio na kuzuia ukatili dhidi ya watoto. Mpango huo ni wa mwaka 2013 - 2016 ambaao unatekelezwa na sekta mbalimbali zikiwemo Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Katiba na Sheria, TAMISEMI, Elimu na Mafunzo ya Ufundi, madhehebu ya dini na asasi zisizo za Kiserikali. Hawa wote tunatekeleza kwa pamoja kwa vile kila sekta inayo mipango yake ya kupiga vita ukatili. Wizara itaendelea kuratibu utekelezaji wa mpango huo kupitia kikosi kazi kitaifa cha kuzuia ukatili dhidi ya motto. Toka kuanza kutekelezwa kwa mpango kuna mafanikio mbalimbali yamepatikana ya kuzuia ukatili dhidi ya watoto na nina matumaini makubwa kwamba tatizo hili litapungua.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Serikali itafuatilia tatizo lililotajwa na Mheshimiwa Al-Shaymaa, Mbunge wa Viti Maalum la watoto wa Buhangija kuhakikisha wazazi wanatakeleza wajibu wao wa malezi na kuwatembelea na kuwapenda watoto hawa. Hili linasikitisha kwa kuwatelekeza watoto wenyewe ulemavu bila kuwaonyesha mapenzi hasa wale wenyewe ulemavu wa ngozi ambao wako Buhangija. Tunawasihi kupitia Bunge hili wazazi wajitokeze waende wakawaone watoto wao. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, suala hili la ukatili limeendelea sana ndani ya jamii na sisi wazazi tunaanza ukatili ndani ya nyumba, watoto na wao wakiwa wakubwa na wao wanawafanya ukatili watoto wao, watoto wetu tuwapende. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, wapo akina mama, mtoto ameiba kipande cha nyama anamkata sikio au vidole, ni tatizo kubwa sana na sasa limeenea. Naomba niwafahamishe kwamba hilo ni kosa la jinai na lazima litolewe taarifa ili wachukuliwe hatua. Huwezi ukamuumiza mtoto kwa sababu ya chakula ambacho ni haki yake. Kwa hiyo, Waheshimiwa wavezesheni Maafisa wenu wa Maendeleo ya Jamii huko mlipo ili waweze kufanya kazi hizi, yote haya wanayaweza.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliyojitekeza ni ukeketaji wa watoto wa kike, Serikali itumie nguvu kupambana na mila hii, hili imechangiwa na Wabunge wengi. Kumeuwepo na jitihada mbalimbali katika kushughulikia tatizo la ukeketaji wa watoto wa kike ambalo limejikita zaidi katika mila na desturi za makabila mbalimbali hapa nchini. Wizara kwa kushirikiana na asasi za kiraia imekuwa ikiendesha programu za kuelimisha umma ili kuondokana na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, elimu kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii na wavezeshaji wengine kutoka asasi za kiraia wametoa mchango mkubwa katika hili. Aidha, programu ya elimu kupitia vyombo vyahabari kama luninga, radio, magazeti na mitandao ya kijamii vimewenza kubadili fikra na mtazamo wa jamii kuacha ukeketaji. Sote tunakiri kwamba uketetaji pia ni ukatili dhidi ya watoto na dhidi ya akina mama. Waheshimiwa Wabunge wamelizungumzia vizuri sana na tupo pamoja tunaendelea na hayo mapambano tukishirikiana na NGOs mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja inayosema ucheleweshaji wa Sera ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Mtoto. Sera hii ipo katika mchakato, Serikali imekamilisha kudurusu Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008 ili kuwa na sera moja itakayoleta masuala ya malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto ya mwaka 2014. Sera hii iko katika stage nzuri ya kufikia kwenye Baraza la Mawaziri. Aidha, mkakati wa sera hiyo pia umekamilika na hivi sasa inasubiri taarifa ya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008, tunaifanyia tathmini kama kiambatanisho muhimu cha Sera ya sasa ili Rasimu hii

Nakala ya Mtandao (Online Document)

iwasilishwe katika ngazi za juu. Katika Sera mpya yapo mapendekezo ya kurekebisha Sheria ya Mtoto Na.21 ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Serikali inavyozingatia agenda ya watoto ambapo viongozi mbalimbali waliisaini mwaka 2012, Serikali imeandaa mpango mkakati wa utekelezaji wa agenda ya watoto kutoka mwaka 2013 - 2016 ambao unatekelezwa kwa kuzingatia maeneo yafuatayo:-

Moja, kufanya kazi na Waheshimiwa Wabunge katika kuhamasisha maeneo 10 ya uwekezaji kwa watoto.

Mbili, kuelimisha jamii kupitia vyombo vya habari.

Tatu, kufanya kampeni mbalimbali kuhusu haki za mtoto na kuimarisha ushiriki wa mtoto.

Mheshimiwa Spika, hoja nyininge ambayo imekuja mbele yetu ni biashara ya usafirishaji haramu wa watoto kutoka vijijiini kwenda mijini na nje ya nchi. Ipo Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu ya mwaka 2008 ambapo inakataza na kuvitaja vitendo hivyo kama ni ukiukwaji wa sheria na haki za binadamu. Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani inakamilisha Kanuni na mpango kazi wa kuzuia usafirishaji haramu wa binadamu. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto imeendelea kuelimisha jamii na kuhamasisha kutokubali kutoa watoto wao kwenda kufanya kazi kwenye maeneo ambayo hawayafahamu.

Mheshimiwa Spika, watoto hawa wanatakiwa walindwe na jamii, jamii yote tunatakiwa tuwe walinzi kwa watoto. Katika maeneo yenu mkiona watoto hawapo au mtoto ameondoka ni vizuri kuuliza na kutoa taarifa kwa wahusika yaani kwa Mtendaji wa Kijiji au kwa Mwenyekiti wa Kijiji kwamba mwezetu mtoto wake amekwenda wapi? Atatoa taarifa! Kama amenunuliwa tutajua na mitaani hivyo hivyo. Lazima sisi tuwe walinzi wa watoto, kila mtu ni mlinzi wa mtoto. Watoto hawana uwezo wa kukataa bali wanapelekwa tu.

Mheshimiwa Spika, hoja nyininge iliyokuja mbele yetu ni kwamba watoto wanachanganywa mahabusu na wakubwa. Sheria ya Mtoto Na.21 ya mwaka 2009 inazuia watoto kufungwa au kuwekwa kwenye mahabusu iliyo na watu wazima. Zipo mahabusu maalum za watoto (*retention homes*) ambazo watoto huwekwa na kupata uangalizi maalum. Aidha, Sheria ya Mtoto Na.21 ya mwaka 2009 haitoi adhabu ya vifungo kwa watoto ila kuna shule za maadilisho ambapo watoto hupelekwa kwa ajili ya kufundishwa tabia njema. Wizara itafuutilia na kulifanyia kazi suala hili.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa kwa michango yao na ninaendelea kuwaomba kwamba sisi Wabunge tutumie Halmashauri zetu kuhakikisha watoto wanapata haki zao. Sisi kama Wabunge kupitia Halmashauri zetu tuhakikishe kwamba fedha za WDF zinatengwa. Inakuwaje Kamati ya Fedha mnagitisha bajeti lakini hamuangalii kwenye kipengele cha fedha kwa vijana na wanawake, ile 10% haipo na sisi Wabunge ni sehemu ya Kamati ya Mipango na Fedha katika Halmashauri zetu? Sasa tukija hapa zile fedha ambazo mnaziona tunapeleka zinaonekana ndogo, fedha zinazotoka Maendeleo ya Jamii ni kama chachu tu, ni ndogo, lakini kuna Halmashauri kubwa ambazo 10% yake inaweza kuzidi hata milioni mia tano au bilioni moja. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano, Dar es Salaam juzi Halmashauri ya llala imeweza kutoa shilingi milioni mia tatu kwa ajili ya akina mama. Tatizo Waheshimiwa, Wakurugenzi wanaona ni nyingi. Wakitazama 10% imeshakuwa shilingi bilioni moja wanaanza kufikiria aah, shilingi milioni mia tano vijana na shilingi milioni mia tano akina mama, ni haki yao imetolewa kisheria. Jinsi wale akina mama na vijana watakavyopata hiyo mikopo watafanya biashara, watalipa leseni mzunguko ule ile Halmashauri itaendelea kupata fedha kutoka kwa haohao waliowakopesha hizo fedha. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kupitia Bunge hili, nawaomba Wakurugenzi na ninaiomba Wizara ya TAMISEMI iendelee kupigania suala hili. Ile 10% isiwe tunabembeleza. Mimi naamini bajeti inayokuja kwenye Halmashauri zetu wote hapa Wabunge tumo mle, mtahakikisha kwamba 10% inatengwa 5% kwa akina mama na 5% kwa vijana *regardless amount* ni ipi kwa sababu kwa kipindi kirefu wameacha kabisa kutoa, wengine wanatoa 1% na wengine hawatoi. Sisi fedha inayotoka Wizarani ni ndogo sana, tunaileta pale kama tunaikumbushia Halmashauri hizi pesa zimefika haya toeni na ninyi lakini wenzetu hawatoi. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunisikiliza na ninaomba kutoa hoja.

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

Matumizi ya Kawaida

Fungu 53 - Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Na Watoto

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kif. 1001 – Administration & Human
Resource Management.....Tshs 2,309,157,012/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mkanga, ndio mshahara wa Waziri!

MHE. MARGARETH A. MKANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Sina haja ya kutoa shilingi lakini napenda tu kupata ufanuzi au nielimishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wenyewe ulemavu kuna wanawake na watoto na Mheshimiwa Waziri katika kujibu ameelezea hilo kwa kifupi. Sasa nataka kufahamu katika Idara ya Jinsia na Idara ya Watoto ndani ya Wizara hii masuala haya ya walemvu wanawake na watoto wenyewe ulemavu mnayazingatiaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Margareth Mkanga kwamba masuala ya walemvu wawe watoto, akina mama au wanaume karibu yote haya yanashughulikiwa na Idara ya Ustawi wa Jamii. Hata hivyo, ilivyo kwa sababu sisi ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii walemvu wanafika kwetu na tunakuwa tunawaelekeza wafanye nini kwa vile Sera yao na Sheria yao iko katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii lakini tumekuwa tukitoa misaada sana kwa walemvu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza!

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi napenda kupata ufanuzi kuhusu Benki ya Wanawake, benki ambayo iliundwa kwa ajili ya kusaidia maendeleo ya wanawake wote lakini ukitazama bajeti yake ambayo Mheshimiwa Rais alisema kila mwaka watakuwa wanaipa hii benki shilingi bilioni mbili. Ukitazama mwaka 2011/2012, Serikali ilitoa shilingi bilioni mbili, mwaka 2012/2013 walitoa shilingi bilioni 1.3 lakini mwaka 2013/2014 walitoa shilingi milioni 450. Kwa hiyo hakuna mkakati maalum wa kuendeleza benki hii ili iweze kwenda kwa wanawake wote, inaonekana ina malengo ya kuendeleza wanawake wa Dar es Salaam peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninapenda kupata commitment ya Serikali kuhusu fedha hizi na kwamba mchezo huu unaofanyika sasa hivi ni kuwahadaa wanawake kwamba itabaki Dar es Salaam na watu wengine wa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mikoani kule kwetu tunakotoka kwa mfano Kagera hatutaweza kupata benki ya wanawake ili wanawake waweze kukopa na kuijendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba ufanuzi na kwa kweli leo kwa mara ya kwanza nitaondoa shilingi kwa mshahara wa Waziri pamoja na kwamba ni kiduchu ili tuweze kupata *commitment* ya kusaidia benki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante!

MWENYEKITI: Mimi nilifikiri hii ungeikaba Wizara ya Fedha, huyu hawezi chochote hata mshahara wenyewe hana, si ninyi wenyewe mmesema hana hata mshahara.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana Mheshimiwa Waziri anakosa hata mafuta kwenye ofisi yake, nimesikia anaweka mafuta kwenye gari. Tunataka atuambie, hii Wizara inadhalilishwa, wanawake, tunaomba na yeye asimame atuambie ataikaba vipi ile kusudi tuweze kupata hiyo fedha.

MWENYEKITI: Aikabe Wizara gani?

MHE. CONCESTA L. RWAMLAZA: Aikabe Serikali yeye kama Waziri!

MWENYEKITI: Hapana bwana, unajua ninyi mnapoteza wakati, ninachokisema mimi, ni kwamba hawa ninyi wenyewe toka asubuhi mnasema kiduchu, kiduchu, sasa anafanyaje? Ninyi jiandae muikabe Wizara yenyewe ambayo inahusika na mengine mumkabe Waziri Mkuu siyo huyu! Ukimkaba huyu siyo sahihi.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimkabe Mheshimiwa Waziri Mkuu?

MWENYEKITI: Ndiyo, kwa wakati wake!

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunaomba ujibu, wanawake wanaumia huko kwetu, msaidie mwanamke mwezeti hapo.

MWENYEKITI: Haya, naomba ukae, Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa concern yake kuhusu benki kwamba angependa iende kwa speed zaidi.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali imekuwa ikijitahidi kutoa fedha kwa ajili ya Benki hii, lakini kutokana na ufinyu wa bajeti na mambo mengi ambayo yametokea hapa katikati, kuna sensa, Bunge la Katiba na kadhalika, kwa hiyo, hata ile azma haikufikiwa lakini tunaamini katika hiki kipindi kifupi kabla ya kumaliza mwaka tutaongezewa fedha, namshukuru sana Mheshimiwa kwa kulisemea hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini amesema kwamba benki hii haifiki Kagera na maeneo mengine, kwa kweli kazi tunayoifanya mpaka watu wanashangaa, kwa kidogo ambacho benki inacho. Kufungua tawi la benki ni gharama kubwa sana. Tumeona kwamba hatuwezi, ndiyo maana tumeshaingia Dodoma, sasa hivi tumefika Mbeya na tumepewa mpaka maeneo, ingawaje hapa kwa vile hatujafungua ndiyo maana hatujaweka. Kwa vile tumefika Mwanza, tunafungua vituo kwenye maeneo yenyewe usalama. Kwa mfano, sehemu zilizokuwa Posta ambazo sasa hazifanyi kazi, tunajua kuna ulinzi na kila kitu, tunapanga pale, tunatoa huduma. Tumefika mpaka Rukwa, tunasubiri kwenda tu na tumeishakubaliana. Ni lazima tujue tunapata eneo ambalo linaweza kufananafanana na kutoa huduma za kifedha na ulinzi uwepo. Kwa hiyo, jinsi tunavyopata hizi fedha za ruzuku ndivyo tutaweza kwenda katika maeneo mengine. Mwaka mwaka huu ruzuku haikutoka vizuri lakini tunategemea katika kipindi hiki kifupi cha mwaka huu tutaongezewa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lolesia Bukwimba.

MBUNGE FULANI: Aah, bado.

MWENYEKITI: Hawakutoa shilingi walikuwa wanazungumza tu.

MBUNGE FULANI: Alitoa.

MWENYEKITI: Sikilizeni, nilisema hivi mkimtolea shilingi huyu haisaidii kitu, tuna utaratibu mwingine wa kutoa shilingi za namna hiyo, *let us be serious*, tutoe mahali ambapo tunajua ndiyo penyewe. Mwenyewe hana hata mafuta ya kuendesha gari lake. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Lolesia Bukwimba!

MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi nilikuwa nahitaji tu ufanuzi kuhusiana na suala la kuajiri watumishi katika sekta ya maendeleo ya jamii, hasa katika ngazi ya Kata na Vijiji, kwa sababu maendeleo hayawezi kuja bila kuwa na wataalam wanaojua shughuli hizo za maendeleo ya jamii. Mara nyingi katika Halmashauri zetu nyingi ikiwemo Halmashauri yangu ya Geita, nikitolea mfano Jimbo langu Kata 16 zote hazina Afisa Maendeleo ya Jamii hata mmoja, maendeleo hayawezi kuja bila kuwa

nao hawa wataalam. Kwa hiyo, ningependa kupata ufanuzi kutoka kwenye Wizara kwamba ina mpango gani sasa wa kuhakikisha angalau kwenye Kata tuwe na wataalam hao? (Makofii)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, maelezo.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Lolesia kwa swali lake zuri. Nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Sera yetu ya Maendeleo ya Jamii ambayo ilipitishwa kama miaka mitano iliyopita inasema kila Kata ni lazima awepo Afisa Maendeleo ya Jamii. Tayari tumekuwa tukijitahidi tuwezavyo kupata hao Maafisa Maendeleo ya Jamii lakini yote inategemea na uwezo wa Serikali katika kuajiri hao Maafisa Maendeleo ya Jamii. Wote kama tunavyojua sasa hivi ikama kubwa inaenda kwenye kuajiri Walimu lakini kidogo kidogo nia ya Serikali ipo hapo kwa vile Sera ile ilipitishwa, tutaweza kupata kila Kata Afisa wa Maendeleo ya Jamii ambaye atakuwa anachochea maendeleo na kubadilisha fikra potofu ambazo baadhi ya wananchi katika jamii wanazo na hivyo kuleta maendeleo kwa kasi zaidi.

MWENYEKITI: Juzi niliwasomea ile Kanuni inayosema Mshahara wa Waziri mtapitia kwenye vyama vyenu maana naona kuna wengine wanasimama hapa na mimi nina majina ambayo yameletwa na vyama. Haya Mheshimiwa Vita Kawawa.

MHE. VITA R.M. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mimi pia naomba nianze kwa kusema kwamba si kama nimekamata Mshahara wa Waziri, ila tu nilikuwa nataka nianze kwa kusema kwamba pamoja na ufinyu wa bajeti Wizara imekuwa ikitekeleza Sera yake ya kuwafikia wananchi kwa kuwafungulia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Mtendaji Mkuu wa Wizara hii. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ufinyu wa bajeti niliwaomba watufungulie Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Wilayani Namtumbo, walitufungulie, walitukarabatia majengo na kutujengea maengine na kutufungulie Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Mputa. Mheshimiwa Waziri mwenyewe alifika na kukifungua chuo kile. Kwa hiyo, wananchi na hasa akina mama wanamshukuru sana. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa naomba kupata ufanuzi. Kwa Mheshimiwa Waziri aliona kile chuo ndiyo kwanza kimeanza, majengo mengine yalikuwa hayajakamilika, naamini kabisa pamoja na ufinyu wa bajeti mwaka huu atakuwa ametuwekea kidogo kuendeleza pale palipoachiwa mwaka jana. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kupata ufanuzi kama kwenye bajeti hii kuna chochote ili wananchi wa Mputa na Wilaya ya Namtumbo waweze kufarijika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Hilo ni swali la kisera! Siyo sera kabisa hapo wewe unataka kuuliza kama kuna fedha ziko wapi? Sasa hilo tutakapofika kwenye vifungu vinavyohusika na utapata maelezo. Mheshimiwa Rajab Mbarouk.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nitangaze nia au azma yangu ya kutaka kuondoa mshahara wa Waziri pale ambapo sitapata majibu ya kuridhisha.

MWENYEKITI: Unaondoa mshahara au unatoa nini? Concepts za humu ndani siyo kuondoa mshahara, unaondoa nini?

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, eeh, pale ambapo sitapata majibu ya kuridhisha.

MWENYEKITI: Unaondoa shilingi siyo mshahara.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka niuchukue wote lakini nitaondoa hiyo shilingi, ahsante. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Mkatalie. (*Kicheko*)

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naweka nia yangu ya kuondoa shilingi katika mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba alitoa taarifa hapa kuhusu WAMA na akataka twende tuka-Google. Nimwambie tu kwamba tayari hiyo kazi ya ku-Google sisi wengine tulishaifanya na tunaijua WAMA juu chini, chini juu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba WAMA inajishughulisha na shughuli za kisiasa, japokuwa maelezo ambayo ameyatoa Naibu Waziri, ameyatoa Waziri lakini udhahiri kupitia WAMA Foundation basi unakuta kwamba WAMA inajishughulisha na mambo ya kisiasa. Si hilo tu, hata huyo Mwenyekiti ambaye ametajwa kwamba alikuwa anazunguka kumsaidia mume wake katika kampeni, ni kweli alikuwa anazunguka lakini alikuwa anatoa ahadi kwa kusema kwamba iwapo Mheshimiwa Kikwete atashinda katika uchaguzi huu basi WAMA itafanya one, two, three. Hayo alikuwa anayaahidi, kwa mfano,

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kusomesha watoto katika kila Halmashauri, alisema kwamba WAMA itasomesha watoto katika kila Halmashauri iwapo Rais Kikwete atashinda. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hivyo, nilipoiangalia WAMA Foundation wakati nina- Google nimekuta Board Members ya WAMA yote ni CCM tupu, tupu kabisa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ninukuu Board Members, Mwenyekiti Mama Salma Kikwete ni m-NEC, Makamu wake Mama Zakia Hamdani Meghji ni Katibu wa Uchumi na Fedha wa CCM na ni m-NEC, Mama Mwanamwema Shein, ni mke wa Rais, Mama Sophia Simba, hili Waheshimiwa lazima tuliangalie. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mheshimiwa Waziri ameanza hotuba yake mpaka amemaliza ameshindwa hata ku- declare interest kuhusu WAMA. Anaitetea WAMA hapa bila ku-declare interest kwamba yeye ni Board Member wa WAMA. Wakati huohuo yeye ni m-NEC na Mwenyekiti wa UWT Taifa na wengine na wengine, wamejaa ma-CCM watupu hapa. Mnaitumia WAMA kwa shughuli za kisiasa, hili halipingiki. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anipatie maelezo ni kwa nini kwa mujibu wa Sheria za NGOs WAMA hajaifuta mpaka leo? Naomba majibu ya Mheshimiwa Waziri na kama majibu yake hayataniridhisha basi nitaondoa shilingi kwenye mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (Makofii)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Naona kwanza ajibu Waziri.

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

(Hapa kulikuwa na minong'ono mionganoni mwa Wabunge)

MWENYEKITI: Maneno ya nini wakati nimempa nafasi Waziri ajibu? Wengine midomo inawasha wakati wote. (Kicheko)

Mheshimiwa Waziri, maelezo.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mama Salma akienda kwenye kampeni haendi kufanya kazi za WAMA, anafanya kazi kwa niaba ya mumewe, anamsaidia mumewe. Anasema ndio hapa patachimbwa kisima, sasa kuna ubaya kumsemea mumewe kwamba atakuja kuchimba kisima? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe mfano, Mama Salma ana shule kule Nyamisati, hebu kaulize wale watoto wanaosoma pale ni wa CCM? Hatujui hata wazazi wao. Watoto wamechukuliwa Tanzania nzima, kila Mkoa. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Na vitanda vya kujifungulia.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mama Salma ametoa vitanda vya kujifungulia, vifaa vya hospitali nyingi sana. Wanaolalia pale ni ma-CCM au ma-CUF? Ametoa msaada huo mpaka Pemba ambako zaidi ya nusu ni ma-CUF, kwa nini ametoa misaada kule? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama *individual* sizuiwi kuwa member wa NGO yoyote.

WAJUMBE: Kweli, sawa!

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Sizuiwi na ninaweza pia kuanzisha NGO yangu kama nikitaka, ilimradi tu isiingiliane na shughuli nyingine za kiserikali ambazo nimepewa. Hata hivyo, hilo la kusema wote ma-CCM mbona UKAWA wote ni ma-CUF na ma-CHADEMA? (Makofi/Kicheko)

MBUNGE FULANI: Ni makubaliano.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Eeh, UKAWA ni ma-CUF, ma- CHADEMA, sasa tufanyaje? Nakushukuru. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Marombwa.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilieleza nia ya kuondoa shilingi kama sitaridhika na majibu.

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Kwanza ngoja utaratibu, Mheshimiwa Marombwa unatoa taarifa tu siyo kujadili hoja hii, kwa sababu haiwezi kujadilika mpaka huyu bwana atoe shilingi yake.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda kutoa taarifa tu kwamba, Mheshimiwa Mbarouk alizungumza kwamba Mama Salma aliahidi katika uchaguzi ule kwamba endapo Rais Kikwete atachaguliwa atawafundisha watoto kutoka maeneo yote ya nchi yetu hii ya Tanzania. Hiyo ahadi si ya kweli. shule ya Sekondari Nyamisati imeanza mwaka 2010, mwezi wa Machi, hata uchaguzi ulikuwa bado. (Makofii)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Wakati huo shule hiyo inaanza ilikuwa inachukua wanafunzi kutoka Mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani, kutoka katika Wilaya zote za Tanzania Bara na Visiwani, haijali huyu wa chama gani na wala hakuahidi hilo. Shule ilikuwa imeanza kabla ya uchaguzi wa mwaka 2010 kufanyika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge asiseme kwamba katika kutembea kwake Mama Salma katika uchaguzi wa mwaka 2010 ndiko kulikosababisha yeye awaambie wananchi waichague CCM atawapeleka watoto kwenye shule ya sekondari, hapana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa yako ni kwamba shule ile ndiyo iliyofanya vizuri zaidi, imefaulisha wanafunzi walioanza mwaka 2010 mwaka 2013 wamefaulu wanafunzi 10 - divisheni I, wanafunzi 20 - divisheni II, wanafunzi 19 - divisheni III na wanafunzi 19 waliobakia divisheni IV. Wanafunzi hao wametoka katika Wilaya zote na Mikoa yote ya Tanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu kumpatia taarifa. (Makofii)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rajab toa shilingi.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na majibu ya Waziri ambayo hayakuniridhisha natoa shilingi ili na wenzangu wapate nafasi waweze kuchangia.

MWENYEKITI: Ila mfahamu kwamba ulimwengu wote First Ladies wanakuwa na chombo cha kufanya kazi, duniani kote. Mimi najua kote kabisa na mimi nilikuwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, nilienda kwenye mkutano wa First Ladies - Geneva. (Makofii)

Mheshimiwa toa shilingi halafu toa hoja yako. Hoja yako iwe specific maana hapa sijaelewa mara siasa, mara wamekwenda wapi, mara wamefanyaje, iwe specific tuweze kujadili!

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shilingi kutokana na kutoridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri. (Makofii)

MWENYEKITI: Tueleze bwana, unaijenga hoja yako.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ambayo Mheshimiwa Waziri ameyatao hayakuridhisha. Amejaribu kujibu kwa kutoa mifano ya UKAWA ambayo haipo, UKAWA siyo NGO na wala haihusiani na hoja ambayo nimeitoa hapa. (Makofii)

MWENYEKITI: Ngoja kwanza, Mheshimiwa Mbunge naomba uketi kwanza tuelewane.

MHE. MOHAMMED RAJAB MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Umetoa shilingi maana yake unayo hoja. Sasa unapaswa uieleze ile hoja yako bila kujali amesema nini ili sisi wote tukusikilize, tujadiliane halafu tufanye maamuzi. Sasa usitupeleke huku mara huko, hatuelewi unasema nini. Wewe unapaswa ujenge hoja yako vizuri sisi tukusikilize, una dakika tano.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba ni kwa nini Waziri asiifute NGO hii kulingana na Sheria ya Usajili wa NGO ya mwaka 2002. Hiyo, ndiyo hoja yangu naomba ijadiliwe.

MWENYEKITI: Kwa nini aifute? Toa maelezo yako ni kwa nini ifutwe? Ndiyo maelezo yanayotakiwa.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ifutwe kwa sababu NGO hii imekiuka Sheria ya Usajili wa NGOs lakini vilevile ni kwamba inajihuisha na mambo ya kisiasa. (Makofii)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja ya kutoa shilingi. Sababu ya kwanza ya kuunga mkono hoja ni kwamba Mheshimiwa Waziri hajajibu hoja ambayo tumeizungumza kwamba kwanza Taasisi ya WAMA ilitumika kisiasa, ilitoa ahadi kisiasa na hiyo shule anayoizungumza siyo kwamba ada anazitoa Mama Salma mikononi mwake ila anakuwa funded na USAID, na USAID imem-fund kwa sababu kile chombo ni cha mke wa Rais kwa ajili ya kuhudumia Watanzania kiujumla na siyo kisiasa. Hiyo ni moja. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili ni kwamba Mheshimiwa Sophia Simba ni Mjumbe katika Bodi ya WAMA. Kanuni zetu zinatueleza kwamba kwanza

Nakala ya Mtando (Online Document)

kabla hujaeleza chochote unatakiwa ku-declare interest, hiyo ni moja, lakini pili hiyo *interest* yako unatakiwa utuambie ni kiwango gani cha maslahi kifedha ambacho una-benefit kutokana na WAMA. Kwa hiyo, tulitarajia kabla hajajibu chochote atuambie akiwa Mjumbe wa Bodi analipwa nini, wakati gani na kwa sababu gani? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, majibu kama hayo ni muhimu kwa sababu *First Lady* siyo wa CCM, *First Lady* ni wa wote. Inapotokea *First Lady* anajibabanabana upande mmoja, anatufanya tuijulize. Wengine wanasema watu tunakatazwa kufanya mikutano Lindi Mjini, *First Lady* anafanya mikutano Lindi Mjini kwa sababu anataka kugombea Jimbo. Sasa kwa nini tusipate majibu ya wazi? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mbarouk, Mheshimiwa Waziri atupe ufanuzi. Kwanza, a-declare interest, pili ajibu ni kwa kiwango gani WAMA ilitumia mgongo wake na fedha za wafadhili kwenda kumpigia kampeni Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, akiwa mgombea wa Chama cha Mapinduzi. (Makofii)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mtanda!

MHE. SAIDI M. MTANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kutounga mkono hoja ambayo imetolewa na Mheshimiwa Mbarouk. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hoja yake kwamba WAMA imekuwa ikitumika kisiasa naomba hili Mheshimiwa Mbarouk aweze kulithibitisha kwa sababu hakuna ushahidi wowote ule unaoashiria kwamba WAMA imekuwa ikitumika kisiasa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 mimi nikiwa mgombea na baadaye kuwa Mbunge, sijawahi kusikia wala Halmashauri yangu haijawahi kuahidiwa kwamba wapo watoto watasomeshwa na WAMA kwa ahadi hiyo ya WAMA. Kwa hivyo, sifikiri kwamba hoja hii kwa sasa ina mashiko. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia suala la Mama Salma Kikwete kutaka kugombea Ubunge Lindi Mjini kwanza halihusiki hapa. Halihusiki kwa sababu yeye binafsi kama kiongozi lakini pia kama raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anao uhuru wa kufanya maamuzi yake. Kwa hivyo, si ajabu kwa kiongozi au Mtanzania ye yote yule kuamua kuonyesha nia au kutaka kugombea uongozi katika eneo lolote la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofii)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, hoja hii haina msingi na ukilinganisha na majukumu na kazi kubwa zilizofanywa na WAMA katika nchi yetu ninaomba kuipongeza WAMA...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Kengele imegonga. Mheshimiwa Machali.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama hapa kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed kwa sababu zifuatazo. Ni uwazi usiopingika kwamba WAMA kwa upande mmoja inahusika kisiasa. Ushahidi wa kwanza ni wa Mheshimiwa Waziri mwenyewe ambaye ni Board Member na ameshindwa ku-declare *interest* mbele ya Bunge lako. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mbali na ushahidi huu wa kwanza ukiangalia Board Members wengi ambao Mheshimiwa Rajab ameweza ku-Google na kuwapata wengi ni Makada wa CCM. Pengine ajaribu kuweza kulithibitishia Bunge lako ni mpinzani gani ambaye ni Board Member wa WAMA? Watuambie kama hakuna *political interest* hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Rajab amesema mwanzoni kabisa wakati ana-raise hoja yake kwamba Mama Salma Kikwete wakati wa kampeni aliahidi yeye kama Mwenyekiti wa WAMA atachimba visima. Sasa kama hivyo ndivyo, anatumia taasisi ya WAMA ambayo ni *non-partisan*, haifungamani na upande wowote, sidhani kama ilikuwa ni busara kwa mtu ambaye anajua kabisa kwamba ni *First Lady* na *First Lady* hapaswi kufungamana na upande wowote alipaswa kuweza kutumia taasisi hiyo kuweza kutafuta kura za mgombea wa Chama cha Mapinduzi ambaye hivi sasa ni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hizo fedha ambazo zinatumika ni fedha za wafadhili kama USAID pamoja na Development Partners wengine, hizo fedha sio fedha za Chama cha Mapinduzi. Kama angekuwa anatumia fedha za Chama cha Mapinduzi katika kuhakikisha anatekeleza miradi mbalimbali tusingelikuwa na problem.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwa mujibu wa Sheria ambayo inahusika na asasi zisizokuwa za Kiserikali NGO's.

MWENYEKITI: Sheria gani?

MHE. MOSES J. MACHALI: The Non Governmental Organisation Act, nafikiri ya mwaka 2002.

MWENYEKITI: Kifungu gani?

MHE. MOSES J. MACHALI: Inazuia asasi za kiraia kujishughulisha na shughuli za kisiasa. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama anasimama kwa umbrella ya WAMA na kuanza kutuambia nitachimba visima ili kura za mgombea wa CCM ziweze kupatikana, ni uvunjaji wa sheria na ni mwendelezo wa vitendo vyta kifisadi ambavyo haviwezi vikakubalika. Tunamtaka Mheshimiwa Waziri aeleze Bunge lako ni kwa nini taasisi hiyo haijaweza kufutwa na Mwenyekiti wa asasi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jafo.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Taifa linatuangalia halafu linatushangaa sana, hilo ndilo jambo la kwanza. Katika hoja ya Bwana Mbarouk, ndugu yangu aliyosema kwamba mionganini mwa Board Member wote ni wana-CCM, nadhani kila kitu unachokifanya unaangalia watu wenye kuaminika kwanza. Katika taasisi yako kuwa na Board Member ambao hata katika kikao watatoka ndani ya kikao mtashindwa kufanya maamuzi, huwezi ukawaweka katika Board Member. (Makofij/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili, nasema Taifa linashangaa kwa sababu kuna watu ambao wazazi wao maskini na ni yatima kabisa. Kuna watoto wengine wanasoma pale wanalia wametoka katika mazingira dhalilifu kabisa lakini taasisi hii imeweza kuhakikisha hivi sasa wanapata elimu. Nadhani inaonekana kuna viongozi ambao hawajui matatizo ya Watanzania tunaowaongoza. Kwa hilo, mimi napata mashaka sana imefikia Wabunge sisi hapa badala ya kuangalia jamii ambazo ziko katika mazingira magumu zinasaidiwa tunawapiga vita wale wenye kusaidia ile jamii. (Makofij)

Ndugu yangu Mbarouk nadhani tunafanya siasa lakini katika mambo mengine lazima tujue kwamba Mwenyezi Mungu kuna mambo mengine atatuuliza katika masuala mazima tunayofanya. Namwomba mtoa hoja ikiwezekana afute hoja hii kwa sababu mimi kwa mantiki yangu naona kwamba haina mashiko katika mustakabali wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kawawa.

MHE. VITA R.M. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Hoja ya msingi ya Mheshimiwa Mbarouk ni kwamba kwa nini WAMA isifutwe. Mimi nasema siungi mkono kwamba ifutwe. Nashangaa sana kwa sababu WAMA imekuwa ikisaidia maisha ya watoto maskini, imekuwa ikisaidia watoto yatima, nilidhani Mbunge kijana msichana atasifia kazi kubwa inayofanywa kuokolewa wasichana hawa kwa kusomeshwa leo anaponda kazi iliyofanywa.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. VITA R.M. KAWAWA: Lakini pia UNDP au USAID hawa wanaotoa misaada leo Marekani wamempa awards chungu nzima Mama Salma Kikwete kwa sababu ya kazi hii nzuri anayoifanya halafu leo sisi Wabunge tunaidhihaki, jaman laizima tuangalie. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hoja hiyo siungi mkono na namwomba Mheshimiwa Mbarouk arudishe shilingi ya Mheshimiwa Waziri.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbarouk maliza hoja.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu bado haijaisha kwa sababu Waziri hajazungumza lolote.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani ananitajataja hovyo halafu mimi nimuachie.

MWENYEKITI: Amemaliza maneno yake na huyu mwenye hoja atajibu sio nyie.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, bado hoja yangu inasimama palepale.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Kuhusu utaratibu! Waziri bado hajajibu kabla ya mhitimishaji.

MWENYEKITI: Hiyo ni kweli. Mheshimiwa Waziri jibu, nawe unajadili anayejibu ni yeye.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii ili niweze kujibu. Kwanza nijibu la maslahi binafsi. Mimi nipo kwenye taasisi ile kama *individual ambaye sipati profit* yoyote sipati kitu, tunajitolea. Katika Bodi yetu ile tunafanya kazi kwa kujitolea. Moja ni kwamba taasisi hizi za wake wa Marais dunia nzima zinashughulika na

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Wizara inayoshughulikia masuala ya wanawake au ya jamii na ndiyo maana niko mle. (Makof)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Taarifa!

MWENYEKITI: Naomba ajibu kwanza. Tunatakiwa wote tufikiri na kusikiliza sasa kila mtu ana-interrupt tunamsikilizaje?

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara 61(1) cha Kanuni zetu hizi maslahi binafsi lazima yawe ya kifedha na lazima utaje kiwango gani. Mimi hapa ni kazi ya kujitolea kwa ajili ya wananchi, ile ni non profit organization...

MHE. JOHN J. MNYIKA: Taarifa!

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Na pale hatugawani fedha, sisi ni watafutaji, tunashirikiana naye kuhakikisha hizi kazi anazifanya. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la kusema WAMA imetumika kisiasa, nasema si kweli. Mama Salma akienda kwenye masuala ya kisiasa kama mke wa Rais haendi kama WAMA. Maana angewachukua na Board Members wake wote pengine, angechukua na staff wote wa WAMA aende nao, anaenda ye ye kama *individual*, kama mke wa Rais. Kama anapata wasaidizi wake wale ambao ni haki yake au stahili yake kama mke wa Rais hawez kwenda bila kuwa nao lakini hachukui ofisi aende nayo pale na yale masuala ni ya kisiasa period. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio anakokwenda kule ni masuala ya kisiasa, niko sawa.

(Hapa baadhi ya Wabunge walishangilia sana)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJEMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Yuko sahihi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilichosema kule anakokwenda anafanya masuala ya kisiasa tatizo liko wapi? Hata hivyo, akiwa WAMA anakuwa na watu wake wa WAMA tunaenda kufanya mambo ya Ki-WAMA, tunaenda kugawa misaada hospitalini, shulen na sehemu mbalimbali WAMA inakwenda lakini kwenye masuala ya siasa hatuwezi kumkataza mke wako wewe mwanihisi au mke wa Rais, wote wanaruhusiwa.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJEMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:
Hata wachumba wanaruhusiwa.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Kama wachumba wanaruhusiwa sembuse mke. (Makofi/Kicheko)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rajab.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sikuridhika na majibu ya Waziri na namshukuru kwa kudhihirisha kwamba Mama Salma anapokwenda katika shughuli zake pamoja na za WAMA anafanya siasa. (Makofi)

WABUNGE FULANI: Aaaah!

MBUNGE FULANI: Afute kauli!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile Waziri alijaribu kujitetea sana kuhusiana na yeze kuwa Board Member wakati anajua kwamba yeze kwa nafasi aliyonayo ya Waziri ndiye mtu ambaye anatakiwa kuzichunguza hizi NGO, kufanya usajili wa NGO na kuziratibu NGO, wakati huohuo yeze yumo ndani ya NGO unategemea kutakuwa na nini hapo zaidi ya siasa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijaridhika na majibu ya Waziri na nazua shilingi.

MWENYEKITI: Haya tunafanya maamuzi sasa wote mtulie.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja illiamuliwa na Kukataliwa)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mkosamali.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nimesimama hapa kutaka ufanuzi wa kisera na naomba nijibewe nisiambiwe kwamba Wizara haina fedha kama wanajua Wizara haina fedha hatuna haja ya kuwa na Wizara ambayo inazidiwa na Idara ya Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kupata ufanuzi juu ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, nililiza hili swali mwaka jana, mkakati wake ukoje? Kuna vyuo ambavyo vina zaidi ya miaka 10 havijapata fedha za maendeleo. Vyuo hivi tunagemea vitumike kuwafundisha watu mambo ya ujasiriamali, mambo ya ufundu na elimu nyingine katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Sasa Wizara hii ambayo ipo kama ka-taasisi tu inazidiwa hata na PCCB. Tunaendesha Wizara kwa gharama kubwa halafu bajeti ya maendeleo ni shilingi bilioni tisa. Kwa nini tutumie fedha nyingi kuwa na Wizara ndogo ya namna hii halafu kila mwaka tukiiliza mkakati wa kuendeleza Vyuo vya Maendeleo haupo, tunaambiwa Wizara haina fedha. Mnapokuwa kwenye Baraza la Mawaziri huwa hamuwezi kudai ninyi Mawaziri wa Wizara hii mkapewa fedha kama Mawaziri wengine? Njooni mtueleze hapa mna mpango gani wa kuboresha vyuo hivi. Pia zile fedha ambazo bado zinapitia Mikoani, fedha za OC, lini zitakuwa zinakwenda moja kwa moja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hawaelezi namna gani wataboresha vyuo hivi natoa shilingi kwamba Wizara hii ifutwe kwa sababu hamna sababu ya kuwa na Wizara ambayo inazidiwa na Idara ya Serikali, tulipe Makatibu Wakuu na Mawaziri na vitu vingine kwa Wizara ambayo inaweza kuwa taasisi kwenye Wizara ya kawaida tu huko Wizara ya Afya na vitu vingine. (Makofii)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kama nilivyosema wakati nafafanua hoja kwamba vyuo hivi huwa vinakarabatiwa na tunavyo vyuo vya aina mbili. Viko Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ambavyo viko 55 nchini na tunavyo Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ambavyo kimsingi viko tisa. Vile vyuo tisa vyenyewe vinakusanya ada, zinakwenda Hazina kuwa accounted halafu zinarudi kama retention. Kama tulivyosema tumeomba sasa hivi retention iwe at source.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija vyuo 55 viko kwenye mpango wa maboresho na vinakarabatiwa kila tunapopata fedha. Vyuo 25 sasa hivi vinatoa program za VETA na vyuo vile vingine viko kwenye Wilaya ambazo hazina vyuo vya VETA. Kwa hiyo, Vyuo hivi vya Maendeleo ya Wananchi vinatumika kutoa program za VETA na vile viliviyobaki ili kufikia 55 tumevipanga kwenye awamu navyo vitatoa program ya VETA. Kwa mfano, Wilaya kama Njombe hakuna VETA lakini Chuo cha FDC kinatoa program ya VETA, kwa hiyo, vinakarabatiwa. Sasa hivi nikuhakikishie Mheshimiwa Mkosamali tumetenga Sh.1,800,000,000 mtakazotupitishia leo tutakapofika kwenye bajeti ya maendeleo. Pia kuna *Education Sector Development Programme* ambayo tunashirikiana na Wizara ya Elimu kuendelea kuvikarabati vyuo hivi.

MWENYEKITI: Ulisema unakusudia kutoa shilingi bado unakusudia?

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Ndio nakusudia.

MWENYEKITI: Haya endelea na hoja yako.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakusudia kwa sababu...

MWENYEKITI: Sio unakusudia, ndio umetoa shilingi sasa endelea.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Naendelea kutoa hoja.

MWENYEKITI: Ukiphasema sikuridhika natoa shilingi, sasa unaendelea.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo hivi kwa bajeti hii ukisema unatoa shilingi bilioni moja, kwa nchi hii ni fedha kiasi gani, yaani shilingi bilioni moja unaweza ukakarabati vyuo vya nchi hii? Tunachosema hapa ni kwamba vyuo hivi, sasa hivi tuna vijana wengi wanamaliza four four, form six wanapaswa kwenda kwenye vyuo ambavyo vinatoa ujuzi, vyuo vinavyo leweka visiwe vyuo vya ubabaishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa vyuo hivi kama vinaendelea kuwa chini ya Wizara hii ambayo haina fedha maana yake tutakuwa na watoto ambao hawapati elimu ya ufundi. Nchi yoyote duniani imeendelea kwa elimu ya ufundi. Sasa ukarabati tu wa Bunge mmeweka shilingi bilioni nane, vyuo vyote nchi nzima mmeweka shilingi bilioni moja! Hivyo vyuo vitafanya nini, vitengenezewe mashine, watu wafundishwe mashine za ujasiriamali za kutengeneza vitu ndio shilingi bilioni ya kutengeneza hivi vyuo au mnazungumzia ukarabati wa vitu gani? Hakuna u-seriousness kwenye vyuo hivyo vya Maendeleo ya Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja ili hoja yangu ijadiliwe ili vyuo hivi kama vinabaki chini ya Wizara hii viongezewe fedha na kama haviongezewi fedha, hii Wizara ifute hizo fedha ziende zote zikaendeleze hivyo vyuo.

MWENYEKITI: Sasa hoja ni ipi maana lazima tuamue tu unatoa shilingi ili kitokee nini?

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Natoa shilingi fedha kwa ajili ya vyuo hivi ziongezeke.

MWENYEKITI: Nadhani katika eneo hilo bado tuna matatizo hatulifanyi vizuri.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mkosamali...

MWENYEKITI: Ambayo ni?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Ya kukataa kwamba tusiipitishe hii bajeti badala yake fedha ziongezwe kwa ajili ya hivi vyuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni vizuri likajadiliwa, hatuwezi kukubali sababu ya kwamba tusubiri Wizara ya Fedha kuiachia hii bajeti ikapita. Kwa sababu kwa uzoefu mwaka jana tulipokuwa na matatizo makubwa kwenye bajeti ya Wizara ya Maji, Bunge lilisimama kidete kwa pamoja tukaweka mguu chini bajeti ya Wizara ya Maji ikaongezewa fedha kwa sababu tuliamua kuwa sauti moja tulifanya uamuzi. Hoja hii ya Mheshimiwa Mkosamali ikikubalika itailazimisha Serikali na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni yuko hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu kuongeza fedha kwa ajili ya jambo muhimu sana la vyuo hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu kwa maelezo ambayo Naibu Waziri ameyaeleza hiyo shilingi bilioni moja iliyotengwa ni kwa ajili ya kujenga vyuo viwili, Chuo cha Maendeleo cha Wananchi Msaginya kwa ajili ya kujenga madarasa manne tu, Chuo cha Maendeleo ya Mto Mbu yaani ni vitu vidogo vidogo wakati vyuo viko 55 katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi katika mchango wangu wa maandishi niliomba Serikali hii, vyuo hivi vinasaidia hata watu wa Dar es Salaam. Kuna Chuo kimoja cha Maendeleo ya Jamii kiko jirani pale Kibaha nikasema tufanye mkakati maalum wa kwenda kufundisha vijana kwa wingi mafunzo ya ufundi stadi, mafunzo ya ujasiriamali na kadhalika. Vyuo hivi vikiwekewa uzito vitasaidia maeneo mbalimbali ya nchi kwa sababu vimesambaa maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, naunga mkono hoja hii kwamba tusiipitishe hii bajeti kwenye kifungu hiki tuondoe shilingi ili fedha ziongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninapinga hoja hii kwa sababu kuongeza fedha ni jambo linalowezekana, tunaweza tukapitisha bajeti hii na tunayo wiki moja, niwaambie Waheshimiwa Wabunge tumeunda Kamati ya Bajeti, kuna wiki moja ambayo tutafanya kazi ya mashauriano, tutaiangalia bajeti za Wizara zote, tutaa kama Bunge wapi tuongeze, wapi tupunguze ili mradi tusiondoke nje ya ile framework ya bajeti tulioipanga. (Makofij)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kuwashawishi Waheshimiwa Wabunge tupitishe bajeti hii lakini katika mambo ambayo tutakayopeleka kwenye majadiliano liwe la Wizara hii. (Makofii)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kirigirini, yuko wapi?

MBUNGE FULANI: Ni Kisangi!

MWENYEKITI: Aah ni Kisangi, tumekosea kuandika.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami siungi mkono hoja hiyo na ninaungana na Mheshimiwa Peter Serukamba kwamba Kamati ya Bajeti ipo itafanya kazi, tutajadiliana.

Lakini pia nataka nimwongezee au nimrekebishe mwenye hoja, lazima aelewe maana ya ukarabati na ujenzi wa kitu kipyua. Unapokarabati ni kwamba unatengeneza kitu kilichobomoka au kilichokuwa kina marekebisho na unapojenga chuo unajenga kitu kipyua. Hapa tumewekewa bajeti ya ukarabati, naomba uelewe. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Keissy.

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nataka kumpa taarifa Mheshimiwa Mnyika, bajeti ya Maji kweli ilisimamishwa, wakaongeza lakini Wizara ya Maji haikupewa fedha za bajeti, walipewa robo ya fedha, hilo ulijue. Hata tukisema bajeti tuisimamishe, fedha hawatapewa, fedha hakuna, Maji walifanya hivyo. Nilizungumza hapa, waliniuzia mbuzi kwenye gunia, wewe ulikuwa wapi? (Kicheko)

WAZIRI WA MAENEDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii. Ni kweli tumeepanga fedha hizo shilingi bilioni 1,800,000,000 kwa ajili ya ukarabati na kwamba fedha hizi tutazitumia kwa kazi ambayo imewekwa kama inavyooneshwa kwenye randama. Tumeamua kwamba hivi vyuo tuwe tunavikarabati kwa awamu kwa sababu huko nyuma tulikuwa tunapata fedha tunagawa kila chuo, anakarabati kidogo, kidogo. Sasa kwa sababu ni vyuo viwili, kwa fedha hizi tulizopata tutamaliza pale, tunaenda kwenye vyuo vingine, ndiyo mpango wetu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mkosamali.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Ninahitimisha hoja yangu na napata shida kwa sababu mtu anapokuwa haungi mkono hoja ya kuendeleza vyuo na yeye Jimboni kwake kuna vyuo, tunataka tuviinue ili vijana wasome, wapate ajira. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua, katika kupinga hoja, uwe unapinga kwa kuangalia unapinga hoja ya namna gani. Sasa wewe unakataa kuunga mkono hoja kwa sababu ya upinzani ili vijana wakose fedha, vyuo visiboreshwe, vijana wako kwenye Jimbo lako waendelee kukosa ajira. Hilo ni jambo la kushangaza sana na kusikitisha. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa shilingi bilioni moja ni fedha kidogo sana kwa vyuo hivi. Kama Wabunge wenzangu wangekubali kuniunga mkono, tungeviongezea vyuo hivi fedha. Mwaka jana kwa mfano, bajeti ya maendeleo ilikuwa ni shilingi bilioni 11 mwaka huu ni shilingi bilioni tisa, kwa hiyo imepungua. Nilichokuwa naomba Wabunge wenzangu, vyuo hivi ndiyo msingi, vijana wanamaliza *form four* wanafeli mitihani, ndiyo vitawafundisha ujasiriamali, namna ya kujitegemea na hakuna ajira. Sasa tunapoacha hii shilingi bilioni moja tunafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi mimi naomba tu tupige kura ili nishindwe kwa sababu maamuzi ya demokrasia ni wengi wape. Nashukuru sana lakini wananchi wameelewa watu wanaopinga vyuo visiendelee. (Makofii)

MWENYEKITI: Wakati tunapojadiliana hapa ni lazima mtu asikilize hoja lakini mara nyingi naona tunapiga kelele hata hoja zenyewe huwa hatusikilizi, kwa hiyo, mtu alichoking'ang'ania ni hichohicho mpaka mwisho. Sasa tufanye uamuzi.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)

(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)

Kif. 1002 – Finance and Accounts.....Tshs.670,052,000/=

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kasma 220200, *utilities, supplies and services*. Mwaka jana kasma hii ilitengewa shilingi milioni 129, mwaka huu shilingi milioni 216. Kuna utata juu ya mambo matatu ambayo ningeomba kupata ufanuzi juu ya kasma hii:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, kwenye randama inaonesha kwamba fedha za mwaka jana zilikuwa ni shilingi milioni 96 lakini hapa imeandikwa milioni 129, ningependa kupata ufanuzi.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini utata wa pili ambao ni mkubwa zaidi, ni nyongeza ya hizi fedha. Kama randama hii inasema milioni 96, safari hii zimekuzwa kuwa milioni 216. Sababu inayotolewa ya ongezeko kubwa namna hii ni kupanda kwa ghamama za umeme kwa sababu hiki kifungu cha *utilities, supplies and services* kinatumika kulipia maji na umeme. Sasa ongezeko la bei ya umeme la asilimia 40 ndiyo inatajwa kuwa sababu ya nyongeza ya kiwango hiki cha fedha. Sasa najaribu kupiga hesabu rahisi sana, kutoka shilingi milioni 96 ambayo iko kwenye randama hata ningefanya umeme ungepanda kwa asilimia 50 ni shilingi milioni takribani 50 hivi, ukijumlisha na hii shilingi milioni 96 kwa vyovyyote vile haiwezi kwenda mpaka shilingi milioni 216. Sasa ni nini ambacho kimeongezeka nyuma ya pazia kilichofanya sasa hiki kifungu cha umeme kifike shilingi milioni 216 tofauti na fedha za mwaka jana ilihali ambapo Wizara hihi masuala mengine ya msingi kama hayo ya matengenezo ya vuo na mambo mengine yanayohusu wanawake na maendeleo kwa ujumla wake hayajaongezewa fedha kwa kiwango hiki. Ningombaa ufanuzi, kwa nini tuongeze fedha nyingi kwenye kifungu hiki wakati ambapo kwenye vifungu vingine tunaambiwa kuna ufinyu wa bajeti?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kifungu hiki kinajumuisha asilimia kwanza 40 ya ongezeko la bei ya umeme lakini pia kinajumuisha maji na umeme na pia kuna madeni ya nyuma, kwa sababu wakati mwengine tunaomba kiwango fulani lakini unapata less. Kwa hiyo, yale madeni ya nyuma yanapaswa kuzingatiwa katika kifungu hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na ile 96 kwamba inatofautiana na 129, ni kwamba ile 96 ni kiwango kilichopokelewa lakini *it was budgeted* 129, lakini kilichopokelewa ni 96. Kwa hiyo, hapo tulipaswa kuandika kiwango kilichopokelewa.

(*Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote*)

Kif.1003 – Policy and Planning.....Tsh.507,610,900/=

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Najielekeza kwenye ile subvote 221000, travelling in country. Kimsingi ukijaribu kuangalia kwa mwaka jana walitenga shilingi 1,800,000/= mwaka huu wametenga shilingi milioni 49.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kufanya sort analysis kuanzia kwenye mafungu mawili ambayo tumemaliza na kuyapitisha muda mfupi uliopita, kuna ongezeko kubwa sana la hizi fedha kwa ajili ya *ku-travel in country*. Sasa nikawa najiuliza, kwenye bajeti ya maendeleo kwa mfano ya mwaka jana, katika bajeti ya shilingi bilioni 25 zilitengwa shilingi bilioni 11. Mwaka huu ambapo tena fedha

Nakala ya Mtandao (Online Document)

ya Wizara nzima imeongezeka shilingi bilioni 30, wametenga shilingi bilioni tisa, fedha za maendeleo zimepunguzwa lakini kwenye fedha za matumizi ya kawaida Wizara wanajirundikia fedha nyingi ambazo kimsingi *justification* yake hai-make sense, naomba nizungumze hivyo. Nasema hivyo kwa sababu hakuna rationale ya kutoka Sh.1,800,000/= na kuja kwenye shilingi milioni 49. Kwenye ile subvote ya administration pale tumeona kwenye mshahara wa Waziri wametenga shilingi milioni 258 kutoka kwenye shilingi milioni 101. Ukienda kwenye mafungi ya mbele kutoka shilingi milioni nne wanakwenda shilingi milioni 43...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali, tukifika hapa tunaomba tu-concentrate katika kile ulichouliza, kwa nini imeongezeka?

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Ninafanya hivyo kwa vile baadaye sitaki kusimama kupoteza muda.

MWENYEKITI: Aha, siyo utaratibu. Wewe sema hivi, mtueleze vyatukosha hizi zimeongezeka kwa sababu gani, ndilo swali lenyewe, basi!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Ninaamini hata hao wanaonipinga wanaelewa ni kitu gani nachozungumza. Naomba nipate kauli ya Serikali ni sababu gani ambazo zimepelekea kuongeza fedha hizi mpaka kuja kufikia shilingi milioni 49 kwa ajili ya kusafiri tu nchini, kusafiri tu, kutoka Sh.1,800,000=? Naomba sababu za msingi na kama sababu zitakuwa hazijaniridhisha, nakusudia kutoa shilingi. Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate sababu za msingi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, maelezo!

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba niseme mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba mwaka wa bajeti uliopita 2013/2014 kifungu hiki...

MWENYEKITI: Sogeza mic kwako.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mwaka 2013/2014 kifungu hiki kilipangiwa Sh.1,800,000/=. Kifungu hiki kinahusu fedha kwa ajili ya kulipia nauli kwa ajili ya Maafisa wa Bajeti, kazi hizo zimepangwa kufanyika nje ya Dar es Salaam, kwa mfano tunapokuja huku Dodoma, Maafisa wa Wizara yetu lakini pia fedha hizi zinaombwa kwa ajili ya posho ya kujikimu kwa watumishi 12 wa Idara ya Sera na Mipango na Maafisa 15 wa Wizara watakaoshiriki kuandaa bajeti na mipango, kazi na mtiririko wa mahitaji fedha.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tulipewa fedha ndogo sana, kulikuwa hamna ujanja, ikabidi tuweke 1.8 kutokana na ceiling lakini matumizi halisi ndiyo hiyo *49 million*. Kwa hiyo 1.8 iliwekwa mwaka jana kwa sababu ya ceiling kulikuwa hamna ujanja, lakini matumizi yake halisi ni milioni 49.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mkosamali!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Mheshimiwa Machali!

MWENYEKITI: Wanasema ni haohao! (*Kicheko*)

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba natoa shilingi. Ninatoa shilingi kwa sababu pamoja na maelezo ambayo ameyatao Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba mwaka jana walitengewa fedha kidogo lakini sijasikia hata siku moja kwenye shughuli za Kibunge Wizara hii walilalamika kwamba ni wapi walikwama kuweza kuja Dodoma na kwenda kwenye maeneo mengine. Napata shida sana Bunge lako wakati huu ambao tumefika kwenye Kamati ya Matumizi tunaelezwa kwamba bajeti ya mwaka jana ni kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kwamba hata kwenye vifungu vingine, hali ni hiyo hiyo. Tutaendelea hivi kuweza kupewa majibu mepesi kwenye maswali magumu mpaka lini? Naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu pasipokujali majina ya vyama vyetu, hivi vyuo ambavyo pengine vimekosa fedha na ninasema kwamba fedha hizi pengine tuzipunguze, tuzihamishe tuzipeleke kwenye bajeti ya maendeleo ambayo imepungua kutoka shilingi bilioni 11 za mwaka jana na kuja kwenye shilingi bilioni tisa. Watu wengine mtakataa tu kwa sababu hoja inatolewa na mimi natoka Upinzani, wewe unatoka CCM lakini elewa kwamba huyo mwananchi ambaye yuko kijijini ambaye amekosa darasa na dawati la kukalia, siyo wa CCM wala wa Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba...

*(Hapa kengele illilia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Kengele imegongwa.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapo, bado naendelea kushika mshahara wa Waziri. Naomba kutoa hoja.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MWENYEKITI: Yaani wewe umeishatoa hoja. Mheshimiwa Mdee! Sasa tunajadili hoja yako, lakini haiko very clear.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi naungana na hoja ya Mheshimiwa Machali kwamba tunaona kwa trend ya bajeti ni kweli kwamba Wizara hii inapewa fedha kidogo lakini mwaka jana Wizara hii ilikuwa na fedha kidogo zaidi kuliko mwaka huu. Mwaka jana bajeti nzima ya Wizara ilikuwa ni shilingi bilioni 25, mwaka huu bajeti nzima ya Wizara ni shilingi bilioni 30. Hata hivyo, utaona licha ya kwamba Wizara imeongezewa shilingi bilioni tano, hizo shilingi bilioni tano badala ya kwenda kwenye vipaumbele imekwenda kwenye OC, imekwenda kwenye matumizi ya kawaida. Vilevile tulikuwa tunatarajia kwamba mwaka jana fedha ya maendeleo ilikuwa nydingi shilingi bilioni 11...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima, tunazungumzia ka-sub item haka, kwa sababu tukiacha open itakuwa kama vile zamani. Tunazungumzia haka, ninyi mnasemaje?

MHE. HALIMA J. MDEE: Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Naomba sana, tukifanya hivyo, tunafungua Pandora's box.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, hatufungi chochote. Hoja anayoizungumza Mheshimiwa Machali ni nyongeza ya fedha.

MWENYEKITI: Hii hapa...

MHE. HALIMA J. MDEE: Hiyo hapo.

MWENYEKITI: Ngapi?

MHE. HALIMA J. MDEE: Na hoja naijenga...

MWENYEKITI: Ni ngapi maana mnasema hiyo hapo.

MHE. HALIMA J. MDEE: Shilingi milioni 49.

MWENYEKITI: Ehe, sasa tuzungumzie hiyo.

MHE. HALIMA J. MDEE: Tunasemaje, kwamba Wizara hii licha ya ufinyu wake wa bajeti kila mwaka, mwaka huu wameongezewa shilingi bilioni tano lakini badala ya kwenda kwenye project ambazo zina faida za maendeleo, zimerudi kwenye OC. Ndiyo maana naunga mkono hoja yake kwamba kuna haja...

MWENYEKITI: Fedha zake huyu ni shilingi milioni 49, hiyo shilingi bilioni tano iko wapi katika kakifungu haka?

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa...

MWENYEKITI: Jamani, naomba tuelewane. Naomba kwanza ukae.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajenga hoja, huwezi kujenga hoja kiroborobo!

MWENYEKITI: Mheshimiwa, ukae kwanza, ndiyo utaratibu wetu na kama mnavunja utaratibu wenyewe basi hatuwezi kufanya kazi vizuri. Tunachokisema, tukishaondoka kwenye mshahara wa Waziri, huku tukifika tunakwenda kwenye item by item. Sasa ukituambia shilingi bilioni tano wenzio tunapata tabu ya kutafuta shilingi bilioni tano, hatuoni. Tunayoona hapa kulikuwa na Sh.1,800,000/= mwaka unaokwisha, sasa shilingi milioni 49, ndiyo swali la Machali nafikiri, kwa nini imeongezeka, ndiyo swali la Machali! Hiyo bilioni nyingine sijui mnatoa wapi, sisi hatuoni. (Makofii)

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee?

MWENYEKITI: Dakika zako zimekwisha.

MHE. HALIMA J. MDEE: Niendelee si ndiyo?

MWENYEKITI: Endelea, uwe kwenye point.

MHE. HALIMA J. MDEE: Ninachosema ilikuwa milioni moja, imeongezeka milioni 49, sawa sawa? Ninachosema ni hivi, hatuwezi kuruhusu Wizara ambayo mwaka jana ilikuwa inalalamika haina fedha za maendeleo, imeongezewa fedha za bajeti zaidi ya bilioni tano badala ya kupeleka kwenye miradi ambayo ina manufaa, wanajiongezea posho. Hiyo ndiyo hoja anayozungumza hapa. Pesa za OC zimeongezeka! Kwa hiyo, mimi najenga hoja katika dhana pana kuja katika hii dhana nyepesi ya shilingi milioni 49. Ukienda katika kila kifungu wamejiongezea fedha.

MWENYEKITI: Halima, Halima, una akili sana, lakini hapa sivyo! Haya, tunaendelea, nani mwingine nilimwona, Mheshimiwa Ole-Medeye.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Machali kwa jitihada anazofanya kuhakikisha kwamba mgawanyo wa rasilimall unafanyika kwa uwiano.

MWENYEKITI: Mkosamali, siyo Machali.

MBUNGE FULANI: Ni Mkosamali!

MWENYEKITI: Aah watoto wangu hawa nawachanganya kila siku. (Kicheko)

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningeomba tu wenzangu na hususan Mheshimiwa Machali tuelewane kwamba tunapopanga matumizi ya bajeti ya fedha tulizopewa kila Wizara, tunapanga kwa kuzingatia vipaumbele vilivyo katika Wizara inayohusika. Haiwezekani leo hii kwa mfano Idara ambayo inahusika na mipango katika Wizara, yenyewe ndiyo inahusika kuandaa maoteo ya bajeti, inaandaa bajeti, inaratibu mapendekezo ya bajeti ya Idara zingine zote na kuwasilisha kwenye Kamati mbalimbali zinazohusika, uwaambie kwamba kwa kuwa mwaka jana hamkupata fedha za kusafiri na mwaka kesho msiwe nazo, haitakuwa halali na hatufanyi hivi kwa nia njema. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi siungi mkono hoja yake ya kutaka kutoa shilingi hapa kwa sababu hoja aliyotoa siyo ya msingi na haina nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

MWENYEKITI: Naomba tufanye maamuzi. Waziri eleza kwanza kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kimsingi mwaka jana tulipopangiwa Sh.1,800,000/= Idara ya Sera na Mipango, katika *travel in country* ni kitu ambacho hakiwezekani. Kuna Wabunge hapa akitoka Jimboni akifika hapa tu ile *amount anatumia single person*. Hii ni Idara ya Sera na Mipango kwa mwaka mzima Sh.1,800,000/= bajeti iliyopita, maana yake ni kwamba shughuli zilikuwa zinaenda kwa madeni (*on credit*), watu walisafiri bila kulipwa stahili zao na kadhalika. Kwa sababu tuna wakandarasi wa kutupa *ticket* labda za usafiri wa ndege au tuna watu tunachukua *bill* ya mafuta, kwa hiyo, Sh.1,800,000/= Idara ya Sera na Mipango mwaka mzima, Waheshimiwa Wabunge hebu tulitafakari, ndiyo maana sasa hivi imekuwa milioni 49 ikimaanisha ndiyo *actual* yenyewe lakini pia inakwenda kulipa na zile stahili ambazo mwaka jana tulifanya *on credit* bila kupokea haki.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali malizia hoja yako.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sasa hivi umekumbuka na jina langu vizuri. Bado ninasema kwamba majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri hayajaweza kukata kiu yangu kwa sababu hakuna namna ambavyo ninaweza kushawishika wakati ambapo ninaona kwamba walitenga fedha kidogo mwaka jana, hivi vyote ni visingizio tu kwamba ceiling ilikuwa hiyo mwaka jana na ndiyo tumekuwa tuna experience hiyo wakati tunapitisha bajeti za Wizara tofauti. Dhamira haipo Serikalini ya kuona kwamba fedha nydingi inaelekezwa kwenye miradi ya maendeleo. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivi kwa sababu kwenye level ya Kamati hata ile 60% ya kutaka fedha za miradi ya maendeleo kwenye Halamsahuri zetu iweze kutengwa imekuja kuwa ni mgogoro mpaka tulipokuja kulazimisha. Kwa hiyo, hata leo sishangai Mheshimiwa Waziri kuendelea kushikilia msiammo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira ya kawaida ni ngumu sana Wabunge wa CCM kuweza kuniunga mkono mtu kama mimi, ninaomba tupige kura tu ijulikane kuwa wao siku zote hawako kwa ajili ya maslahi ya wananchi. Ninaomba niishie hapo. (Makofii)

MWENYEKITI: Maneno ya mwisho sahihi, sasa ninawahoji.

(Hoja ilitolewa ilimuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Ninaomba tu-stick kwenye items tusiingie kwenye Pandora's box nyingine tulishapita kule, Katibu!

Kif. 1004 – Internal Audit Shs. 272,822,500/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kif. 1005 – Government Communication
UnitShs.307,028,500/=

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, bado na mimi ninakuwa na mshangao mkubwa kwa Wizara ambayo inasemekana fedha yake chache kabisa...

MWENYEKITI: Twende kwenye item.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Niko kwenye item 221200 inahusu *Communication and Information*. Naendelea kuwa na mshangao mkubwa kwa Wizara ambayo fedha yenyewe ni chache mwaka jana walipewa shilingi milioni kumi na moja lakini safari hii zimekuwa ni shilingi milioni tisini na mbili kuna ongezeko la shilingi milioni themanini na moja, pamoja na kwamba kuna haja ya kuongeza lakini unaongeza kiasi hiki, Wizara ambayo fedha yake ni chache kabisa? Kwa kweli ninataka ufanuzi wa kutosha.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinahusu *Government Communication Unit*, kwanza kuna masuala ya matangazo lakini pia kuna masuala ya uanachama. Kwa kweli kama nilivyosema mwanzo kwamba kipindi kilichopita ilitengwa shilingi milioni kumi na moja na haikukidhi haja lakini shughuli zilikwenda. Kwa hiyo, milioni tisini na mbili ndiyo matumizi halisi ya kifungu hicho cha Idara ya *Communication and Information*.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kif. 1006 - Procurement Management Unit...Shs.291,993,700/=

Kif.1007-Information, Communication
and Technology.....Shs.194,622,000/=

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa
na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1008-Legal Services Unit..... Shs. 101,605,900/=

MHE. SUSAN L.A. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kifungu kwanza kinaonekana ni kipyा.

MWENYEKITI: Kipi?

MHE. SUSAN L.A. KIWANGA: Kifungu cha 1008 lakini ninakwenda kwenye kifungu kidogo 221300, *Education Material, Supplies and Services*. Kifungu chote kwa ujumla pamoja na hiki ninachozungumzia miaka miwili ya nyuma kulikuwa hakuna chochote lakini mwaka huu wamekitengea shilingi laki mbili na hamsini. Sasa hapo mimi ninashangaa hii Idara ya Huduma za Kisheria kama inawekewa hela ndogo namna hii na matatizo yalivyokuwa mengi katika Wizara hii kubwa ya Wanawake na Watoto, hii hela itaenda kufanya nini katika kifungu hiki?

MWENYEKITI: Ahsante, laki mbili na hamsini elfu.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo ni fedha za kugharamia vitabu kwa mtumishi mmoja tu atakayehudhuria mafunzo ya muda mrefu kama ilivyooneshwa kwenye randama lakini Kitengo hiki ni kipyä, Wanasheria wetu zamani walikuwa katika kila Department lakini sasa hivi wote wako katika Department moja.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na
Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kif. 2001- Training and Folk Development

Colleges..... Shs. 10,079,302,400/=

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kasma 221400, *Hospitality Supplies and Services*. Kasma hii inahusu utoaji wa chakula pamoja na mambo mengine kwa wanafunzi kwenye Vyuo hamsini na tano vya Maendeleo ya Wananchi. Sasa vyuo hivi vina jumla ya wanafunzi elfu arobaini mia sita na tisini na mbili na hizi ni pesa za chakula kwa wanafunzi. Mwaka uliopita zilitengwa shilingi bilioni moja nukta moja na mwaka huu zimepungua imekuwa ni bilioni moja peke yake. Kwa maneno mengine hata pesa za chakula kwa wanafunzi zimepunguzwa kwenye Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ningependa kupata ufanuzi kutoka kwa Waziri na katika eneo hili kama maelezo hayataniridhisha nitaomba kuondoa shilingi. Ni kwa nini matumizi yote yaliyoonekana ni muhimu kupunguzwa Wizara imeamua kwenda kupunguza fedha za chakula kwa wanafunzi kwenye hivi vyuo? Maana yake ni kwamba hali hii ikiachwa wanafunzi hawa wanaofundishwa ujasiriamali, stadi za kazi na kadhalika, elimu yao itakwenda kuathirika kwenye vyuo hamsini na tano vilivvoko kwenye Wilaya mbalimbali za nchi za nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina maslahi katika hili kwa sababu jirani kabisa na Jimbo la Ubungo, jirani na Kiluvya pale pemberi tu Kibaha, kuna Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha na ninajua kwamba kuna wanafunzi kutoka Jimbo la Ubungo wanasoma pale na walikuwa wanalamika hata kwa fedha hizi masuala ya chakula yalikuwa hayako vizuri. Sasa haiwezekani wakati ambapo masuala ya chakula hayako vizuri pesa za chakula zinazidi kupunguzwa. Jambo hili haliwezi kukubalika, ninaomba ufanuzi kwa Wizara ana iwapo hautaridhisha nitaomba kuondoa shilingi kwenye eneo hili.

MWENYEKITI: Wewe suala lako kubwa hapa kwa mara ya kwanza, ni kwa nini fedha zimepungua hivyo? Basi, ndio hilo.

WAZIRI WA MAENDELEO JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hizi ni fedha za chakula na kutokana na *ceiling* ya bajeti kwa jinsi tulivyopanga mipango yetu tumeona tuwapangie hivi. Kubwa ni kwamba Vyuo vingi vya Wananchi vina mashamba, vinajitegemea, vinalima, vina matunda na kadhalika. Kwa hiyo, kuna vyuo vingine unakuta vinaweza kujimudu vyenyewe (*self sustained*). Kwa hiyo, ndio maana kwenye Folk Development Colleges tofauti na cha Kibaha kuna wengine wanalima mashamba makubwa na vyuo hivi viko chini ya ulezi wa Halmashauri ambapo viro kwa hiyo mara nyingi wanasaidiwa hata katika kulima, wana matrekta na vitu kama hivyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika shilingi yako itoe sasa.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuondoa shilingi ili Wabunge kutoka maeneo mbalimbali ya nchi yetu ambao kwenye Vyuo vyao, Mheshimiwa Waziri anasema kwa kuwa vina mashamba vina uwezo wa kujilisha waweze kutoa uzoefu kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitoe uzoefu wa Chuo cha Kibaha ambacho kabla ya kuwa Mbunge...

MWENYEKITI: Ngoja kwanza, yaani katika maeneo haya ni kuwa focused maana ukieleza tena habari za Kibaha hizi hela wamegawiwa shilingi ngapi, hicho chuo unachosema wewe?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nakaa kwa sababu ulikuwa umesimama ninaomba niendelee sasa.

MWENYEKITI: Sawa, ndio nakuuliza hapa wamepewa shilingi ngapi?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Bunge kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 63 ni kuishauri na kuisimamia Serikali na kwa kufanya hivyo tunapitisha bajeti.

MWENYEKITI: Sawa kuna utaratibu.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Katika mazingira ya kazi hiyo, ninaomba nimalizie.

MWENYEKITI: Naomba tuwe focused kwa sababu tunaenda nje.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Ndiyo niko kwenye jambo hilihili moja kwa moja. Mheshimiwa Waziri alipaswa kutueleza hapa kiwango kinachopungua kutoka shilingi bilioni moja pointi moja kwenda shilingi bilioni moja peke yake kwa zaidi

ya shilingi milioni mia moja, atueleze sasa hiki kiwango kipyä, atupe mchanganuo hapa vyuo hivi hamsini na tano kila kimoja kitagawiwa kiasi gani ili tuwe na uhakika hapa kwamba hivi vyuo kweli vitapata chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila mimi nataka kutoa uzoefu tu kwamba chuo cha jirani yangu pale Ubungo cha Kibaha mnapowapunguzia fedha kiasi hiki wanafunzi wanapata shida. Wakuu wa Vyuo wale wakitaka kuziba hili pengo wanaanzisha michango au gharama kubwa ya ada mpaka katika hivi vyuo vya chini kabisa vya wananchi. Sasa tukipitisha hii tunakwenda kuwaumiza ama wanafunzi kwa maana ya kutokupa chakula ipasavyo au kwenda kuwabebesha mzigo wa gharama na wengine watashindwa kusoma, hivi ndio vyuo vya maskini na vya ngazi ya chini kabisa. Kwa hiyo, naomba jambo hili lijadiliwe hizi pesa zisipungue kwa kiasi hiki, sijaridhishwa na maelezo ambayo Waziri ametoa. (Makofii)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jafo hii siyo hoja yako, sasa tunajadili hoja ya Mheshimiwa Mnyika.

MHE. SELAMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kweli siyo hoja yangu lakini mwanzo nilisimama kwa ajili ya kipengele hichohicho.

MWENYEKITI: Endelea kuchangia.

MHE. SELAMANI S. JAFO: Concern yangu na mimi ilikuwa ni kuihoji Serikali katika eneo hilo, ni jinsi gani tutafanya hapo, maana ukilinganisha na bajeti ya mwaka jana mwaka huu tumeshuka. Kwa hiyo, hata mwanzo nilivyosimama nilitaka tuzungumze hoja hiyo pamoja na Mheshimiwa Mnyika kwamba kwa nini hizi pesa haswa kwa suala zima la chakula kwa vijana zimeshuka zaidi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba kauli ya Serikali hapa ni jinsi gani itafanya utaratibu wa kuhakikisha kwamba vijana wetu hawaathiriki kwa sababu tunajua bajeti hii mwisho wa siku ni kwamba vijana wale walioko shulenii watapata shida. Kwa hiyo, tunaomba kauli ya Serikali, tutafanyaje hapa ili vijana wetu wasiweze kuathirika katika suala zima la chakula ambalo ndilo msingi wa masomo kwa vijana wetu wakiwa vyuoni, ahsante.

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mnyika lakini nizungumze kidogo na Wabunge wenzangu.

MWENYEKITI: Tuwe kwenye hoja hii, hakuna kuzungumza na Wabunge wenzako.

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono, kufanya hivyo ilivyo itaonyesha dhahiri kabisa tunawabebesha mzigo wazee ambao watoto wao ni maskini, wanahitaji kupata huduma hii vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina-declare interest kwamba ni Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii na kuna Wabunge wenzangu humu ndani tunatoka katika Kamati hiyo pamoja na Mawaziri walioko mbele yetu, tumekubaliana pamoja twende Bungeni tukawasaidieni ili Wizara iweze kukamilisha majukumu yake. Sasa ajabu ni kwamba tunapojitahidi kujenga hoja hii ili Serikali ione umuhimu wa kuboresha Wizara hii bado Wabunge wengine ambao tumekubaliana mle ndani tunapingga hoja hii ndani ya Bunge hili, tunafanya hivi kwa maslahi ya nani? (Makofij)

Mheshimiwa Waziri umetuambia tuje tukusaidie hapa Bungeni ili hii bajeti iweze kuongezewa pesa lakini sasa inaonekana kuwa Wapinzani ndiyo wenyewe hoja hiyo, Wabunge ambao tuko ndani ya Kamati ile tunashindwa kumsaidia Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mnyika. (Makofij)

MBUNGE FULANI: Kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Kama ndiyo hivyo, ngoja tuzungumze. Utaratibu ambao upo katika mfumo wa new budget system kila Kamati iliyokuta mahali palikuwa contentious wameandika na iko Kamati inayopokea na hivi sasa wanaendelea kuchambua vitu kama hivyo. Kama mlizungumza hivyo kwenye Kamati yenu na kule kwangu dokezo limeletwa linalohusu mambo hayo. Ndiyo maana siku ile nikawaambia haya mapitio tunayopitia hapa ni provisional kwa sababu kutatokea mabadiliko mengi tu. Ndiyo maana unakuta Wizara kubwa ile maji kwa sababu mwaka jana tulikuwa na priority ya maji, tulikuwa tuna priority ya umeme, tulikuwa na priority ya eneo fulani...

(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa wanaongea)

MWENYEKITI: Naomba mnisikilize kwani tukisikilizana ndiyo tunaelewana lakini tukiwa tunataka kila mtu anavyotaka haiwezekani, ninasema utaratibu wetu uko hivi. Kwa hiyo, kila Wizara wanapitisha kwangu lakini imeundwa unit wanapokea na kupeleka kwenye Budget Committee. Kwa hiyo, Budget Committee inaangalia yale miliyokubaliana kwenye Kamati yenu kwamba hii hela haitoshi inakwenda kule. Sasa Budget Committee itaangalia wigo wote wa matumizi ya Serikali na kwamba kama ni finyu sasa tuweke nguvu mahali gani. Ndiyo maana nikawaambia makadirio tunayopitisha sasa hivi kwa kiwango fulani ni provisional kwa sababu yatakapotoka kwenye Budget Committee siyo

kwamba kutakuwa na hela zingine tutazi-reshuffle hizihizi. Sasa na Kamati hiyo ya kwenu nayo wameleta kwangu dokezo, kwa hiyo siyo kwamba mbishane hapa hamuwezi kuongeza, kubishania hapa ongeeni tu lakini ni kwamba mnajenga hoja. Ndiyo tunavyofanya kwenye Budget Committee sasa. Mheshimiwa Susan.

MHE. SUSAN A.J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Mnyika kuhusiana na fedha ndogo za chakula katika vyuo hivi. Ni kweli kwamba kwa sasa hivi vyuo vingi vinakosa chakula na matokeo yake hasa kwa watoto wa kike wanajiua na kwa maana hiyo tutasema kwamba Serikali hii inasababisha watoto wetu wapate magonjwa mbalimbali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo nilikuwa ninaiomba sana Serikali ihakikishe kwamba suala la chakula kwa wanafunzi wetu siyo tu wa vyuo hivi, wa vyuo vyote wanapata fedha zao kwa wakati ili tuepukane na tatizo la watoto wetu hasa wasichana kujiua na hivyo kuliletea Taifa hili athari kubwa za magonjwa ya kuambukiza. Nashangaa Wizara hii inaongozwa na wanawake lakini wanaona ugumu kutetea suala la fedha kwa watoto wetu wa kike ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante ila umezidisha, Mheshimiwa Serukamba.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa John Mnyika ukiangalia fedha iliyopunguzwa ni shilingi milioni mia moja, ukichukua shilingi milioni mia moja kugawa kwa watoto hao elfu arobaini maana yake kilichopunguzwa ni shilingi elfu mbili na mia tano. Nataka tukubaliane kwamba Bunge hili, kwamba elfu mbili na mia tano maana toka mwaka jana mpaka mwaka huu kilichopungua ni shilingi elfu mbili na mia tano tu kwa ile ambayo ungempa kwa mwaka huyo mwanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaamini chuo kama cha Kihinga wanachuo wengi wanakaa nyumbani. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba vyuo vyote watu wanakaa kwenye hosteli. Kwa sababu hiyo ni lazima tutarajie gharama kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ambalo ninataka kusema zinaonekana fedha zimeongezeka bilioni tano lakini zimeongezeka kwenye mshahara na sisi wenyewe tumekuwa tukisema kwamba wafanyakazi wa nchi hii waongezewe mshahara. Kwa hiyo, tulipokuwa tunalalamika kwa nini tumeongeza shilingi bilioni tano ni kwa sababu ukiangalia hapa hata kwenye college tumeongeza shilingi bilioni nne kwa ajili ya mshahara. (Makofi)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi siungi hoja yake kwa sababu ninaamini fedha hii hatuna pa kuitoa kwa sababu wanafunzi wanakaa nyumbani.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAENDELEO JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niongezee tu kwa kusema kwamba kule kwenye hivi Vyuo vya Wananchi zile ada zinazotolewa ziliwa ndogo sana ndiyo maana tumekuwa tukiwapelekea hizi pesa lakini zile fedha zinazopatikana zinabaki kulekule zinasaidia pia katika kununua chakula. Kuna *cost sharing* baina yetu sisi na wao, hizi ni nyongeza. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumewashauri waongeze, ada ilikuwa ndogo sana, kwa hiyo wameongeza ada kidogo itasaidia kuziba lile gap. Hizi fedha tulizowapelekea ni sehemu tu zile ambazo wanatoa kama ada inabaki kule itawasaidia kuongeza kwenye chakula.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika, naomba tu-stick to the point otherwise tunaogelea every where.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna shaka nitajikita kwenye jambo hilihili. Utaona mgongano mkubwa kati ya mchango wa Mheshimiwa Peter Serukamba aliyedai kwamba kwa sababu wanafunzi wanakaa nyumbani wataweza kujihudumia hakuna haja ya kuongeza hela ya chakula na majibu ya Mheshimiwa Waziri ambaye anakiri kwamba kweli kutakuwa na tatizo na ufumbazi wa hilo tatizo wanakwenda kuongeza ada kwa wanafunzi kule chini. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua tofauti na vyuo vingine hizi *Community Folks*, ni vyuo vya chini kabisa vya wananchi wa kipato cha chini kabisa kwa ajili ya kujisaidia kujikwamua. Sasa haiwezekani Vyuo vya Wananchi wa kipato cha chini kabisa kuwafundisha ujasiriamali, kuwafundisha maarifa walioshindwa kwenda chuo kikuu au vyuo vingine vya elimu ya juu ili angalau wajajiri na vyenyewe tunaendelea kuwaongeza kodi kwa sababu ambazo hazina msingi kwani kuna mafungu mengine ambayo tungeweza kuziba kabisa kuziba hilo ombwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi siridhiki na jambo hili na ningeomba lipigiwe kura ili wale ambao wanataka kwenda kuwaongeza ugumu wa maisha wale watu kule vijijini kwenye Wilaya mbalimbali wapige kura ya 'ndiyo' na sisi ambao tunaona kwamba kuna maeneo mengine ambayo Serikali hii inaweza kubana matumizi kwa ajili ya kwenda kuwasaidia chakula wanavyuo waweze kusoma kwa ufanisi tupige kura ya kuunga mkono hoja hii.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Mna-politicize, hizi ni fedha kidogo tu. Sasa tunafanya maamuzi.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja ilimuliwa na Kukataliwa)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Pareoso!

MHE. CECILIA D. PARESO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa nataka tu ufanuzi kidogo kwenye kasma 210100 - Basic Salaries. Ukiangalia mwaka jana ilikuwa shilingi 4,000,000,000 na sasa hivi ni shilingi 8,000,000,000, kuna ongezeko kubwa sana. Tungependa kufahamu ni Watumishi wangapi wameongezeka?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri maelezo!

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wameongezeka Watumishi 295, lakini pia kuna ongezeko la mishahara.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2002 - Community Development.....Sh.3,839,970,800

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Mheshimiwa tumepita tuendelee.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tupate ufanuzi katika...

MWENYEKITI: Tumeshapitisha tumesema Ndiyo tayari.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Okay, sawa.

Kif. 2003 - Community Dev. College - Tengeru Sh.1,136,267,100

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kif. 3001 – Gender Development.....Sh.723,144,200

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rashid!

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nipo katika Item 221000, inayohusu Travel- In-Country.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana kifungu hiki kilitengewa shilingi milioni kumi, lakini mwaka huu kimetengewa shilingi milioni 152; ni ongezeko la shilingi milioni 142! Mheshimiwa Waziri alisema kwamba, katika Halmashauri wapo Maafisa wake mbalimbali wa Huduma za Jamii ambao wanashughulikia masuala yanayojitokeza kule. Kwa nini fedha hizi zinaongezeka kwa kiasi kikubwa kama hiki katika Wizara ambayo inasema haina fedha? Naomba maelezo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma anaona ilikuwa milioni mbili, milioni kumi. Hapa pana kazi nyingi sana za kusafiri. Department hii ndiyo inayoshughulikia masuala ya ukatili wa wanawake Kanda ya Ziwa. Kila mahala hawa ndiyo wanaokwenda. Vilevile hapa kuna madeni makubwa sana ya tiketi za ndege, masuala ya safari pamoja na mambo mengine yanayohusiana na kusafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ilipata OC asilimia 25 tu. Hii ina maana hizi pesa nyingi ambazo mnaona zimeongezeka ni ile asilimia 16 ambayo tumeongeza na tutalipia madeni katika Departments mbalimbali.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 3002 - Children Development....Sh.357,079,676

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 4001 - Non-Government Organizations.....Sh.425,273,312

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti. Kasma 229900 - Other Operating Expenses, Matumizi Mengineyo. Mwaka juzi hakikutengewa fedha, mwaka jana hakikutengewa fedha, mwaka huu kimetengewa shilingi milioni 25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Randama ya Wizara, kifungu hiki ni kwa ajili ya kulipa posho ya Vikao vya Bodi, shilingi milioni tano na shilingi

Nakala ya Mtandao (Online Document)

milioni 20 ni kwa ajili ya kumlipa Mtaalamu Mwelekezi kwa ajili ya kufanya tathmini juu ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Hotuba ya Waziri ameeleza kwamba, kila mwaka wamekuwa wakifanya tathmini juu ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Tafsiri yake ni kwamba, Wizara imekuwa ikifanya tathmini na kuandaa Ripoti na imetueleza Ripoti kuhusu utendaji wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Ghafla safari hii kuna suala la Mtaalamu Mwelekezi wa kuandaa hiyo Ripoti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeomba ufanuzi wa Wizara kwa nini safari hii wanaamua kutumia Mtaalamu Mwelekezi wakati kuna Maafisa wa Wizara ambao wameajiriwa kwa ajili ya kufanya kazi hiyo na wamekuwa wakiifanya? Iwapo sitaridhika na ufanuzi kwenye jambo hili, nitaomba kutoa hoja, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya kuhamisha kiwango cha fedha kitoke katika kijifungu hicho kihamie kwenye kijifungu kingine cha 221600 - *Printing, Advertising and Information Supplies and Services*, ili sasa kwanza, kabla ya kwenda mbele tuweze kuchapishiwa ripoti za tathmini za mwaka jana, ziletwe hapa Bungeni tuzijadili ili tuone Mashirika yasiyo ya Kiserikali yaliyofanya vibaya, Mashirika yaliyofanya vizuri, Mashirika yaliyotumika, tuje tuyajadili hapa. Kwa hiyo, hizi pesa zitumike kuchapishia ripoti tuletewe Bungeni.

Kwa hiyo, naomba ufanuzi, nisiporidhika naomba nafasi ya kutoa hoja, kwa mujibu wa hii Kanuni ya 102, ili niweze kuhamisha hilo fungu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika kifungu hiki, Wizara ina mpango wa ku-review Sera ya NGO na kufanya tathmini ili iweze kufanya kazi vizuri zaidi. Tangu tuanze mpaka sasa tumefikia wapi, kuna malalamiko mengi na kuna mambo mengi ambayo tunataka tujue baada ya hii Sheria kutungwa na hii Sera kuwepo. Sasa hizi ni kweli zitatumika katika shughuli hiyo ya kuwa na Mtaalam Mwelekezi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa ulisema unataka kutoa shilingi? Ulisemaje?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa hoja siyo ya kuondoa shilingi ila kwa mujibu wa Kanuni ya 102, Fasili ya Pili na naomba Wabunge zangu waniunge mkono...

MWENYEKITI: Itabidi u-justify kwelikweli kwamba, hizo printing ziko wapi.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna shaka. Nilichokuwa nakisema hapa, naomba kutoa hoja kwamba, hii milioni 20 hii iliyoko hapa, badala ya kulipwa Mtaalamu Mwelekezi mmoja, hizi pesa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

zihamishiwe kwenye kifungu cha machapisho ili ripoti za utafiti za miaka iliyopita ambazo tunaelezwa tu kijuujuu hapa na Wizara, ziweze kuchapishwa na ziletwe hapa Bungeni. Tujadili kwanza ripoti zilizotangulia kwa sababu kama ni tathmini ya Mashirika, tayari Wizara inayafanya tathmini ya Mashirika kila wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo ni la msingi sana na niseme tu kwamba, nasikitika Mheshimiwa Waziri amelidangaya Bunge. Anapaswa kutuambia kipi ni cha kweli; kwenye Randama hajasema kwamba, Mtaalamu Mwelekezi ni kwa ajili ya kufanya mapitio ya Sera, hapana! Mtaalamu Mwelekezi ni kwa ajili ya tathmini ya utekelezaji wa Sera. Maana yake tathimini ya utendaji wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali ambayo kila mwaka imekuwa ikifanyika.

Kwa hiyo, maelezo aliyoyatao Mheshimiwa Waziri, yasikubalike badala yake tusiende kumlipa mtu mmoja hizi pesa. Pesa hizi ziende kutimiza kazi ambayo sisi wote Wabunge tunashiriki, ikiletwa hii ripoti humu tutaweza kubaini NGOs zilizokiuka Sheria katika masuala mbalimbali ikiwemo hii ya WAMA ambayo tulikuwa tunaijadili hapa. (Makof)

MWENYEKITI: Hapo unachanganya mambo! Sasa sisi kama kule haipo ni kitu gani hicho tunachokubali kihamishiwe kikaprintiwe hatukioni? Kitu gani tunacho-print? Kanuni ya 125 kwanza ni kinyume cha PPR.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 102 inasema hivi: "Katika Kamati ya Matumizi, Mbunge ye yote anaweza kutoa hoja ya kutaka kufanya mabadiliko katika Makadirio ya Matumizi ya Serikali, iwapo mabadiliko hayo hayatabadili madhumuni ya Fungu lile lote." (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi sibadili madhumuni ya hili Fungu la uratibu wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Fasili ya Pili inasema kwamba, endapo hoja iliyotolewa kwa ajili ya kupunguza kifungu fulani katika Fungu lolote haijapitishwa, hoja nyingine inaweza kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Kanuni hii, tunaruhusiwa kutoa hoja ya kupunguza kiwango na kuhamishia kwingine. Ninachokisema ni kwamba, Waziri amesema hapa, tayari wamekwishafanya tathmini ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali na wamefanya utafiti. Hiyo ripoti sisi hatujaiona! Kwa hiyo, sasa natoa hoja kwamba, milioni 20 badala ya kumlipa mtu mmoja kufanya kazi ambayo kila mwaka Wizara ilikuwa inaifanya, zihamishiwe kwenye machapisho ili sasa tuletewe ripoti Bungeni, tujadili juu ya performance ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja na Wabunge wenzangu waniunge mkono na ambao wapo tayari kuijadili waijadili.

(Hapa Wabunge fulani walismama)

MWENYEKITI: Naomba mkae chini. Hoja za wakati wa matumizi ya fedha haziungwi mkono. Hoja ya shilingi ndiyo nzuri inachangiwa. Mheshimiwa Mnyika, tunaendesa hii kitu kwa kufuata taratibu. Hoja ya kuondoa shilingi Kanuni yake inasema mnawenza mkajadiliana hapa na mantiki yake ikaeleweka. Sasa hapa tukianza kwamba, unahamisha shilingi wakati hoja yenewe hukutujengea vizuri sisi wenzako ukatuambia hapa hasara zake ni nini na huku faida yake ni nini; hatuwezi kufanya maamuzi hapa, tutavuruga bajeti yote iliyoko hapa.

Kwa hiyo, hoja yako hata kama ni nzuri hivyo, lakini tunaiona imeelemea upande mmoja. Tunapoamua kufanya bajeti lazima tuwe na hoja. Ukiiondoa hoja ya shilingi na ina mwisho wake, ile ya shilingi inasema kwamba utachukua shilingi yako hata kama wakikuunga mkono itapita bajeti lakini inaondoka kwa shilingi moja. Huu ndiyo utaratibu, lakini hii ni hoja mahususi ya kubadilisha. Usome kifungu kingine kile, kipo kingine kinachozungumzia namna ya kubadilisha matumizi ya fedha. Kwa hiyo, mimi hii hoja siikubali kwa sababu inaleta fujo katika utaratibu wa kazi. (Makof)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 53 - Wizara ya Maendeleo Jamii, Jinsia na Watoto

Kif.1001 - Administration and HR Management..Sh.700,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.1003 - Policy and Planning.....Sh.451,153,880

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan umesimama au unafanya nini, maana yake na nguo umevaa na matambaa basi hatujui kama unavaa kanga au vipi! Haya Mheshimiwa Susan! (Kicheko)

MHE. SUSAN A.J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu 1003, kifungu kidogo cha 6290 - Programming and Data Processing Project chenye total ya 300,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kwa sababu kifungu hiki hela zinazoombwa hapa hakiendani na Randama, zinahusiana vilevile na *training*. Sasa naomba kujua inakuwaje fedha za *training* zinakuwa kwenye maendeleo wakati tuna kifungu kule nyuma kwenye re-current ambacho pia kinahusiana na masuala hayo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, umekiona hicho kifungu? Tunaomba maelezo.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kinazungumzia *Programming and Data Processing Project*; hii ni Project ndiyo maana imeingia kwenye Miradi. Hii itafanywa kuwajengea Maafisa Bajeti wa Wizara, uwezo kuhusu ukusanyaji wa takwimu, ufuatiliaji na tathmini ya kuandaa mfumo wa ufuatiliaji tathmini, kukusanya takwimu za awali zinazohusu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na kununua vitendea kazi kwa ajili ya matumizi ya Wizara.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif.1005 - Government Communication Unit.....	Sh.60,000,000
Kif.1008 - Legal Service Unit.....	Sh.28,700,000
Kif. 2001 - Training and Folk Development	
Colleges	Sh.1,842,732,520
Kif. 2002 - Community Development.....	Sh.61,000,000
Kif. 2003 - Community Development	
College-Tengeru.....	Sh.939,000,000

(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 3001 - Gender Development..... Sh.4,393,340,000

MHE. RAJAB MOHAMED MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, Subvote 3001, Kifungu 4943 - *Women Enomic Empowerment Project* ambacho kina shilingi bilioni nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuangalia Randama, nakuta kati ya fedha hizi, bilioni mbili ni kwa ajili ya Benki ya Wanawake. Benki hii ya Wanawake inamilikiwa na Serikali kwa asilimia 99 na asilimia moja tu ndiyo inamilikiwa na watu wengine. Kwa hiyo, ni kusema kwamba, sasa hivi Benki hii ina wajibu wa kuwa Shirika la umma. Mbali na hivyo ni kwamba, Benki hii

Nakala ya Mtandao (Online Document)

haijawahi kukaguliwa, haijapeleka hesabu zake kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokitaka mimi ni commitment tu ya Serikali kwamba katika mwaka ujao hii Benki itapeleka hesabu zake kwa Mkaguzi Mkuu wa Serikali ili zifanyiwe ukaguzi kwa sababu hii siyo Benki ya kisiasa.

MWENYEKITI: Mimi nafikiri ungeuliza hii Benki inakaguliwa na nani? Hata iwe hela yake useme inakaguliwa na nani?

MHE. RAJAB MOHAMED MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniwekea sawa.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Benki hii inakaguliwa na MS Innovates, ambao wameteuliwa na Controller and Auditor General.

MWENYEKITI: Samahani, Mheshimiwa Mnyika nilimruka.

TAARIFA

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo kwenye kasma hiyo ya 49, ila kwa sababu imeshaamuliwa, nampa tu taarifa Mheshimiwa Waziri, ukaguzi wa mwaka huu wa CAG umesema kwamba, Mkaguzi Mkuu ame-query kuwa Benki hiyo haikaguliwi na Mkaguzi Mkuu na ametaka ikaguliwe na Mkaguzi Mkuu. (Makofi)

Advantage ya kufanya hivyo siyo kwa ajili ya kuzuia mianya ya matumizi mabaya ya fedha. Jambo kubwa ni kwamba, CAG angekuwa anakagua, hivi ambavyo Serikali hai-comply bajeti; kwamba, bajeti inapitishwa Benki ipewe bilioni mbili, Serikali inatoa milioni 450 peke yake, CAG angeweka query ya maana sana juu ya compliance ya Serikali.

MWENYEKITI: Haya mambo ya CAG muwe mnatusomea hapo palipoandikwa maana tunasikia CAG, CAG, sisi hatujasoma!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kusema kwamba, bado kama alivyosema Mheshimiwa Mbarouk, commitment ya Serikali, Benki hii sasa ikaguliwe moja kwa moja na CAG, kama CAG mwenyewe alivyosema kwenye Taarifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali, itawasaidia Wanawake wa Tanzania.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MWENYEKITI: Taarifa ya kuhusu nini?

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuwapa taarifa rafiki yangu Rajabu na Mnyika kuwa Mabenki yote Tanzania yapo registered under BoT Act na Msimamizi Mkuu anayefuatilia kujua kama Benki hii inafaa kuendelea kuwa Benki ni Benki Kuu. Kwa hiyo, kama Benki hii haipelekewi mtaji, maana yake by now ingekuwa imeshanyang'anywa leseni na Benki Kuu.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema taarifa na mimi nina haki ya kujibu hiyo taarifa.

MWENYEKITI: Bwana hizo taarifa na sisi wote tunajifunza. Tunaendelea!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Maana amenipa mimi hiyo taarifa na kuna ripoti hapa kutoka kwa CAG, jambo hilo analolisema halina uhalisia.

Kif. 3002 - Children Development Sh. 541,617,600

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

TAARIFA

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu, limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Matumizi ya fedha ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka 2014/2015, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo basi, ninaliomba Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka 2014/2015
yalipitishwa na Bunge)

Hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Kama Ilivyosomwa Bungeni

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2014/2015 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kutimiza majukumu yangu kama Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Mohammed Gharib Bilal na Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kwa kuiongoza nchi yetu vema na kwa utekelezaji mzuri wa llani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe mwenyewe, Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti wa Bunge, kwa uendeshaji bora wa shughuli za Bunge.

Nachukua fursa hii, kuwapongeza na kuwashukuru wasaidizi wangu wa Wakuu walioteuliwa hivi karibuni na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaao ni Naibu Waziri, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho; Katibu Mkuu, Profesa Sifuni Ernest Mchome; na Naibu Katibu Mkuu Bibi Consolata P. Mgimba. Aidha, napenda kuwapongeza na kuwashukuru kwa ushirikiano mzuri, Kamishana wa Elimu, Prof. Eustella Bhalalusesa, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Wakuu wa Taasisi mbalimbali za Elimu zilizo chini ya Wizara yangu, kwa ushirikiano wao wa karibu katika kuandaa bajeti hii. Pia, nawashukuru Wahadhiri, Wakufunzi, Walimu na Watumishi wengine pamoja na Wanafunzi wote kwa kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. (Makofii)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, pia nawashukuru Viongozi wa Vyama vyatuhusu na Wafanyakazi na Vyama vyatuhusu na Wanataluma, Wanafunzi na Washirika wa MAendeleo, kwa ushirikiano wao katika kuiendeleza Sekta ya Elimu. Ninawashukuru pia Wazazi, Walezi na Wananchi wote kwa ujumla, kwa jinsi ambavyo wameendelea kushirikiana na Sekta ya Elimu katika kuendelea kuimarisha elimu na mafunzo nchini.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kutoa salamu za pole kwako na kwa Bunge lako Tukufu, kwa vifo vyatuhusu na Wabunge wenzetu wapendwa; Mheshimiwa William Agustao Mgimwa, aliyekuwa mbunge wa Kalenga na Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Said Ramadhani Bwanamdogo, aliyekuwa Mbunge wa Chalinze.

Mheshimiwa Spika, aidha, natoa pole kwa Wananchi wangu wa Jimbo la Bagamoyo, kwa athari za mafuriko yaliyowakumba katika baadhi ya maeneo. Niwahakikishie tupo pamoja na mara baada ya majukumu haya, nitashirikiana nao kushughulikia athari zilizotokea. Aidha, natoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wote waliofiwa na ndugu na wapendwa wao, kutokana na maradhi, ajali, majanga na matukio mbalimbali yaliyotokea nchini mwetu. Namwomba Mwenyezi Mungu, azilaze roho za Marehemu mahali pema peponi; amina.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Wabunge wapya amba ni Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa - Mbunge wa Kalenga, Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete - Mbunge wa Chalinze na Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein - Mbunge wa Chambani, kwa kuchaguliwa kwao kwa kura nyangi na hivyo kupata fursa ya kuchangia maendeleo ya Taifa kwa kuwakilisha Wananchi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Hati Idhini iliyounda Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundsi iliyotolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tarehe 17 Disemba, 2010, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundsi ina majukumu yafuatayo:-

- (a) Utungaji wa Sera za Elimu zinazohusu Elimu ya Awali, Elimu ya Msingi, Elimu ya Sekondari, Elimu ya Ufundsi, Mafunzo ya Ufundsi Stadi, Elimu ya Juu na Elimu ya Watu Wazima;
- (b) Utekelezaji wa Sera za Elimu;
- (c) Mafunzo ya Ualimu;
- (d) Usajili wa Shule;
- (e) Ukaguzi wa Shule na Vyuvo vyatuhusu na Ualimu;

- (f) Uchapati wa Machapisho ya Elimu;
- (g) Utoaji wa Huduma za Maktaba;
- (h) Uratibu wa Shughuli zinazotekelizwa na Kamisheni ya Taifa ya UNESCO;
- (i) Uratibu wa Shughuli za Taasisi na Wakala zilizo chini ya Wizara;
- (j) Usimamizi wa Utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali ya Wizara; na
- (k) Uendelezaji wa Rasilimali Watu na Uongezaji tija ya Watumishi walio chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 kuanzia tarehe Mosi Julai, 2013 hadi tarehe 31 Machi, 2014.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa mwaka 2013/2014 kupitia Idara na Taasisi ilikadiria kukusanya jumla ya shilingi 171,518,704,600 na hadi kufikia Machi, 2014 makusanyo ya maduhuli jumla ya shilingi 129,122,797,993.42, sawa na asilimia 75.3 ya makadirio.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, bajeti ya matumizi ya kawaida ilikuwa 617,083,004,000, mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu ilikuwa jumla ya shilingi 306,000,000,000, sawa na asilimia 79.5 ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2013, Wizara yangu ilitumia jumla ya shilingi 486,573,220,250.94, sawa na asilimia 79 ya bajeti ya matumizi ya kawaida. Asilimia 93.5 matumizi mengineyo zilitumika kwa ajili ya mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na Taasisi.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2013/2014 Wizara ilitengewa jumla ya shilingi 72,598,051,000, ikiwa ni Bajeti ya Maendeleo. Fedha za ndani ni 18,830,000,000, na fedha za nje ni shilingi 53,768,051,000. Matumizi jumla yalikuwa shilingi 14,921,545,855.46.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kutoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2013.14 kulingana na Hati Idhini kama ifuatavyo:-

Nitangulize utungaji wa Sera za Elimu.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, moja ya jukumu kubwa la Wizara yangu ni kutunga Sera mbalimbali za Elimu na Mafunzo katika ngazi zote. Sekta ya Elimu ina Sera nne ambazo ni Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 1995, Sera ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu ya Mwaka 1996, Sera ya Taifa ya Elimu ya Juu ya Mwaka 1999 na Sera ya Matumizi ya TEHAMA katika Elimu ya Msingi ya Mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2013/14 pamoja na mambo mengine Wizara yangu ilitekeleza mambo yafuatayo:-

- (a) Kukamilisha Rasimu ya Sera ya Elimu na Mafunzo ambayo itawasilishwa Baraza la Mawaziri kwa maamuzi.
- (b) Kukamilisha Rasimu ya Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Kitaalam ya Walimu Tanzania na kuiwasilisha katika Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri.
- (c) Kukamilisha Rasimu ya Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Ithibati na Uthibiti wa Ubora wa Elimu ya Msingi na Elimu ya Sekondari.
- (d) Kukamilisha na kuwasilisha katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Muundo wa Utumishi wa Walimu katika kada mbalimbali na pia Muundo wa Uongozi katika ngazi za Elimu ya Msingi, Sekondari na Ualimu ikiwemo Ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, lengo na madhumuni ya kuweka Sera mpya na mikakati itakayoandaliwa ya utekelezaji wa Sera ni pamoja na kuhakikisha kwamba, changamoto zinazohusu elimu na mafunzo ambazo ni za Kisera au ni za Kimkakati zinatatuliwa.

Mheshimiwa Spika, usajili wa shule ni muhimu kwa ajili ya kuipa shule ithibati na idhini ya kufundisha. Kwa Mwaka wa Fedha 2013/14 pamoja na mambo mengine, yafuatayo yalitekelezwa:-

- (a) Shule 106 zilisajiliwa hadi kufikia Machi, 2014, ambapo Shule za Awali pekee ni mbili, Shule za Awali na Msingi 53, Sekondari za Serikali 17, Sekondari zisizokuwa za Serikali 32 na Vyuo vya Ualimu visiviyokuwa vya Serikali viwili, hivyo kuongeza idadi ya Shule na Vyuo hadi kufikia jumla ya Shule za Msingi 16,609, Sekondari 4,573, Vyuo vya Ualimu 123.
- (b) Vibali vya Ujenzi wa shule 127 vilitolewa ikiwemo Shule za Awali vibali vitano, Shule za Msingi tatu, Awali na Msingi 74, Sekondari 40, Vyuo vya Ualimu vitano.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(c) Shule za Msingi tano, Sekondari tano, pamoja na Chuo Kimoja cha Ualimu zilifungiwa kwa sababu mbalimbali, ikiwemo ukiukwaji wa vigezo vya ubora wa shule.

Mheshimiwa Spika, katika Ukaguzi wa Shule na Vyuo vya Ualimu, Wizara yangu pamoja na mambo mengine ilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Asasi 8,483 zikiwemo Shule za Msingi 6091, Sekondari 2308 na Vyuo vya Ualimu 84 vilikaguliwa hadi kufikia mwezi Machi, 2014, sawa na asilimia 79.4 ya asasi 10,684 zilizolengwa kukaguliwa.

(b) Wakaguzi wa Shule 139 walioteuliwa kati ya mwaka 2010 na 2013 walipatiwa mafunzo kabilishi na Wakaguzi wa Shule 148 walipatiwa mafunzo ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu.

(c) Walimu 217 wenye vigezo vya kuwa Wakaguzi walibainishwa na kuombewa uhamisho kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI ili kuimarisha Ukaguzi katika Halmashauri mpya na zile zenye upungufu.

(d) Mfumo wa kieletroniki wa ukusanyaji na usimamizi wa taarifa za ukaguzi ulikamilika na kufanyiwa majoribio katika Shule za Msingi 139 katika Halmashauri saba ambazo ni Temeke, Makete, Siha, Magu, Hai, Mtwara Vijijini na Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, Mafunzo ya Ualimu; moja ya nguzo ya kuhakikisha Elimu bora inatolewa ni maandalizi ya Walimu kulingana na mitala inayotumika. Wizara imetekeleza jukumu hili katika Mwaka wa Fedha 2013/14 kama ifuatavyo:-

(a) Elimu ya Ualimu iliendelea kutolewa katika Vyuo vya Serikali na Vyuo vya Binafsi na kupata jumla ya Walimu 36,338 waliohitimu. Ngazi ya Cheti ni Walimu 17,928, ngazi ya Stashahada ni 5,416 na ngazi ya Shahada 12,994. Kati ya Walimu hao, Walimu wa masomo ya sayansi na hisabati ni 2364. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) imewaaajiri wahitimu hao katika Halmashauri mbalimbali na hivyo kubakiza mahitaji ya Walimu 30,949 wa Shule za Msingi na Walimu 24,596 wa Sekondari wa Sayansi na Hisabati.

(b) Kuweka utaratibu wa kuanza kutoa ruzuku na mikopo kwa Wanachuo wenye sifa watakaojiunga na mafunzo ya Stashahada ya Ualimu wa Sayansi na Hisabati.

(c) Kurejesha utaratibu wa kuijunga na mafunzo ya Ualimu kwa Walimu wa Sekondari wa Masomo ya Sayansi kwa miaka mitatu kwa wahitimu wa Kidato cha Nne ama *half combination*.

(d) Kukamilisha Mfumo wa Kielektroniki wa kudahili wanafunzi wa kujiunga na programu ya ualimu ngazi ya Stashahada na ambao utaanza kutumika kwa Programu ya Stashahada ya Ualimu wa Elimu ya Msingi katika Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ina Taasisi na Wakala zenyе majukumu mbalimbali katika kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo. Kati ya hizo, Taasisi tatu ni za Ithibati na Uthibiti wa Ubora wa Elimu ya Juu, Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi; mbili ni za mitaala na mitihani, mbili ni za mikopo na ruzuku mbalimbali, moja ni Bodi ya Huduma za Maktaba, moja ni Tume ya Taifa ya UNESCO na kituo kimoja cha Hazina Data Dakawa. Taasisi hizo pamoja na mambo mengine, zilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Sheria mbalimbali ikiwemo Sheria ya Mamlaka ya Elimu Tanzania (Sura Na. 412), zimerekebishwa kuitia Sheria ya *Written Laws Miscellaneous Amendments Act No. 3/2013* ili kuupatia Mfuko wa Elimu vyanzo vya mapato vya ziada na endelevu kwa kuweka asilimia isiyopungua mbili ya Bajeti ya Serikali ya mwaka ya matumizi ya kawaida ukitoa Deni la Taifa.

(b) Programu za Elimu mbalimbali zilianzishwa ikiwemo Programu ya Stashahada ya Ualimu wa Shule za Msingi ambayo itaanza kutolewa mwaka 2014/15 katika Chuo Kikuu cha Dodoma.

(c) Kuzinduliwa na kuanza rasmi kwa ujenzi wa Hospitali ya Kufundishia ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili Kampasi ya Mloganzila.

(d) Kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa Chuo Kikuu cha Kilimo na Sayansi Shirikishi cha Mwalimu Julius Nyerere Butiama. Wizara inaendelea kuwasiliana na Tume ya Mipango, Hazina pamoja na wadau mbalimbali ili ujenzi wa Chuo hiki uanze katika Mwaka wa Fedha 2014/15.

Mheshimiwa Spika, Taasisi zingine na Wakala zilizo chini ya Wizara katika mwaka 2013/14 zilitekeleza mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/14 Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima pamoja na majukumu mengine, ilitekeleza mambo haya yafuatayo:-

(a) Ilidahili Wanafunzi 881 kati ya ngazi ya Cheti, Stashahada na Shada katika Programu ya Elimu ya Watu Wazima na Mafunzo Endelevu.

(b) Ilitoa Elimu ya Sekondari kwa njia ya ujifunzaji huria na masafa kwa kuandika moduli za hatua ya tatu kwa masomo kumi na moja yakiwemo

Nakala ya Mtandao (Online Document)

English, French, Basic Applied Mathematics, Advanced Mathematics, History, Geography, Kiswahili, General Studies, Economics, Commerce na Accounting.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/14, Taasisi ya Elimu Tanzania pamoja na mambo mengine, imekusanya maoni ya wadau kuhusu maboresho ya mitaala pamoja na kuchambua mihtasari ya masomo ya elimu ya awali na elimu ya msingi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/14, Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilitoa mafunzo ngazi ya Cheti kwa wanachuo 457, Stashahada 339 pamoja na mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 98 katika Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka (SLADS).

(b) Imeendelea na ujenzi na ukarabati wa majengo kwenye Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka na kufanya ukarabati wa awamu ya kwanza wa majengo ya Maktaba ya Mkoa wa Mara na Mkoa wa Mtwara.

(c) Iliendelea na ujenzi wa Hosteli ya Wanafunzi wa Kike katika Chuo cha Ukutubi SLADS Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/14 Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilitoa mafunzo ya Stashahada ya Uongozi wa Elimu kwa wanafunzi 762 katika Vituo vya Bagamoyo na Mwanza, yenyе lengo la kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa shule.

(b) Ilitoa mafunzo kwa Wakuu wa Shule wa Serikali 2,982 na 2,287 wa Shule zisizo za Serikali ili kuimarisha Menejimenti ya Shule za Sekondari.

(c) Ilitoa mafunzo kwa Waratibu wa Elimu Kata 1,765 kutoka Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Kagera, Kilimanjaro, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Ruvuma, Singida na Tabora.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya UNESCO, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2013/2014, pamoja na mambo mengine, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilianda ripoti ya hali ya uhifadhi wa maeneo ya Tanzania yaliyoorodheshwa kwenye Orodha ya Urithi wa Dunia ili kutathmini utekelezaji wa Mkataba wa UNESCO wa mwaka 1972.

(b) Iliendelea kuelimisha jamii kuhusu shughuli za UNESCO hususan masuala ya mazingira, elimu, sayansi asilia, sayansi jamii, utamaduni,

Nakala ya Mtandao (Online Document)

mawasiliano na habari, kwa kuchapa na kusambaza nakala 742 za Tanzania and UNESCO Magazine na nakala 2,500 za vipeperushi.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Mitihani la Tanzania katika mwaka 2013/2014, pamoja na mambo mengine lilitekeleza yafuatayo:-

(a) Liliwatahini wanafunzi waliomaliza Elimu ya Msingi 868,083, Elimu ya Sekondari Kidato cha Nne 427,938 na Kidato cha Sita 46,378, Mtihani wa Ualimu watahiniwa 26,614 na kuendesha Mtihani wa Maarifa (*Qualifying Test*) kwa watahiniwa 18,214.

(b) Baraza lilianza ujenzi wa kituo cha data kwa ajili ya kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu na taarifa za mitihani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu lilitekeleza yafuatayo:-

(a) Lilikagua, kusajili na kutoa ithibati ambapo vyuo 45 vilikaguliwa na kusajiliwa na vyuo vinne vilipatiwa ithibati.

(b) Liliratibu udahili wa wanafunzi katika vyuo vya ufundu ambapo kwa ngazi ya cheti na stashahada wanafunzi 13,375 na shahada wanafunzi 5,081 walidahiliwa.

(c) liliidhinsha mitaala 39 na kuratibu mafunzo kwa walimu 132 kuhusu jinsi ya kutumia mitaala inayozingatia umahiri.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere katika mwaka 2013/2014 kilitekeleza yafuatayo:-

(a) Kilidahili jumla ya wanafunzi 745, katika yao wanafunzi 122 wa Programu za Cheti, 220 Programu za Stashahada na 403 wa Progamu za Shahada ya Kwanza.

(b) Kiligharamia mafunzo kwa wahadhiri 18 wa ngazi ya uzamili na uzamivu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 Chuo cha Ufundu Arusha kiliendelea kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kilidahili jumla ya wanafunzi 493 wa mwaka wa kwanza.

(b) Kilianzisha programu ya *Biomedical Engineering*.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(c) Kilihuisha mitaala sita ya programu zilizopo za ufundi sanifu.

(d) Kilitoa kozi za awali za kuijunga na chuo kwa kushirikiana na Mfuko wa Elimu Tanzania (*TEA*), ambapo jumla ya wanafunzi 126 wa kike walijiunga na Chuo kwa utaratibu huo.

(e) Kilishirikiana na Mradi wa *Technical Education and Labour Market Support Program (TELMS)*, ambao ulitoa msaada wa vifaa vya kufundishia kwa fani za uhandisi na mawasiliano ya anga, ujenzi, barabara, mitambo na magari. Pia wanafunzi bora sita wa kike walizawadiwa kompyuta pakato (*Laptops*) moja kila mmoja na wanafunzi 93 walipewa ufadhili wa ada ya shilingi 180,000 kila mmoja.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Elimu na Ufundi Stadi (*VETA*) katika mwaka 2013/2014 ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Kuanza maandalizi ya awali ya ujenzi wa vituo vitano vya Wilaya ya Kilindi, Namtumbo, Ludewa, Ukerewe na Chunya, ambapo zabuni zimetangazwa na ujenzi unatarajiwa kuanza mwanzoni mwa mwezi Juni, 2014.

(b) Ilitoa mafunzo ya umahiri ya ufundishaji mafunzo ya ufundi stadi kwa walimu 100 kutoka vyuo 25 vya maendeleo ya jamii vinavyotoa mafunzo ya ufundi stadi.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Elimu Tanzania (*TEA*) katika mwaka 2013/2014 ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Iligharamia mafunzo ya *Pre-entry* kwa wanafunzi wa kike 260 ili kuwawezesha kupata sifa stahiki za kuijunga na Vyuo vya Elimu ya Ufundi nchini.

(b) Iligharamia mafunzo ya *Post-primary* kwa wanafunzi wa kike 260 ili kuwawezesha kupata sifa stahiki za kuijunga na Vyuo vya Elimu ya Ufundi nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Iliratibu na kusimamia udahili wa wanafunzi 52,538 katika Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki nchini.

(b) Ilirkamilisha na kuzindua mwongozo wa gherama ya kumsomesha wanafunzi wa elimu ya juu ama *student unit cost framework* utakaoanza

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kutumika katika mwaka wa masomo 2014/2015 hivyo kuondoa utozaji wa ada kiholela katika elimu ya juu.

(c) Ilikagua na kufanya tathmini ya maendeleo ya vyuo vilivyopewa ithibati ili kuweza kujua kama vinatekeleza malengo yake ipasavyo na iliidhinisha programu 46 za masomo.

(d) Iliratibu upatikanaji wa wanataaluma 17 kutoka vyuo vikuu nchini waliojiunga na masomo ya uzamivu chini ya makubaliano ya Serikali ya Tanzania na Ujerumanu kupitia Shirika la DAAD.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilitoa mikopo kwa wanafunzi 95,589 na hivyo kuongeza fursa ya upatikanaji wa elimu ya juu.

(b) Ilikusanya marejesho ya mikopo kiasi cha shilingi 12,345,412,587.66 hadi Machi, 2014, sawa na asilimia 43 ya lengo kwa mwaka 2013/2014 na hivyo kufikia jumla ya shilingi 47,349,582,373.11, sawa na asilimia 55 ya madeni yaliyoiva.

(c) Ilifungua Ofisi ya Kanda ya Ziwa na kuimarisha Ofisi za Kanda ya Zanzibar na ya Dodoma kwa kuzunganisha na Mfumo wa Utoaji Mikopo wa Makao Makuu ya Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika mwaka 2013/2014 kilitekeleza yafuatayo:-

(a) Kilidahili wanafunzi 1,350 katika fani za sayansi na uhandisi, 2,435 wa uzamili na uzamivu.

(b) Kiliendelea kufanya utafiti kuhusu mabadiliko ya tabianchi.

(c) Kiliendelea na utafiti kupitia miradi mbalimbali ikiwemo Mradi wa Integrated Water Resources Management wa kutoa mafunzo na kufanya utafiti kwa wanafunzi wa hapa nchini na nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam katika mwaka 2013/2014 kilitekeleza yafuatayo:-

(a) Kilidahili wanafunzi 1,247; 220 wa fani ya sayansi; na 42 wa cheti katika fani mbalimbali za elimu.

(b) Kiliongeza vifaa vya kufundishia na kujifunzia vikiwemo madawa kwa ajili ya matumizi ya maabara za kufundishia na vifaa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum pamoja na kununua samani na vitabu kwa ajili ya maktaba.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Mkwawa katika mwaka 2013/2014 kilidahili wanafunzi wanawake 255 na wanaume 723.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine katika mwaka 2013/2014 kilitekeleza yafuatayo:-

(a) Kilianzisha programu ya mafunzo ya Post Harvest Engineering Systems ngazi ya shahada ya uzamivu.

(b) Kilifanya utafiti msingi na tumizi (Basic and Applied Research) katika Miradi 135.

(c) Kilikamilisha ujenzi wa majengo manne yenye kumbi za mihadhara tisa, Ofisi arobaini na mabaara nne yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 10,565 na wahadhiri 881 na kukarabati bweni la Kampasi ya Solomon Mahlangu na Karakana ya Idara ya Uhandisi Kilimo kupitia Mradi wa STHEP.

(d) Kilifanya utafiti wa athari za mabadilko ya tabianchi na tahafifu katika Kanda za Nyanda ya Juu Kusini, Kaskazini na Kati.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Biashara Moshi, kilitekeleza yafuatayo:-

(a) Kilidahili wanafunzi 4,463.

(b) Kiligharamia mafunzo kwa wanataaluma 53 katika shahada za uzamili na uzamivu ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa elimu.

(c) Kilifanya tafiti 20 kwa kushirikiana na wadau nje na ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa mwaka 2013/2014 kilitekeleza yafuatayo:-

(a) Kilidahili wanafunzi 8,935 katika ngazi ya shahada na cheti, sawa na asilimia 99 ya lengo la kudahili wanafunzi 9,000. Aidha wanafunzi 2,943, sawa na asilimia 105.9 ya lengo walidahiliwa katika shahada ya uzamili na uzamivu.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(b) Kilijenga maabara ya kompyuta katika Vituo vya Zanzibar, Mtwara, Dodoma, Shinyanga na Kinondoni pamoja na kukamilisha ukarabati wa Ofisi na Ukumbi wa Mitihani katika Kituo cha Shinyanga.

(c) Kilifanya ukarabati wa awamu ya pili katika Kituo cha Zanzibar.

(d) Kilikamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa 10 kuitia Miradi wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.

(e) Kilifanya utafiti katika maeneo mbalimbali yakiwemo usalama wa matumizi ya TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 Chuo Kikuu Ardhi kilitekeleza yafuatayo:-

(a) Kilikamilisha ujenzi wa ofisi sita za walimu katika Jengo *Lands Building*.

(b) Kiliunganisha Mtandao wa TEHAMA wa Chuo kwenye Mkongo wa Taifa.

(c) Kilifanya utafiti na kutoa ushauri katika masuala ya ardhi na maendeleo ya makazi.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kwa mwaka 2013/2014 kilitekeleza yafuatayo:-

(a) Kilidahili wanafunzi 448 wa Shahada ya Kwanza, Uduktari wa Binadamu 256, Madawa 66, Uuguzi wanafunzi 63, Uduktari wa Meno na Kinywa wanafunzi 43, Afya, Sayansi na Mazingira wanafunzi 20 na wanafunzi 220 wa Shahada za Uzamili.

(b) Kiliendelea na ujenzi wa hospitali na miundombinu ya barabara, maji na umeme katika Kampasi ya Mloganzila.

(c) Kilichambua takwimu za utafiti wa *TaMoVac - I* na kuwasilisha chapisho kwenye jarida la kimataifa mwezi Machi, 2014 na kuendeleza utafiti wa *TaMoVac - II*.

(d) Kiligharamia mafunzo kwa wanataluma 48 kuitia Miradi mbalimbali na wafadhili ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa elimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 Chuo Kikuu Mzumbe kilitekeleza yafuatayo:-

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(a) Kilidahili wanafunzi 4,488 katika Programu za Cheti 297, Stashahada 383, Shahada ya Kwanza 2,087, Shahada ya Uzamili 1,692 na Shahada ya Uzamivu Programu 29.

(b) Kilikamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa tano kwa ajili ya vyumba vya ofisi, madarasa na kumbi za mihadhara, kiligharamia watumishi 21 katika mafunzo ya shahada ya uzamili na saba shahada ya uzamivu.

(c) Kiliimarisha masuala ya menejimenti, uongozi na sayansi ya jamii, kwa kukamilisha utafiti katika maeneo tisa ya kutoa ushauri wa kitaalam katika maeneo 25.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 Chuo Kikuu cha Dodoma ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Kilidahili wanafunzi 6,101.

(b) Kilikamilisha ujenzi wa maabara na madarasa kwa asilimia 80. Aidha, kilikamilisha ujenzi wa matanki mawili yenyewe uwezo wa kuhifadhi lita milioni saba na nusu za maji kwa ufadhili wa Benki Dunia.

(c) Kiliimarisha mazingira ya kutolea mafunzo kwa kuweka miundombinu ya umeme na TEHAMA katika vyuo vya sayansi za asili, hisabati na sayansi za ardhi.

Mheshimiwa Spika, usimamizi na utekelezaji wa Programu na Miradi. Wizara yangu pia ina Programu na Miradi mbalimbali ambayo iko chini ya Wizara. Katika mwaka 2013/2014, Wizara pamoja na mambo mengine ilitekeleza yafuatayo katika eneo hili:-

(a) Ilitekeleza mikakati ya Mpango wa Matokeo Makubwa ya Sasa katika elimu msingi, pamoja na mambo mengine kwa kutoa mafunzo kazini kwa walimu 12,476. Kati ya hao, walimu 8,400 wa masomo ya sayansi na hisabati, 4,076 masomo yanayosomwa na wanafunzi wote, yaani Mathematics, Biology, English na Kiswahili. Pia wakuu wa shule 3,152 walipatiwa mafunzo katika mwongozo wa usimamizi na uendeshaji wa shule.

(b) Ililikamilisha tathmini ya stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu pamoja na umakini katika uongozi wa shule kwa kutumia EGRA na EGMA.

(c) Ililikamilisha awamu kwanza ya Mradi wa Sayansi, Teknolojia na elimu ya Juu (STHEP) kwa ufanisi, majengo mapya 17 yenyewe vyumba vya mihadhara 48, maabara za sayansi 93 na Ofisi 302 za wafanyakazi zilijengwa.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Majengo hayo yataongeza nafasi za kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi 47,622. Vyo viliyonufaika na Mradi huu ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu Ardhi, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Chuo Kikuu Huria Tanzania, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (*DIT*), Taasisi ya Afrika ya Nelson Mandela ya Sayansi na Teknolojia ya Chuo Kikuu na Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar.

(d) Ilikamilisha na kuzindua Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Ufundis na Mafunzo ya Ufundis Stadi (*Technical and Vocational Education and Training Development Programme - TVETDP*), mwaka 2013/2014 hadi mwaka 2017/2018 uliozinduliwa tarehe 13 Desemba, 2013.

(e) Ilikamilisha majadiliano ya Mradi wa *Literacy and Numeracy Education Support (LANES)*, wenyewe thamani ya Dola za Kimarekani milioni 94.8 katika kuinua kiwango cha kumudu kusoma, kuandika na kuhesabu kwa wanafunzi wa darasa la kwanza na darasa la pili.

(f) Ilizinduliwa kutekeleza mradi wa kupata takribani vitabu milioni sita vya sayansi na hisabati kwa elimu ya sekondari ili kupata uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi katika masomo hayo. Mkataba wenyewe thamani ya Dola za Kimarekani milioni tisa tayari umesainiwa kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Shirika la Maendeleo la Marekani (*USAID*).

(g) Ilizinduliwa Wiki ya Elimu ya Taifa ambayo itakuwa inafanyika kuanzia ngazi ya Halmashauri, Mkoa hadi Taifa kila mwaka, ili kutoa fursa kwa Wananchi na Wadau wa Elimu kujadili masuala na maendeleo katika maeneo yao na kubaini changamoto na mbinu za kuendeleza na kuimarisha ubora wa elimu. Kwa mwaka 2013/2014 wiki ya elimu ifanyika tarehe 3 hadi 10 mwezi Mei na kauli mbiu ilikuwa Elimu Bora Inawezekana, Timiza Wajibu Wako.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu na bajeti ya mwaka 2013/2014, Wizara ilikabiliana na baadhi ya changamoto katika maeneo mbalimbali inayoyasimamia ikiwemo hizi zifuatazo:-

(a) Upatikanaji wa walimu mahiri wa kufundisha stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu kwa kiwango cha kutosha kwa wanafunzi wa madaraa ya chini (Darasa la I na la II).

(b) Upatikanaji wa Wataalam wa Kitanzania katika fani za gesi, mafuta, chuma, urani, makaa ya mawe na madini mengine.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(c) Upatikanaji wa rasilimali ili kuwezesha ukaguzi wa shule kufanyika kwa ufanisi kulingana na miongozo ya ukaguzi kutokana na ongezeko la Mikoa na Halmashauri mpya.

(d) Kuimarisha mfumo wa ukaguzi wa shule ili kuendana na mabadiliko ya kisayansi na kiteknolojia.

(e) Ongezeko la mahitaji ya walimu wa masomo ya sayansi na hisabati katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

(f) Upatikanaji wa fedha za kutosha kutoa mikopo ili kugharamia elimu ya juu na elimu ya ufundi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2013/2014, naomba sasa niwasilishe vipaumbele vya Wizara na kisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele vya Sekta ya Elimu ambavyo Wizara yangu itavitekeleza vimeainishwa katika Mwongozo wa Maandalizi ya Bajeti kwa Mwaka 2014/2015 kama ifuatavyo:-

(a) Kuinua ubora wa elimu na kujenga stadi stahiki katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

(b) Kuongeza upatikanaji wa fursa ya elimu kwa usawa katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

Mheshimiwa Spika, katika utungaji na utekelezaji wa Sera za Elimu, Wizara yangu itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kukamilisha Sera ya Elimu na Mafunzo na kuandaa mpango mkakati wa utekelezaji wake.

(b) Kuimarisha mfumo wa kitaasisi wa kusimamia ubora wa elimu msingi kwa kuanzisha mamlaka ya ithibati na uthibiti wa elimu ya msingi na sekondari ili kuhakikisha kuwa utoaji wa elimu unazingatia sera, miongozo na mitaala ya elimu yenye kukidhi mahitaji ya soko na jamii.

(c) Kukamilisha taratibu za uanzishwaji wa Bodi ya Kitaalamu ya Walimu Tanzania itakayosimamia masuala ya Walimu ikiwemo usajili, uendelezaji wa Walimu na Maadili ya kazi ya Ualimu.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(d) Kuimarisha ha Taasisi ya Elimu Tanzania katika kushughulikia Ithibati na Uthibiti wa vitabu, zana na vifaa mbalimbali vyta elimu ya msingi na sekondari.

(e) Kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na wadau wengine, kuweka mfumo na muundo utakaosaidia wanafunzi wengi kuendelea na masomo ya Elimu ya Sekondari ya Juu, ili kufikia lengo la wanafunzi 250,000 ifikapo mwaka 2016.

(f) Kuhuisha Mitaala na kuimarisha mfumo wa utoaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

(g) Kuimarisha ufuutiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo katika ngazi zote kwa kuandaa na kutoa Miongozo.

(h) Kuhuisha na kuoanisha Programu za Elimu ya Juu pamoja na Ufundi, ili utoaji wa elimu hizo uzingatia mahitaji ya soko la ajira kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, katika usajili wa shule, Wizara yangu itaendelea kusajili shule za msingi na sekondari kwa kutilia mkazo zaidi shule za ufundi na sayansi, kuimarisha mfumo wa usajili wa shule na kuhuisha Mwongozo wa Usajili, ili uendane na wakati.

Mheshimiwa Spika, katika ukaguzi wa shule na vymo, Wizara yangu itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuimarsisha taratibu za ukaguzi na kuendelea kukagua shule na vymo vya ualimu kwa ufanisi zaidi.

(b) Kufungua Ofisi za Ukaguzi katika Wilaya Mpya na Wilaya ambazo hazina Ofisi hizo.

Mheshimiwa Spika, katika kusimamia utoaji wa mafunzo ya ualimu, Wizara yangu itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuimarisha ufundishaji wa Walimu katika Stadi za KKK.

(b) Kuanza kuratibu utoaji wa ruzuku na mikopo kwa wanafunzi wanaosomea Stashahada ya Ualimu wa Sayansi na Hisabati, kulingana na vigezo vitakavyowekwa katika vymo vilivyoteuliwa.

(c) Kuimarisha mafunzo ya ualimu na kuweka muundo endelevu wa weledi na maendeleo ya Mwalimu.

(d) Kuvipatia vuo vya ualimu 34 ithibati ya NACTE, ili viweze kuingia rasmi katika mfumo wa ithibati na uthibiti wa ubora unaotambulika Kitaifa katika Sekta ya Elimu ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, katika kusimamia Taasisi na Wakala zilizo chini ya Wizara, zimelenga kutekeleza majukumu yake ya kawaida ikiwa ni pamoja na haya yafuatayo:-

(a) Kuendelea kuinua ubora na kuimarisha vuo vya elimu ya juu pamoja na ufundi, ili viwe Vuo vya Maendeleo Kizazi cha Tatu (*Third Generation Development Institutions*), kulingana na kasi ya maendeleo iliyopo Duniani na kuweza kufikia Malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025 kwa haraka.

(b) Kuendelea kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa kuweka mifumo ya kidijiti ili kuwezesha Walimu na Wanafunzi kupata maandiko mbalimbali muhimu kwa maendeleo ya Elimu na Taifa kupitia TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Taasisi na Wakala katika mwaka 2014/2015, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima imelenga kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuandika Mihitasari na Moduli za Masomo ya Biashara na Sayansi Hatua ya Pili, sawa na Kidato cha I na cha II, ili kuongeza fursa ya utoaji wa Elimu ya Sekondari kwa njia ya ujifunzaji huria na masafa.

(b) Kusimamia Mpango Tarajali wa Elimu Changamani badala ya msingi katika Wilaya 13 kwa kushirikiana na UNICEF.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015 Taasisi ya Elimu Tanzania imelenga kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kufanya tathmini ya utekelezaji, kupitia na kuboresha Mtaala wa Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu.

(b) Kutoa mafunzo kuhusu utekelezaji wa Mtaala kwa Walimu, Wakaguzi wa Shule, Maafisa Elimu na Waratibu wa Elimu Kata.

(c) Kufanya utafiti kuhusu ufundishaji na ujifunzaji kwa masomo ya sayansi na hisabati.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015 Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania imelenga kutekeleza yafuatayo:-

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(a) Kutoa machapisho 50,000 ili kuinua ubora wa huduma za Maktaba katika Mikoa 21 Tanzania Bara.

(b) Kutoa mafunzo ya ukutubi na uhifadhi nyaraka kwa walengwa 700 wa Cheti, 500 wa Stashahada na 500 wa Mafunzo ya Awali kwa ajili ya Wafanyakazi wa Maktaba.

(c) Kuendeleza ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka (SLADS) Bagamoyo, ikiwemo maabara ya computer na nyumba za wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2014/2015 Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu imelenga kutekeleza majukumu yake ya kawaida ikiwa ni pamoja na yafuatayo:-

(a) Kutoa Mafunzo ya Stashahada ya Ugaguzi wa Shule kwa Wakaguzi 240 wa Halmashauri za Tanzania Bara na Mafunzo ya Cheti cha Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Walimu Wakuu 720 katika Wilaya 12 za majoribio ya UNICEF.

(b) Kutoa mafunzo ya muda mfupi ya uongozi, uendeshaji na usimamizi wa elimu kwa Wajumbe 9,000 wa Kamati na Bodi za Shule, Wakuu wa Shule 4,300, Wakaguzi wa Shule 240, Maafisa Elimu 884 wa Mikoa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 Tume ya Taifa ya UNESCO imelenga kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kushirikisha na kuhakikisha wadau wanashiriki katika kupanga na kutekeleza Programu za UNESCO katika nyanja za Elimu, Sayansi Asilia, Sayansi ya Jamii, Utamaduni, Habari na Mawasiliano.

(b) Kushirikiana na wadau katika kutafuta fedha za kutekeleza miradi saba ya ushirikishaji (*Participation Projects*).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015 Baraza la Mitihani la Tanzania limelenga kutekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kuendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa Watahiniwa 998,295 mwaka 2014.

(b) Kuendesha Mitihani ya Sekondari Kidato cha IV kwa Watahiniwa 492,129, Maarifa Watahiniwa 20,946 kwa mwaka 2014 na Kidato cha VI Watahiniwa 61,335 kwa mwaka 2015.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(c) Kuendesha Mitihani ya Ualimu kwa Watahiniwa 35,297 kwa mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2014/2015 Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu limelenga kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kukagua, Kusajili na Kutoa Ithibati kwa Vyuo vya Ufundu 50, ili kukidhi ubora wa elimu.

(b) Kutengeneza Mitaala ya Kitaifa 10 na kuidhinisha Mitaala 40 ya ngazi ya Cheti, Stashahada na Shahada pamoja na kuratibu mafunzo ya Walimu 150 kuhusu kufundisha kwa kutumia Mitaala inayozingatia umahiri kwa Vyuo vya Ufundu.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2014/2015, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kimelenga kuanzisha Mafunzo ya Cheti na Stashahada katika Rasilimali Watu na Cheti katika Maendeleo ya Uchumi (*Certificate in Economic Development*).

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2014/2015 Chuo cha Ufundu Arusha, kimelenga kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuanzisha Programu ya Stashahada ya Ualimu wa Masomo ya Sayansi na Ufundu Sanifu katika Fani ya Magari na Mitambo Mikubwa.

(b) Kuandaa Mpango Mkakati wa kuanzisha Kituo cha Mafunzo ya Kutengeneza Mashine Ndogondogo za kuzalisha umeme na wa kukarabati Kituo cha Kuzalisha Umeme Kikuletwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015 Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu Stadi (VETA) imelenga kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuanza ujenzi wa vyuo vinne vya VETA vya Mikoa ya Geita, Simiyu, Njombe na Rukwa na vya Wilaya za Kilindi, Chunyu, Ukerewe, Ludewa na Namtumbo, pamoja na kukarabati Vyuo vya Wilaya za Korogwe na Karagwe.

(b) Kufanya utafiti wa soko la ajira katika maeneo ya machimbo ya gesi, madini ya chuma na makaa ya mawe katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Iringa, Njombe na Ruvuma, pamoja na kufanya mapitio na kuandaa Mitaala kwa ajili ya mafunzo katika Sekta ya Gesi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015 Mamlaka ya Elimu Tanzania imelenga kutekeleza yafuatayo:-

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(a) Kuimarisha uwezo wa ugharamiaji elimu kwa kuendelea na uchangishaji wa fedha ili kupata bilioni 2.3 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni 30 ya wasichana kwenye Halmashauri saba za Wilaya za Geita, Lushoto, Kasulu, Lindi, Musoma, Songea na Manyara.

(b) Kuongeza fursa kwa wasichana kuijunga na elimu ya ufundi kwa kuendelea kufadhili Mpango wa Pre-entry kwa wanafunzi wa kike.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2014/2015 Tume ya Vyuo Vikuu (*TCU*) imelenga kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kukagua na kutathmini mipango ya kuanzisha Vyuo Vikuu 20, ili kusimamia ubora wa elimu itolewayo na Vyuo Vikuu Nchini.

(b) Kuvijengea uwezo Vyuo Vikuu katika kuandaa na kuhuisha Programu za Masomo kwa kuzingatia Mfumo wa Tuzo unaotumika (*University Qualifications Framework*).

(c) Kuratibu upatikanaji wa Wanataluma 30 kutoka Vyuo Vikuu nchini watakaojunga na Masomo ya Uzamili na Uzamivu chini ya makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na Ujerumani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015 Bodii ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu imepanga kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kutoa mikopo ya wanafunzi 95,881 wakiwemo waombaji wa mara ya kwanza 27,878 na wanafunzi wanaoendelea 67,953 wa Vyuo vya Elimu ya Juu, 3,000 wa Stashahada ya Elimu ya Ualimu wa Masomo ya Sayansi na Hisabati.

(b) Kukusanya marejesho ya mikopo yanayofikia jumla ya shilingi 36,610,694,661.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2014/2015 Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam kimepanga kukarabati miundombinu ya majitaka pamoja na maeneo ya makazi ya wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2014/2015 Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar-es-Salaam kimelenga kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuongeza fursa za kuijunga na Elimu ya Juu kwa kudahili wanafunzi 1,800.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(b) Kukarabati Jengo la Kitivo cha Sayansi za Jamii na Hyumanitia (*Humanities*), Jengo la Utawala kwa ajili ya Ofisi za Wafanyakazi waendeshaji, Jengo la Maabara na Madarasa katika Shule ya Sekondari ya Mazoezi na uzio kuzunguka Chuo.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2014/2015 Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa kimelenga kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kukamilisha ujenzi wa Ukumbi wa Mihadhara wenyewe uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 na kukarabati miundombinu ya chuo.

(b) Kuendelea kugharamia masomo ya Wahadhiri 16 walioko masomoni katika viwango vya Shahada za Uzamili na Uzamivu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015 Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimelenga kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuanzisha Shahada mpya za kwanza tatu na tatu za Uzamili na masomo yasiyo ya Shahada matano, ili kuelekea katika kufikia lengo la kuongeza idadi ya wanafunzi kutoka waliopo 8,261 hadi 11,000 mwaka 2017.

(b) Kukamilisha miundombinu na majengo mapya yanayogharamiwa na Mradi wa *STHEP* na kuanza maandalizi ya ujenzi wa maabara kubwa moja kwa ajili ya Kitivo cha Sayansi inayogharimiwa na Mradi wa *EPNAV*. Aidha, kuendeleza ujenzi wa jengo moja la ghorofa moja linalogharamiwa na Mradi wa *Climate Change, Impact, Adaptation and Mitigation in Tanzania* ambalo litakuwa na vyumba vya semina, ofisi, maabara za computer pamoja na vyumba vya mihadhara, kukarabati kumbi 10 za mihadhara na nyumba za wafanyakazi zilizopo Kampasi ya Solomoni Mahlangu na Kampasi Kuu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015 Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Biashara Moshi kimelenga kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kukamilisha taratibu za kukiwezesha kuwa Chuo Kikuu kamili.

(b) Kuimarishe Vituo vinne vya Mikoani Mtwara, Iringa, Mwanza na Singida, ili kuielimisha jamii katika masuala ya Vyama vya Ushirika, Maendeleo ya Ushirika, utunzaji mazingira na mikakati ya upunguzaji wa umaskini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015 Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kimelenga kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kukamilisha ujenzi wa Maabara za Computer katika Mikoa ya Dodoma, Lindi, Mtwara, Mara, Njombe na Tabora.

(b) Kukarabati majengo ya chuo awamu ya pili katika Mikoa ya Kagera, Mtwara, Lindi, Kilimanjaro, Ruvuma, Kinondoni na Rukwa.

(c) Kujenga Maabara ya Sayansi na Jengo la Madarasa Makao Makuu ya Chuo, Bungo Kibaha.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2014/2015, Chuo Kikuu Ardhi kimelenga kuendelea na ujenzi wa *Lands Building*, ukarabati wa karakana za mafunzo na mabweni ya wanafunzi na kutayarisha michoro kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Wanafunzi na kutoa huduma za ushauri nasaha kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kimelenga kuendeleza ujenzi wa Hospitali ya Kufundishia ya Kampasi ya Mloganzila na kukarabati hosteli za wanafunzi katika eneo la Chole.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2014/2015, Chuo Kikuu cha Mzumbe kimelenga kutekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kuendeleza ujenzi wa madarasa na Kumbi mbili za Mihadhara pamoja na kukarabati mabweni manne ya wanafunzi, mfumo wa maji na majengo ya kilichokuwa Kitengo cha Uchapaji ili kuyabadili kuwa kituo cha wanafunzi.

(b) Kukamilisha utafiti katika maeneo 16 ya kutoa ushauri wa kitaalamu katika maeneo 37 ya Menejimenti ya Uongozi na Sayansi za Jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, napenda tena kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge; samahani, nimeruka sehemu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa kunisikiliza. Kwa niaba ya Wizara yangu, napenda pia kuwashukuru kwa dhati wadau wote wa Sekta ya Elimu, ikiwa ni pamoja na Washirika wetu wa Maendeleo, Viongozi wa ngazi mbalimbali, Wananchi wa Tanzania kwa ujumla, ambao wamechangia katika kufanikisha utekelezaji wa mipango ya elimu na mafunzo. Baadhi ya Washirika wetu wa maendeleo ni kama ambavyo wameorodheshwa katika Hotuba yangu, naomba nisiaisome kwa sababu muda haupo.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa mwaka 2014/2015. Baada ya Taarifa hii, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı ya jumla ya Shilingi 799,020,389,000 kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, ili kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, katika maombi haya:-

(a) Shilingi 93,247,873,000 zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Idara, ambapo Shilingi 52,976,832,000 ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi 40,271,041,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

(b) Shilingi 250,959,183,000 zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Taasisi. Kati ya hizo, Shilingi 215,779,416,000 ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi 35,179,767,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

(c) Shilingi 454,813,333,000 zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Fedha za ndani ni Shilingi 383,734,000,000; kati ya hizo Shilingi 306,000,000,000 ni kwa ajili ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Shilingi 71,079,333,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Hotuba hii inapatikana pia katika Tovuti ya Wizara kwa Anuani ya www.moe.go.tz.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Hoja hiyo imeungwa mkono. Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia Hoja hiyo.

Najua mmechoka. Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia Hoja hiyo, hayupo?

Aah, Mheshimiwa Ngonyani, nilikuwa naangalia kwingine kabisa. (Makofii)

Kwa niaba yake Mheshimiwa Ngonyani, Makamu Mwenyekiti au? Eeh, Makamu Mwenyekiti.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA ZA JAMII): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti makini wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mama Magreth Sitta, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha

Nakala ya Mtandao (Online Document)

2014/2015, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) na Kanuni ya 117 (11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na afya njema kuweza kutumikia Wananchi wangu wa Jimbo la Korogwe Vijijini. Naahidi kufanya kazi nao bila kujali na uwezo wangu wote nitashirikiana nao. Aidha, nakushukuru sana Mheshimiwa Spika na Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii pamoja na Wabunge wote, kwa kunifariji wakati nilipopata msiba wa marehemu baba yangu.

Mheshimiwa Spika, naomba Taarifa yote ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii inakiliwe kwenye Hansard kama ilivyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Spika, katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu na kujiridhisha na utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, Kamati ilifanya vikao na ziara katika taasisi mbalimbali za Wizara ikiwemo Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu (*National Council of Technical Education – NACTE*), Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, Chuo cha Mafunzo ya Elimu ya Ufundu Stadi Dar es Salaam, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na Baraza la Mitihani la Taifa.

Kamati pia ilifanya ziara Mkoani Mtwara kukagua utekelezaji wa shughuli za Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2013/2014, tarehe 3 - 7 Februari 2014. Kamati ilikagua Mradi wa Uimarishaji Elimu ya Msingi (MMEM) School Wash Programme katika Shule ya Msingi Chikwaya, Mradi wa Uimarishaji Elimu ya Sekondari (MMES) katika Shule za Sekondari za Naliendele na Mikindani, Mradi wa Ukarabati wa Chuo cha Ualimu Kitangali na Mradi wa Ukuzaji Ajira kupitia Elimu ya Mafunzo ya Ufundu Stadi Mkoani Mtwara.

Mheshimiwa Spika, maoni yanayolenga kuboresha utekelezaji wa shughuli za Wizara ikiwemo Miradi ya Maendeleo iliyotekelizwa ni sehemu ya Taarifa hii ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, tarehe 3 Mei, 2014, Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii ilikutana Dodoma kujadili Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 iliyowasilishwa na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu, Mheshimiwa Shukuru Kawambwa.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Waziri ilikuwa na maeneo mahususi yafuatayo:-

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(i) Utekelezaji wa maoni ya Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii katika bajeti ya Wizara ya Mwaka 2013/2014.

(ii) Utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

(iii) Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, katika rejea ya maoni na mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, napenda kulitaarifu Bunge hili kwamba, Serikali imezingatia na kufanya kazi baadhi ya ushauri wa Kamati ikiwemo kutenganisha fedha za mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kutoka katika fedha za Matumizi ya Kawaida ya Wizara, ambapo fedha hizo zimehamishiwa katika fedha za Miradi ya Maendeleo ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inaona bado kuna umuhimu wa kufanya kazi zaidi maeneo muhimu yafuatayo:-

(i) Mfumo unaotumika kuhudumia walimu nchini (*Teachers Service Delivery System*) unaohusisha vyombo zaidi ya kimoja kuhudumia walimu na kusababisha urasimu katika kupata stahiki za walimu.

(ii) Kuwezesha Idara ya Ukaguzi wa Elimu kuwa wakala ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

(iii) Utoaji posho maalumu kwa walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu (*Retention Scheme*).

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2013/2014 Wizara ilikadiria kukusanya shilingi bilioni 171,518,704,600. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2014 Wizara ilikusanya maduhuli ya shilingi bilioni 129,122,797,360, sawa na asilimia 75. Matumaini ya Kamati ni kwamba. Wizara itakamilisha makusanyo ya maduhuli yaliyobaki katika Robo ya Nne ya Mwaka wa Fedha husika.

Mheshimiwa Spika, Bunge liliidhinisha jumla ya shilingi bilioni 689,681,055,000 kwa Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, ambapo shilingi bilioni 617,083,004,000 zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 72,598,051,000 zilitengwa kwa ajili ya kutekeleza wa Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2014, Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 486,573,220,250.94, sawa na asilimia 79 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 14,921,545,855.46 sawa na asilimia 21 kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa fedha kwa ajili ya bajeti ya Miradi ya Maendeleo hauridhishi kwani hadi kufikia Robo ya Tatu ya kipindi cha bajeti, asilimia 21 tu ya bajeti ya Miradi ya Maendeleo ilikuwa imepokelewa na imetumika. Hali hii imeathiri utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya Wizara. Ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali izingatie kutekelezwa kwa malengo ya bajeti ya Wizara yaliyowasilishwa na kuidhinishwa na Bunge hili kwa kutoa fedha kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, changamoto mbalimbali zinazoikabili Sekta ya Elimu nchini zilibainika kama ifuatavyo:-

- (i) Ukosefu wa mpango ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu unaolenga kutekeleza vipaumbele walivyojiwekea;
- (ii) Fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge kutotolewa kwa wakati;
- (iii) Kuongeza makusanyo ya ndani ya Wizara kwa kubuni vyanzo vypya vyaa makusanyo;
- (iv) Mfumo dhaifu wa kuhudumia walimu unaohusisha vyombo zaidi ya kimoja na hivyo kusababisha urasimu katika upatikanaji wa haki za walimu nchini;
- (v) Ukosefu wa posho ya mazingira magumu kwa walimu;
- (vi) Utendaji kazi usioridhisha wa Idara ya Ukaguzi wa Elimu nchini kutokana na ufinyu wa Bajeti;
- (vii) Upungufu katika Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu (NACTE) inayolenga kudhibiti utoaji holela wa mafunzo ya elimu ya ufundu stadi nchini;
- (viii) Mchango wa Skill Development Levy katika utekelezaji wa majukumu ya VETA kutotosha;
- (ix) Uhitaji wa programu maalumu ya mafunzo ya walimu katika kuweka Mafunzo ya KKK (Kusoma, Kuandika na Kuhesabu);
- (x) Kukosekana kwa utaratibu maalumu wa kuwatumia wahitimu wa mafunzo ya elimu ya juu wanapopata ufadhili wa Serikali kuitopia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kuitumikia Serikali;

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(xi) Utoaji huduma kwa wanafunzi wenyе mahitaji maalumu kutengewa fedha za kutosha katika jukumu hilo kwa ufanisi; na

(xii) Ongezeko la wanafunzi wa elimu ya juu wanaohitaji mikopo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 imekusudia kukusanya mapato yenyе jumla ya shilingi 239,366,784,212. Aidha, Wizara imeomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 799,020,389,000 ambapo shilingi 344,207,056,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (*Recurrent Expenditure*) na shilingi 454,813,333,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo (*Development Expenditure*) kwa Mwaka 2014/2015. Aidha, shilingi 73,525,913,460 zimetengwa kutekeleza Miradi ya Wizara iliyopo katika Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa taarifa ya mgawanyo wa fedha katika Bajeti ya Wizara hii na kubaini uhitaji wa fedha kwa baadhi ya vifungu vyenyе mahitaji ya lazima, ikiwemo kifungu cha Ukaguzi wa Elimu nchini, Mafunzo ya Ualimu na Mamlaka ya Elimu Tanzania. Kamati ilishauri kuhamisha fedha katika baadhi ya vifungu vya Wizara ili kuiwezesha kuitendaji vifungu husika vyenyе uhitaji.

Mheshimiwa Spika, tarehe 3 Mei, 2014 Kamati ilikutana Dodoma na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundı na kupewa mrejesho kuzingatia ushauri wa Kamati na kufanya marekebisho kibajeti katika vifungu vya Wizara. Jumla ya fedha zilizoongezwa katika vifungu hivyo ni shilingi 1,977,234,248 kama zilivyofafanuliwa hapa chini.

Kifungu 5001 – Kasma 221700, tengeo la awali Sh. 7,969,500,000, fedha iliyooongezwa Sh. 1,005,009,324, tengeo jipya Sh. 8,974,509,324; Kifungu 2002 – Kasma 230400, tengeo la awali Sh. 53,601,360, fedha iliyooongezwa Sh. 16,398,640, tengeo jipya Sh. 70,000,000; Kifungu 2002 – Kasma 230300, tengeo la awali Sh. 430,731,000, fedha iliyooongezwa Sh. 269,269,000, tengeo jipya Sh. 700,000,000; Kifungu 2002 – Kasma 221000, tengeo la awali Sh. 754,564,000, fedha iliyooongezwa Sh. 286,557,248, tengeo jipya Sh. 1,041,121,284; Kifungu 7001 – Kasma 270400, tengeo la awali Sh. 2,044,357,000, fedha iliyooongezwa Sh. 400,000,000, tengeo jipya Sh. 2,444,357,000; Jumla Sh. 1,977,234,248.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı kwa kuzingatia ushauri wa Kamati na kufanya mabadiliko ya ndani ya vifungu vya Wizara ili kuwezesha Idara ya Ukaguzi wa Elimu, Mamlaka ya Elimu Tanzania na Mafunzo ya Ualimu, kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

SPIKA: Kwa mujibu ya Kanuni ya 28(5), naongeza muda usiozidi dakika thelathini mpaka amalize Hotuba hii. Endelea tafadhali!

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa maoni na ushauri unaolenga kuboresha utolewaji wa elimu nchini katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha utekelezaji wa Mpango wa Serikali wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) katika Sekta ya Elimu Nchini. Mpango huu utaweka misingi katika kufikia maendeleo endelevu ya nchi na Wananchi kwa ujumla. Pamoja na juhudzi za Serikali kutenga jumla ya shilingi milioni 73.52 kwa Wizara kutekeleza Mpango huu katika sekta ya elimu nchini, ni ushauri wa Kamati kwamba, Miradi ya BRN katika Sekta hii iwekewe vigezo vya kutekelezwa inavyopimiwa katika kupata matokeo yake. Hatua hii itawezesha kuthamini mafanikio yanayopatikana.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundzi yenye idadi ya taasisi 28, imekusudia kukusanya mapato yenye jumla ya shilingi 239,366,784,212. Aidha, Wizara imekusudia kutumia jumla ya shilingi 344,207,056,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kamati inaamini bado kuna umuhimu wa kuongeza makusanyo ya ndani ya Wizara ikilinganishwa na kiwango cha Matumizi ya Kawaida, kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Wizara ibuni vyanzo vipyta vya mapato ya ndani; kwa mfano, kuiwezesha Taasisi ya Elimu Tanzania kutegemea mapishano mbalimbali kwa matumizi ya jamii ndani na nje ya nchi.

(ii) Kuwezesha Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kufanya matengenezo ya mashine kubwa ya uchapishaji ili kuongeza makusanyo ya ndani.

(iii) Taasisi zinazoonesha upungufu katika ukusanyaji maduhuli zifuatiliwe kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, katika kujadili malengo ya Wizara ya Elimu kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, Wizara imejiwekea vipaumbele vyake kutekeleza majukumu. Ni ushauri wa Kamati kwamba, vipaumbele husika vya Wizara vizingatie vigezo vya SMART kwa lengo la kupima matokeo. Aidha, mikakati madhubuti itumike ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara hii imekuwa ikikwama kutokana na ukosefu wa fedha za utekelezaji wa Miradi hiyo. Hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2013/2014, ni asilimia 21 tu ya fedha za Miradi ya Maendeleo ambazo zilipokelewa na Wizara. Kamati inaishauri Serikali iwezeshe Wizara kutekeleza Miradi ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu ambayo ni moja ya Sekta zilizoko kwenye Mpango wa Serikali wa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Matokeo Makubwa Sasa, kwa kupeleka fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2013/2014: Katika kufuutilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Fungu 46, Kamati imebaini changamoto mbalimbali na kushauri ifuatavyo:-

(i) Ili kuwezesha utekelezaji endelevu wa Miradi ya kuongeza sifa na kuajiriwa kupitia mafunzo ya VETA Mtwara, unaofadhiliwa na Kampuni ya British Gas, ni vyema Shirika la TPDC lihusike katika kufadhili utekelezaji wa Mradi huu ili kuwezesha kudumu endapo Kampuni ya British Gas itamaliza muda wa kufadhili. Mradi huu ni muhimu kwani una lengo la kuwawezesha wahitimu wa mafunzo haya kutumia fedha mbalimbali zinazoambatanishwa na ugunduzi wa gesi Mkoani Mtwara.

(ii) Mradi wa uimarishaji wa Elimu ya Sekondari hususan katika ujenzi wa miundombinu ikiwemo maabara. Baada ya Kamati kubaini mchanganyiko katika matumizi ya ramani za ujenzi wa meza za maabara, inashauri kwamba, miongozo ya ujenzi wa miundombinu hii ya shule izingatiwe. Aidha, kuna umuhimu wa kuangalia upya miongozo iendane na hali halisi ya mazingira ya uhitaji wa shule.

(iii) Mradi wa ukarabati wa Maktaba nchini ikiwemo Maktaba ya Mtwara. Pamoja na juhudzi za Serikali kukarabati maktaba mbalimbali nchini ili ziweze kutoa huduma kwa ufanisi, ni ushauri wa Kamati kwamba, Serikali ichukue juhudzi za makusudi kuinua utamaduni wa kupenda kusoma vitabu nchini.

Mheshimiwa Spika, moja ya mambo yanayosababisha walimu kutohudumiwa ipasavyo ni mfumo unaotumika kuwahudumia (*Teachers Service Delivery System*). Walimu wanahudumiwa na vyombo zaidi ya kimoja na kusababisha adha nyingi ikiwemo urasimu katika kupanda madaraja, kuijendeleza kimasomo, utekelezaji wa malipo ya haki zao mbalimbali kama mishahara na likizo. Kamati inasisitiza yafuatayo:-

(i) Serikali iangalie upya mfumo wa kuhudumia Walimu kwa kuanzisha Tume ya Utumishi wa Walimu ili kukabiliana na adha inayowakibili walimu wetu nchini.

(ii) Serikali iwakutanishe wadau mbalimbali wa Sekta ya Elimu nchini kujadili na hatimaye kufikia mwafaka kuhusu kuwa na utaratibu maalumu wa kuwahudumia walimu kama njia mojawapo ya kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa Serikali wa Matokeo Makubwa Sasa katika Sekta ya Elimu.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, imedhihirika kwamba, upungufu wa walimu hasa katika maeneo ya vijiji unasababishwa kwa kiasi kikubwa na uwepo wa mazingira magumu katika kutekeleza majukumu yao. Kamati inaendelea kuishauri Serikali ikamilishe mapema iwezekanavyo, mchakato wa kutoa posho ya mazingira magumu kwa walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu ili kuwafanya wabaki katika mazingira hayo na kuipenda taaluma yao.

Mheshimiwa Spika, utoaji wa mafunzo kwa walimu kazini ni jambo la msingi katika kuboresha utekelezaji wa Mpango wa Serikali wa Matokeo Makubwa Sasa katika Sekta ya Elimu. Pamoja na juhudni mbalimbali za Serikali zinazochukuliwa kuboresha utoaji wa elimu nchini, Kamati inasisitiza kwamba, mafunzo kwa walimu kazini yapewe kipaumbele na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu iratibu utekelezaji wa utoaji mafunzo kazini kwa walimu ikiwemo kutenga Vyuo vya Ualimu katika ngazi ya Kanda ili kutekeleza jukumu hilo muhimu.

Mheshimiwa Spika, ili kusimamia viwango vya Elimu inayotolewa nchini sambamba na ongezeko la taasisi mbalimbali takribani 20,000 zinazotoa elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu, Kamati inasisitiza yafuatayo:-

- (i) Serikali iiwezeshe Idara ya Ukaguzi wa Elimu nchini kuwa wakala unaojitegemea ili kutekeleza majukumu yake kikamilifu.
- (ii) Serikali iiwezeshe Idara hii kifedha na kivifaa. Aidha, fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza jukumu la Ukaguzi wa Elimu zitumike kwa kuzingatia kusudi hilo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema ya Serikali ya kujenga Chuo kimoja cha VETA katika kila Wilaya nchini, Kamati imebaini changamoto za uhitaji wa fedha kuwezesha VETA kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Kamati inashauri kwamba, *Skills Development Levy* inayopelekwa kuhudumia utolewaji wa mafunzo ya ufundu iongezwe kutoka asilimia mbili kwenda asilimia nne ili kuwezesha VETA kufanya kazi kikamilifu na pia kuweza kuvisaidia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kutoa huduma za Mafunzo hayo muhimu kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto kubwa ya udhibiti wa utoaji wa mafunzo ya elimu ya ufundu stadi nchini. Hatua inayosababishwa na upungufu katika Sheria ya NACTE kuwezesha utekelezaji wa jukumu hili muhimu. Kamati imeshauri kwamba, Sheria ya NACTE iboreshwe, kuiwezesha taasisi hii kusimamia kikamilifu suala la ubora wa mafunzo ya elimu na ufundu stadi nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudni kubwa ya Serikali ya kutenga kiasi kikubwa cha fedha kuhudumia Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu mwaka hadi mwaka, kwa lengo la kuwezesha idadi kubwa ya wanafunzi kupata Elimu ya Juu nchini, Kamati inashauriyafuatayo:-

(i) Ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa watumishi katika sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Elimu hususan katika maeneo ya pembezoni, Serikali ibuni utaratibu maalumu utakaowezesha wahitimu wanaonufaika na mikopo kufunga Mikataba Maalumu kwa kutumikia nchi katika maeneo mbalimbali nchini kwa kipindi maalumu.

(ii) Pamoja na utaratibu unaotumiwa na Serikali kutoa mikopo hiyo kwa kuzingatia masomo ya vipaumbele, suala la kutoa mikopo kwa kulenga wanafunzi wanaotoka katika familia duni pia lipewe umuhimu unaostahili, ikiwa ni dhununi la msingi la utoaji wa mikopo hiyo.

(iii) Ili kuwezesha kuinua uwezo wa kutoa mikopo kwa idadi kubwa ya wahitaji, Serikali iendelee kuchukua juhud za makusudi kuongeza makusanyo ya Mikopo iliyokwishatolewa tangu mwaka 1991.

Mheshimiwa Spika, watu wenyе ulemavu ni kundi muhimu linalohitaji mazingira rafiki na vifaa maalumu vya kuwawezesha kupata elimu kwa maendeleo yao na Taifa kwa ujumla. Kamati inaitaka Serikali kuwa na mkakati wa makusudi wa kuboresha mazingira ya utoaji elimu kwa wenyе ulemavu nchini kwa kutenga fedha za kutosha. Aidha, Serikali itoe Mwongozo wa Kitaifa wa ujenzi wa miundombinu rafiki ikiwemo matumizi ya lugha ya alama na alama mguso katika utaratibu wa kutoa mafunzo kwa kuzingatia mahitaji ya watu wenyе ulemavu.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kufanya ziara katika Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima ilibaini uwepo wa uhitaji wa ukarabati mkubwa wa mashine ya kutengeneza machapisho mbalimbali na hivyo, kusababisha uwezo mdogo wa Taasisi kukusanya mapato ya ndani. Kamati inashauri kwamba, Serikali iwezeshe ukarabati wa mashine hiyo muhimu mapema iwezekanavyo. Hatua hii itaiwezesha Taasisi kukusanya mapato yake ya ndani kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, ilipata fursa ya kuhudhuria Maadhimisho ya Wiki ya Elimu nchini yaliyofanyika katika Viwanja vya Jamhuri Dodoma. Kamati imeipongeza sana Serikali kwa kuanzisha maadhimisho haya kwani yatatoa fursa kwa wadau mbalimbali wa elimu kushiriki, kutafakari, kutathmini na kubuni mikakati mbalimbali yenye lengo la kuboresha hali ya utolewaji wa elimu nchini. Ili kufanikisha suala hili, Kamati ilishauri kwamba, shughuli zinazotekelizwa katika kipindi hiki ziboreshwe ili zilenge katika kuinua kiwango cha elimu nchini. Aidha, matumizi ya TEHAMA kwa kutumia "The Tireless Teacher" kama teknolojia mbadala ya kufundishia masomo ya sayansi ienezwe katika maeneo mengi nchini ili kukabiliana na upungufu wa walimu wa sayansi.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijadili kwa kina Taarifa ya Wizara kuhusu upangaji wa alama za ufaulu na utunuku wa madaraja katika mitihani ya elimu ya sekondari nchini ambayo imefafanuliwa katika Jedwali Namba II, lililopo ukurasa wa 21. Taarifa hii inaonesha kwamba, A itakuwa na marks kuanzia 75 – 100, ambayo ni bora sana (*Excellent*); B+: itakuwa 60 – 74, ambayo ni vizuri sana (*Very Good*); B: 50 – 59 vizuri (*Good*); C: 40 – 49 wastani (*Average*); D: 30 – 39 inaridhisha (*Satisfactory*); E: 20 – 29 hairidhishi (*Unsatisfactory*); na F: 0 – 19 feli (*Fail*). Aidha, Kamati ilielezwa kwamba, kiwango cha chini cha ufaulu (*pass*) katika somo ni Gredi D wenyewe alama 30 – 39 waliopewa maelezo ya inaridhisha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kamati kuelezwa kwamba, Bodi ya Baraza la Mitihani Tanzania imeshiriki katika kuboresha mchakato huu, inashauri kwamba, Serikali itoe elimu kwa wadau mbalimbali wa Sekta ya Elimu nchini kuhusiana na suala hili ili kuondoa mchanganyiko uliopo katika jamii.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe binafsi kwa kushirikiana na Kamati yangu, kila tulipokuwa tunahitaji ushauri kutoka kwako ulikuwa unatupa ushauri mzuri na ulikuwa unatuelekeza vizuri. Ninamshukuru Katibu wetu wa Bunge na Dada Stella, ambaye alituongoza sana katika kuikamilisha Hotuba yetu nzuri tuliyoitoa leo. Ninamshukuru pia Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundı - Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, Naibu Waziri wa Elimu ya Mafunzo - Mheshimiwa Jenista Mhagama, dada yangu na Watendaji wote wa Wizara ya hii, wakiongozwa na Katibu Mkuu Profesa Sifuni Mchome, kwa kushirikiana na Kamati.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mama Margaret Simwanza Sitta, kwa kushirikiana nami katika kuiongoza vyema kamati.

Kwa namna ya pekee, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge wa Huduma za Jamii, kwa busara na umakini katika kujadili Bajeti ya Wizara ya Elimu ya Mafunzo ya Ufundı kwa Mwaka 2014/2015.

Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta – Mwenyekiti, Mheshimiwa Stephen Hillary Ngonyani – Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, Mheshimiwa Faki Haji Makame, Mheshimiwa Christowaja Gerson Mtinda, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Ezekia Dibogo Wenje, Mheshimiwa Antony Gervas Mbassa, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa Gregory George Teu, Mheshimiwa Abia Muhamma Nyabakari, Mheshimiwa Salome Daudi Mwambu, Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, Mheshimiwa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mohamed Gulam Dewji, Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kanalwanda Kahigi, Mheshimiwa Hasnain Mohamed Murji, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso na Mheshimiwa Abdulaziz Mohamed Abood.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, akiwemo Katibu wa Kamati hii Ndugu Stella Mlambo, chini ya Uongozi mahiri wa Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. Ahsante sana.

SPIKA: Maji Marefu leo umejitahidi kweli.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kutumia dakika nilizonazo, napenda niwatambue wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo, ambao ni Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakaguzi na Maofisa mbalimbali wanaoongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo - Profesa Sifuni Mchome; alipo anaweza kusimama ahsante sana.

Yupo Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Kinondoni na Viongozi 45 wa Kata 34 wakiongozwa na Ndugu Salum Madege. Huyu ndiyo Mwenyekiti mwenyewe; Ndugu Salum yuko wapi? Huo ndiyo ujumbe wa kutoka Kinondoni; karibuni sana maana asubuhi mlikosa nafasi.

Tunao Walimu 15 ambao ni Viongozi wa CWT Taifa wa Mkoa wa Dodoma, wakiongozwa na Ndugu Stella Milinga - Katibu Manispaa ya Dodoma. Naomba hawa wote wasimame walipo; ahsanteni sana.

Nina tangazo lingine la kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Peter Serukamba, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, kesho tarehe 18 Mei, 2014 kutakuwa na kikao cha Kamati kwa ajili ya kukamilisha taarifa kuhusu makadirio ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi ya Mwaka wa Fedha 2013/2014. Hakusema mahali, lakini nadhani baada ya ibada labda saa tano, nafikiri saa tano mkutane huko, maana ni Siku ya Jumapili.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nichukue nafasi hii, kuwashukuru sana kwa kazi tulioifanya wiki hii, ilikuwa nzito lakini mmeweza kufanya vizuri. Naomba kila siku tunapofanya kazi yetu upendo uendelee kuwepo pamoja na sisi. Sisi sote tunatetea kitu kimoja, tunatetea masilahi ya Wananchi, hizi tabia za

Nakala ya Mtandao (Online Document)

vuta nikuvute bila sababu, nadhani tuangalie, katika mambo mengine siyo lazima.

Ninawashukuru sana kwa wiki hii nzima na niwatakie Jumapili njema, kesho, tuendelee kukutana Siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi.

(Saa 2.09 usiku Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumatatu,
Tarehe 19 Mei, 2014 Saa Tatu Asubuhi)